

5 JUNI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Tatu - Tarehe 5 Juni, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):

Randama ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

5 JUNI, 2013

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa tunaanza maswali Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 343

**Miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi
Chini ya PPP**

MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED) aliuliza:-

(a) Je, ni miradi mingapi ya miundombinu ya kiuchumi chini ya PPPimeainishwa hadi mwaka 2012?

(b) Je, baada ya Kanuni za PPP kuwa tayari utekelezaji wake umefikia wapi na ni Wawekezaji wangapi waliojitokeza kwa ajili ya miradi hiyo?

(c) Je, kiasi gani (fedha na hisa) cha kushiriki katika miradi hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2012 jumla ya miradi 9 ya miundombinu inayoweza kutekelezwa kwa ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi imeainishwa kama ifutavyo:-

Mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze (*Road toll*); Mradi wa ujenzi wa barabara la Arusha-Moshi (*Road toll*); Ujenzi wa Bandari ya Mbegani-Bagamoyo; Ujenzi wa Bandari ya Mwambani Tanga; Ujenzi wa Bandari ya Nchi kavu Kisarawe (Kisarawe *Cargo Freight Station*); Upanuzi na uboreshaji wa Bandari ya Mtwara; Uboreshwaji wa Bandari ya Kilwa; Upanuzi wa Bandari ya Kasanga pamoja na Upanuzi na Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma.

(b) Baada ya Kanuni za *PPP* kukamilika, Serikali imechukua hatua za kuanzisha Kitengo cha Uratibu chini ya Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) na Kitengo cha Fedha chini ya Wizara ya Fedha. Aidha, Maafisa Dawati (*Desk Officer*) wameshateuliwa kwenye Wizara na baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo kuwapatia mafunzo maalum ya kuwajengea uelewa Maafisa Dawati 60 kutoka Mamlaka za Serikali na Sekta binafsi ili waweze kuratibu ubainishaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya *PPP*, Wawekezaji wanatarajiwa kupatikana baada ya Mamlaka husika za Serikali kuwa zimekamilisha upembuzi yakinifu wa miradi na kuitangaza kwa lengo la kupata wawekezaji watakaoingia ubia na Serikali. Mchakato wa upembuzi yakinifu unaendelea katika maeneo mbalimbali kabla ya kuitangaza miradi itakayohusika.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeleo yangu ya ufanuzi katika sehemu (b) ya swali hili, fedha na hisa katika miradi inayotarajiwa kuwekezwa kwa utaratibu huo wa *PPP* bado hazijaainishwa.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yak mazuri, pamoja na majibu hayo, nitakuwa na swali moja tu la nyongeza.

Miradi iliyoainishwa, ni miradi tisa, tena mikubwa sana, Mheshimiwa Waziri, hauoni kuna haja ya kuweka kipaumbele miradi michache ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

5 JUNI, 2013

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la nyongeza kama ifuatavyo:-

Miradi iliyoainishwa ni tisa, ni michace, hapana siyo michache, miradi hii, umesema ni mingi, lakini mimi naona ni michache, kwa sababu tunatarajia kila Sekta na kila Wizara iainishe miradi ambayo inaweza kufaa kwa utaratibu huu wa *PPP*. Kwa sababu hii miradi yote hatutegemei kwamba itachukuliwa au itajengwa na Kampuni moja, sisi tunatangaza, na watu wa mataifa yote, ni tenda ya Kimataifa, mtu ye yeyote Duniani anaweza kuja kuchagua mradi mmoja aka- *invest* kwa mradi ambao anaona unafaa kuingia *PPP* kati yake na Serikali kwa aina yoyote ya Sekta.

Kwa hiyo, ingawa wewe nafikiri ni mingi, lakini mimi nafikiri ni michache, na sisis Serikali bado tunaendelea kuainisha miradi mingine na ndiyo maana tumewaelimisha wale vijana katika kila Sekta ili wajue namna ya kuainisha, ni aina gani ya miradi ambayo inaweza kuingiwa kwa ubia kati ya Sekta binafsi na Sekta ya umma.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na mafanikio kadhaa katika *Public Private Partnership*, kuna changamoto ambazo zimejitokeza ukimemo urasimu, ikiwemo kutokuwa na uwazi katika mipangilio yote ya *PPP* na vilevile kutokuaminiana kati ya wawekezaji na Serikali. (*Makof*)

Je, Serikali inatoa kauli gani sasa ili tufikie sasa muwafaka wa kuweza kuwa elimisha watanzania na hatimaye kuwa na mafanikio katika miradi ya *PPP*?

SPIKA: Mheshimiwa wa Nchi naomba ujibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Leticia Nyerere kama ifuatavyo:-

Urasimu, ndiyo, lakini kutokuelewana, hakupo, kwa sababu miradi hii hatujaanza kutekeleza, na kama unavyoja kwamba Sera yake imepitishwa mwaka 2009, halafu tukatunga Sheria ya mwaka 2010, na Kanuzi zake tumetayarisha 2011, na kwa mujibu wa Sheria tunatakiwa kuanzisha *units* mbili za kusimamia mambo hayo, moja itakuwa *TIC* na nyingine Wizara ya Fedha.

Sasa kwenye upande wa urasimu na sisi tumeona kwamba jambo hili ili liende haraka lazima liwe na *one stop center*, liwe na *unit* moja badala ya kuwa na *units* ambazo zinasimamiwa na Wizara mbili tofauti.

Kwa hiyo, marekebisho haya yanafanywa, tutaleta ndani ya Bunge ili tuwe na *unit* moja ya kusimamia badala ya *units* mbili, lakini mpaka sasa hayo unayoyasema ume-*experience*, hatuja- *experience* bado sisi, ya kwamba kuna kutokuelewana, au mpalaganyiko wowote, hapana. Tunaendelea vizuri, sasa hivi kama nilivyo sema tunaainisha miradi ya kutosha ili tuweze kuifanyia upembuzi yakinifu, tuitangaze, tupate watu ambao wanaweza kuwa na nia ya kuwekeza pamoja na Serikali.(*Makof*)

SPIKA: Naona tuendelee na swali linalofuata, muda.

Na. 344

Upatikanaji wa Maji Katika Mji wa Muheza

MHE. HERBERT J. MNTANGI Aliuliza:-

(a) Je, Serikali itasaidia lini jitihada za kuipatia Halmashauri fedha kuelekea kutekeleza miradi ya maji ya visima na kuboresha vyanzo vya maji?

(b) Je, ahadi ya kuipatia Mji wa Muheza maji kutoka chanzo cha Mto Zingi itatekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Muheza unafikia asilimia 56.3 ya mahitaji yote ya wakazi wa eneo hilo. Ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji maji katika Mji wa Muheza, Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 ilitenga shilingi milioni 302.6 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji katika vijiji vya Ubembe, Kwembosi, na Kisiwani.

Aidha, katika mwaka huo, Halmashauri iliidhinishiwa maombi maalum ya shilingi milioni 100.0 ambazo zinatumika kwa ajili ya kuendeleza kisima kilichopo eneo la Polisi Mang'anya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, kiasi cha shilingi milioni 232.9 zilitengwa na hadi sasa zimetolewa shilingi 170.6 sawa na asilimia 73.3 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji katika kijiji cha Kibanda.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2013/14, Serikali imeidhinisha jumla ya shilingi milioni 116.4 na zinatarajia kujenga mradi wa maji ya bomba kutoka katika kisima chenye uwezo wa kuzalisha lita 26,000 kilichoko katika kijiji cha Kigongomawe. Serikali itaemdelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutatua taizo la maji katika Mji wa Muheza, Serikali inapanga kutumia chanzo cha Mto Ziggi ambacho ni cha uhakika. Tayari upembuzi yakinifu umefanyika kuititia Kampuni ya Ushauri ya Misri (*Arab Consulting Engineers*).

5 JUNI, 2013

Baada ya usanifu, gharama zinazohitajika ili kutekeleza mradi huo ni shilingi bilioni 13.4. Andiko la mradi huu limewasilishwa katika Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa ajili ya kufanyiwa kazi ili kupata fedha zitakazowezesha utekelezaji wa mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha Mto Ziggi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naombakumshuru sana Mheshimwia Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu, hata hivyo nina mawili ya nyongeza.

Moja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji alifika Muheza katika kisima hicho cha Polisi Mang'anya, na akaona teknolijia mpya ambayo tumetumia ya kutumia sola kuweza kuwasilisha maji katika maeneo mengi ndani ya Mji wa Muheza. Sasa tumegundua maji katika maeneo mengine makubwa manne, ndani ya Mji wa Muheza, pale Genge na Michungwani, lakini hatua fedha za kuweza kununua teknolojia hiyo mpya.

Je, Wizara itatusaidia kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili waweze kuleta fedha kwa haraka tuweze kufanikiwa kupata kujenga miundombinu hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la pili, wapo Wamarekani wamefika Muheza kutusaidia katika kutafuta maji, na wamekuja na mashine mpya nzuri ya kisasa ya kiuweza kutafuta na kuchimba na wamefanikiwa katika visima hivyo ambavyo nimevitaja vinne, na wako tayari kutuuzia mashine mashine hiyo kwa shilingi milioni 200 tu, lakini hatuna fedha.

Je, Wizara inawez akutusaidia ili tusipoteze nafasi hii ya kuweza kupata mashine hiyo? (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii *development* anayoizungumzia Mheshimiwa Herbert Mntangi ni mpya, lakini nikielewa kwamba, kuna mipango ambayo tuliweka kwa ajili ya miji na kwa ajili ya miji midogo, na ninachoelewa hapa hatuwezi kumkatalia jambo hili kwa sababu ni jambo ambalo linaonekana kwamba wakati tunapofikiria huu mradi mkubwa wa Ziggi ambao unakwenda bilioni 13, ni mpango ambao uanweza ukasaidia kusaidia wananchi wakaendelea kupata huduma hiyo mpaka wakati tutakapokuw atumefikia katika huu moango mkubwa ambao utachukua muda murefu.

Kwa hiyo, nitamuomba baadaye tukutane tukae vizuri ili tuweze kuona, kwa sababu hiki ni kitu kipyा amekileta hapa, bajeti ya kwanza inakwenda kwenye milioni 304, sasa tutaona jinsi ambavyo tunaweza tukawasaidia, ili tuweze kuona kuna nini.

Sasa anazungumza tena habari nyingine tena ya Wajerumani kwamba wamekwenda kule...

SPIKA: Wamarekani.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOÀ NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Wamarekani, samahani.

Wamarekani kwamba wamekwenda kule na wamepata, zinatakiwa shilingi milioni 200. Sasa milioni 200 mimi hapa ninaandiko, ambalo limetoka Wilaya ya Muheza, andiko hili la mto Ziggi likapelekwa Mpango, na kutoka kuele Mipango likaletwa kwetiu sisi TAMISEMI, na sisi tumelipokea, tumeliandikai, na sasa hivi nipozungumza hapa, nimelileat ahapa, kwa sababu nilijua hapa inaweza ikatokea zogo, tayari temepeleka Mipango.

Sasa Mheshimiwa Mbunge aniamnbie, niache huu mpango niingie kwenyempango wa milioni 200, au twende na mipango yote miwili, mimi niombe Mheshimiwa, kupanga ni kuchagua, kama tunaona kwamba huo mpango

anaozungumza unaweza ukasaidia ukatuondoa katika hili jambo la bilion 13, lakini nataka nimwambie kwamba kiuma mpango mahususi wa kiserikali ambao una *endorsement*. Kwa hiyo, sasa hapa tukae tiufikirie vizuri, mimi siuna tatizo, lakini mpango tulionao hasa ni huu hapa.

SPIKA: Tunaendelea, mtajua na ninyi wenyewe.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa, Mto Ziggi ni chanzo cha maji cha uhakika, na tumeona kuwa vyanzo vya maji vya uhakika vinazidi kupungua. Sasa Serikali inachukua hatua gani madhubuti kuhakikisha kuwa vyanzo hivi vyamaji vya uhakika vinatunzwa ili navyo visipotee, ili viweze kuwapatia maji, siyo isiwe Wilaya ya Muheza tu, lakini pia Wilaya ya Tanga na Mkinga, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Nundu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili wakati alipokuwa nazungumza ofisi ya Makamu wa Rais, alipokuwa anatoa hotuba yake Dkt. Huvisa, wali-*address* hili jambo ni kweli kabisa kinachosemwa hapa, kuna tatizo kwa Tanzania nzima kabisa, vyanzo vya maji vimechezewa chezewa sana kiasi ambacho tuna hatari sasa kwamba tunaweza tukafika mahali tukawa hatuna kabisa maji, na Mkoa wa Tanga huo anaouzungumza Mheshimiwa Mbunge, ni Mkoa mmoja ambao umeathirika katika hali hiyo.

Mpango tulinao sasa hivi ni kwanza tuna *By Laws* katika Halmashauri, tumezuia watu wasichunge Ng'ombe, wasilime katika vyanzo vya maji n akuzuia kabisa mita 30 kutoka kwenye mito pale kuzua kwamba watu wasiendelee kulima lim akule na nini, ili kuhakikisha kwamba tunahifadhi maji.

5 JUNI, 2013

Kwa hiyo, tumefanya hayo, kuna hizo Sheria ndogo, tunapanda miti, na tunaemndeala kuhamasisha Taasisi mbalimbali zilizopo katika Halmashauri kuhakikisha kwanza vyanzo nya maji vinatunzwa ili maji yazidi kuendelea kupatikana.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 345

Upanuzi wa Taasisi ya Mifupa- *MOI*

MHE. MUSSA Z. AZZAN (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI) aliuliza:-

Mkoa wa Dar es Salaam ni miongoni mwa Mikoa yenye majanga mengi ya ajali za barabaran na matukio mengi ya hatari:-

(a) Je, upanuzi wa Taasisi ya Mifupa- *MOI*, utakamilika lini?

(b) Je, vitengo nya mifupa kwenye Hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala vyenye vifaa na Wodi za wagonjwa wa mifupa vitaanza kufanya kazi lini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko wapi, hili linajibwi na nani? Na wewe mwenyewe, *okay*, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Utawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam N. Kisangi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimi wa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mariam N. Kisangi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo jipya la Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*) litakalokua na ukubwa wa vitanda 310 ulianza Oktoba, 2012. Ujenzi unachukua muda wa wiki 58 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2013. Baada ya kukamilika, Taasisi itakuwa na jumla ya vitanda 342, kwa mgawanyo ufuatao:-

Vitanda 240 kwa wagonjwa wa kawaida, 62 kwa wagonjwa wa huduma binafsi (*private patients*) na 40 kwa wagonjwa wanaohitaji uanganlizi maalum (*Intensive Care Unit*). Kati ya vitanda 62 vya wagonjwa wa huduma binafsi, vitanda 32 vipo tayari kwneye jengo la sasa. Hadi kufikia Mei 31, 2013, ujenzi ullkuwa umefikia katika hatua za ghorofa nne kati ya ghorofa sita zitakazojengwa. (Kutoka *semi basement, basement, ground, 1st, 2nd, 3rd to 4th*).

(b) Mheshimiwa Spika, huduma kwa wagonjwa wa mifupa katika Hospitali za Amana na Temeke hutolewa na Madaktari Bingwa wa Upasuaji (*Surgical Specialist Doctors*) kwa kuzingatia taratibu za tiba. Katika kutoa huduma hizi, zipo changamoto zinazozikabili hospitali hizi zikiwemo: - Ukosefu wa Wodi maalum ya matatizo ya mifupa, upungufu wa watumishi na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya ujenzi.

Aidha, hospitali ya Mwananyamala pekee ndiyo ambayo hitoi huduma hizo kwa sasa. Wagonjwa wenye mahitaji ya tiba ya mifupa hupewa rufaa kwenda Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Katika Hospitali za Amana na Temeke wagonjwa wa dharura (*emergency cases*) hupatiwa rufaa kwenda Taasisi ya Mifupa ya *MOI*.

Kwa sasa hospitali zote tatu za hazina Wodi mahsusini (*orthopedic wards*) kwa wagonjwa wa mifupa. Wagonjwa wenye matatizo ya mifupa wanapohudumiwa hulazwa katika wodi za kawaida za upasuaji (*surgical wards*).

5 JUNI, 2013

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Zungu swali la nyongeza!

MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN: Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la Serikali moja ya changamoto imeonyesha ni ufinyu wa wodi na maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hospitali ya Amana, eneo la jengo la Amana Social Hall kwenye *Government notice* ya zaidi ya miaka 10 iliyopita, eneo hili wamekabidhiwa Manispaa ya llala lakini mpaka leo eneo hili Serikali bado hajatoa msaada wowote wa kulisaidia eneo hili lirudi kwa Manispaa ya llala ili sasa iweze kupata eneo hili na kujenga hospitali kubwa ya kusaidia wananchi. Jengo hili ni mali ya Serikali na wananchi hawa ni wa Serikali. Je, Serikali inasema nini sasa kuhusu jengo hili kulirudisha kwa Manispaa ya llala kwa mujibu wa *Government notice* ya Serikali yenyewe?

NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu kama ifuatavyo:-

Naomba ni-*confess* kwamba ndiyo nalisikia hili jambo hapa sasa hivi kuhusu hilo jengo pamoja na kwamba anataja kwamba kuna *Government notice*, nitamwombwa Mheshimiwa Zungu anipe details zote halafu nitafuatilia halafu baadaye nitampa majibu mahususi.

MHE. ZARINA SHAMTE MADABIDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama alivyojibu kwenye jibu lake la msingi kwamba hakuna vitengo hivi katika Hospitali ya Mwananyamala, Temeke wala llala. Je, Serikali haionti kwamba kuna umuhimu wa kuweka hata sehemu za dharura ambazo wagonjwa wanaweza kuhudumiwa kwa sababu sasa hivi kila mgonjwa ni lazima apelekwe kule na hali ya ajali imekuwa kubwa sana kama unavyojua Dar es Salaam wananchi ni wengi sana.

Je, Serikali inatuambia nini kuhusu kuweka vitengo vya dharura katika hospitali hizo tatu?

5 JUNI, 2013

WAZIRI WA NCHI, OFIRI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, hospitali za Mwananyamala, Temeke na Ilala ni hospitali za Mkoa kwa Dar es Salaam, kwa hiyo, ni jukumu la Mkoa wa Dar es Salaam kupanga na kutekeleza huu mradi na kuweka hicho kitengo.

Wakati wowote watakapoamua Serikali au Wizara ya Afya iko tayari kushirikiana nao kama wanavyoshirikiana na vitengo kama hivyo na uanzishwaji wa vitengo kama hivyo katika hospitali za mikoa. Serikali imeshapandisha hadhi hospitali hizo na imeshateua baadhi ya hospitali nyingine yaani vituo vya afya ambavyo sasa vimekuwa hospitali za wilaya.

Kwa hiyo, ni jukumu la Mkoa kuititia vikao vyao RCC ili kuamua na kujenga na kutekeleza hilo miradi katika hospitali zao.

Na. 346

Huduma za Matibabu kwa Mama Mjamzito na Watoto

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Serikali ilitangaza matibabu bure kwa Mama Mjamzito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, tamko lililokataza Mama Mjamzito anapokwenda kujifungua asilizwe kupeleka vifaa kama nyembe, mipira, groves na kadhalika.

Je, agizo hilo la Seriali liliishia wapi kwani akina Mama wajawazito bado wanadaiwa kutoa vifaa wakati wa kujifungua?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawaziri leo siwaoni wengine!

NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mwanza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa Sera ya afya ya mwaka 2007, Serikali imeweka utaratibu wa kutoa huduma ya matibabu bila malipo kwa Mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mtano. Huduma kwa Mama mjamzito na watoto chini ya miaka mtano, inahitajika kutolewa kwa wakati, ili kuhakikisha kunakuwa na matokeo mazuri kwa mama mjamzito na mtoto. Ili kuhakikisha kwamba kila mwanamke mjamzito na watoto chini ya umri wa miaka mitano wanaptaiwa huduma bora na kwa wakati, Wizara iliandaa sera ya afya ilikusimamia huduma zitolewazo.

Mheshimiwa Spika, afya ya Mama na mtoto ni moja ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika sera na hujumuisha mfumo wa utoaji huduma maalum kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa na watoto wa umri chini ya miaka mitano. Huduma kwa wanawake wajawazito na watoto ni pamoja na kutambua vidokezo vya hatari kwa wajawazito na watoto, chanjo, tiba, elimu ya uzazi , lishe na uzazi salama.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za utoaji huduma bila malipo kwa kundi hili. Katika kuhakikisha kuwa huduma kwa Mama wajawazito na watoto zinaimarishwa, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inafanya utafiti wa kifurushi cha dawa na vifaa muhimu kama gloves, kifungo cha kitovu, mpra, pamba, nyembe na kadhalika kwa Mama mjamzito. Kifurushi kinatolewa wakati Mama napaohudhuria kliniki ya ujauzito ili kufanikisha ya azma ya kuwa tayari kabla ya kujifungua (*birth preparedness*).

Kwa sasa mpango huu unatekelezwa kwa majaribio katika Mikoa ya Pwani na Dodoma. Matokeo ya uzoefu utakaopatikana utatumika katika kueneza mpango huu katika Mikoa yote nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa Mama mjamzito anapokuja kujifungua anakuwa na vifaa na dawa muhimu anazohitaji kwa dharura bila kulazimika kununua.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa nia ya Serikali ni kutoa huduma kwa Mama wajawazito chini ya umri wa miaka mitano bila malipo ipo palepale, haijabadiilika. Kwa mantiki hii, mtumishi yejote atakayethibitika kuwatoza Mama wajawazito na watoto wa umri wa miaka mitano, atakuwa amefanya kosa kwa mujibu wa sera. Serikali haitasita kuchukua hatua za kinidhamu dhidi yake kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma kama atafanya vinginevyo.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema mtumishi atakayemtoza Mama mjamzito na mtoto chini ya miaka mitano atachukuliwa hatua kisheria kwa sababu sera inasema asitozwe.

Na kwa kuwa, tunapitisha hapa Bungeni pesa kwa ajili ya kupeleka huko Wizara ya Afya chini lakini pesa hizo haziendi.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni anatoa matamko ambayo yanawalaghai Watanzania kwa kitu kisichotekelezeka? (*Makof!*)

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba ni mwaka mmoja sasa tangu tuambiwe kwamba kutakuwa na *delivery kits* katika Mikoa ya Pwani na Dodoma kwa ajili ya majaribio na sasa yapata mwaka mzima matokeo hayajatoka ya utafiti huu wa kuwasaidia akina Mama.

Ninapenda kujuu, katika huu mwaka mmoja tu ni utafiti gani ambao wamegundua unaoweza ukawasaidia akina Mama kuititia hiyo delivery kits ili uweze kuenea nchi nzima? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga wa Viti Maalum kutoka Mwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili jambo linalosemwa hapa ni jambo kubwa na hili jambo tunalolizungumza hapa ni jambo ambalo tukifanya mchezo watu watakuufa.

Mimi nataka tuelewane vizuri hapa, mimi nimetoka katika Mikoa ya Kusini nimezunguka yote na ujumbe tunaoutoa hapa, na ninaomba mningalie macho yangu na muangalie midomo yangu, habari ya kutuambia kwamba kuna mtu anatoza fedha kwa akina Mama wajawazito haipo katika sera za Serikali, watoto wenye umri wa miaka mitano kwenda chini haipo, wa *TB* na Kifua Kikuu na mambo mengine yoyote kama Saratani haipo katika utaratibu wa sera ya Serikali.

Nataka niseme hapa na kama kuna Wabunge wanajua kuna vituo ambavyo vinatoza akina Mama wajawazito, ninaomba nipewe orodha yao, naomba mtupatie, mtupatie kabisa kwani this is a serious matter. Tumepita nchi nzima tunawaambia watu hakuna kutoza Mama mjamzito hapa Tanzania. Nataka tuelewane vizuri hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo linalozungumzwa hapa ni kwamba baada ya kuona hii yote inayozungumzwa hapa na inayoleta matatizo kwa sababu mambo ya msimamo ni lazima tuseme kwa msisitizo na ndiyo maana unaona sauti inapanda. Hapa tumesema hivi, tunaona tunapata tatizo

katika hili eneo, hebu fanya pilot study, nenda Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dodoma hapa tulipo, fungasha kifurushi hivi mpe Mama wakati anapokwenda kuangalia hali yake na mimba inavyoendelea kukua, mfunganishie aende na hicho kifurushi badala ya kuwenda kulipa akadaiwa na vitu vingine hivi vyote vinavyosemwa mfungashie. (*Kicheko*)

Hili jambo Waziri wa Afya akaja hapa akatuambia kwamba utaratibu huu tukifanikiwa tutau-roll over wanaita ku-scale up ka nchi nzima ili tuondokane kabisa na hii habari ya kumtoza Mama mjamzito. Kwa hiyo, utaratibu huu unaanyiwa majaribio.

Sasa Mheshimiwa Kimwanga anaposema hii itachukua muda gani mbona inachukua muda mrefu, mimi nataka nikubaliane na wewe kwamba kuna haja ya kufanya haraka ili kazi hii iweze kumallizika. Lakini kama tulimsikiliza vizuri Waziri wa Afya na sisi TAMISEMI tunesema hapa ni mpango wote ambao tunataka tuondokane nao ili Mama mjamzito anapokwenda hospitali tuhakikishe anakwenda pale anapata hivyo vifaa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, na kule kwako Njombe wambiieni kabisa kwamba hatutaki Mama mjamzito atozwe senti tano na kama mna majina mtupatие haraka. (*Makof*)

SPIKA: Waziri katoa semina na muda umekwisha, nakwenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Mheshimiwa Kabati atauliza swali hilo.

Na. 347

Mgawo wa Matrepta Mkoani Iringa

MHE. RITA E. KABATI aliuliza:-

(a) Je, ni matrepta mangapi ya *Power Tiller* yamegawanywa katika Mkoa wa Iringa kwenye Wilaya ya Kilolo, Mufindi na Iringa vijijini?

- (b) Je, ni matrekta mangapi bado yanafanya kazi?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuhimiza matumizi ya zana za kilimo ili kupunguza harubu na kuongeza ufanisi katika kilimo. Idadi ya matrekta makubwa yanayofanya kazi nchini imefikia 9,148 na madogo yaani power tillers ni 5520.

Kutokana na kuongezeka kwa matrekta eneo linalolimwa kwa matrekta sasa limeongezeka kutoka 10% hadi 14% ya eneo lote linalolimwa nchini. Aidha, eneo linalolimwa kwa jembo la mkono limepungua kutoka 70% hadi 64%, eneo lilllobaki sawa na 22% linalimwa kwa kutumia wanyamakazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto za matumizi ya power tillers kutokana na kumekuwa na changamoto za matumizi ya *Power tillers* kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo maopereta kutokuwa na ujuzi wa kutosha kuyatumia na mahali pengine matrekta madogo kulima kulima mashamba yenye udongo mgumu kinyume na matumizi yake sahihi kwa sababu matrekta madogo siyo mbadala wa matrekta makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Rita E. Kabati Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, jumla ya matrekta madogo ya mkono *Power tillers* 434 yalisambazwa katika Mkoa wa Iringa ambapo kati ya hayo Wilaya ya Kilolo ilipatiwa matrekta 62, Mufindi matrekta 140, Iringa Manispaa matrekta 26 na Iringa Vijiji matrekta 206.

- (b) Mheshimiwa Spika, kati ya matrekta hayo yaliyosabamzwa Mkoani Iringa matrekta 388 yanafanya kazi na matrekta 46 hayafanyi kazi.

5 JUNI, 2013

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri katila swali la msingi. Lakini nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Iringa una mabonde na miinuko na udongo wa hali tofauti. Je, katika uamuzi wa kununua matrekta hayo ya power tiller Serikali ilizingatia utaalamu wa hali ya udongo, miinuko na mafunzo kwa watumiaji?

Pili, Serikali inatoa kauli gani kwa power tiller ambazo zinatumika kubebaa matofali, kuni , maji na kadhalika kinyume na malengo yaliyotarajiwा zikitumika kama makwama?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kabati kama ifuatavyo:-

Kaman ilivyosema matrekta haya madogo yanatumika wakati mwингine kinyume na matarajio au na makusudio. Sisi kama Wizara tumetoa miongozo kwa Halmashauri zote, tumetoa taratibu na viwango vinavyotakiwa ili mzabuni au mnunuzi wa matrekta haya anapoyanunua ajue matrekta haya ambayo mengi yanaishia *horse powers 16* yanatumika katika maeneo gani. Sasa miongozo hii tumeisambaza katika Halmashauri zote ili zitumike kwa ajili ya wale wanunuzi wanaonunua matrekta haya na yanapofika yaweze kujulikana yanatumika katika maeneo gani.

Kwa hiyo, ni jukumu sasa la Halmashauri za Wilaya kule kuzitumia vizuri ofisi za kilimo zilizopo katika kila Halmashauri na katika kila Halmashauri tunaye Afisa wa Zana ili aweze kuwaelekeza matumizi sahihi ya *power tillers* hizo kwa sababu kazi yake kwa kweli siyo kweli siyo kwenda kukwatua mashamba yenye udongo mgumu, kazi yake ni kama

kuchavanga, kunyunyizia na wakati mwingine hata kupulizia dawa au kupampu maji yaani kazi zile ndogondogo za kuchavanga mashamba.

Sasa wale ambao pia wanatumia kwa kazi nyingine ya kusomba mazao hilo pia siyo tumizi bayo kwa sababu trekta lile lina *trailer* na kazi mojawapo baada ya kufanya kazi za kawaida za mashambani ni pamoja na kufanya kazi nyingine kama kubeba kuni za mkulima kwa sababu amenunua trekta lile ili limsaide kupunguza harubu zote pamoja na kazi za mashambani na hata za nyumbani.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kuitia Wizara yako na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, wananchi wengi sana wamehamasika katika suala la kilimo, hata vijana wengi ambao wanamaliza elimu ya juu na wafanyakazi wengi wanaoishi mijini wameshakwenda kutafuta maeneo kwa ajili ya kulima. Sasa tatizo kubwa ni zana za kilimo na hasa matrekta.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuleta matrekta mengi ya kumwaga ili kila anayetaka kutumia matrekta hayo aweze kuyapata kiurahisi? Ahsante sana!

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba ujibu kwa kifupi tu kuhusu matrekta ya kumwaga.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matrekta pia ni biashara kwa hiyo, sisi tunachohamasisha ni uingizajiwa matreka nchini, tuna taratibu tunatumia Serikali lakini tunawatumia hata wafanyabiashara binafsi kuingiza matrekta nchini. Ninachowea kusema kwa wale vijana ambao wanataka kuijingiza katika kilimo na ninawapongeza kwani wapo wengi kama Igunga, Mtwara wapo wameanza na kadhalika. Ninachowea kusema ni kwamba vijana kama hawa

tutawasaidia kuweza kupata mikopo rahisi na hasa kupitia kwenye mfuko wetu wa pembejeo ambao upo chini ya Wizara yangu na wengi wameshafika ofisini kwangu na ninawa-*encourage* kabisa waje kwa sababu tutajaribu kutafuta upendeleo maalum ili waweze kuutumia mfuko huu wa pembejeo za kilimo vijana ili waweze kujingiza kwenye kilimo.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali illagiza na kuingiza nchini matrekta kupidia *SUMA JKT*, na iliyakopesha nchi nzima lakini yamekwisha na walituahidi kwamba wataleta matrekta mengine hasa Mkoa wa Ruvuma.

Je, utaratibu huo umefikia wapi kwa sababu wakulima wamejandaa kuyasubiri matrekta hayo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita R. Kawawa kama ifuatavyo:-

Kama mlivyoshuhudia wenyewe matrekta yale yaliyoingizwa nchini na SUMA JKT baada ya kupunguzwa bei yalinunuliwa vizuri na wananchi wameitikia. Sasa Serikali wakati ule tulipata mkopo wa masharti nafuu kutoka India lakini hivi sasa Sizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa bado tunaandaa utaratibu mwingine kuangalia uwezekano wa kupata tena mkopo mwingine wa masharti nafuu.

Sasa mkopo unachukua hatua mbalimbali kwa kweli sasa hivi siwezi kusema kwamba yataingia lini kwa sababu taratibu za mkopo huo bado hazijakamilika. Lakini lengo letu ni kuhakikisha kwamba matrekta hayo yanaongezeka hata kama siyo huo mkopo tutatafuta njia nyingine kupata matrekta.

5 JUNI, 2013

Na. 348

Kupeleka Umeme Kwenye Wilaya Mpya

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Serikali imeamua kusogeza huduma za utawala karibu na wananchi kwa kuanzisha Mikoa na Wilaya mpya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Wilaya mpya za Kakonko, Uvinza na Buhigwe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha inafikisha nishati ya umeme katika Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zote. Hadi sasa, kati ya Wilaya 133 ni Wilaya 16 tu ambazo hazijapatiwa umeme zikiwemo Wilaya mpya za Kakonko, Uvinza na Buhigwe. Utekelezaji wa miradi ya umeme katika Wilaya hizi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme za misongo mbalimbali, ufungaji transforma na kuunganisha wateja wa awali wapatao 4,235.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kupeleka umeme katika Wilaya zote tatu za Kakonko, Uvinza, Buhigwe inakadiriwa kuwa na jumla ya shilingi b ilioni 10.32. Kazi ya kupeleka umeme katika Wilaya hizo itaanza mwaka huu 2013 chini ya mpango kabambe wa Umeme Vijijiini awamu ya pili (II) chini ya uvezeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijiini (REA).

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

5 JUNI, 2013

Swali langu la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kazi hiyo itaanza mwaka huu wa 2013, wananchi wale wanahitaji kujua ni lini sasa watapata umeme huo?

Swali la pili, katika utekelezaji wa llani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010 wakati Rais akipita kunadi sera za Chama cha Mapinduzi aliahidi kwamba, kila makao makuu ya Wilaya yatapatiwa umeme. Wilaya za Kasulu na Kibondo tayari zimeishapatiwa umeme kwa kupitia jenereta na umeme huo ni mwingi sana.

Wananchi walio wengi wameishalipia gharama ili waweze kusambaziwa umeme katika maeneo yao, na mwaka jana wakati akijibu swali Naibu Waziri, George Simbachawene, alisema ifikapo mwezi wa Kumi na Moja, 2012, wananchi wote ambao tayari waliishalipia gharama ili wapatiwe umeme watakuwa wamepatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, nataka Naibu Waziri awaambie wananchi wa Kasulu na Kibondo ni lini sasa watapatiwa umeme kwa sababu tayari waliishalipia gharama kwa ajili ya kuwasambazia umeme?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kwamba, kwenye Bajeti hii tuliyopitisha juzi ziko fedha katika Bajeti hii shilingi bilioni 71 ambazo ni kwa ajili ya kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya zote mpya nchini na miongoni mwa hizo ni pamoja na hizi za Uvinza, Buhigwe na hizo nyingine ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba fedha za kutekeleza mradi huu zipo, tena mlizipitisha ninyi wenyewe hapa wakati wa bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, kwenye Ilani ya Uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi mipango ya kupeleka umeme katika wilaya za Kasulu na Kibondo. Tumeweza kutekeleza mipango hiyo na umeme ni mwingi na ni kweli ni dhamira ya Serikali kuhakikisha tunasambaza umeme au wananchi wanawenza kuweka umeme katika nyumba zao na maeneo mbalimbali ya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tu kwamba baada ya kushusha gharama ya kuunganishiwa umeme majumbani wamejitokeza wateja wengi wanaotaka kuwekewa umeme na hiyo kuwa kidogo ni changamoto kwa *TANESCO* kwa sababu vifaa vinavyotakiwa kwa nchi nzima pia ni vingi.

Nitamwomba tu Mheshimiwa Mbunge nipate taarifa ya kutosha kuhusu Kasulu na Kibondo ni watu wangapi, halafu nione ni namna gani tunaweza tukasaldiana na mameneja wa *TANESCO* kule tuone ni namna gani tunaweza tukatekeleza ile miradi kwa wale waombaji ambao tayari wameomba na kulipia.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, asante. Wilaya ya Uvinza katika mpango wa Wizara itapata umeme kutokea Kigoma Mjini kutokana na ziada ya umeme pale Kigoma Mjini. Hata hivyo, bado jenereta ambazo zinazalisha umeme pale Kigoma Mjini zina tatizo kubwa sana la mafuta kiasi kwamba, kila mwezi umeme unakatika kwa zaidi ya wiki nzima.

Sasa ningependa Wizara itupatie majibu ili Uvinza tusije tukapata tatizo kama la Kigoma Mjini, kwamba ni namna gani Serikali itahakikisha tatizo la mafuta linakoma katika mkoa wa Kigoma ili kusudi ule umeme unaozalishwa kwa kutumia jenereta uwe wa uhakika.

SPIKA: Mheshimiwa sema tatizo linakwisha bwana, unasema linakoma kwani unagombana na nani? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, tatizo la mafuta yanayotumika kuendesha majenereta katika sehemu mbalimbali na hasa maeneo yote ambapo tunatumia majenereta, mara chache hutokana na sababu za kawaida, lakini kubwa hapa huwa ni sababu za kizembe kwa sababu kama wewe ni meneja mahali hapo na unajua umeme wako unatokana na mafuta mpaka yanakwisha uko wapi?

Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge tukubaliane tu kwamba, nadhani kuna watu wanaofanya uzembe, kama itatokea itabidi tupate sababu za kina na vinginevyo tutachukua hatua kwa wote wanaosababisha uzembe huu kutokea.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Wakati anajibu swal la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema bado wilaya 16 hazijapatiwa umeme na mojawapo ni wilaya ya Nanyumbu ambapo Naibu Waziri alikuja mwaka jana akatoa ahadi kwamba, umeme utakuja hapa Nanyumbu.

Sasa namuuliza mbona ule umeme mpaka sasa haujafika na utafika lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli nilitembelea Nanyumbu na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwani pamoja na kwamba alikuwa mgonjwa lakini alishiriki kwenye ziara yangu.

Tulikubaliana na ninaona umuhimu wa kituo kile cha afya ambacho niliona ni lazima kipate umeme na sitakubali ahadi yangu ipite bure. Nitajaribu kuangalia ni nani amekwamisha ahadi hiyo na nimuombe Mheshimiwa Mbunge nikimaliza kujibu swal hapa tuonane.

5 JUNI, 2013

Na. 349

Ahadi ya Rais ya kupeleka Umeme Malangali

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

(a) Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ya kupeleka umeme Malangali itatekelezwa lini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kupeleka umeme Malangali ili kutimiza ahadi iliyotolewa na Serikali kuititia Waziri wa Nishati na Madini Bungeni kuwa ifikapo mwaka 2015 asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata umeme?

(c) Je, Waziri wa Nishati na madini yupo tayari kufika Kata ya Malangali na kuongeza na Wananchi juu ya mpango wa kupeleka umeme jimbo la Mufindi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme Malangali chini ya Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka huu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika kipengele (a) hapo juu mradi wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Malangali umejumuishwa katika Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini, Awamu ya Pili chini ya uwezeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013.

Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, lengo la Serikali liliromo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 ni kufikisha angalau asilimia 30 ya Watanzania wenye umeme ifikapo mwaka 2015. Kazi ya kupeleka umeme Malangali itajumuisha ujenzi wa njia za umeme za misongo mbalimbali, ufungaji wa transfoma na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 310. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.94.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubali na niko tayari kufika Malangali na kuzungumza na wananchi.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Napenda niulize swali moja tu la nyongeza kwamba, umeme utatoka Makambako na utapita vijiji vya Nyigo - Iramba - Kinegembasi - Mbaramaziwa - Malangali hadi lhowanza.

Je, Naibu Waziri anaweza akaniruhusu sasa hivi nianze kuwahamasisha wananchi wale waanze kufanya maandalizi ya awali katika nyumba zao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kigola kwa namna anavyofuatilia suala hili, kila tunapoonana ni lazima ataje Malangali.

Mheshimiwa Spika, jibu ni ndiyo aanze kuwahamasisha wananchi waanze maandalizi ya kupokea umeme kwa sababu ahadi ya Chama Cha Mapinduzi ni ya kweli.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Kibona labda kwa sababu mko karibu.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mara zote tumekuwa tukisikia Wabunge wakisema ahadi ya Rais kuhusu umeme na barabara. Pale lleje kuna kata ya Ndola na Itale ziko jirani kabisa na makao makuu ya wilaya,

je, Naibu Waziri anaweza kunisaidi kwamba, bila ahadi ya Rais, wananchi wale ni lini wanaweza kupata umeme?

SPIKA: Swali jipya kabisa! Nilisema Malangali ana moja tu, hebu Mheshimiwa Naibu Waziri jibu tu kama unaweza maana nasikia wewe ni kompyuta.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Tunatekeleza miradi kwanza kutokana na program ya Serikali na kama tulivyosema tunataka kufikia asilimia 30 ya Watanzania wanaotumia umeme. Hii inatokana na maombi ya Waheshimiwa Wabunge, wananchi na ahadi za Mheshimiwa Rais. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nina imani katika orodha ya kata ambazo zitawekewa umeme katika awamu hii ya Phase II ambazo ni pamoja na kata za Ndola na Itale. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge tuonane baada ya hapa ili kama pengine ziliachwa tuone ni namna gani tunaweza tukafanya ili kuweza kuwapatia umeme wananchi hawa. (*Makof!*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, asante sana. Swali hili halina tofauti na wilaya ya Misenyi. Katika wilaya yetu ya Misenyi, kutoka makao makuu ya wilaya kwenda Mtukura, mpakani mwa Uganda na Tanzania, ni kilomita 20 tu. Upande wa Uganda umeme unawaka lakini upande wa Tanzania hauwaki. Ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atatusaidia kuweka umeme ili na Wanamisenyi wallipo mpakani mwa Uganda na Tanzania waweze kujiona kwamba, nchi hii kweli inawajali. (*Makof!*)

SPIKA: Ni swali jipya lakini naomba ujibu tu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anapozungumzia wilaya ya Misenyi na Mtukura mimi nilifika na nimeona hali ya pale inadhalilisha kwa sababu upande wa wenzetu umeme upo...

(Hapa microphone ya Mheshimiwa Naibu Waziri ilizimwa)

5 JUNI, 2013

SPIKA: Jamani Bunge linaendelea! Naona mazungumzo yanaendelea, tutakuwa tunawataja Wabunge wanaozungumza. Mheshimiwa Naibu Waziri naombe uendelee.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, upande wa Mtukura Uganda umeme upo lakini upande wa Tanzania haupo. Mji wa Bukoba unatumia umeme unaotoka Uganda, kwa hiyo, bila kupepesa macho kama anavyosema Mheshimiwa Mwanri hapa, mniangalie midomo na macho yangu, na mimi ninamhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hali ile niliyoiona haiwezekani na haikubaliki hivyo ni lazima tuhakikishe tunaweka umeme kati ya mwaka huu na ujao.

SPIKA: Hii habari ya midomo mliyoanzisha sasa hivi tunalogopa sana. Tatalonaje midomo yenu? (*Kicheko*)

Na. 350

Ujenzi wa Barabara ya Musoma – (Majita) Busekela

MHE. AMINA N. MAKILAGI aliuliza:-

Wilaya ya Musoma Vijijini ni miongoni mwa halmashauri zinazochangia uchumi wa taifa kupitia sekta ya madini, uvuvi, kilimo na mifugo:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Musoma-(Majita) Busekela, yenye urefu wa kilomita 80 kwa kiwango cha lami ili wananchi wa tarafa ya Nyanja waweze kuondokana na adha ya ubovu wa barabara hiyo?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Musoma – Busekela – Makojo yenyeye urefu wa kilomita 78.77 ni ya mkoa inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) mkoa wa Mara. Aidha, sehemu ya barabara kutoka Makojo – Busekela (km 12) ni ya wilaya chini ya halmashauri ya wilaya ya Butiama.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kwa sasa ni ujenzi wa barabara kuu nchini kwa kiwango cha lami. Barabara za mikoa zitafuata baadaye kutegemea na upatikanaji wa fedha. Barabara ya Musoma – Majita – Busekela, inayoombewa na Mheshimiwa Mbunge ni ya mkoa. Aidha, ujenzi wa kilomita 4 uliofanywa katika barabara hii ni wa kutumia lami nyepesi (*Otta seal*) kwa kufuata mwelekeo (*alignment*) wa barabara iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Serikali katika Bajeti ya mwaka huu wa fedha, 2013/2014 imetenga jumla ya shilingi milioni 1,592 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii kama ifuatavyo:-

(i) Rehabilitation (km. 4.5) shilingi milioni 90 fedha za mfuko wa barabara;

(ii) Matengenezo ya muda maalum (lami kilomita 0.9) shilingi 683 fedha za mfuko wa barabara;

(iii) Matengenezo ya muda maalum (Changarawe/udongo kilomita 39.8) shilingi milioni 718.96 fedha za mfuko wa barabara; na

(iv) Matengenezo makubwa ya madaraja (daraja 1) shilingi milioni 100 fedha za mfuko wa barabara.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na kuipongeza sana Serikali yetu kwa kufanya kazi nzuri sana ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami

5 JUNI, 2013

na changarawe katika Tanzania nzima ikiwemo hii barabara ya Majita – Makojo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, halmashauri ya wilaya ya Musoma Vijiji ni imekuwepo kabla ya uhuru na kwa kuwa, halmashauri hii na hasa tarafa ya Nyanja haina barabara ya lami inayowaunganisha wananchi wake na makao makuu ya mkoa, mikoa jirani ya Mwanza, Simiyu, Arusha na hata nchi jirani ya Kenya, na kwa kuwa, tarafa hii ndiyo imekuwa ikichangia pato la taifa kutokana na uchumi wake wa samaki, ningependa kujua sasa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kama ambavyo imefanya kazi nzuri kwa kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika wilaya ya Chato na maeneo mengine hata kama siyo ya mkoa na taifa? (*Makof*)

SPIKA: Naomba swali la pili liwe fupi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, suala la ujenzi wa kiwango cha lami katika barabara hii ya Musoma – Busekela – Makojo ni ahadi ya baba wa Taifa ya mwaka 1962 aliyoitao wakati akiongea na wananchi wa tarafa ya Nyanja, ahadi ya Mheshimiwa Rais Mkapa, aliyoitao katika kijiji cha Busekela wakati wa kampeni mwaka 2000, na pia ni ahadi ya Mheshimiwa Kikwete aliyoitao mwaka 2010, ningependa kujua sasa je, ahadi za viongozi hawa akiwemo muasihi wetu zimepuuzwa? (*Makof*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumthibitishia Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi kwamba, ahadi za viongozi wetu wanazozitoa katika ujenzi wa barabara mbalimbali hazijapuuzwa na ndiyo maana sasa hivi katika nchi nzima kuna ujenzi wa zaidi ya kilomita 11,154 za barabara kuu ambazo zinajengwa kwa lami. Hata hivyo, umuhimu wa barabara hii bado uko palepale na ndiyo maana sasa hivi kuna kilomita 4 za lami ambazo zinaendelea kujengwa kwa mpango wa *Otta Seal*/katika barabara hii na takribani zitajengwa kama kilomita 6.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu nimeeleza kwamba kuna fedha ambazo zimetengwa shilingi milioni 687, lakini katika barabara yote zimetengwa zaidi ya shilingi milioni 1,592 ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua, tumepanga tunaanza na barabara kuu zitengenezwe kwa kiwango cha lami, tukimaliza tutaingia kwenye barabara za mikoa.

MHE. NIMROD H. MKONO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Tatizo la barabara ya kutoka Musoma – Busekela ambayo siyo kilomita 75 tu, ni kilomita 90, limekuwa ni tatizo kubwa kwa watu wa Busekela maana Busekela ni karibu na Ukerewe, kwa hiyo, wavuvi wote wa visiwa kutoka Ukerewe kuja huku wanapeleka mali zao kuja Musoma. Barabara hii Rais alikwenda akashindwa kupita maana kuna millima upande mmoja na upande mwingine ni ziwa. Kwa hiyo, wananchi wa Busekela wana matatizo makubwa kabisa.

Je, inakuwaje vigumu kwa Serikali kutafuta angalau fedha za nyongeza kutoka kwa wafadhili wengine kama China ili watusaidie tumalize tatizo hili la Busekela ambalo ni kero kwa miaka mingi sana? Ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod Mkono kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hii inayokwenda mpaka Busekela umuhimu wake ni mkubwa na mimi ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge Amina pamoja Mheshimiwa Mkono na ndiyo maana bajeti ambayo imekuwa ikitengwa kwa ajili ya barabara hii imekuwa ikiongezeka kutoka mwaka hadi mwaka.

Katika mwaka 2011/2012 Bajeti ya matengenezo katika barabara hii zilikuwa milioni 381.22, katika mwaka wa 2012/2013 Bajeti kwa ajili ya barabara hii zilikuwa milioni 400. Lakini katika mwaka huu kwa kutambua hayo ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Mkono na Waheshimiwa

5 JUNI, 2013

Wabunge Bajeti ya barabara hii ni milioni, 1500,092. Kwa hiyo, tunaendelea kuishughulikia barabara hii ili iweze kupitika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, lakini hili suala la wawekezaji kama wanaweza wakapatikana Wachina au mahali popote mimi nitashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kama atatusaidia kuwapata wawekezaji watakaokubali hata kwa njia ya PPP au kwa njia ya *building operate own and transfer* watakaoweza kukubali kujenga kwenye barabara hii kwa kiwango wanachokitaka cha lami na sisi tutakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Barabara hii moja tu majibu yamekwisha. Sasa Mheshimiwa Mkono anasema hivi, mimi nilikuwa Jimboni kwa tatizo sugu la Buhemba Mine, tumeypata muafaka mambo sasa ni shwari. Sasa ni mambo yapi hayo mtaongea wenyewe huko. Lakini anasema ni shwari imeingia kwenye Hansard. (*Makof*)

Sasa kuna tangazo moja tu. Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CUF, naomba *attention*. Anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha CUF kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 5 Saa saba mchana kwenye Ukumbi namba 231 Katibu wa Wabunge wa CUF.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya kwa Mwaka 2013/2014 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunao wachangiaji wetu leo asubuhi tunaanza na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, atafutiwa na Mheshimiwa Mwighulu

Mchemba atafuatiwa na Mheshimiwa AnnaMarystella Mallac na Mheshimiwa Susan Lyimo atafutiwa na Mheshimiwa Mchunga Mwanjale na wengine nitawataja.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Elimu na Ufundi.

Mheshimiwa Spika, mimi nimecheza mpira wa miguu na mkitaka kushinda lazima mcheze kama timu, kuna golikipa, kuna mabeki, kuna mid field, kuna *ma-forward* na ushindi unapatikana kwa kushirikiano wa nafasi zote hizo.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kulaumiana sana kuhusu kushuka kwa kiwango cha elimu nadhani sisi sote *we don't play our part* hatutimizi wajibu wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, kuanzia mwaka 2004 kulikuwa na Mpango wa Uendelezaji Elimu wa *SEDP*, mpango mzuri tu. Lakini ilipofika mwaka 2006 ukabadilishwa bila matunda. Mwaka 2008 aliyekuwa Waziri wa Elimu na Ufundi akatoa kauli kwamba wanafunzi wanaofeli kidato cha pili *form two* wanaoshindwa kutimiza *markszinazotakiwa* kwenda *form three* waendelee mpaka *form four*, matokeo yake ndiyo haya tunayoyapata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya kukuza mitaala inafanya mabadiliko kila wakati mpaka inawachanganya walimu mpaka sasa hivi mtaala uliopo masomo hayana vitabu ndicho kinachochanganya taaluma yetu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, pia ukaguzi umekufa kabisa, wakaguzi ni wachache waliopo hawana vifaa, hawana magari, hawana fedha. Kwa hiyo, walimu wanajifundishia watakavyo, wanajua hakuna watu wa kuwakagua.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi sasa ni la walimu. Nitatoa mfano, walimu kwanza *morale* yao ipo chini sana sana. Kuna siku mimi mwaka 2009 nilikuwa natoka Jimboni kwangu natoka Kata fulani inaitwa Sangambi naenda

kwenye kijiji kinaitwa Shoga ni jina la kijiji kama kilomita 16, 17 nilipita kwa mtendaji wa Kata hiyo nikamkuta mwalimu binti kama wa miaka 20 amehama kutoka Makongolosi anaenda Shoga, kule Shoga ni nje ya barabara kuu kama kilomita 30 ni kijijini kweli kweli ndani, pembezoni. Mtendaji akaniomba nimpeleke huyo mwalimu nimempeleka nilipomfikisha wakati ninaondoka nilimwangalia usoni alivyokataa tamaa ni kama nilimuacha msituni. Sasa walimu wa namna hiyo wa pembezoni wanapaswa wawe na posho za kuwapa hamasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia walimu ni kada pekee nchini Tanzania ambao wanahangaika sana kupata mishahara ambayo ni haki yao, wanahangaika sana. Kwa Wilaya za pembezoni kama Chunya, Wilaya yangu mimi mwalimu kutoka Ngaraje kwenda Chunya kufuata mshahara ni siku mbili, kwenda siku mbili kwenda na siku mbili kurudi. Mwalimu kutoka Tambikatoto kwenda Chunya kufuata mshahara ni siku mbili, siku mbili kwenda na siku mbili kurudi. Mwalimu kutoka Namkukwe au kutoka Katalala kufuata mshahara Chunya ni mbili kwenda na siku mbili kurudi.

Kwa hiyo, mwalimu huu anapoteza wiki mzima kufuata mshahara, anafundisha wiki tatu kwa mwezi na wiki moja ya kufuata mshahara. Naomba sana utaratibu huu urekebishwe tuangalie walimu hawa kwa jicho la huruma, na sasa hivi kwa kuwa, kuna teknolojia ya simu naomba Halmashauri zote ziwafundishe au ziwapatie simu hawa walimu ambao wapo pembezoni sana ili waweze kupata mishahara yao kwa kuitia kwenye simu tuweze kupunguzia hilo wafundishe darasani kwa muda wa wiki nne zote ili kuinua kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamesema hii ya walimu kutojua baba ni nani na mama ni nani ni tatizo kubwa sana. Wapo TAMISEMI, wapo Wizara ya Elimu na Ufundis, sasa ni upi ambaye atakuwa anawaangalia walimu na kuwapa mafao yao. Naomba hili liangaliwe sana ili liweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamesema ningeomba nitoe takwimu kidogo hapa ambazo nimeziangalia kwenye kitabu cha Wizara hii shule ambazo zinatakiwa kukarabatiwa mwaka huu Mheshimiwa Waziri alisema natoa *sample* tu kidogo nimetoa kwenye kitabu hiki.

Wilaya ya Musoma Vijijini zitakarabatiwa shule 16, Wilaya ya Serengeti zitakarabatiwa shule 15, Wilaya ya Tarime zitakarabatiwa shule 25, Wilaya ya Chunya zitakarabatiwa shule 7 na Jimboni kwangu mimi shule mbili, Wilaya ya Chunya shule 7, Wilaya ya Mbarali shule 5, Wilaya ya Morogoro Vijijini shule 15, Wilaya ya Geita shule 22, Wilaya ya Rombo shule 22, Wilaya Moshi Vijijini 34. Sasa jamani tunasema aliyenacho unamwongezea, yule ambaye hana hata kile kidogo unamnyang'anya?

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani sisi ambao ni wa pembezoni ambao tupo nyuma sana ndiyo walingekarabati shule nyingi zaidi kuliko wenzetu ambao wametangulia. Ilitakiwa sisi ambao tupo nyuma tukimbie wale wenzetu muwapunguze kasi hiyo ndiyo ilikuwa sera ya marehemu Mwalimu Nyerere, sasa wale ambao wapo mbele mnawapa kasi zaidi. Sisi ambao tupo nyuma tutabaki nyuma zaidi.

Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa kufanya majumuisha urekebishe hili wale ambao tupo nyuma shule zetu nyingi zikarabatiwe wale ambao wametanguliwa wapunguziwe kasi kidogo ili kuleta uwiano wa maendeleo katika nchi hii. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana sitaki kutoa shilingi katika mshahara wako Mheshimiwa Waziri kwa sababu mimi kwanza nimekaa karibu na waridi si lazima ninukie waridi.

Mimi Jimboni kwangu kuna Naibu Waziri ndivyo ilivyo nipo karibu na waridi ninukie waridi. Naomba sana Waziri utakapovskyokuja kwenye majumuisho urekebishe hili sisi ambao tupo nyuma shule zetu nyingi ziweze kukarabatiwa na wenzetu ambao wapo mbele wapunguziwe kasi kidogo.

5 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkao wa Kagera katika Wilaya ya Karagwe, ni sera ya Serikali kupeleka vituo vya VETA kwa kila Mkao. Na pia baada ya kutoka Mkoani kwenda Wilayani.

Mkao wetu wa Kagera ambaeo upo pembezoni kabisa na nchi hii hauna hata kidogo Taasisi ya VETA. Tumevyo vituo vidogo vya Gera pamoja na Kanyanga KVTC ambavyo kusema kweli havikidhi viwango hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namtaka Mheshimiwa Waziri katika hili awe serious sana. Mkao wa Kagera tunazo Wilaya nydingi, Ngara, Karagwe, Biharamulo, Muleba, Kyerwa, tunahitaji VETA ya uhakika. VETA ambayo itawafanya watoto wetu walale *boarding*, ambayo itawafanya watoto wetu wapata kozi kumi na mbili na kuendelea siyo ya kutudanganya ya kutupa Gera pamoja na ile ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nalisema hilo kwa sababu Kagera mara nydingi wanatusahau sana sijui kwa sababu sisi ni wapole.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie kufeli kwa wanafunzi. Mojawapo ya sababu ya wanafunzi wetu kufeli ni kwa sababu Wizara ya Elimu imeshindwa kuunganisha Baraza la Mitihani pamoja na Taasisi ya Elimu, hakuna kiunganishi hapa ni kama kimekufa, hakuna kiungo. Kwa sababu Taasisi ya Elimu yenye we inatunga mitaala, Baraza la Mitihani linatunga mitihani bila kuzingatia hii mitaala. Mheshimiwa Waziri itakusumbua sana kama hutatengeneza kiungo kizuri cha kuunganisha hili jambo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nizungumze kubadilika kwa mitaala na mihutasari siyo jambo baya, lakini katika kufanya hivyo naomba wadau mbalimbali washirikishwe. Kwanza, wawepo walimu washirikishwe, wanafunzi wenyewe, waandishi wa vitabu, wachapishaji wa vitabu pamoja na wazazi katika kubadilisha mitaala yote hii.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu mimi jambo moja nilimwombe sana sehemu ambayo ni muhimu sana katika Sekta yake sehemu ya Wakaguzi. Shule zetu hapa nchini zimekuwa kama hazina mwenyewe ni kwamba tumejenga tumeacha huko tu hakuna hata mmoja ambaye anakagua. Nenda kwenye shule za *Private* uangalie Meneja wa shule anaingia pale kuanzia 12 anatoka saa nne usiku anakagua shule yake. Kwetu hakuna hata mkaguzi hata mmoja tumetekeleza shule zetu.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi wapo ndiyo Mawilayani kwetu huko, lakini Mkaguzi hana gari, mkaguzi hana mafuta, mkaguzi huyo yupo chini ya Mkurugenzi wa maendeleo akamkague boss wake haiwezekani. Kwa hiyo, naomba na hili lenyewe liangaliwe vizuri sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lingine utakuta kuna walimu wazuri sana wachapa kazi, lakini walimu wetu tunawapimaje, kuna walimu wanakaa darasani anafundisha masaa mawili baadaye anaondoka. Utafiti unaonyesha kwamba ili mwalimu aweze kufanya kazi yake vizuri lazima akae darasani sio chini ya masaa matano na achape kazi. Lakini kama hakuna mkaguzi wa kumsimamia hizo kazi hazitafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mishahara ya walimu. Nipende kusema hatutafanya mabadiliko hata kidogo hata tungepiga kelele kama walimu hawajapewa maslahi mazuri. Walimu sasa hivi wananyongonyea, walimu wanachuki, wana hasira, wanafanya kazi tu bora liende kwa sababu mishahara ni midogo sana.

Mheshimiwa Waziri, katika jambo ambalo unatakiwa kulifanya kazi haraka sana ni maslahi ya walimu wetu kuanzia shule za awali, shule za misingi mpaka vyuo , mishahara ni midogo sana hata ukienda vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, angalia hapa mshahara kianzio cha mwalimu mwenye cheti wa shule ya msingi anaanzia shilingi laki 277,000 na mwenye diploma anaanzia mshahara 309,9000, mwenye digrii anaanzia mshahara 530,000, lakini ukienda kwa upande wa kilimo huyu anaanzia sh. 800,000 kwa nini iwepo tofauti kubwa namna hii?

Kwa nini walimu tunawadharau kiasi hiki, walimu ni kama bomu ambalo linasubiri kulipuka kwa mguso mdogo *slat taste provocation*, kwa sababu huyu mtu ana hasira anaona kama vile hammjali. Mheshimiwa Waziri atafuta mbinu zozote zile mishahara ya walimu ipendeze angalau kima cha chini kianzie kwenye 800,000, 900,000, 1,000,000 mtaona mabadiliko ambayo walimu watayafanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie uwiano wa mwalimu mmoja pamoja wanafunzi anaofundisha. Sasa hivi uwiano wa walimu na mwanafunzi ni mkubwa sana, kwenye *Private* ambako wanafanya vizuri shule za dini utakuta uwiano wa mwalimu na mwanafunzi ni mwalimu mmoja na *at least* na wanafunzi 40. Lakini huku kwetu hizi shule zetu za Serikali utakuta uwiano ni kuanzia labda mwalimu mmoja na wanafunzi 100 na kuendelea. Huyu mwalimu lazima atachoka hawezi kufanya kazi zote hizi. Kwa hiyo, tuangalie uwiano na wenyewe uende vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumelaumu sana Wizara, Waziri tumemlaumu sana, lakini kuna mchango mwingine wa kufeli ambao watoto wenyewe wanafunzi wanasababisha vijana wengi siku hizi kuanzia shule za Msingi na Sekondari hawasomi hawajitumii.

Lakini na sisi wazazi hatusimamii. Sasa kama mtoto hasomi hata angefundishwa na mwalimu wa namna gani mwenye akili ya namna gani hizo akili zitaingia namna gani kichwani. Ingekuwa ni mgonjwa ungesema labda huyu tumwekee *drip* ya maji apate nguvu.

Lakini sasa mwalimu atafundisha lakini mtoto hasomi. Hiyo ni changamoto ambayo sisi Wabunge na wazazi kwa kweli ni lazima tuliangalie hilo. Na watoto wengine ni watoro hata ukiangalia kwenye takwimu watoto wanaonza darasa la kwanza au *form one* siyo wote wanaomaliza wengine wanaishia huko mitaani. Kwa hiyo, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, ninatambua juhudini nzuri sana za Serikali inazofanya katika kumaliza malimbikizo ya fedha za walimu natambua hilo. Lakini Mheshimiwa Waziri mimi nimwombe ahakikisha kwamba mwalimu anadai shillingi yake hata moja deni ni deni linanyima raha. Ahakikisha kwamba mwalimu analipwa malipo yake stahiki kama sisi Wabunge tunavyolipa, sisi kwa spika hatukopi wala hatuna madeni. Usikubali mwalimu naye akudai Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naona hakuna mkakati wa makusudi wa kumaliza matatizo ya nyumba za walimu, hakuna kabisa. Tumekuwa na mkakati mzuri wa kujenga barabara za lami ni vizuri, lakini leteni mkakati wa makusudi wa kumaliza matatizo ya nyumba za walimu. Walimu wetu waishi katika maisha mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tatizo lingine haiingii akilini kuona mpaka sasa hivi kwamba kuna watoto ambao wanasona chini ya mti katika wakati kama huu. Mheshimiwa Waziri mimi nitakuomba utembelee kwenye Jimbo langu la Karagwe upate *sample*, nina shule ya msingi inaitwa Rwentwe iko kwenye Kata ya Kanoni watoto wote wanakaa chini ya mti mvua ikinyesha hawawezi kusoma. Kuna shule ya msingi inaitwa Bukinzo, katika Kata ya Nyakabanga watoto wote na walimu wanosomea chini ya mti kwa kweli haipendezi.

5 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nawomba Mheshimiwa Waziri mimi natambua changamoto ni nyingi sana na mnafanya kazi nzuri sana mimi ninawaunga mkono, kwa sababu Wizara yenu ni mgumu wala mimi sina matatizo na hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho tatizo la fedha zinazopitishwa hapa Bungeni tunapitisha Bajeti ya Serikali kwa ajili ya Wizara hii lakini fedhahaziendi. Sasa Waziri tutakusurubu bure na watu wako kama fedha hupati wewe utafanya nini? Mimi ninamsubiri Waziri wa Fedha anaona yupo hapa anisikilize kwa makini sana, Wizara yako kuna fedha zinavunja, kuna fedha tunapitisha hapa wewe huwapelekei Mawaziri wenzako unataka wao wasurubiwe wewe uendelee kutesa humu ndani, hatukubali na mimi ninakusubiri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ongea na Spika tabia ya ku-*attack* watu siyo sahihi, ongea na mimi. Okay tunaendelea Mchungaji Mwanjelwa atafuatia na Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac na Susan Lyimo.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini jina langu ni Mwanjale siyo Mwanjelwa samahani sana.

SPIKA: Nimekosea Mwanjale.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la elimu kila mahali duniani lipo ni kubwa. Mwaka 2006 mimi nilikuwa Marekani pale mwenyeji wangu aliniambia kwamba elimu siku hizi imeshuka, alisema kwamba mitihani ambayo tulifanya sisi *form six* zamani, leo hii watoto wetu hawawezi kufanya.

Kwa hiyo, tunapozungumzia maendeleo ambayo yapo na kwa vyovyote vile yanapotoka mabadiliko makubwa kama haya elimu lazima ina *tendencyya* kushuka.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nilitaka kuzungumzia suala la walimu. Kuna walimu wengi ambao wamejijendezea wamesoma, lakini cha ajabu ni kwamba badala ya kupanda daraja zao za mishahara zinashuka na sijui kwamba Wizara inasema nini hapo kwa sababu tulikuwa tunafikiri kwamba kama mtu amejiendezea amejisomesha halafu amepata digrii ya kwanza au ya pili na matokeo yake baadaye tena badala ya kumshukuru anateremshwa daraja mshahara wake inakuwa kitu cha ajabu sana.

Kwa hiyo nilikuwa naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha anieleze kwa sababu kwangu kule kuna kero nyingi za namna hiyo na wengi wamepiga simu, wameniandikia *message* wamenieleza kwamba bwana tunashangaa kuona kwamba madaraja yetu yanateremshwa badala ya kupanda.

Lakini la tatu ni kwamba hao walimu ambao wanafundisha shule za msingi tunataka tuwapatie motisha fulani na hasa wale ambao wanatoka katika maeneo ya vijijini na wengi nafikiri wameongea hapa lakini kwa kweli mazingira ya vijijini ni magumu sana na tunaishukuru Serikali kwa wakati huu angalau kidogo inaanza kufikiria kupeleka umeme kwa vijiji vingi na hiyo bila shaka itasaidia sana kuweka uwiano wa watu hawa ambao wanaenda vijijini hawapati huduma ya umeme wala maji itawasaidia sana kuwa-*retain*kubaki kule katika vijiji. Lakini kwa sasa hivi tatizo limekuwa ni kubwa barabara hazipitiki, maji hakuna, umeme hakuna. Kwa hiyo wengi wa walimu hawa ambao wanapelekwa huko wanakimbia wanakwenda mijini ambako wanapata manufaa fulani.

Nimesikia wachangiaji wengi wakisema hapo kwamba kwa kweli elimu yetu imeshuka, ni kweli. Lakini tukiangalia Watanzania wanapotoka wanaenda huko nje

wanaenda Ulaya, Marekani, Uchina *performance* yao inakuwa ni nzuri sana sasa unashangaa kwamba elimu hii ya kwetu imeshuka mbona wanapokwenda huko Ulaya wana-*perform* vizuri sana kuna nini.

Kwa hiyo wakati mwininge tusijidharau na kuona kwamba hatuwezi na kwamba pengine elimu hii haifai. Labda kitu ambacho kinawashinda kidogo wakati wakitoka nje pengine lugha ambayo hilo nilitaka nizungumzie kwamba lazima sasa tutoke na maamuzi ambayo yatakuwa ni sahihi ni lugha ipi itaanza kufundishwa katika mashule yetu.

Je, ni Kiswahili au Kiingereza na Kiingereza kukitupa moja kwa moja nako ni vigumu sana kwa sababu kila mahali duniani watu wanahangaika kujifunza lugha hiyo, Kiingereza, Kifaransa. Kwa hiyo nilikuwa nafikiria kwamba labda turudishe mtindo ule wa zama ni ambao unaanza shule darasa la tatu unaanza kusoma Kiingereza mpaka unamaliza huko sekondari mpaka Chuo Kikuu, tofauti na sasa hivi.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Wizara ijaribu kufikiria namna gani sasa ije na mkakati maana mwaka jana tumeongea habari za lugha na mwaka huu tunaongea habari ya lugha hiyo hiyo je, mpango huu sasa utakamilika lini na lugha ipi ianze kutumika katika mashulenii, tuanze maana hatuwezi kukwepa hapo.

Kwa hiyo nilikuwa naomba kwamba lugha ni muhimu kabisa tujifunze na watoto wajifunze wapate lugha ambayo kwa kweli itawasaidia na tukiangukia katika Kiswahili kwa kweli tutajikuta tuko peke yetu tuko kisiwani. Mimi nilikuwa naomba kwamba tujaribu kuangalia namna gani sasa tuboreshe elimu ikiwa ni pamoja na kuboresha lugha hii ya Kiingereza na Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, sehemu ambayo nilitaka kuchangia ilikuwa ni hii Bodi ya Mikopo. Nafikiri uko bado kuna matatizo tunahitaji kuweka mkakati mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba kwa kweli kwenye Bodi ya Mikopo kuwe na mpango mwininge kabisa maalum ambao kwa kweli

utasaidia watoto hawa waweze kusoma. Kwa sababu nikiangalia fedha hapa za Wizara ya Elimu karibu nusu nzima inaenda kwenye mikopo, lakini ukiangalia fedha za maendeleo kwa Wizara hiyo katika shilingi bilioni 72 ambazo zimetengwa shilingi bilioni 18 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 53 ni fedha za kutoka nje.

Je, hawa watu wasipoleta fedha hiyo kutakuwa na maendeleo kweli, shule zetu zitaboreshwa. Sasa hivi ukienda huko vijijini shule za msingi karibu zingine zinaanguka zimekwisha kwa sababu ubora wake umekwisha na nilifikiri kwamba Wizara hiyo ingetenga fedha za kutosha ziwe nydingi za kuhakikisha kwamba nyumba za walimu zinajengwa na shule nydingine zinaboreshwa pia ikiwa za msingi au sekondari. Kwa hiyo hicho ndicho kitu cha kwanza ambacho kwa kweli ni muhimu Serikali na kufikiria itasaidia vipi hasa wananchi wale ambaao wako huko nje vijijini kabisa.

Kwa hiyo Bodi ya Mikopo ni muhimu kabisa ifanyiwe mpango mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba nafikiri mwaka jana tulikuja na mapendekezo hapa, mapendekezo ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu alileta hapa sijajua mpango huo unatengenezwa vipi, kwa sababu nilifikiri kwamba pengine sasa Wizara ingekuja na mkakati kwamba kwa yale ambayo mwaka jana mltiuambia tunafikiri kwa hayo sasa tunakuja na moja, mbili, tatu.

Lakini hapa tunapitisha itakuja tena mwaka kesho tunazungumza yale yale. Nilikuwa naomba ule mpango ambaao Mheshimiwa Mwigulu alikuwa amewasilisha hapa basi ungezungumzwa ungepata mjadala mrefu utengeneze lakini tukiacha hivi hivi hewani mwaka kesho itapita watakuja wengine mwaka kesho hivyo hivyo, kwa hiyo elimu itaendelea kuyumba vilevile. Nilikuwa naomba kwamba hapo tuangalie tuone kwamba namna gani suala hilo linaweza likashughulikiwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru tu Wizara lakini naunga mkono hoja nikijua wazi kwamba watakuja na mpango na watakuwa na majibu sahihi ya

kulturidhisha sisi Wabunge ili tuweze kujua kwamba kweli kwa mwaka huu mambo yatakuwa hivyo. Lakini kwa bajeti hii iliyopo sasa hivi kwa kweli hairidhishi maana fedha ambayo inatolewa ni kidogo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac na Mheshimiwa Susan Lyimo dakika tano, tano.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo katika suala zima la elimu. Nianze kuchangia kwa kusema ni kweli elimu ya sasa imeshuka sana na hili kila Mbunge atalionegelea, elimu sasa hivi imeshuka tuko nyuma sana na limekuwa pigo kubwa kwa wazazi kwa mlundikano wa watoto tunaoendelea kuwalea badala wangejitegemea, lakini wanashindwa kujitegemea kutokana na mfumo mbaya wa elimu ya sasa.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la walimu. Hili suala la walimu tutalionegelea wote kwa sababu ni suala pana. Walimu kweli wanastahili kupewa kipaumbele, Serikali iwaangalie walimu kwa kuwapa kipaumbele wapate maisha bora ili wapate moyo wa kuwafundisha watoto wetu. Walimu wana mazingira mabaya sana mimi mwenyewe nilikuwa mtoto wa mwalimu lakini nikiangalia maisha niliyoishi kwa baba yangu na walimu wanaoishi sasa hivi ni vitu viwili tofauti.

Walimu hawana nyumba bora za kuishi, yaani kama vile wameshushwa thamani mijengo yao wenyewe ya walimu ambayo wanayojengewa sasa hivi kwa wale wanaobahatika kupata nyumba hazina thamani inayolingana na mwalimu jamani.

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa Wizara iangalie inapowajengea majumba iwajengee kwa kufuata ramani za mijengo ya kisasa, isiwajengee majengo ambayo kwa kweli kama vile sio binadamu wanaostahili haki. Wako nyuma sana na wengi wanaishi uraiani, wanaishi wanadharauliwa kiasi kwamba hata leo hii mwalimu akija kuomba uchumba

kwako unajiuiliza ni nani akisema ni mwalimu unasema potezea. Sio vizuri naomba Serikali iwajali sana walimu hasa katika suala zima la maslahi, mishahara yao ni midogo na hata kama wanapata mishahara hailingani na elimu yao.

Kuna baadhi ya walimu wa sekondari wana digrii zao lakini unakuta mshahara wao unalingana labda na Wauguzi ambao ni ngazi ya cheti wamesoma mpaka Kidato cha Nne tena kwa kupata *Division Four* au D mbili wawe wanalingana na wale walimu waliosomea digrii. Serikali iangalie suala hilo iwape mishahara watumishi wote kulingana na elimu zao na hadhi ya elimu yao waliyosomea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umbali wa sehemu za kazi zao walimu wanaishi umbali sana na kazi zao, wengine wanatembea maili kama mia moja na kitu kufuata mshahara lakini anakuwa hana hata shilingi ya nauli wanakuwa wamemaliza fedha zao kutokana na ujira wao mdogo bado wanatakiwa nauli wapate usafiri kwenda mjini Makao Makuu ya Wilaya au Mkoa kufuata mshahara hawana usafiri.

Naomba Serikali iwafikirie kuwakopesha hata pikipiki ya kuweza kufanya kazi zao au kufuatilia mishahara ule umbali. Mawasiliano ni shida mwalimu anashindwa kabisa anapopatwa na dharura kule atawasilianaje na Makao Makuu ya Wilaya yake au mkoa wake, mawasiliano hamna. Kwa hiyo walimu wapewe kipaumbele kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la ukaguzi, sekta ya Ukaguzi naomba Serikali iipe kipaumbele, bila Wakaguzi hatujapata wasomi wazuri na wenye maadili mazuri. Kwa sababu Wakaguzi wale ndio wanaoangalia suala zima la ufundishaji na ufundishwaji wa wanafunzi pamoja na maadili kwa walimu wenyewe.

Watoto wetu wengine wamekuwa wakipewa mimba na walimu nani anawadhibiti wale walimu, nani anajua uhalifu wao, nani anaweza kuwaweka akawasema. Kwa hiyo ni suala la ukaguzi, ukaguzi upewe kipaumbele kabisa,

5 JUNI, 2013

nilitembelea mwezi Januari nikiwa kwenye Kamati ya Huduma.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia japo kidogo katika Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme na nirudie kusema tena kwamba siku zote ukweli unauma lakini ni lazima tuukubali ukweli huo na ndio maana tunapougua tunameza dawa japo ni chungu ili tupone. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba baadhi ya Wabunge baada ya kuona hali mbaya ya elimu hapa nchini bado wanaona kwamba Waziri asiwajibike. Jambo hili linasikitisha sana ni wazi tunajua kwamba ni Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi walioleta suala linaloitwa *D by D*. Niseme tu mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Huduma za Jamii mwaka 2005 mpaka 2010 na wazo hili la ugatuaji wa elimu nililipinga sana ndani ya Kamati.

Lakini leo hii Serikali hiyo hiyo ambayo ilipanga mpango wa ugatuaji wa elimu leo wanaona kwamba ugatuaji ule ulikuwa mbovu na kwamba sasa shutuma zinaenda kwenye Wizara ya TAMISEMI. Kimsingi wanaposema TAMISEMI ndio kuna matatizo maana yake ni kwamba wanaposema Waziri Mkuu ndio mwenye matatizo kwa sababu Waziri Mkuu anayeongoza TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye suala zima la Wizara ya Elimu na nzungumzie suala la matokeo ya mwaka 2012 matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne. Labda nzungumze jambo moja la msingi sana ambalo naomba wananchi wanisikilize kwa makini. Wakati Mheshimiwa Lukuvi anatoa ripoti hapa Bungeni alisema hivi "Matokeo ya Kidato cha Nne yafutwe na yaandaliiwe upya" na sababu moja aliyoisema alisema *standardization* ifanyike na kwamba watumie mfumo wa zamani yaani wa *flexible grading*.

Lakini wakati Waziri wa Elimu anatangaza matokeo juzi amesema hivi "Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2012 yalitangazwa tarehe 14 Februari, 2013 na kufutwa mwaka 2013 kutokana na sababu za kitalamu katika matumizi na taratibu za kuchakata matokeo, matokeo yalifutwa yalikuwa yamechakatwa kwa kutumia utaratibu wa *fixed grade ranges*, matokeo yanayotangazwa sasa yamechakatwa kwa utaratibu huo huo lakini yamefanyiwa *standardization*".

Sasa kama Mheshimiwa Lukuvi alisema yaende yakatengenezwe kwa mfumo wa *flexible* iweje leo hii Waziri aende kulitangazia Taifa kwamba yale yaliyokubalika hapa na wananchi walielewa kwamba utaratibu unaoenda kufanyika ni ule wa zamani, lakini amekiuka ameenda kutumia utaratibu uleule, lakini badala yake akafanya *standardization*. Sasa naomba kujua kama Mheshimiwa Lukuvi ndio alitudanganya au Mheshimiwa Waziri wa Elimu ndio aliyetudanganya. Nasema kwamba baadaye jioni tutakuwa tunashika vifungu na hatutaelewana humu ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile nimpongeze sana Bwana Rakesh kwa kujitoa kwenye ile Tume na vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Mbatia kwa kukataa kwenye ile Tume kwa sababu wote tunajua kwamba Tume ya mwaka 2010 ambayo imetumia fedha za walipa kodi ilitoa mapendekezo 27 na tatizo kubwa la Wabunge wengi hatusomi ripoti na ndio sababu jana Mheshimiwa Komba anasema kwamba CHADEMA ndio wanaosababisha mporomoko wa elimu, lakini ripoti zote hakuna mahali CHADEMA imetajwa kama sababu ya kuporomosha elimu.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Nchemba Mwigulu.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Tarehe 31 Januari, 2013 nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba naomba kunukuu "Elimu ndio mapigo ya moyo ya Taifa letu, mapigo ya moyo yakienda kinyume na asilia yake uhai uweza kupotea, tunao wajibu

wa kuokoa uhai huo" Na nikaliomba Bunge lako Tukufu kuchunguza udhaifu wa kimfumo katika sekta ya elimu hapa nchini na kupendekeza hatua za kuchukua ili Taifa liondokane na aibu ya udhaifu huo hatarishi kwa mfumo wa elimu ya Tanzania na leo tunavuna tulichoamua ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ziko fedha za *change* ya rada ambapo tarehe 18 Machi, 2013 Serikali ilisaini mkataba na Makampuni mbalimbali wazabuni zaidi ya 10 kwa ajili ya kusambaza vitabu katika shule zetu, vitabu na mihtasari ipatayo 18,000,000. Fedha zenyewe ni zaidi asilimia 75 ya shilingi bilioni 73 ni shilingi bilioni 55.2. Vitabu vyenyewe tulivyoomba ...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge pale nyuma ni nani anayezungumza? Mheshimiwa Mariam na wenzake mnatoka nje sasa hivi. Mariam na mwenzio tokeni nje. Ebu *Sergeant at Arms* watoe hao. (*Makofii*)

Naomba uendelee Mheshimiwa Mbatia, msifanye kama Bunge ni mahali pa kuzungumza tu.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru nitaomba muda wangu ulindwe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema tarehe 18 Machi, 2013 siku ya Jumatatu Serikali ilisaini na wazabuni zaidi ya 10 kusambaza vitabu na mihtasari zaidi ya 18,000,000 katika nchi yetu na hizi fedha ni fedha za *change* ya rada asilimia 75 ya shilingi bilioni 73 ambazo ni shilingi bilioni 55.2. Sasa vitabu vyenyewe ni vipi. Inasikitisha baadhi ya vitabu vyenyewe ninavyo hapa ukiangalia kwa mfano kitabu cha Hisabati darasa la kwanza mwanafunzi huyu unamwambia shilingi 100/= toa senti 50 toa senti 20 unapata senti 30. Je, kiuhalisia tuna senti katika nchi yetu tunafundisha vitu ambavyo ni *practica?*

Mheshimiwa Spika, ukija kitabu cha Jiografia hata neno Jiografia ni tatizo imeandikwa "Jografia" na maudhui yake ni matatizo mengi tu. Njoo kitabu cha darasa la pili, kitabu cha darasa la pili kimeandikwa nataja machache 2 X 7 ni 15.

MBUNGE FULANI: Mama yangu wee!!!!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, njoo kitabu cha darasa la nne kimeandikwa 0 gawanya kwa 0 jibu ni 0. Sifuri ukigawanya kwa namba yoyote haigawanyiki hii ndio sumu ninayosema inalishwa Taifa letu. Ukija kitabu cha Uraia, Uraia wa kawaida tu darasa la nne kinasema Mtaa uundwa na Vitongoji kadhaa ambavyo huongozwa na Wenyeviti wa Vitongoji "Mtaa".

MBUNGE FULANI: Mungu wangu !!!!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, sasa tunalamika nini wakati sisi wenyewe ndio tunaua elimu ya Taifa hili na hii ni hoja kwa vielelezo. Hapa unasema wananchi wengi wanaoishi kwenye Mitaa ni watumishi wa umma, viwanda na Makampuni ni vitabu hivi vinavyotumika. Hatuuzi na vimepewa ithbati na *EMAC*, *EMAC* imetoa ithbati yote. Ndiyo maana nasema *EMAC* ivunjwe jamani *EMAC* haliitendei haki Taifa hili Mheshimiwa Waziri na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, njoo kitabu cha Kiingereza darasa la kwanza wanafunzi wanafundishwa kusoma kwanza kabla hawajaanza na *alphabet*. Mimi nilipoanza kusoma nilianza kufundishwa *vowels* herufi kule tunaimba kabisa unasema a, e, i, o, u hizi ni herufi kuu tamka kwa sauti kuu ndio a, e, i, o, u na kikombe u, u, u, kama jicho e.e, e, mwenye mpira o, o, o, ni kikombe u, u, u, huu ndio msingi wa kufundisha wa kumlisha mtoto wa darasa la kwanza.

Lakini leo hii ni vitu tofauti kabisa mtoto atajifunzaje Kiingereza kwa vitabu hivi, yaani ukiangalia hali yote hii inatisha.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walioko kwenye shule sasa hivi, wanafunzi anzia *primary* mpaka vyuo vikuu ni takribani milioni 10.5 ambayo ni asilimia 23.3 ya Watanzania wote. Je, bajeti hii ya elimu inatosha? Bajeti yote ya nchi hii ni shilingi triliuni 17.7, asilimia 23.3 ya bajeti hiyo ni shilingi triliuni 4.12/- . Kwa hiyo, bajeti unayopewa Mheshimiwa Waziri haiwezi ikafanya lolote itakuwa ni manung'uniko tu. Tunataka tuone shilingi triliuni 4.12/- inawekezwa kwenye elimu kwa sababu kipaumbele cha kwanza, cha pili, cha tatu mpaka cha kumi ni elimu ili tuondokane na udhaifu huu ambao upo katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hizi shilingi triliuni 55.4/- ni ujisadi kama wamenunua vitabu hivi na hatuwezi tukakubali. Lazima fedha hizi zirudishwe kwa Watanzania. Hatuwezi tukasema hapana, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, badala ya kuzungumza hoja za msingi na naomba Watanzania wote tuwaombe radhi, badala ya kuzungumza elimu ambayo iko juu ya itikadi zetu za kisiasa na imani zetu za kidini. Tunapoanza kuzungumza kwamba kuna Bwana mmoja katika Baraza la Mitihani ambaye anachakachua au anatoa *grades* tofauti, kama kuna mtu binafsi uchunguzi ufanyike ashtakiwe lakini sio isemwe ni Baraza zima la Mtihani. Mama Joyce Ndalichako, naomba uendelee na kazi yako, unafanya kazi nzuri sana kwa Taifa hili na wala usiogope. Mama huyu tumpongeze kwa dhati. Kamishna wa Elimu, Profesa Bhalalusesa anafanya kazi nzuri sana na akina mama hawa wameonyesha uwezo mkubwa sana, tuwape uwezo zaidi na tuwatie moyo wafanye kazi kwa Taifa letu hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, itikadi hizi zitatuharibu sana. Tusikubali kutumia Bunge hili Tukufu kuligawa Taifa kwa misingi ya dini. Kama ni udhaifu basi watu wachukuliwe hatua. Jamani chondechonde na niliombee Bunge hili radhi kwa wote wanaotoa kauli za kuchochaea udini ndani ya Taifa letu kupitia Bunge lako Tukufu. Kwa kuwa Taifa hili ni letu sote, amani ikitoweka tutaangamia sisi sote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, siku ya mwisho mbele ya Mwenyezi Mungu hatutaenda kuulizwa wewe ni CCM, CHADEMA, NCCR, CUF, TLP na UDP, tutaulizwa matendo yetu mema tuliyowafanya watoto wa Mwenyezi Mungu tulivyokuwa hapa duniani. Sasa kwa nini tulisambaratishe Taifa la Tanzania kwa misingi ya mambo ambayo hayaeleweki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mtume Mohammed (S.A.W.) anawahusia waumini wake kwamba ukitaka akhera na usome, ukitaka dunia na usome na ukitaka vyote na usome. Elimu ni kitu chake kilichompotea mumini, popote akipatapo kitu hicho na akichukue. Kwa Wakristo, ni Mithali 4:13 inasema, mkamate sana elimu usimwache aende zake maana ye ye ni uzima wako na Mithali 1:7 inasema, kumcha bwana ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu wanashindwa kuwa na hekima na adabu. Sasa Taifa letu tunalipeleka wapi? Mithali 29:12 inasema, mtawala akikumbatia uongo basi watumishi wake wote wanakuwa waovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 30/4/2013 alisema Jijini Mbeya kwamba elimu yetu ina udhaifu, mitaala ni migogoro, Rais amelikiri hili, mbona nyie Wabunge wake mnashindwa kulikiri hili? Tatizo liko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hili nampongeza Rais kwa dhati kabisa, alisema elimu ya Taifa hili ina migogoro, mitaala ina migogoro, amelisema kwa moyo wa dhati. Taifa hili ni letu sote, halina itikadi za vyama.

Mheshimiwa Spika, niseme na niombe tena, tuangalie shule zetu, angalia shule za vijijini, angalia Mtwara, angalia Bashnet kule shule hazina maabara, ziko kwenye hali mbaya sana. Sasa napendekeza, ili tuondoke hapa tulipo au hata mpaka vyuo vya elimu ya juu, fukuza fukuza ya wanafunzi, Wahadhiri hali zao sio nzuri, wanafunzi 210,000 waliopata ziro tunawapeleka wapi; tuunde Kamisheni ya Kudumu ya Elimu itakayoangalia viwango vya elimu, marupurupu ya Walimu, mishahara ya Walimu, mazingira magumu ya

kufanyia kazi, vitabu viko kwenye hali gani ili tuondokane na hii aibu inayoliangamiza Taifa letu. Kwa kuwa elimu iko juu yetu sote, Taifa likiangamia tunaangamia sisi sote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niombe chondechonde, kukiri kosa sio udhaifu, kushindwa kutumia madaraka ni udhaifu na kutumia madaraka vibaya ni udhaifu pia. Sasa kukiri kwamba ni kosa tumefanya si udhaifu hata kidogo lazima tukubali kwamba Taifa tunaailbu, watoto wamejitoa maisha yao, utu wa mwanadamu... (*Makofî*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante muda umekwisha. Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Zahra Ali Hamad wajiandae.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Martha Mlata kwa kunipa hizi dakika ili niseme na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nianze kwa kusema naunga hoja mkono na niwashawishi Wabunge wenzangu wote ambao Tanzania iko moyoni mwao waunge mkono hoja hii. Tunaunga mkono hoja kwa sababu fedha zinaenda katika maeneo tofautitofauti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo hii fedha tunazopitisha ndizo zitakwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu. Kwa wanaosema tusiunge mkono hoja hii wanataka, watoto wetu wa vyuo vikuu waishi namna gani? Ndizo zinazokwenda kwenye mishahara, ndizo zinazokwenda kwenye kuendesha vyuo pamoja na vyuo vya mafunzo vya Serikali lakini pamoja na vyuo vya ualimu. Kwa hiyo, kwa namna hiyo ni lazima tupitishe kwanza bajeti na kitakachofuata, tutaelekeza Serikali katika mambo ambayo tutayaona ni vyema Serikali iyafanyie kazi, tuache kuigiza. Leo hii kuna mambo hayawezি yakasimama yakasubiri bajeti,

tunahitaji tupitishe bajeti, kazi iendelee na shule ziendelee kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo nitaomba Serikali iyafanyie kazi, la kwanza, Serikali inajua idadi ya Walimu watakaomiliza na sehemu tutakapowapeleka kwa sababu mpango huo upo na tunafukuzana nao na tunataka mpaka ifikapo 2015 tuwe tumemaliza suala hili. Serikali inajua idadi ya watakaoenda na inajua mahitaji hayo. Inakuwaje Walimu wanapangiwa mpaka wanaenda eneo la kuripti wanakosa fedha ambayo walitakiwa waende nayo? Hii si nzuri na tunawanyanya watoto wa watu kwa sababu maeneo wanakokwenda wanakuwa hawana ndugu wala hawana pa kufikia. Waziri zingatieni kwa kuwa tunajua tunakowapeleka Walimu na tunajua watamaliza lini kila anapopangiwa apewe na fedha ya kule anakoenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili na hasa nilisema na wakati ule, mgogoro wote huu kuhusu sekta ya elimu ni wa kibajeti. Bunge limebadilika lakini Waziri uliahidi kwamba ungeleta katika Bunge hili hoja ile ya kubadilisha Sheria ya Bodi ya Mikopo pamoja na Mamlaka ya Elimu ili kuweza kutengeneza Mfuko wa Elimu. Sasa nakuomba utakapojuisha useme katika Bunge ijalo ni kitu gani utafanya ili tuweze kuondokana na mgogoro huu. Bodi ya Mikopo iwe na Mfuko wake na Mamlaka ya Elimu iwe na fedha ambazo zinatengwa kuweza kushughulikia miundombinu ya elimu. Tutengeneze ule Mfuko ambao kwenye vyuo vikuu wanauita Mfuko wa Mwigulu na naamini kabisakabisa utamaliza mgogoro wote huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi niwaambie Watanzania, wengine wote msidhanie wanawaonea huruma kwenye hili lilitokea. Wanachekelea kwa sababu dhana yao tangu mwanzo ni kuona jambo hili halifanikiwi, la kuanzisha shule za kata. Walikuwa wanatamani sana lisifanikiwe lakini kwa Watanzania mnaopenda Tanzania niwaambieni tatizo hili limetokea kwa sababu tumefanya *over expansion* katika sekta ya elimu na kwa mtu yejote ambaye ni mkweli na kweli

iko nafsi mwake ni lazima atatambua kwamba hili lazima lingetokea. Kwa mfano, ukienda kwenye shule za msingi tangu uhuru mpaka mwaka 2001, kulikuwepo na ongezeko la wanafunzi kutoka laki nne mpaka milioni nne lakini kutoka mwaka 2001 mpaka 2011, imeongezeka mpaka milioni nane. Kwa kipindi hiki hapa, hata Waziri uwe na vichwa viwili lazima ukutane na tatizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo iliyosababisha tukajenga shule za kata na namna tulivyosema tutajenga shule za kata, tulipeleka kwa kupitia llani. Wakati huo shule za sekondari zilikuwa 1700 lakini katika kipindi cha kutoka 2005 mpaka sasa tuna zaidi ya shule 4,500. (*Makof!*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Ooo!

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Kwa vyovypote vile, lazima ukumbane na changamoto ya aina hiyo. Hili v i kujenga ingekuwa rahisi tangu vyama vingi vianze CHADEMA wamepanga kuanzia makao makuu mpaka Wilayani, kwa nini hamjawahi kujenga hata jengo moja mnapanga chumba kimojakimoja? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa hili la kujenga kwanza na unapojenga lazima kwanza *uta-sacrifice quality*, umeweza kusimamia ujenzi wa aina hii na namna ya kujenga ni lazima tutakumbana na changamoto. Hata katika nyumba ya kuishi, unapofanya *expansion*, hauwezi ukaanza na *tiles*, unaanza kwanza kujenga kuta iko rafurafu baadaye ndiyo unatengeneza *quality*, hili ndilo lilitotokea. Kwa mtu yeypote ambaye hawezikuyaona haya, hajui tunachokifanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niseme moja tu, jana nilimsikia ndugu yangu Mheshimiwa Lissu akisemea kwa uchungu kama vile na yeye ana uchungu na elimu. Wakati kule Jimboni kwake Singida, Serikali ilikuwa inajenga madarasa, amepiga marufuku wananchi kushiriki kwenye kujenga madarasa, amepiga marufuku wananchi kujenga nyumba za Walimu,

amepiga marufuku kujenga maabara, mpaka sasa hivi amepiga marufuku...

MHE. MARTHA M. MLATA: Hata chakula hataki watoto wapewe chakula.

MBUNGE FULANI: Mgogoro mtupu.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mgogoro mtupu na sisi tulipeleka llani kwamba hivi ndivyo ambavyo tutafanya lakini wamepiga marufuku. Inakuwaje leo hii na nyie mnakuwa kati ya watu ambao wanaona uchungu kwenye elimu? Leo hii tulivyoenda Iramba kulikuwa na vijiji nane na vitongoji 30, walikataliwa kwa sababu wanazuia kujenga shule na watu wanataka kupeleka watoto wao shulen. Eti wanaandika kwenye kitabu chao kwamba tunaona vivu kuchukua mambo yao waliyoweka kwenye llani, hatujayachukua mliyoyaweka kwenye llani kwa sababu mlipopeleka ile llani ilikataliwa, sisi ni wajinga tuchukue mambo yaliyokataliwa? Mengine tumeyakataa kweli. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mambo mengine mnasema eti elimu ya msingi kuwa ya miaka saba ni ndogo sana, kwa hiyo pelekeni tisa mpaka kumi na tano. Mtoto wa Msukuma umpeleke miaka 15 shule ya msingi, utapata watoto wangapi wa Kimasai waende shule? Mbona mnataja vitu vya nadharianadharia. Twendeni kwenye hoja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi niseme jambo moja la msingi hapa maana naona kuna mambo mengine yameanza kuja ya ajabuajabu, kama hamjui namna Serikali zinavyoendeshwa tafuteni muda hata muelezewe. Hapa leo hii mnamnyooshea kidole Waziri, Sheria zetu zinasemaje? Tumewawajibisha Mawaziri wangapi lakini kila Waziri anayekuja watendaji/wataalam wasio waaminifu wanawa-late down Mawaziri. Mara ngapi tumefanya hayo na wanafanya hivyo? (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi leo niwaulize, tumejenga shule za kata, mwaka juzi ndizo zilizochangia zaidi ya asilimia 50 ya vijana walioenda kidato cha tano. Tuliposifasifia hapa na wengine walikwenda kwenye shule za vipaji maalum mkanuna hata kwenye sherehe ya kuwapongeza waliofanya vizuri kutoka kwenye shule za kata hamkuja, eti kisa CCM inapata sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Selasini alisifia shule za kata, jioni mkamweka kwenye kikao, eti kwa nini anasifia shule za kata...

MHE. MARTHA M. MLATA: Akatolewa na Uwaziri.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Akatolewa na Uwaziri Kivuli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo hii shule za kata zinafanya vizuri, wataalam wanakaa wanashauri kwamba ibadilishwe *grade*. Hivi hawa wataalam walisoma kwa kodi za Watanzania, wanajua tuna upungufu wa Walimu, wanajua tuna upungufu wa vitabu na maabara, walitoa wapi ujasiri wa kupeleka pendekozo la kupandisha *grade* kama sio ni hujuma ndani ya hujuma kuhakikisha kwamba hii idadi ambayo imekuwa ikifanya vizuri ya wanafunzi haifanikiwi.

Mheshimiwa Spika, leo hii kama hamjui, Waziri anapelekewa katarasi kama hii kutangaza. Wanaopitisha mapendekozo yote ni wataalam kule, anapelekewa kwamba tangaza hapa na asiposoma wanasesma siasa zinaingilia. Hamyajui hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Leo hii nyie mnahangaika na yule tu, mnahangaika na CCM, sasa kwa taarifa yenu niwaambieni, waambieni na wale mnaowatuma wakahujumu kule kwenye idara mbalimbali, hakuna nchi inayoitwa CCM, nchi inaitwa Tanzania na wananchi wake wanaitwa Watanzania na yejote anayehujumu Serikali ya Chama cha Mapinduzi akidhani anaihujumu CCM, ajue

anawahujumu Watanzania na atalaaniwa na Watanzania.
(*Makofi/Vigelele*)

Mheshimiwa Spika, mimi niliseme hilo kwa sababu katika hali ya kawaida fuatilieni, tulikamata barua ya pamba ikimwagiza Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba kwamba ukishusha bei ya pamba tu tunachukua nchi. Tukapata lingine maeneo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa, ahsante.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. (*Makofi*)

SPIKA: Namwita Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Mheshimiwa Zahra wajiandae.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, elimu nchini, tumekuwa tuna matatizo kwa miaka mingi tangu tupate uhuru na sioni kwa nini leo sisi Wabunge tuanze kumsakama Waziri wa Elimu wa leo kwamba amekosea, sioni sababu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuko tunaendeleza fikra mbalimbali, tumeanza na elimu ya msingi, tumefanikiwa, elimu ya awali bado tunasusua, elimu ya sekondari na vyuo vikuu tumefanikiwa sana. Leo ukiona hapa Dodoma tuna Chuo Kikuu cha UDOM, ni mafanikio makubwa sana. Hii kazi imefanywa vizuri na Chama cha Mapinduzi nami nasema nafurahi kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi katika mchango wangu, napenda kutoa mawazo tu. Mawazo yangu yanajikita kwa mambo ya Idara inayohusika na Mafunzo ya Elimu ya Awali. Jimboni kwangu Musoma Vijijiini, ukianza kuhesabu shule za awali, kama zikifika kumi nitashangaa kweli, hazipo. Ningombaa sana Serikali ianze kuweka nguvu mpya na kasi mpya kwa elimu ya awali maana ndiyo msingi. Ndiyo *foundation* ya elimu. Vijana watajifunza lugha wakiwa bado hawajafika miaka mitano maana wana-study haraka sana. Tukisubiri waende mpaka *form one* waanze kujifunza Kiingereza haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri tu, tujaribu kupata Walimu wanaoweza kwenda chini kwenye elimu ya awali, waweze kuwafundisha vijana wetu ili waweze kupata elimu ya kisasa. Ndivyo nchi jirani zilivyofanya na nchi za Ulaya zinafanya hivyo. Marekani leo wanaanza kuwafundisha watoto wakiwa kwenye mimba, wanaanza kwenda *ku-check* kule, je, hawa watoto wanaweza kumudu kujua kukimbia ama kusema, wakiwa tumboni. Leo sisi tunaanza kuwafundisha watoto wakiwa na miaka saba, *too late*, haiwezekani na karne ya sasa haitaki hivyo.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili, vyuo vikuu. Vyuo vikuu viko vingi, nafurahi sana kusikia kwamba Serikali inayoongozwa na CCM inafikiria kuanzisha Chuo cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere pale Butiama. Chuo cha Kilimo cha Kisasa pale Butiama, nawapongeza sana na nimefurahi sana kusikia hivyo maana Butiama iko Jimboni kwangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nadhani mchango wangu utakuwa hapo, hiki chuo kikijengwa kitakuwa kama Chuo cha *UDOM* ambapo majengo kwa sasa yanaanza kupasukapasuka au kitakuwa chuo cha kudumu. Majengo ndiyo ya msingi, tukianza kutumia jina la Mwalimu kwa chuo basi tumfikirie Mwalimu na hadhi yake ilikuwaje, yale majengo yawe ya kudumu na yasiwe majengo hovyo hovyo kama yalivyo ya *UDOM* ambayo yameanza kupasuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shule zingine ni shule za Jimboni kwangu, nilitoa mchango wangu kwa shule kama tatu hivi, nikazikabidhi kwa Serikali, shule *modern* kabisa lakini inaonekana Serikali inaogopa hata kuzigusa zile shule maana ni safi, badala yake wamezitelekeza Walimu wa sayansi hawapo. Sayansi ndiyo kitu cha msingi sana.

Mheshimiwa Spika, hizi shule za sayansi nilizokabidhi Serikalini na hapa ni-*declare interest* zilikuwa ni changamoto kwangu kuwa Serikali iweze kushirikiana na watu binafsi kuendeleza elimu ya sayansi. Nasikitika sana kuona shule ambayo ilikuwa nzuri kitaifa kwa majengo, imekuwa ya mwisho kitaifa, ni shule ya Oswald Mang'ombe. Nataka nipewe maelezo kutoka kwa Waziri wa Elimu, hiyo shule mnaitaka ama hamuitaki? Kama hamuiwezi basi mseme niwape madhehebu mengine ili waweze kuiendesha. Ni aibu sana kuona kila kitu kipo Chief Wanzagi, Chief Oswald Mang'ombe lakini watoto wanaojifunza sayansi hawana *chemicals* za kuweza kuendesha zile maabara, ndiyo maana wamekuwa wa mwisho kitaifa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa nini Serikali imeitupilia mbali shule ya Oswald ambayo inafundisha wanafunzi wa Sayansi. Mheshimiwa Rais amefika mara mbili kuona ile shule na akaipenda sana lakini nashangaa kuona hakuna Waziri ye yote aliye kwendwa pale tangu ifunguliwe, *as a result* ndiyo matokeo mabovu ambapo vijana wetu wanaojifunza kuwa Madaktari wamefeli kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuuliza, ni shule ya ufundi, hii ni Wizara ya Elimu na Ufundis. Jimboni kwangu kuna shule moja pale Kyarano iliyahi kuwa *primary school* wakati wa Ukoloni lakini mpaka sasa iko pale imefanywa kama shule ya ufundi. Ukienda pale shule ile imeoza kabisa, hakuna hata madawati, hakuna hata randa, lakini inaitwa shule ya ufundi. Nataka kujua kutoka kwa Waziri anayehusika, ni lini alitembelea shule hiyo au ni lini atakubali kuja kwangu ili nimpeleke aone shule ya Kyarano ilivyo. Hii ndio shule ya ufundi pekee katika Wilayani ya Musoma Vijijiini

ama Wilaya ya Butiama. Napenda kupata maelekezo zaidi vinginevyo sitaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu *sports* katika shule. Najua Wizara mfumo wake haujaka vizuri, maana *sports* ipo katika Wizara nyingine. Hawa Walimu wanaofundisha *sports* katika shule zote hawana uzoefu wowote, wala hawakujifunza *sports, as a results* unakuta shule hizi hata kama wakienda mashindano nje ya nchi wanashindwa maana hawajui kuogelea, hawajui kucheza *basketball*, hawajui kucheza *netball*, wao wanachojua ni *football*. Utakuwaje unafundisha mpira wa miguu tu lakini *sports* zingine zisikubalike?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono naomba nipate majibu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Zahra na Mheshimiwa Vita Kawawa. Mheshimiwa Dunstan Mkapa hayupo, kwa hiyo anaifuata Mheshimiwa Zahra, tafadhali.

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia bajeti hii leo.

Mheshimiwa Spika, maana ya uongozi ni kuonyesha njia, kiongozi anatakiwa aonyeshe njia na sisi tulipo hapa ni viongozi ambao tunawakilisha Majimbo yetu, ndiyo ambayo yametuleta hapa, kazi yetu ni kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia tu watu wazima, mara nyingi mtu mzima anakuwa ni mwenye hekima, mtu mzima ikiwa hana hekima watu wanasema ni mtu mzima hovyo. Ni lazima tuwe na hekima tutazame wapi tumetoka na wapi tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, tumetoka mbali na kugumu. Mheshimiwa Mulugo hapa alizungumza kuhusu Skuli za Kata,

zimesaidia sana kila mtoto wa Mtanzania aliye na uwezo wa kusoma anapata elimu. Sisi hatupo peke yetu, tupo katika dunia, tunaridhia mikataba ya kimataifa, Bungeni hapa kuna mikataba ambayo tunaipitisha, moja ni hii kila mtoto apate elimu. Tumeweza, tumefikia asilimia kubwa ya mtoto wa Kitanzania kupata elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini maendeleo yoyote yana changamoto zake. Sasa kama viongozi tutizame changamoto ambazo tunazo. Zipo changamoto sikatai, tuna tatizo la Walimu kwa sababu kwanza tumeanza kujenga skuli na jambo lolote kupanga ni kuchagua, lipi linakuja mwanzo, lipi linakuja kipindi cha katni na lipi litakuja mwisho. Tumeanza kujenga skuli, sasa Wizara itazame uwezekano wa kupelaka Walimu shulenii. Wizara itizame uwezekano wa kupata vitabu kwa wanafunzi, vitabu kwa Walimu, madeni ya Walimu, Walimu wapate mishahara mizuri ili waweze kufanya kazi kwa bidii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hilo haliwezi kufikiwa kwa bajeti hii ambayo inatengwa kwa Wizara ya Elimu. Ukitazama katika *figure* unaweza ukasema ni bajeti kubwa kuliko bajeti yoyote katika Wizara ambazo zipo, lakini tutizame ukubwa wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye bajeti hapa Wizara imetengewa shilingi bilioni mia sita themanini na tisa, bajeti yote ya Wizara hii. Kwenye taasisi za Wizara, kuna bajeti ya shilingi bilioni mia tano na kumi na nane, ukitoa mishahara inabakia shilingi bilioni mia tatu na thelathini, ukitoa Bodii ya Mikopo ambayo imo katika taasisi hizi inabakia shilingi bilioni mia tatu na sita. Kinachobakia hapa ni shilingi bilioni 24 katika taasisi nyingine zote. Shilingi bilioni 24, kuna vyuo vikuu 11, kuna Taasisi ya Elimu, kuna vyuo vya ualimu 34, kuna shule za mazoezi 50, kuna pia ukaguzi na nyingine ambazo sikuzitaja.

Mheshimiwa Spika, Bodii ya Mikopo peke yake inachukua shilingi bilioni mia tatu na sita. Kwanza, ningeshauri kwamba hii Bodii ya Mikopo pesa yake itoke Hazina, kwa sababu inanenepesha hili fungu unaona kama ni fungu

kubwa ukilitizama kwa mara moja na kwa kweli tunahitaji watoto wetu wapewe mkopo, watoto wa kimaskini na watoto wa Tanzania wasome lakini hela hii iwekwe Hazina moja kwa moja, Bodii yenye kuna marejesho ambayo inarejeshewa ya mikopo ambayo wanafunzi wamekopa, wataongezea, lakini vilevile watatuta vyanzo vingine vyaa mapato ili wahakikishe waombaji wanapata mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itizame sasa katika hizi taasisi zingine izationgezee bajeti. Kama nilivyosema kuna vyuo vikuu ambavyo vinahitaji kufanya *research*, watafanya viyi *research*? Kuna vyuo vyaa ualimu ambako huko ndiko tunazalisha Walimu. Tunataka Walimu wazuri wenyewe uelewa, Walimu ambao wamefunzwa wakafunzika, Walimu ambao wana maadili, lakini pesa ni ndogo, haitoshi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unatarajia Walimu ambao wanafundisha Walimu wenzao, yeeye mwenyewe kompyuta hajawahi kuiona toka azaliwe, hajawahi kuifanyia kazi, ni viyi atawezeku kumsomesha Mwalimu mwenzake akajua kama kompyuta ni *TV* au ni *radio*! Leo tunakaa tunamlamu Waziri, jamani myonye myongeni haki yake mpeni! Tatizo bajeti ni ndogo sana haitoshelezi kwa Wizara, tutakamatana uchawi, tunajifanya vipofu macho yako wazi, hatuoni kweli hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu nafahamu elimu ilivyokuwa ina kazi kubwa. Nafahamu mahitaji ya Walimu, wapo katika hali ngumu na Walimu hao ndio ambao tunatarajia watupasishie watoto na mimi sifirkii katika hili, kama kuna Waziri yeoyote ambaye atakasirika kwa kuwa Wizara ya Elimu imeongezewa pesa. Kwa sababu kama Wizara ya Afya hao Madaktari wanatokana na elimu, kama ni Injinia ni lazima kwanza wapate hiyo elimu. Kwa hivyo, kama ambavyo Maandiko yetu Matakatifu yanavyotuambia wakati anapewa Utume, Mtume Mohammed (S.A.W), jambo la kwanza aliambiwa ‘*Iqra Bismirabikal-ladhi khalaq*’, soma, utakaposoma ndio utafahamu, utaelewa, utatambua na utapambanua. Elimu

ndiyo ambayo inamjenga mtoto na ndiyo ambayo inanyanya uchumi wa nchi. Kwa hivyo nadhani hilo Serikali wanalisikia, na ninaamini ni wasikiu wataona uwezekano wa kuiongezea Wizara hii bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia *NECTA*. Mimi sina tatizo kubwa na *NECTA*. Ninafahamu namna ambavyo wanafanya kazi zao, wanajitahidi. Suala kubwa ambalo ninawasifu wameliweza, ni kudhibiti uvujaji wa mitihani. Mitihani ilikuwa ovyoovyo tu. Kesho mtihani unafanywa leo darasani unasikia mtihani umevuja, watoto wanapigiana simu, wanaandikiana ujumbe kwenye simu kuna mvujo tayari. Leo *Alhamdulillah*, miaka miwili hii wameweza kudhibiti wizi wa mitihani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna haya mambo madogodogo ambayo siku zote moto unaanza kwa cheche moja..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana, umechangia kwa mara ya kwanza lakini umechangia vizuri. Nilisema nitamwitwa Mheshimiwa Vita Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Mheshimiwa Mwaiposa ajiandaye.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsate kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara yetu hii ya Elimu. Ninaanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, nitaanza hotuba yangu kwa kuchangia suala la mgawo wa ukarabati wa shule zetu za sekondari. Wengi wamelaumu mgawo huu ulivyowekwa. Mimi ushauri wangu ni kuwa, kwa kuwa awamu hii ya kwanza ya ukarabati wa shule hizi wamezipanga vizuri shule mbilimbili karibu Wilaya zote nchini Tanzania, basi iwe ndiyo *trend* hiyo hiyo ili kuondoa lawama mkazifumue zile shule 528 mlizoviweka katika mchakato ule wa tathmini ya mahitaji

ya miundombinu ili awamu ya pili itakapokuja kama ni shule nnenne basi ziende kwa mfumo wa nnenne Wilaya zote nchini. Mwisho wa siku mtakuta mmezimaliza Wilaya ambazo zina shule chache, zitabaki Wilaya au Mikoa yenye shule nyingi na hakutakuwa na lawama tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo kuzungumzia kuhusu Walimu wa mikataba. Wakati tunaanzisha shule zetu za kata tulikuwa hatuna Walimu wa kutosha na Serikali iliingia mkataba na Walimu waliostaafu ili waweze kusaidia kufundisha shule zetu za sekondari za kata. Katika Wilaya yetu ya Namtombo tunao Walimu zaidi ya 14 waliomaliza mkataba lakini mpaka leo hawajalipwa mafao yao, miaka mitatu iliyopita ndiyo walimaliza mkataba wao. Tumefuatilia mafao yao, mwisho wa siku tunaambiwa kwamba eti walikuwa wanakatwa *PSPF* wakiwa ndani ya mkataba, kwa hiyo kwanza *PSPF* warudishe makato yale Hazina ndipo waweze kulipwa sasa yale mafao. Hili ni tatizo kubwa kweli, maskini wa Mungu, hawa Wazee hawa Wastaafu siyo makosa yao. *PSPF* ndiyo iliakata, kwa nini wabebeshwe mzigo huu? Tunaiomba Serikali iwalipe mafao yao Walimu hawa wapo zaidi ya 14 wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na hayo makato yafuatiliwe na Serikali *PSPF* halafu iyarudishe kuliko kuwoanea hawa wazee kwa kosa wasilolifanya.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mishahara ya Taasisi za Elimu na Halmashauri. Licha ya kuwekwa katika mtandao wa *LAWSON* au *Human Capital Management Information System* lakini Taasisi za Elimu ya Juu na baadhi ya Halmashauri bado kuna wimbi la wafanyakazi ambao hawajaingizwa katika *payroll* ya Serikali. Mantiki ya kuwa na *LAWSON* ni kuhakikisha mfanyakazi anaingizwa kwenye *payroll* na kumbukumbu za Serikali mara tu anaporipoti kituoni lakini sasa kumekuwa na ucheleweshaji wa kuwaingiza watumishi katika *payroll*. Hii inasababisha migomo baridi na migomo moto kwa watumishi au kwa Walimu na watumishi wa taasisi za elimu, kwani siyo haki kumtumikisha mtu kazi bila kumpa haki yake.

Mheshimiwa Spika, lakini wanapochelewa kuingizwa huku Taasisi hizi za Elimu ya Juu, Halmashauri zetu huwa zinawalipa hawa Walimu au Watumishi wa Taasisi za Elimu posho na siyo mishahara ambapo husababisha Halmashauri zetu kuwa na gharama au kupunguza fedha za gharama za uendeshaji za Halmashauri na Taasisi hizo. Halmashauri inapoiomba Serikali kurejesha fedha zile za *OC walizowalipia wafanyakazi* hawa ambao walikuwa hawapo katika *payroll*, Serikali huwa inasita kuzirejesha fedha hizo, halafu tunakaa tunawalaamu watu hawa-*perform*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba ni lazima hawa ma-*desk officers* wa *LAWSON* wasimamiwe ipasavyo ili wawe makini, wawe wanafanya tathmini ya kuwaingiza wafanyakazi hawa wapya, wawe wanapewa malengo kwa siku, kwa wiki na kwa mwezi. Kwa sababu hapa ndipo chanzo cha matatizo yote ya migomo na madeni yanayolimbikizwa ya madai ya mishahara na posho za watumishi hawa. Ni kutokana na mtumishi wa *LAWSON* ambaye anatakiwa aingize *data* za watumishi wapya anapochelewa kuingiza kwa nchi nzima. Kwa hiyo, ni lazima tuliangalie suala hili kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zetu hizi za Elimu za Kuu ikiwemo ya *UDOM*, bajeti za maendeleo kwa fedha za ndani mpaka sasa hivi hawajapewa, athari yake ni kubwa sana. Wote tunafahamu kwamba moja ya athari yake kubwa ni kuongezeka kwa gharama za madeni, mradi unapochelewa, riba ya adhabu kwa kutolipa hati zile za madai kwa wakati huwa inajilimbikiza mwaka hadi mwaka, kwa hiyo gharama inakuwa kubwa kwa Serikali. Athari ya pili taasisi na shule zetu hizi hushindwa kununua zana za kufundishia na zana za maabara, matokeo yake watoto wetu wanashindwa kupata elimu wanayostahili kuipata. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ipeleke fedha hizi za maendeleo kama inavyostahili na kama tunavyopitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna baadhi ya taasisi na vyuo zinaonekana mpaka sasa hivi tunavyozungumza wamepata chini ya asilimia hamsini ya *OC* zao. Sijui ni lini

Serikali itailipa Wizara ya Elimu kutoka Hazina ili iweze kupeleka fedha katika taasisi na vyuo vyetu vya elimu ili waweze kukidhi mahitaji yao kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa huo na ahsante sana kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Mwaiposa na Mheshimiwa Shekifu ajiandaye, Mheshimiwa Akunaay na Mheshimiwa Christowaja Mtinda pia wajiandaye.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzlo ya Ufundı.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niunge mkono hoja hii lakini lazima nitamke wazi kwamba sekta ya elimu Wilayani Nanyumbu ni mbaya mno kuliko mnavyofikiria.

Mheshimiwa Spika, mtihani uliopita wa kidato cha nne, wanafunzi waliofaulu ni 53 tu, watatu *division* ya tatu na hamsini waliobaki ni *division* ya nne. Sasa utaona hapo kwa kweli hali hii imekuwa ni mbaya mno. Tuna mapungufu mengisana Wilayani Nanyumbu, kuna upungufu wa nyumba za Walimu 124, madarasa vyumba 59, maabara hakuna, vyoo 134 lakini kubwa zaidi ni hosteli za wanafunzi tunahitaji kama 22. Sasa kukosekana kwa nyumba za Walimu na miundo mingine, Walimu hawakai, wakifika wanatoroka. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri hali ya Nanyumbu ni mbaya kuliko matarajio. Niwakumbushe tu kwamba Nanyumbu tuko nyuma kwa sababu Taifa hili walitumia Wilaya ya Nanyumbu na Mkoa mzima wa Mtwara kama uwanja wa mapambano wakati wa Ukombozi wa Msumbiji na Afrika Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jamani mtukumbuke, wakati wenzenetu walikuwa wanakimbia sisi tulikuwa tumekaa au tunatambaa. Sasa hivi mgeuke Wizarani huko, Serikali

tafadhalii tuoneeni jicho la huruma Wilaya ya Nanyumbu, tunapata taabu sana.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Elimu haina gari iwe ya Msingi hata ya Sekondari, wao kila siku wako ofisini, sasa watatembelea vipi shule kuziangalia zilivyo? Ofisi ya Elimu haina ofisi, wanabanana humohumo. Kwa kweli hali ni hatari sana. Mimi naomba sana Waheshimiwa Mawaziri tupeni upendeleo Wilaya ya Nanyumbu hasa hasa katika sekta hii ya elimu. Mathalani Idara ya Elimu ya Msingi kuna upungufu wa nyumba za Walimu 557, vyumba nya madarasa 456, matundu ya vyoo 1,646, madawati 8,100. Wanafunzi kule ukiwaona kila mwanafunzi walio wengi kaputura zimechanika, wanakaa chini, wengine wanakaa juu ya mawe. Kwa hiyo, nguo zimechanika siyo kwa sababu wanachana ni kwa sababu hawana madawati ya kukalia. Kuna upungufu wa Walimu 258, hiyo ndiyo hali halisi ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, natamani kulia lakini humu ndani hairuhusiwi kulia lakini tafadhalii sana Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Kawambwa, Mheshimiwa Mulugo, tuoneeni jicho la huruma Wilaya ya Nanyumbu, nawaomba sana mtutembelee kwa sababu mnaweza kusema hapa labda natia chumvi, naomba mtembelee muone vijana wanavyojisaidia vichakani. Muone vijana wetu wanavyokaa chini, muone Walimu wetu wanavyonyanyasika hawana ofisi, hawana vitendea kazi, hawana vitabu, hayo yote ni ndani ya Wilaya ya Nanyumbu. Naomba sana tena sana, narudia wito huu kwenu Mawaziri mtembelee Wilaya ya Nanyumbu muje msikilize kero yetu, mjionee hali halisi ya miundombinu ilivyochakaa na isiyokuwepo katika sekta hii ya elimu ndani ya Wilaya ya Nanyumbu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la orodha ya shule 528 kati ya 1,200 zilizo katika mchakato wa tathmini ya mahitaji ya miundombinu, Wilaya ya Nanyumbu imepewa shule mbili tu. Sasa hebu ona, tuko nyuma kielimu halafu hapohapo mnatubania, mnatupa shule mbili tu. Mimi naona hii siyo sawa, naomba sana tena sana mtuongezee shule

nyingine ili ziweze kukarabatiwa na kuweza kuinua hali ya elimu Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, hii orodha, yejote aliyetengeneza, nadhani alifanya kitu upendeleo. Kuna maeneo yamependelewa na mimi naomba Kamati ya TAMISEMI au ya LAAC iwatafute hawa watu waliotengeneza hii orodha, tuwajue wanatokea wapi, wana maslahi gani na orodha hii? Haiwezekani wengine wanapendelewa shule ishirini na kitu, Nanyumbu mbili tu, kwa nini, tumekosa nini? Kwani watu wa Nanyumbu hawalipi kodi? Watu wa Nanyumbu hawapo Tanzania hii? Haiwezekani! Kuna watu wana maslahi binafsi ndiyo walioandaa hii orodha na wasakwe wafahamike ni nani na wako katika kivuli gani na kwa nini wamefanya hivi? Tunazo Kamati za TAMISEMI, tunaomba sana mfuatilie watu hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla, Wizara hii wapishi ni wengi sana na ndiyo maana mchuzi unaharibika. Nina maana gani? TAMISEMI wapo kwenye Wizara hii, Wizara Mama ipo kwenye shughuli hizihizi kuanzia shule ya awali, shule ya msingi, shule ya sekondari na vyuo vikuu. Sasa inakuwa ni vigumu kwa kweli. Mimi sijui mnaratibu vipi, mnawasiliana vipi katika shughuli nzima ya elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kidogo juu yetu sisi wananchi hasa wazazi, wazazi hatufuatillii maendeleo ya watoto wetu. Hatuna muda kabisa, mtoto anatoka shulenii wewe huna habari naye, anaamka anakwenda shulenii huna habari naye. Pia huko mijini maana kwangu Nanyumbu hakuna mzazi anayeweza kumnumulii simu ya shilingi laki sita lakini utawaona na simu zenye gharama tu, muda wote wako kwenye mitandao na wazazi wengine hushiriki hata kununua hiyo mitihani. Wazazi wanawapa hela watoto wao wakatafute hiyo mitihani, sasa hapo elimu lazima itashuka tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe rai moja, jamani tupunguze kuzaa watoto wengi. Ukienda huko mashulenii ndiko utaona kwamba jamani tumefumuka, tunazaasana.

Syo wewe unayenitazama, sikutaji wewe, ila nasema tu kwamba tupunguze kuzaa Watanzania watoto ni wengi sana, ukitaka kushuhudia watoto nenda mashulenii na ndiyo maana wanakaa wanee, wanee watano, watano kwa sababu uzazi ni mkubwa sana tupunguze. (*Kicheko/Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante umemaliza vizuri, punguzeni kuzaa. Mheshimiwa Eugine Mwaiposa, atafuatiwa na Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Akunaay na Christowaja, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Masoud Salim Masoud, Vita Kabati na Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nishukuru kupata fursa hii ili na mlimi niweze kuchangia hii bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niendelee kuwapongeza sana Mawaziri pamoja na Watendaji na Serikali kwa jinsi ambavyo wanaendelea kutatua changamoto nyingi ambazo ziko katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ina changamoto nyingi na changamoto hizi zimezungumziwa sana na wachangiaji walio wengi. Mimi kipekee nipende tu kusema kwamba sioni ni kwa nini tunataharuki kwa sababu ya changamoto hizi za Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, changamoto mara nyingine zikitumiwa vizuri, huwa zinaweza zikatuvusha sana katika nyanja ya maendeleo. Changamoto mara nyingine hutokana na hatua moja ambayo imechukuliwa na Serikali kwa sababu ya kutatua tatizo. Kwa mfano, upanuzi wa shule nchini ndio ambao umezaa changamoto zote ambazo tunazungumzia hapa Bungeni kuanzia jana hadi leo. Bila upanuzi huo ni kwamba tusingewenza kabisa kuwa tunaongelea changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sioni ni kwa nini tunataharukui kwa ajili ya hizi changamoto. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunatembea kifua mbele pamoja na changamoto hizi lakini tukiangalia pia kwamba upanuzi huu wa shule umeleta faida gani katika Taifa letu. Watoto wamesajiliwa wengi, wamepata fursa wengi zaidi kuijunga na shule lakini pia hata ajira imeongezeka sana kwa Walimu pamoja na wafanyakazi wengine. Kwa hiyo, ni lazima tujue kabisa kwamba changamoto hizi zinatokana na faida hizo na kinachotakiwa sasa siyo kuendelea kulaumiana, ni kuhakikisha kwamba tunazitumia sasa fursa zilizoko kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi kwa nchi kama ya Tanzania, nchi inayoendelea siyo za kushangaza sana. Ni changamoto ambazo tulikuwa tunazitegemea kwa sababu kukosekana kwa madawati, kukosekana kwa Wallimu wa kutosha, kukosekana kwa maabara, tulikuwa tunategemea kwa sababu tulifanya upanuzi. Kwa hiyo, mimi niombe tu kwamba Serikali sasa kwa sababu tunajua uwezo wake na tunaendelea kulalamika hapa kwa sababu inawezekana hatujui uwezo wa kiuchumi wa nchi yetu, hii ni nchi inayoendelea. Kwa hiyo, changamoto hizi zitaendelea kutatuliwa moja baada ya nyine kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Mimi niendelee kuwapongeza sana Mawaziri na Serikali na niendelee kuwaomba tu waendelee kusonga mbele na kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinatatuliwa ili tuweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Spika, hapa tumeongelea sana suala la mdau mmoja tu wa elimu ambaye ni Serikali lakini wapo wadau wengine ambao ni muhimu sana ambao bado hawajapata nafasi ya kuzungumzwa sana hapa Bungeni. Kuna wadau ambao ni wanafunzi wenyewe, kuna wadau ambao ni wazazi, lakini kuna hata jamii yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mdau wa kwanza wa elimu ni mwanafunzi mwenyewe lakini mwanafunzi huyu ni lazima aonyeshe nia ya dhati ya kutaka kuelimika. Kama hajaonyesha nia ya dhati ya kuelimika hata Serikali ingefanya

nini, hata mzazi angefanya nini, hata jamii ingefanya nini, hawezi kupata elimu itakayomfikisha mbali. Wanafunzi wetu mnawaona lakini ndugu zangu Watanzania? Mhawaona jinsi ambavyo wako barabarani kuanzia asubuhi mpaka saa tano hata mabasi yenyewe hayajaja a lakini hawataki kupanda. Wanafunzi wetu mnawaona kwenye ma-*internet*, hivi mnawaona?

Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa elimu. Mmeshaona simu hizo za hao watoto na *message* zilizoko huko? Watoto wetu wamejiingiza kwenye mambo makubwa ambayo kwa kweli ni hatari lakini ni mambo ambayo ni adui mkubwa wa elimu. Watoto wetu wamejiingiza kwenye mapenzi wakiwa wadogo mno na hakuna adui mkubwa wa elimu kama suala la mahusiana ya kimapenzi, huwezi ukaenda navyo viwili. Ni lazima watoto waamue kuwa watoto wanapokuwa shulenii lakini wanapojifanya ni wakubwa na kufanya mambo ya kikubwa wakiwa shulenii, hata tungefanya nini ndugu zangu hatuwezi kuwaokoa watoto hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wameingia kwenye siasa, asubuhi badala ya kupanda mabasi wako mahali magazeti yanauzwa wanaangalia magazeti, utawakuta kwenye *internet* kama nilivyosema, utawakuta kwenye *video*, sasa elimu haiendi hivyo. Kumfanya mtu aelimike siyo kama Daktari anavyomtibu mgonjwa. Huwezi kuchukua sindano ukamchoma mtu ukamwingizia elimu. Elimu ni lazima yeye mwenyewe awe na ile *willingness* ya kujifunza. Ni sawasawa na kumpeleka puna kwenye maji wakati hataki kunywa maji, hatakunywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watoto wetu hawa hata tungefanya nini, je, wana maono kwamba wanataka kuwa nani kuanzia mwanzo? Watoto wetu wanakwenda shule kwa sababu ameambiwa na mzazi aende shule lakini hana maoni kabisa ya kwamba anataka kuwa nani baada ya hapo. Haoanishi kabisa elimu anayoipata na maisha yake ya baadaye. Kwa hiyo, ni lazima tusimame kifua mbele tuwaambie hawa watoto na tuwakemee kwamba suala la

kufanikiwa katika elimu analo mikononi mwake mwenyewe.
(Makofî)

Mheshimiwa Spika, mimi wakati ambapo ninasoma nikiwa mdogo nilifika *Form Four* sikuwa na Mwalimu wa hesabu lakini tulijisomea na nilipata 'D' ya hesabu ambayo ilinifanya mimi nikaenda *Form Five* lakini watoto wanakaa tu wanang'ang'ania kwamba hakuna Walimu na hakuna kipindi ambacho Tanzania tumeshawahi kutumia *tuition* kama kipindi hiki. Watoto ni *tuition* lakini hata *performance* yao inakuwa ni mbovu. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba pamoja na Serikali na changamoto hizo bado watoto wanatakiwa *wa-play their parts* katika kuhakikisha kwamba wanapata *performance* nzuri katika elimu. *(Makofî)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye mdau mwiningine muhimu ambaye ni mzazi. Wazazi kutokana na uchumi na hali kuwa ngumu wamekuwa wanatumia muda mwingu sana kukimbizana na maisha lakini wamesahau kabisa utunzaji wa watoto, ufuatiliaji wa watoto. Kama hujajua kwamba mtoto wako amekwenda shulenii mara ngapi kwa wiki, hivi huyo mtoto unamtupia Mwalimu halafu iweje na hasa ukizingatia sasa hata kule shulenii kwenyewe viboko navyo tumevikaza. *(Makofî)*

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofî)*

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Akunaay, Mheshimiwa Chritowaja na Mheshimiwa Mfutakamba wajiandaye.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru lakini pia nimshukuru Mungu na wananchi wangu wa Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Spika, mengi yamechangiwa. Mimi niseme nitachangia mambo machache ambayo kwa ujumla yamepewa uzito lakini uzito wenyewe pengine niujazilie.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Waziri na kumpongeza na kumpa pole kwa tuhuma nydingi. Ndugu zangu, Wizara ya Elimu imelaumiwa katika hatua nydingi tu, nilikuwepo humu Bungeni kuanzia 1995, kulikuwepo na Mawaziri akina Mungai, Mama Sita, akaja Maghembe na leo yuko ndugu yangu Waziri Kawambwa, kwa njia moja au nydingine wamelaumiwa. Wamelaumiwa kwa sababu ya mafanikio. Kitu kinachokwuwa siku zote kinabadilika sura. Mtoto anazaliwa, anafikia hatua anaanza kuota meno, anaanza kulia. Ukiuliza kwa nini, anaota meno na meno ndio yatakayomsaidia. Sasa ukimkuta mtu mzima na akili zake analalamika kwa nini mtoto analia na huku anaota meno kwa manufaa yake mtoto basi huyomtu ana matatizo. Mimi sioni sababu ni kwa nini tulalamike kuwaondoa madarakani viongozi wetu, huko ni kutokomaa tu. Yeyote atakayekuja kwa sababu chombo hiki kinaendelea atabadilika. Sasa nisingependa niende kwenye malumbano hayo, nikupe moyo tu Mheshimiwa Waziri chapa kazi na tunakuhakikishia tuko nyuma yako, tunakuunga mkono, ni chombo cha Chama cha Mapinduzi tutakulinda kwa nguvu zote zile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nije katika uchangiaji, mimi nitajielekeza katika mambo matatu muhimu. La kwanza ni vyuo vikuu. Tunalo tatizo, vyuo vikuu, hawa maprofesa sio walalamikaji sasa lakini kwa sasa hivi vyuo vikuu mpaka sasa vinadai zaidi ya shilingi bilioni 18 na mpaka leo hivi hawajui mwelekeo kama watalipwa au hawatalipwa. Nichukue mfano mmoja tu na ninaomba hapa ku-*declare interest*, mimi Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria. Chuo Kikuu Huria kinadai Serikali nyongeza za mishahara shilingi milioni 26, kupandishwa madaraja shilingi bilioni 1.1, kiinua mgongo (*gratuite*) shilingi bilioni 149, posho za madaraka Wakuu wa Vyuo, shilingi milioni 76, posho za madaraka, Wakuu wa Idara, shilingi milioni 559, *Expatriet Allowance*, shilingi milioni 10, jumla Chuo Kikuu Huria tu kinadai shilingi bilioni 2.5. Ni ukweli hawalalamiki, lakini unategemea nini? Kama Walimu

unaowakodisha wakusahihishie mitihani yako huwalipi, wale watasahihishaje kwa uadilifu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema tunamlalamikia na tunaweza kumlalamikia sana Waziri wa Elimu, lakini mimi nafikiri tuiombe Serikali nzima kwa ujumla. Kama tunesema elimu ni kipaumbele, basi tutoe kipaumbele hicho na tutenge fedha za kutosha na tijiwekee mipango ambayo inaeleweka. Vyuo vikuu vikiambiwa mwaka huu mtatengewa hiki, mwaka kesho hiki, wakijua hivyo ni rahisi hata kutoa elimu kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika vyuo vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini sio hiyo tu, shughuli za maendeleo katika vyuo vikuu. Chuo Kikuu Huria ni kikubwa, ukiangalia mahitaji yao ya fedha na upanuzi wao ulivyo kwa nchi nzima, Mikoa yote 30 na Zanzibar, mahitaji ni makubwa. Katika miaka hii miwili wametengewa shilingi milioni 128, kwa maendeleo kama Chuo Kikuu Huria, hutegemei kupanuka kitadumaa na kikidumaa yale mafanikio yote yanakwisha. Mimi ninashauri na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, utakapoamka hebu tuambie una mpango gani katika hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine la ujumla ni hili la Mheshimiwa Waziri na mimi niliunge mkono kabla ya muda, nikuombe sana kama Wabunge wengine walivyoshauri, ile idadi ya shule 528 achana nayo kama ilivyoletwa, anzeni upya ili uondokane na matatizo. Ukiamka hapa ili tukupe sifa anza kutamka hilo. Ukianza mengine watakuwa wakali, anza kuwaambia ukweli, wale waliopendekeza shule zile walikuwa na malengo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili *TEA*. *TEA* ni Mamlaka ya Elimu lakini sasa amezaliwa mtoto hana miguu hana nini, hebu kama tulivyoamua katika ule Mfuko wa Mcemba, hebu maamuzi yafanyike haraka fedha zipelekwe, *TEA* ikue, mimi nina uhakika kwa mifano walivoonesha, wamechangia kwa mfano kule Lushoto, Chuo changu Kikuu SEKUKO, vifaa vya Walemavu mbalimbali kwa ajili ya kufundisha Walimu wa

Walemavu, wanaona maeneo muhimu ya elimu, hebu tuwape nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije, baadaye nitaongeza labda nikiwa na muda, nije kwenye Wilaya yangu ya Lushoto. Wilaya ya Lushoto katika Mkoa wa Tanga, ndio Wilaya iliyo na wanafunzi wengi kuliko Wilaya yoyote...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, ni ya kwanza naamini?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, ukichukua upande wa sekondari tuna upungufu wa Walimu 520, tuna upungufu wa maabara 245, madarasa tuna upungufu wa 567, tukija katika majengo ya utawala tuna upungufu wa majengo 53 na ukiangalia maeneo yote, tuna matatizo. Sasa mimi sisemi wengine wasipewe, lakini kuangalia kwa uwiano, twendeni kwa uwiano wa mahitaji na wingi wa wanafunzi na wingi wa shule. Sisi pale mwaka huu tuna wanafunzi waliofanya mtihani karibu 28,000, waliofaulu ni karibu 13,000 hawa wana mahitaji. Sasa ukitupima na wengine utatuonea sana.

Mheshimiwa Spika, tukija katika shule za msingi, katika suala la Walimu tuna upungufu wa Walimu 453, miundombinu kwa ujumla, madarasa, nyumba za Walimu, vyoo, tuna upungufu wa karibu 5,000. Madarasa tuna upungufu wa 1,650, nyumba za Walimu upungufu wa 3,002, vyoo 2,024, ukija katika samani ndio usiseme. Sasa katika hali ya namna hii hata tungekulaumu vipi na hata tungelaumu vipi na tungependa vipi elimu ipande haiwezi kupanda. Hebu sasa tuje na mikakati. Tukija na mikakati tutaweza kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mapendekezo kidogo na ninaomba Serikali kwa ujumla, anayemwakilisha Waziri Mkuu yupo na amshauri Rais, mfumo wa Wizara ubadilike.

Kujikosoa na kukosolewa sio tendo la fedheha ni kujiiamarisha na wala kwa kukubali kukosolewa, hakupunguzi urafiki wetu. Kwa hiyo, mimi naomba sana muundo wa Wizara ubadilike.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, muda ni mfupi.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa bu Mheshimiwa Akunaay, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Eng. Mfutakamba na Mheshimiwa Masoud wajiandae. Mheshimiwa Akunaay, dakika tano.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya hii, ili nizungumze mbele ya Bunge hili. Pili, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda mfupi, naomba nianze tu kutoa elimu ya uraia kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanawapotosha wananchi wa Tanzania kwamba vyama vya siasa hasa CCM inajenga barabara, CCM inajenga shule, CCM inapeleka *Aspirine* hospitalini. Yote hayo yanajengwa au yanatengenezwa na kodi za Watanzania na ndio maana leo hapa tunazungumzia bajeti ya Wizara ya Elimu na Ufundı ili fedha hizo zikipatikana zilete mishahara ya Walimu na vifaa vya elimu katika nchi hii. Kwa hiyo, si kweli CCM imejenga shule za kata, shule za kata zimejengwa na Serikali ya Tanzania na CHADEMA isije ikaulizwa barabarani kwamba shule iliyojenga iko wapi, hakuna chama cha siasa kinachojenga shule. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba pia hakuna Mbunge mwenye uwezo wowote wa kukataza wananchi wasijenge shule. Katika Halmashauri yoyote au katika Kata ikipita michango, wananchi watachanga na *By Laws* zitatumika katika Wilaya hiyo na Sheria itatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda kwa sababu wengi wamezungumza na kwa sababu wameshatamka matatizo, mimi nitatoa *solutions*. Katika sekta hii ya elimu, tatizo la kwanza kwa nini elimu ya Tanzania imeshuka, Waheshimiwa Wabunge wametamka kwamba, ni upungufu wa Walimu. Sasa, ili Walimu wapatikane, tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ni kuoneza Walimu na kuwalipa vizuri na kuongeza maslahi yao. Sasa hivi *ratio* au uwiano wa Walimu ni mdogo kwa sababu Walimu hii kazi hawaitaki. Hii kazi ni kazi ya wito, kwa hiyo, ili wanafunzi waliofaulu katika elimu ya sekondari wapende hii kazi, lazima kuwe na kitu kinawaita, mshahara ndio kitu ambacho kinaweza kuwaita. Kwa hiyo, tuwapangie mshahara wa juu na pia wao kuwe na vigezo ambavyo vinatumika kwamba ni watu wenye utaalamu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nizungumzie juu ya mazingira, shule kujengwa peke yake haitoshi kama mazingira ya shule hizo hayafai. Shule nyingine zimejengwa katika maeneo ambayo hayafai, kuna ugomvi kati ya wananchi na wakazi wa eneo hilo na Walimu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali, itizame suala hili na maeneo ya shule yalindwe.

Mheshimiwa Spika, tatu, wazazi wengi hawasomi na watoto wao. Maana elimu ina wadau watatu, Mwalimu, Mzazi na Mwanafunzi. Sasa Mwalimu hata kama akiboreshwa, kama wazazi hawajaboreshwa ili waweze kuwalea watoto wao vizuri ili wawe *receptive* katika elimu, tutakuwa tunafanya kazi bure. Hii ni hali ya hatari sana kwa sababu si ajabu tunatengenezewa mazingira ya kwamba tuwe na watoto ambao wanapokea elimu ambayo ni duni, wawe wajinga, baadaye tutawaliwe upya. Kwa hiyo, lazima tulitazame kama jamii kwamba tunatoa *products* ambazo wanakuwa baadaye na ufundi stadi yaani wawe na *skills*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi katika dunia zinakaa kwa *blocks*. Sasa kama *block* ya kwetu ambao tunahusiana nayo Tanzania itakuwa na watu wa elimu ya chini, basi sisi

tutakuwa tunatawaliwa au nafasi nyingi katika nafasi za kazi zitachukuliwa na watu wanaotoka katika nchi nyingine. Hapa nazungumzia *East African Community*, nchi nyingine zote nne zitachukua nafasi zote za Urdktari mpaka Katibu Kata, hii ni hali ya hatari sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya uamuzi wa Serikali kufanya *standardisation* ya mtihani wa matokeo ya *Form Four* mwaka jana. Kile kilikuwa ni kitendo cha aibu kwa sababu, mtoto aliyefeli hata akiongezewa *marks*, je, ule uelewa wake ameongezewaje? Ina maana hata aliyekuwa ameandika matusi ameongezewa *marks* na ameweza kufaulu akaendelea kusoma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti Profesa Mchome, mimi namfahamu, ni Mwanasheria mwenzangu, ni Mwalimu wa Sheria. Sasa sijui tena ametoka wapi kwenye utaalamu wa Ualimu, alikuwa sio mtu wa kukaa pale, kwa hiyo, amei-*mislead* ile Tume. Mimi nashauri kwamba elimu ya namna hiyo, kwa mfano wale wanafunzi ambao watakwenda *Form Form this time*, watakuja kutoka *product* ya ajabu sana. Kwa hiyo, ni kilio na njanga la Taifa, ingetakiwa mtihani ule ufutwe waanze upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kufaulu mtihani sio...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Christowaja?

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kabla sijachangia, naomba tu nimpe taarifa kaka yangu mpendwa Mheshimiwa Mwigulu Mchemba kwamba shule za kata zimeendelea kutoa matokeo yasiyordhisha kuanzia mwaka 2008 na haya sio maneno yangu, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Lukuvi, akitoa Ripoti ya Awali ya Tume ya Waziri Mkuu, akisema:-

"Matokeo ya Kidato cha IV kuanzia mwaka 2008 yamekuwa na mserereko wa kushuka kuliko miaka iliyotangulia kwa sababu mbalimbali ikiwepo changamoto zinazotokana na mafanikio yaliyopo sasa ya kuongezeka sana kwa idadi ya shule za msingi na za sekondari, hususan kati ya mwaka 2001 na sasa 2013 na hivyo kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi walioko shulen." Hiyo, ndio sababu ya kufeli shulen ni matokeo mabaya ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze mchango wangu kwa kuendelezea alipoishia Mheshimiwa Akunaay kwamba siasa imeingia sana kwenye elimu na hasa kwenye matokeo na kwenye Baraza la Mitihani. Nasema hivi kwa sababu, matokeo yanayotolewa sasa hivi na NECTA hayana uhalisia, yamekuwa ni matokeo ambayo yanaongozwa na Wizara ya Elimu na kupangiwa ni kwa jinsi gani mwanafunzi afaulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wamesema wenzangu kwamba Ripoti ya Awali ya Tume iliposomwa hapa na Mheshimiwa Lukuvi, ilielekeza kwamba matokeo yachakatwe kwa kutumia mfumo uliokuwa unatumika zamani yaani *flexible grade ranges*. Sasa tumeelezwa kwamba baadaye haikutumika tena hiyo *flexible grade ranges*, matokeo yake ikatumika *fixed grade ranges* kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alitutangazia.

Mheshimiwa Spika, hiyo imefanyika baada ya kuona kwamba kwa kutumia *flexible grade ranges*, kama ambavyo Waziri alielekeza hapa, wale wanafunzi waliokuwa wamefaulu awali walionekana kufeli. Hiyo, ingetuwa tena aibu nydingine kwa Wizara ya Elimu na kwa Waziri mwenye dhamana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapohapo Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Kifungu Namba 20 cha Sheria ya NECTA ya Namba 21, alielekeza tena matokeo yachakatwe upya kwa kutumia *fixed grade ranges*. Maana yake ni kwamba kwa *fixed grade ranges*, huwezi kufanya *standardisation* kwa aina yoyote ile, Walimu wote wataniunga mkono, huwezi kufanya

standardisation kwa fixed grade ranges, utafanya kwa flexible grade ranges. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri aliekeza kwamba, zile *low marks* yaani *marks* za mwisho za mtihani wanafunzi alizozipata ndio zifanyiwe *standardisation* baada ya hapo ndio sasa watumie *fixed grade ranges* ku-*grade* hizo *marks*. Hii elimu tunaipeleka wapi? Utaratibu wa aina gani na wa nchi gani huu ambapo *low marks* zinafanyiwa *standardisation*, halafu unatumia *fixed grade ranges*, nchi hii tunaipeleka wapi? (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba siku moja ukipata nafasi tembelea Baraza la Mitihani, uoneshwe *samples* za wanafunzi wanavyojeleza kwenye mitihani kwa uchungu. Wanamwandikia *Memo* Waziri Mkuu wakati wanajibu mtihani wa *chemistry* kwamba sisi hatuna Walimu tangu tumenza *Form I* mpaka *Form IV*, Mheshimiwa Waziri Mkuu tutafanya nini? (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesoma. Hii ni aibu kwa Taifa ambalo lina miaka 50, zaidi ya umri wangu mimi. Aibu kutumia siasa kwenye ku-*grade marks* za wanafunzi. Huu utaratibu umeoneshwa kwamba uwe ni endelevu, kwa faida ya nani? (Makof)

Mheshimiwa Spika, historia ya wanafunzi hawa waliomaliza mwaka 2012, walimaliza Darasa la VII mwaka 2008, walikuwa na *average* ya ufaulu ya 45. Wenzao waliomaliza 2007, *average* yao ya ufaulu Kitaifa ilikuwa ni 53. Wanafunzi hawa wa mwaka 2002 hawakufanyiwa mchujio wa Kidato cha II mwaka 2010, watafauluje hawa? Kitengo cha Ukaguzi hakifanyi kazi, Kamati ya Huduma za Jamii, nikiwa Mjumbe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Injinia Athumanzi Mfutakamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim na Mheshimiwa Ritta Kabati kama yupo.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia. Kwanza naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kueleza, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwenye ukurasa wa 176, Halmashauri ya Tabora Vijijini yaani Uyui, Uyui ina Majimbo mawili; Jimbo la Igalula na Jimbo la Tabora Kaskazini. Kwa masikitiko makubwa wakati ule wa mgawo wa maabara za Serikali, sekondari zilizopewa maabara hizo ni Sekondari ya Ndono na Idete zote ziko Tabora Kaskazini, Igalula tukasahauliwa tukavumilia. Sasa kwa bahati mbaya zaidi kwenye mgawo wa hizi sekondari ambazo zinaboresha imepewa Sekondari ya Ikongolo, Sekondari ya Lolangulu, zote Tabora Kaskazini. Mheshimiwa Waziri, naomba arekebishe hali hiyo. Pia nimeona kuna ujenzi wa Vyuo vya Ufundji Stadi, kwa Wilaya ya Uyui nimeona ni namba moja, naomba hicho chuo sasa kipelekwe Jimboni Igalula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Mwanasheria Mustapha Akunaay, hili suala la kwamba hakuna chama kinachojenga sekondari, Jumuiya ya Wazazi ya CCM ina sekondari zaidi ya 30 na wanasoma wanafunzi wa itikadi zote, wa dini zote na wa mirengu yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, CCM, *University of Dodoma, UDOM*, japokuwa haikuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lakini busara za Mwenyekiti wa CCM, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kajenga *UDOM* na wanafunzi pale wa maeneo yote wanasoma *UDOM*, Serikali ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology*, wanafunzi wanasoma Shahada za Uzamivu na Uzamili. Yote hii ni taratibu nzuri ya Wizara ya

Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Serikali ya CCM chini ya Dokta Jakaya Mrisho Kikwete; tumeteleza kidogo lakini hatukuteleza. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika Sekondari za Kata. Mimi japokuwa nina sekondari tano kwenye Jimbo la Igala, lakini ninashukuru sana Sera ya Ujenzi wa hizi Sekondari za Kata, wananchi walichangia na Serikali ilichangia, vijana tumewatoa vijiweni, tumewaweka kwenye madarasa. Sasa tunajipanga, nimepata taarifa Wizara ya Elimu na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametamka kwamba tunapata Walimu kutoka Jamaica, watakuja kufundisha masomo ya sayansi na watafundisha Kingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesoma *PCM*, kabla ya *PCM*, *O-Level*, nilipata *Division I* ya hesabu tena *Pure Mathematics*, *Physics* na *Chemistry*. Kwa hiyo, ninajua vijana wetu watapata utaratibu mzuri. Ni suala la kujipanga, tumwachie Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Philip Mulugo, warekebishe hizi dosari ndogondogo tuweze kusonga mbele na tuwape *support* kwa uhakika kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye suala la maabara pamoja na mabweni. Mimi Jimbo langu ni kubwa na linauhitaji mkubwa sana wa mabweni ya wasichana. Wananchi wako tayari kuchangia mawe, kuchangia nguvu kazi, kuchangia kokoto pamoja na mchanga na mafundi. Serikali tusaidiane ili tuweze kujenga maabara, tuokoe wanafunzi wa kike kwa sababu wanatembea kilomita 5 - 10 kila siku na athari tunazifahamu ili waweze nao kupata elimu ya kutosha tupate kina Dokta Asha-Rose Migiro wengi kutoka Igala wenye *PhD*. ili itusaidie jitihada za kuleta maendeleo kwenye Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende pia kwenye suala la maabara. Suala la maabara nalo ni muhimu siyo Jimbo la Igala tu lakini sehemu zote. Niseme kitu kimoja ni utaratibu

huu mzuri ambao mimi nimekuwa mtaalam muelekezi (*consultant*), nimekwenda kufanya kazi Lyamungo. Lyamungo kule kila kijiji kina sekondari. Mimi niwapongeze sana ndugu zetu ambao wamejenga hizi sekondari lakini nataka kusema ni utaratibu mzuri wa Sera ya Chama cha Mapinduzi kwenye elimu ndiyo tumeweza kupata, Mheshimiwa Mwanri aliniambia katika kila nyumba *per capital degree* yaani watu wenyе shahada kule kwenye Jimbo lake kila nyumba ina mtu moja ana shahada ya kwanza. Hii ni kwa sababu ya utaratibu mzuri wa Serikali ya CCM na mimi naomba mchango huu tuupeleke nchi nzima hasa sisi wenyе Majimbo pamoja na Mikoa ambayo iliyosahaulika, rasilimali sasa zielekezwe huko na sisi tuwe na mfano kama Mikoa ya wenzetu kule, tupate wataalam wengi wenyе elimu za juu na wenyе fani mbalimbali ziweze kutusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa letu. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye suala la Walimu wa sayansi na vitabu vya kiada na ziada. Tuna tatizo kubwa sekondari zangu zote tano hakuna vitabu vya kiada, hakuna vitabu vya ziada na hasa kama tunataka wanafunzi wetu waweze kutoa wataalam wengi katika fani hizi za *PCB, PCM, PMM, PGM*, kwa kweli suala la Walimu wa sayansi, hisabati na kiingereza tuongeze ile idadi. Kwa hiyo, mimi ningewomba Mheshimiwa Waziri atupe mkakati na ninajua anao na Wizara inayo, tuongeze Walimu wa Sayansi, Hisabati na wa Kiingereza. Najua Walimu wa Kiswahili tunao wa kutosha lakini tukisukuma kwa ongezeko la hawa Walimu na tuwajengee mazingira bora pamoja na Halmashauri zetu ziweze kushirikishwa ili tuwe na Walimu sisi ambao tuko katika Majimbo ya vijijini Walimu wa kutosha wapelekwe kule.

Mheshimiwa Spika, mimi katika kila sekondari nimezungumza na Waheshimiwa Madiwani, tuweke utaratibu wa kuongeza angalau nyumba moja ya Walimu na mimi nitachangia ambayo inakuwa *three in one* hata waweze kukaa Walimu watatu ili tuwavutie kwenye maeneo haya ya pembezoni lakini tusiweke walimu wote mijini. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa *DC* kule Kilolo, Walimu wote walikuwa wanataka kukaa kwenye barabara ya lami....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofii*)

SPIKA: Sasa nitamwita Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Philipa Mturano na Esther Matiko halafu nitawataja wengine.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uzima na afya njema hadi nikichangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Spika, nami kwa kuanzia, naomba nianze kwenye matokeo mabaya ya darasa la 12 mwaka 2012 pamoja na marekebisho yake ambapo pale ambapo waliopata sifuri wanafunzi 30,063 walipata daraja la nne baada ya merekebisho na waliokuwa daraja la nne wengine wakapata fursa ya kuendelea na masomo yao. Kwangu swali linakuja la kwanza, wale ambaeo walipata matokeo yasiyotarajwa baadaye wakalazimika kujinyonga au kujiua, Serikali ina mpango gani wa familia za wanafunzi wale? Naomba ukifanya majumuisho Mheshimiwa Waziri Kawambwa na Manaibu wako wote wawili, mtueleze kwa sababu matokeo yaliyotokea ya kujinyonga na kujiua yalikuwa ni makubwa zaidi, hilo lilikuwa la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili tatizo lingine la matokeo mabaya katika tafiti mbalimbali imeonekana ni suala zima la usahihishaji wa mitihani. Umakini, uadilifu umekuwa ni mdogo sana hasa. Katika hali hii, imeonekana baada ya kuwahoji Walimu mbalimbali, Walimu wanasema posho wanayopewa wakati wa kusahihisha mitihani ni kidogo,

hawana utulivu, umakini haupo. Sasa katika hili, namwomba Mheshimiwa Waziri utueleze mna mkakati gani wa kuweza kuboresha maslahi ya Walimu wakati wanaposahihisha. Hili ni jambo moja kubwa sana ni kipindi kizito, kipindi kigumu cha wakati wa kutafuta haki za wanafunzi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko pia vilevile wakati wa kuwapata hawa wanaosahihisha mitihani yetu kwamba baada ya Baraza la Mitihani kupeleka barua kwenye shule mbalimbali ni kwamba baadhi ya Walimu Wakuu wanatumia kuelewana ama undugu na urafiki. Je, hili Mheshimiwa Waziri unalijua na kama hujalisikia, je, utafanya utaratibu gani wa kuweza kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu zaidi na kuwataka Waheshimiwa Mawaziri wetu hawa, kuna tatizo ambalo linazungumzwa sana kwamba wakati wa kusahihisha mitihani kipindi kile kunakuwa na idadi ya karatasi ambazo anapangiwa Mwalimu aweze kusahihisha na muda unakuwa ni mrefu, je, hili nalo ni kwa nini utaratibu huu kama ni kweli unatumika vibaya?

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pia na Waziri amegusiagusia baada ya tatizo hili kutokea, akasema siyo wakati wa kulaumiana, tusitafute mchawi, yote yakasemwa hayo tutafute suluhisho. Mimi nataka niseme moja tu kwamba kila Mbunge hapa alikuwa akiongelea kwa ukali sana mchawi mwingine kuwa ni bodi kwamba ina matatizo, Mheshimiwa Waziri vunja bodi, bodi ina matatizo, bodi ina madudu kama huwezi kuvunja itakunja wewe, shauri yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme tu kwamba mambo haya yamekuwa ni mazito sana. Wanafunzi wetu wakiwa hawafaulu inakuwa na tatizo ambapo kila mtu anapiga kelele. Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri pamoja na michakato yote inayokuja, niombe Serikali na kupitia Katibu Mtendaji Ndalichako, mtupe semina angalau ndogo kuhusu *fixed grade range* na *flexible grade range*, ili tuelewe nini kilichopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la madai na malalamiko ya Walimu. Miaka miwili, mitatu iliyopita wakati wa sherehe ya Siku ya Walimu Duniani kule Mtwara, Rais wa Jamhuri alikubali kuwapatia Walimu posho ya kufundishia yaani *teaching allowance* mpaka leo mmebakia kimya nyie Serikali tatizo nini, mna kigugumizi gani kwa nini hamtekelezi ahadi ya Rais? Mmewahidi Walimu, Walimu wanalamika, Walimu wanasononeka hamwatekelezei kile ambacho mmesema, ni jambo kubwa alisema Rais kule Mtwara jamani, *teaching allowance*, posho za kufundishia, lini itapatikana, Mheshimiwa Mulugo, *mbukwenyi!*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niishauri Serikali ni kuhusu mafunzo ya Walimu kazini, *in service training*. Vituo hivi viboreshwe, zijengwe *Teachers Resource Centre* yaani (*TRCs*) itapelekea Walimu kufanya kazi na kupata mafunzo kwa gharama nafuu. *Teachers Resource Centre*, mmeziacha, pangeni mikakati yenu baadaye mje mtuambie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna Walimu walioajiriwa hivi karibuni ambao walitakiwa wapate *perdiem* ndani ya siku saba, hamjawapa, wanalamika wengine wamepata, wengine bado. Hilo mnalo na malalamiko hayo mnayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelewa vilevile ni Walimu wangapi wamepigwa na wanavijiji katika maeneo tofauti ama wamevunjiwa heshima nyingine, mkija mtueleze hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, usafiri wa wanafunzi, hakuna asiyejua, miaka mitatu iliyopita wanafunzi kule Rufiji walikuwa wakivuka mto kwa kutumia mtumbwi na walikufa nane. Mkaenda kule Serikali mkasoma risala, msoma risala akatoa machozi, Walimu nao walilia wengine kule, wazee wakalia, wanafunzi walilia kupita kiasi na mliahidi mtapeleka boti ya kisasa, mkaesema jambo lile la vifo vyta wanafunzi itakuwa ni historia. Hamjapeleka boti, mlisema uongo mchana kweupe bila giza, acheni wanalamika. Mlisema

mtapeleka boti ya kisasa, ya kileo ambayo itaweza kuharakisha kupatikana kwa usafiri mzuri, hamjapeleka boti. Jamani, hivi ninyi mnatoa machozi kumbe yalikuwa siyo ya kweli, ya uongo, hamwoni haya, hamwoni vibaya, acheni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine kwa haraka haraka, muda unakwenda. Naomba niishauri Serikali, Chombo cha Kusimamia Taaluma ya Walimu (*Teachers Professional Board*), lini mtakiunda chombo hiki? Mbona kuna kusuasua, malalamiko yamekuwa mengi na ya muda mrefu, kigugumizi kiko wapi, tatizo nini?

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, mwenzangu Mheshimiwa Mbatia alisema pale, tatizo la kudhibiti vitabu visivyo na ubora, Serikali andaeni Muswada wa Sheria mtuletee hapa namna ya kudhibiti vitabu vile maana vitabu feki ni vingi, vinapotosha maendeleo yetu ya elimu na ninyi mmebakia kimya wakati ninyi ndio wenyewe dhamana, sisi tutawaambieni ninyi tu. Tatizo ni nini, kwa nini hamleti Muswada wa Sheria kudhibiti vitabu feki, mambo yamekuwa ni mengi hapa, tunasema sana tu Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachelea kupeleka *format za mitihani ili Walimu sasa nao wajitayarische*. Tatizo hili ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kidogo limepigiwa kelele sana, mnaajiri Walimu ambao hawana sifa na pia hawana taaluma ya ualimu. Hizi ni kelele zinapigwa sana. Tabia hii hasa lini mtaiaacha kwa sababu mnalifahamu, limekuwa ni la muda mrefu. Tatizo lenu ninyi hamtaki kutekeleza yale ambayo sisi tunawashauri, kwa nini basi mmekuwa na kigugumizi kikubwa? Mimi nadhani kwa vyovoyote vile Serikali ni vyema ikae kitako, yale ambayo sisi tunayazungumza hapa, tunapendekeza basi waweze kuyafanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wenu walioko rje ya nchi wengine hawasomi na wazazi nawaambieni kuitia

hana kuwa baadhi ya wanafunzi walioko nje hawasomi. Mnapeleka fedha, mfuatilie, wanawadanganya. Wanafunzi wenu walioko nje wengine wanafanya biashara, ni aibu, mnafikiria kwamba mmewapeleka huko wanasona, hawasomi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana. Naomba Mheshimiwa Philipa Mturano na Mheshimiwa Esther Matiko dakika tano tano halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Njwayo.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mama Ndlichako kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Tangu ameingia pale uvujaji wa mitihani umepungua sana. Anafanya kazi kubwa sana mwanamke huyu, tumpongeze na tusimvunje moyo, anafanya kazi kubwa sana, *big up* Mama Ndlichako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako nimjibu mdogo wangu Mwigulu. Amesema kwamba tunalalamika bure tunahujumu elimu wakati tunajua tatizo liliopo kwamba bajeti ni finyu. Mimi nataka nimwambie kwamba suala la bajeti kuwa finyu ni lingine na suala la uhujumu wa elimu ni kitu kingine. Watunzi wa vitabu ambavyo vinafundishwa shulen, tumeandika kwenye hotuba yetu ukurasa wa 48 - 49 mnaweza mkasoma, moja ya Kampuni ambayo inatunga vitabu vinavyofundishwa katika shule zetu na vitabu ambavyo vimethibitishwa kwamba vinatoa *material* feki, ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni nani anayehujumu elimu kama siyo wao na ye ye ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala ambacho ndicho kilichotoa

Mbunge huyu, ambacho ndicho kimetoa Mawaziri hawa. Ni lazima tusema kwamba wao ndiyo wanaohujumu elimu. Kinachotakiwa hapa tuwe kitu kimoja, tutafute *solution* lakini siyo kunyosheana vidole, nimetaka nimjibu kwa hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano, mwezi Mei alisema kabisa kwamba kuna udhaifu katika elimu kwa sababu mitaala pia ina migogoro. Hilo linaonekana na linajulikana, Mheshimiwa Mbatia alisema lakini alipuuzwa hapa. Tunaomba hilo lifanyiwe kazi. Hizo ni hujuma nyingine. Sasa kama Mheshimiwa Waziri wewe ambaye ndiye Mkuu wa Wizara hii ni lazima tukuseme kwa sababu wewe ni msimamiaji wa Wizara hii, kama watu wanakuhujumu ndani ya Wizara, ni wewe uwaangalie na uwafahamu, sisi lazima tukuambie wewe. Mtani anapokuwa jirani yake amefariki mtani kazi yake ni kumweleza yule mtu kwamba anapaswa afanye hivi bila kumwonea haya, bila kumwogopa na hili inamsaidia kuweza kujipanga sawasawa wakati mwingine asirudie kufanya vitu kama vile na sisi ni lazima tuseme ili Mawaziri hawa wa Wizara ya Elimu wajue kwamba hatupendi na wala Watanzania hawatakubali kuona watoto wao wanachezewa. Hii ni sehemu pekee ya kuweza kumtoa Mtanzania ambaye ni maskini kuweza kupata elimu na kufikia ndoto zake anazozitaka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Temeke, katika kitengo cha *TSD*, hakuna vitendea kazi, hakuna *computer*, je, kumbukumbu hizi za Walimu zitapatikana wapi? Walimu wanadai madaraja yao, hakuna sehemu ya kutunza kumbukumbu. Akitaka kutunza kumbukumbu aende akaombe *computer* sehemu nyingine hapohapo habari zina-leak. Ni kwa nini vitengo hivi havipatiwi vifaa na bajeti zinatengwa kila siku, ni kwa nini basi tusilalamike? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni lazima tuilaumu Serikali, wanapanga Walimu katika maeneo yao kufanya kazi lakini haohao ndiyo wanaoleta vi-note vyenye shinikizo Mwalimu huyu mwondoe, mpeleke sehemu fulani matokeo yake baadhi ya shule hazina Walimu, baadhi ya shule zina Walimu wengi. Ni lazima tuseme Serikali muarubaini huo

muumeze ili muweze kututendea haki. Hatuwezi kukubali kuona kwamba Watanzania wanaendelea kuhujumiwa katika nchi yao. Nimesema kwamba ni sehemu pekee ambayo inaweza ikamtoa hata yule maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ambacho mimi nataka niseme ni mazingira ya shule. Shule zetu unakuta zimezungukwa na baa, *guest house* na sehemu za starehe. Mtoto akitoka shule anadakwa huku baa, huku *guest house*, huku muziki unapigwa, huyu mtoto atakuwa katika mazingira gani, lazima ashawishike. Ni nani anayetoa vibali, ni Serikali! Ni kwa nini shule tusiziache zikawa katika mazingira ambayo ni rafiki, mazingira ambayo hayataweza kumu-*entertain* mtoto kuingia katika vitendo viovu? Watoto unakuta wanacheza *pool/mchana*, ni kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati Mheshimiwa Makamba akiwa Katibu Mkuu alilikemea hili kwamba hizi *pool* zisichezwe mchana lakini zinaendelea kuchezwa na watoto wanacheza...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami naomba nijibu kidogo kwa wachangiaji wawili Wabunge wa CCM waliotangulia. Kwanza Mheshimiwa Mfutakamba, sijawahi kusikia kuna *division one* ya hesabu najua kuna 'A' ya hesabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili Mwigulu Nchemba wakati anachangia alisema kwamba kushuka kwa elimu ni kwa sababu ya *over expansion* ya shule. Hivi ninavyoongea kuna wanafunzi wanasoma kwenye miti, kuna shule unakuta madarasa mawili tofauti wanasoma kwenye darasa moja, kuna ubao mwengine mbele, ubao mwengine nyuma. Hasa hii *over expansion* ina maana hawana wataalam wa kuwashauri wasi-expand zaidi lakini wahakikishe

wanakarabati shule zilizopo na kuongeza shule kwenye sehemu zile ambazo wanasomea kwenye miti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuchangia kwanza kabisa kwa Wizara kutopeleka fedha za maendeleo kwenye vyuo vikuu vyetu. Unakuta tunapitisha fedha kwa mfano Chuo Kikuu cha Ardhi kwa mwaka 2011/2012 zilipitishwa shilingi bilioni moja, milioni mia tano hamsini lakini walipelekewa 7.6% tu ambayo ni sawasawa na 117,000,000. Mwaka 2012/2013 hawakupeleka hata asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, vyuo vikuu vina changamoto nyingi kwa mfano Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam miundombinu yao ni chakavu, ni vyuo vya zamani, kuna uhaba wa *lecture theatres*. Mimi nakumbuka wakati nafundisha pale, unakuta hadi wanafunzi wanakuwa wanasimama nje wakati wanakusikiliza Mwalimu ukifundisha. Tunatumia teknolojia ambayo ni ya zamani vyuo vikuu na hii yote ni kwa sababu hawapelekewi fedha za maendeleo, zinapitishwa lakini hampeleki. Tunaomba kabisa muwe mnapaleka fedha za maendeleo kwenye vyuo vikuu vyetu, mabweni ni machakavu pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia pia kuhusu utungaji wa mitihani hasa kwa shule za misingi na sekondari. Siafiki kabisa kwa wanafunzi wa shule za misingi kutungiwa mitihani ya kuchagua au *multiple choice* na hasa kwa somo la hisabati. Huku ni kuua elimu. Mimi ni Mwalimu wa hesabu, hauwezi ukamtungia mwanafunzi wa shule ya msingi *multiple choice* hisabati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa Wizara hii nillleta mfano, kuna mtihani wa *mock* ultungwa Mara, maswali zaidi ya kumi yamekosewa, ni *multiple choice* lakini yote hamna majibu sahihi. Mwanafunzi anapoteza muda na hamna jibu sahihi pale na nikauliza huyu mwanafunzi au Mwalimu anaenda kusahihisha nini kwa sababu mtihani mzima umekosewa. Kwa hiyo, naomba kabisa Wizara mfute mtihani wa *multiple choice* hasa wa hesabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia pia, kuhusu upungufu wa Walimu. Uwiano kati ya Mwalimu na wanafunzi kwenye shule nyingine ni Mwalimu mmoja, wanafunzi 600. Mwaka jana wakati naangalia taarifa ya habari, nafikiri ni shule ya msingi Pwani au Dar es Salaam kwenye Wilaya za pembezoni. Mwalimu ni mmoja, Mwalimu huyo mmoja ni Mwalimu Mkuu, ndio Mwalimu wa *academics* na ndio Mwalimu wa nidhamu na masomo yote wa kuwafundisha wanafunzi wote wa shule hiyo ya msingi. Halafu mnategemea miujiza ipi watoto hawa wafaulu?

Mheshimiwa Spika, kwanza, wakae chini hakuna madawati, hakuna vitabu vya kutosha, hakuna Walimu wa kuwafundisha. Ningomba tuwe wakweli kama kweli tuna dhamira ya kweli ya kuweza kukuza elimu yetu. Hakuna mactaba, hakuna maabara, hakuna madawati, mwisho wa siku wanatungiwa mtihani sawa na wanafunzi ambao wana Walimu wa kutosha, vitabu na maabara, hii siyo haki.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka sana na kwa dakika zangu chache nitazungumzia pia *EMAC*. *EMAC* rushwa inatawala sana, *Oxford walikataliwa*, walipigwa marufuku ku-supply vitabu Tanzania, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kushangaza kuna vitabu tena kwa kutumia fedha za RADA vinaingizwa nchini pamoja na upungufu wote ulioainishwa, vinasambazwa Tanzania, hii inaendelea kudidimiza elimu yetu. Tunaomba hii *EMAC* ichunguze kwa makini, na hata ikiwezekana wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie kuhusu miundombinu sasa kwa ujumla wake. Miundombinu ya shule zetu za misingi na sekondari. Shule zetu za sekondari hazina maabara, zote za Kata hizi mnazojivunia, hazina maabara, hazina Maktaba, hazina walimu wa kutosha wa *chemistry, biology, physics* na *mathematics...*

(*Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi mchana huu ili niungane na wenzangu kuchangia hoja iliyoko mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana maana nilikata tamaa kwamba, pengine nisingeweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja. Pia, naamini sana kwenye *Law of Nature*. *Law of Nature* moja ya zile sheria tatu zinasema, *where there is positivity, there is negativity as well*. Nataka niiambie Serikali yapo mafaniko na zipo changamoto. Kwa hiyo, ni wajibu wenu kama Serikali mlioko madarakani sasa, kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha changamoto hizo zinapungua au zinakwisha kabisa. Hii itapunguza maneno maneno, mwongeze jitihada, mwongeze juhudhi mambo yapungue.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao:-

Kwanza, liko jambo la llani, katika uchaguzi wa mwaka 2010. Moja ya mambo kwenye Sekta ya Elimu ilikuwa ni kuhakikisha tunakuwa na shule ya kidato cha tano na sita kila Tarafa. Wananchi wa Tandahimba wamejitalidi kwenye hili jambo, tumewekeza pale Tandahimba kwenye shule yetu ya sekondari. Majengo ya kutosha, tume-retain Walimu wa kutosha kwa ajili ya *combination* za HGK na HGL.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza, pamoja na kupewa barua mwaka 2011, yenye Kumb.Na. EM.667Vol.1/144 ya terehe 4 Julai, 2010 na kupewa namba ya usajili wa shule kuwa kidato cha tano, namba S. 677 mpaka leo tunavyoongea shule ile haijapata wanafunzi. Uwekezaji uliofanywa kule, kama Mbunge napigwiwa kelele, Mkurugenzi anapigwiwa kelele na DC anapigwiwa kelele.

Mheshimiwa Spika, naomba *selection* hii ihakikishe inapeleka wanafunzi pale. Inawezekana kwa sababu *combination* hizi zilikuwa ni kwa wasichana, siyo lazima tuwapeleka wasichana tu! Tunaweza tukaifanya co-

education school. Tukawapeleka wasichana na wavulana, ili *investment* kubwa iliyofanywa pale, isadifu nia ya dhati tulyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine, ni kwamba, huko nyuma Walimu tuliwapa kitu kinachoitwa *teaching allowance* na kwa kweli ilisaidia sana kujenga motisha kwa Walimu. Walimu walipata uhakika wa kuandaa *lesson plan* zao, kutafuta zana za kufundishia na kujifunzia. Kuhakikisha wanasahihisha kazi za wanafunzi, kufuatilia na kusoma vitabu vyta ziada, ili kuongeza maarifa kwa Walimu wenyewe na kwenye masomo husika.

Mheshimiwa Spika, hali sasa imekuwa tofauti, Walimu hawafanyi hayo, kwa sababu wanahangaika na mambo ya maisha huku duniani. Hakuna mtu anayehangaika na *lesson plan* leo, hakuna anayehangaika kujenga maarifa, maana njaa kali. Turudishe utaratibu ule ili tuongeze tija kwenye elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine. Katika utaratibu zoezi lile la ugatuaji, tuliwapunguza sana Walimu wa shule za sekondari tukawapeleka TAMISEMI kwa maana ya Halmashauri zetu. Tukawaacha Walimu wa vyuo wahudumiwe na Wizara, ili huduma iwe nyepesi na rahisi.

Mheshimiwa Spika, kilichopo sasa hali ni ngumu sana kwa Walimu wa vyuo. Huduma kwa ujumla siyo nzuri, Walimu wa vyuo kupanda kwao madaraja ni shida. Fedha za likizo hawapati, huduma nyingine za msingi walizonazo zinachukua muda mrefu na kwa hiyo, utendaji wenyewe umekuwa siyo mzuri sana. Naomba tutengeneze utaratibu mzuri wa kuboresha utendaji wa Walimu wa vyuo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, liko jambo kwenye hivi vyuo. Kuna shule hizi za mazoezi, Mwalimu anapoajiriwa kuanza kazi kwenye shule za mazoezi mwaka wa kwanza, anafanya kazi hapo mpaka anazeekea hapo. Anamfundisha mtoto, anamfundisha baba, anamfundisha mjukuu. Hivi kweli tutajenga ufanisi?

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa wa kubadilika kuendana na muda. Huwezi kumfanya mtu acae kituo kimoja mpaka anastaafu, anapofikia miaka 60. Huwezi kutengeneza ufanisi hapa, naomba Serikali hasa Wizara hii ya elimu, iangalie upya, tuangalie utaratibu ambao utajenga kwa Walimu wale kwenye vyuo vyetu hivi na shule za mazoezi.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine pia, jambo lenyewe ni kwamba, ningependa kushauri hapa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kimetusaidia sana kupunguza *gap* la wataalam hapa nchini, hasa kwenye sheria na ualimu na kwa kweli, elimu inayotolewa ni bora tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza udahili na nini, kwa mfano, mwaka jana tumeambiwa hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba, kulikuwa na udahili kwa watu wanaofanya shahada za Uzamili na Uzamivu waliofikia 2,391. Idadi hii ni kubwa kuliko chuo chochote cha *Conversional University* hapa kuchukua watu 2,300 na ushee. Hata hivyo, kilichoko kule pamoja na udahili huu mkubwa unaofanywa na hata wale walio *undergraduate* kuna shida kubwa ya mafungu. Kuna shida kubwa ya fedha za kuendeshea chuo. Ni vizuri sasa Wizara na Serikali kwa ujumla, tukawapa pesa za kutosha ili waendelee kupunguza *gap*, la watu wenye taaluma nchini.

Mheshimiwa Spika, zaidi, nataka pia nishauri uongozi wa chuo na wenyewe una ukiritimba wake pale. Kwa mfano, juzi hapa tumeanzisha ujenzi wa ghorofa kumi, lile jengo la mradi wa Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu. Hivi kwa nini halikujengwa, kwenye kituo chao cha Kibaha, Makao Makuu ya Chuo. Kwa nini wameendelea kuwekeza pale? Kwa nini tuna-*congest* Dar es Salaam *unnecessary*? Halafu hata Mkoa wa Pwani hauna Chuo Kikuu hata kimoja. Wangekwenda pale, ingeleta maana fulani kwa Watanzania na kwa watu wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, iko kada ya Waratibu Elimu wa Kata. Sioni wanafanya nini? Hebu Serikali iwatazame upya, Waratibu Elimu wa Kata ni matatizo, sasa hizi wanafanya siasa

tu kule. Inawezekana hawana vitendea kazi, inawezekana hawajatengenezewa mazingira mazuri. Basi, kama hatuwatoi, tuwatengenezee mazingira mazuri yanayoweza kuchochea tija na ufanisi kwenye elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba kufanya mabadiliko kidogo kwenye wakaguzi wetu wa elimu. Kwa hali iliyoko sasa ni kwamba, ngazi ya shule ya msingi wanafanya kule kwenye...

*(Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mungu akubariki sana na Watanzania wote tubarikiwe. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Njwayo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kiwango cha ufaulu katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi na sekondari kinapanda hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2015, ni muhimu sana Walimu wakawekewa mazingira mazuri ya kufundisha ikiwa ni pamoja na maslahi mazuri na ya kutosha, mishahara inayoridhisha, vitendea kazi vya kisasa, zikiwemo nyumba.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni muhimu sana Walimu wakapatiwa elimu ya muda mfupi mara kwa mara (*refresher courses*) ili kuendana na hali ya sasa na kuwapa uelewa wa njia na mbinu mpya za ufundishaji. Hiyo itakuwa ni sawa na kuwapa motisha Walimu amba wengi wao wamekata tamaa ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Walimu wengi wa lugha kwa mfano Kiswahili na Kiingereza, hawana ustadi wa kutosha kuongea na kuandika lugha hizo kwa ufasaha. Matokeo yake kile wanachokijua ndicho wanachowafundisha wanafunzi na

ndio maana tunakuwa na wanafunzi wengi hata waliofika chuo kikuu wasiweza kuongea na kuandika Kiswahili au Kiingereza moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, badala yake huchanganya lugha hizo na kupata kitu kinachoitwa huko mitaani *Kisw anglish*. *Kisw anglish* sio Kiswahili na wala sio Kiingereza na wala *Kisw anglish* sio lugha rasmi ya kufundishia shulenii lakini kwa kipindi kirefu kimeruhusiwa kutumika kufundishia wanafunzi wetu jambo ambalo limeleta madhara makubwa na uharibifu wa lugha hizo ambazo kimsingi zinatakiwa zitumike kila moja peke yake, tena kwa ufasaha badala yake zinavunjwavunjwa.

Mheshimiwa Spika, wataalam wa lugha waliobobeaa wanakiri kwamba uelewa wa lugha fulani ni pamoja na kujua mila na desturi za watumlaji wa lugha husika. Tunaporuhusu *Kisw anglish* kutumika, je, tunadumisha mila na desturi za lugha gani? Wastaarabu wa kale, karne zilizopita, walijua wamestaarabika kwa kujifunza na kuitumia lugha katika ukamilifu wake, yaani kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Walimu wetu wa lugha ni vema wakapata *study tours*, safari za mafunzo za mara kwa mara katika nchi zinazozungumza lugha ile anayoitumia kufundishia ili waendelee kuboresha na kuinua kiwango cha lugha wanachojua na hivyo kuwa Walimu bora zaidi. Hii itapunguza kuendelea kuwategemea Walimu kutoka nchi jirani ya Kenya ambaa kimsingi wanapata nafasi za kazi katika shule za binafsi zaidi.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu nchini kwa sasa umekosa dira sahihi. Katika kipindi cha sera ya ujamaa na kujitegemea tulikuwa na dira ya elimu ya kujitegemea lakini je, kwa sasa nchi yetu inafuata dira ipi ya elimu? Wote tunakumbuka kwamba Sera ya Elimu ya 1995 inasema wazi kuwa msingi wa kupata cheti cha kuhitimu ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo utakuwa ni upimaji na tathmini ya kila siku na matokeo ya mtihani wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia mifumo hiyo ya kutathiniwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ikiwa amefeli na tunaona ikitoa matokeo ya kushangaza kwa kuruhusu wasiojua kusoma na kuandika kufaulu mitihani. Ni dhahiri kwamba Watanzania tunahitaji kuwa na Sera mpya ya Elimu itakayotoa mwongozo sahihi na wenyе tija katika kuwatahini wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanamaliza shule/ elimu ya sekondari wakiwa hawawezi kujitegemea kwa kukosa maandalizi mazuri. Tunahitaji sera mpya itakayokuwa na mpango wa kuimarisha elimu ya ufundi na ujasiriamali shulenii. Hii ina maana kwamba itakuwa ni Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya masomo, vijana wataweza kujiajiri kutokana na elimu ya ufundi watakayokuwa wameipata. Hata Walimu nao watapata nafasi ya kujiedeleza kitaaluma na hivyo kuwa na Walimu bora wanaoendana na wakati uliopita.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, ni lazima tukakubali kwamba kuwapo kwa Sera makini ya Elimu pamoja na mkakati imara wa utekelezaji, hutoa mwongozo/ mwelekeo mzuri wa elimu. Hivyo basi, Sera nzuri ya Elimu husaidia kutoa mwongozo wa upatikanaji wa fursa za elimu na namna ya kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, tutapata Watanzania walioelimika na wenyе ujuzi na maarifa katika kuchangia maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kinyume na hapo, Taifa litaendelea kutia aibu. Dunia nzima inaona kinachoendelea katika sekta ya elimu. Hivi sasa dunia imekuwa ya elimu. Hivi sasa dunia imekuwa ndogo, kama wanavyosema wengine imekuwa kijiji.

Mheshimiwa Spika, hakuna kinachofanyika kijijini na wanakijiji wengine wasijue, ni dhahiri kwamba yale yote yanayotokea katika elimu hapa Tanzania, dunia nzima inajua na inatushangaa kwamba ni kwa nini hatushtuki na kurekebisha mambo kwa kutengeneza Sera nzuri ya Elimu

itakayoweza kuleta mageuzi/mwongozo mzuri wa kubadilisha elimu yetu na kuifanya yenye kuleta tija kwa watoto wetu na kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa tunasikia katika vyombo vya habari kwamba shule fulani katika Mkoa fulani imefungwa kwa kukosa matundu ya choo. Watanzania kwa ujumla wake wamelemaa kwani hivi kweli wanakijiji wanashindwa kuchimba matundu ya choo kwa ajili ya shule iliyopo kijijini?

Mheshimiwa Spika, Watanzania sijui wamepatwa na nini, wanasubiri mfadhili awajengee. Inaelekea ndivyo walivyolelewa kuombewa misaada nchi za nje. Tujitegemee kwa yale yaliyo katika uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, ukurasa wa 99 – 100, Mamlaka ya Elimu Tanzania katika 2013/2014 itaendelea kukamilisha taratibu za kubadilisha Sheria ya Mfuko wa Elimu No. 8 ya mwaka 2001 ili kuupatia Mfuko vyanzo vya mapato vya uhakika na endelevu. Pia kuendelea na uchangishaji wa rasilimali ili kupata shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana katika maeneo yaliyotajwa katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyiningine itakayofanywa na Mamlaka ya Elimu ni kuandaa maandiko ya miradi 12 ya kuwasilisha kwa wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi ili kupata fedha kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo. Pia kuendelea kufadhili mpango wa *Pre-entry* kwa wanafunzi wa kike wanaojiunga na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Mghembe amezungumza katika vyombo vya habari kwamba Serikali itatenga shilingi milioni 300 kila mwaka kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Elimu ya Ufundı wa Maji (*WTF*) ambao una lengo la kuwasaidia wanafunzi wenye wazazi wasio na uwezo kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Maghembe alisema wakati wa uzinduzi wa Mfuko huo kwamba mbali na Serikali kutoa fedha hizo lakini pia itawashawishi wahisani wengine kuchangia Mfuko huo. Alisema wanafunzi ambao si wa elimu ya juu, wengi wamekuwa wakishindwa kumaliza masomo yao licha ya kuwa na uwezo mkubwa kitaaluma kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo kifedha.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni hodari sana wa kuanzisha *programu* nyingi zinazofanya jambo lilelile. Pia Mifuko mingine imeanzishwa kwa faida ya wanaouendesha. Ni kwa nini Wizara ya Mheshimiwa Maghembe iwe na Mfuko wa Elimu na kutafuta ufadhili kutoka nje na ndani kwa ajili ya wanafunzi wenyewe wazazi wasiojiweza wakati Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı pia inafanya kitu hichohicho? Je, ni Mamlaka gani itasimamia Mifuko hiyo ili kuhakikisha fedha inayotafutwa kwa wafadhili inawafikila walengwa?

Mheshimiwa Spika, katika uzinduzi wa Mfuko huo aliouelezea Prof. Maghembe, Dkt. Diana Mwiru ambaye ndiye Mwenyekiti wa Mfuko huo alisema ameweka lengo la kukusanya shilingi billioni 4.6 katika kipindi cha miaka mitano. Inatia shaka, Mifuko mingi inapoanzishwa ili kufanya jambo linalofanana. Serikali iwe makini sana, inaposhindwa kusimamia Mifuko iliyopo, je, itawezaje kusimamia Mifuko ya Fedha ya Ufadhilli inapoongezeka?

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali kuititia Mamlaka ya Elimu Tanzania itaendelea kuwafadhili wanafunzi wa kike wanaojiunga na vyuo vya ufundı, pamoja na kutafuta fedha nje kwa wafadhili na hapohapo Serikali itatenga kila mwaka shilingi milioni 300 kuwasaidia wanafunzi wenyewe wazazi wasio na uwezo kuititia Mfuko mpya ulioanzishwa kwenye Wizara ya Maji, je, Wizara ya Elimu imeshindwa kusimamia? Ni kwa nini Mfuko huu mpya chini ya Wizara ya Maji ufanye kazi ileile ya Mamlaka ya Elimu Tanzania?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hotuba yake kuhusu uanzishwaji wa Mfuko huo chini ya Wizara ya Maji ambao

kimsingi unafanya kazi ileile ya Mamlaka ya Elimu Tanzania. Je, huo utaratibu sio matumizi mabaya ya fedha za wafadhili? Kwani Mifuko inapokuwa mingi ni dhahiri kwamba usimamizi wake unakuwa mgumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa William Lukuvi alitoa uamuza wa kufuta matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012 yaliyotangazwa mwishoni mwa Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, uamuza huo wa Serikali unadaiwa kufikiwa mara baada ya Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu, Mizengo Pinda kuchunguza kiini cha kushuka kwa kiwango cha elimu kwa matokeo ya kidato cha nne, 2012 ambayo yalioneckana kuwa mabaya zaidi kuliko miaka yote illyotangulia.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Tume kukabidhi ripoti ya uchunguzi kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lukuvi alisema kwamba Serikali kupitia Baraza la Mitihani walijadili katika kikao chao na kuamua kwamba matokeo ya 2012 ya kidato cha nne yafutwe. Uamuza ukatolewa wa *standardization* ili wanafunzi wengi zaidi waweze kufaulu ikilinganishwa na matokeo ya awali na mfumo wa zamani utumike kusahihisha.

Mheshimiwa Spika, uamuza huo wa Serikali ulisababisha madhara makubwa, tumesikia wapo wanafunzi waliopoteza maisha yao kwa kujua, wadau mbalimbali wa elimu wanauliza wanafuta, je, uamuza huo wa Serikali kufuta matokeo ya kidato cha nne ndio suluhisho kuhusu mustakabali mzima wa elimu nchini? Uamuza huo wa Serikali ulifanyika kisiasa zaidi kwani sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo katika hali halisi ndio chanzo cha hayo yote.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa wa Shirika lisilo la Kiserikali (*Tanzania Coalition on Debt and Development – TCDD*) na kutolewa Januari, 2013. Katika utafiti ule, *TCDD*

iliangalia pamoja na mambo mengine kuchunguza ni kwa kiwango gani malengo ya MKUKUTA katika sekta ya elimu na afya yamefikiwa na jitihada gani zinahitajika kuchukuliwa ili kuboresha mkakati huo. Pia kuchunguza usahihi katika uandaaji wa bajeti ya elimu ya msingi katika Wilaya zilizochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo sugu yaliyogundulika baada ya utafiti huo, mengine yanafahamika na niyaelezee kama ifuatavyo:-

(i) Ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari;

(ii) Uwiano kati ya idadi ya wanafunzi na Walimu hailingani, Walimu ni wachache, idadi ya wanafunzi ni kubwa sana;

(iii) Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa shule za awali/msingi ni mabovu;

(iv) Bajeti ya elimu ni ndogo sana na miundombinu ni mibovu; na

(v) Idadi ya wanafunzi walioacha shule ni kubwa sana, mfano ultolewa wa Wilaya ya Iramba ambayo mwaka 2009 ilikuwa na wanafunzi 2,457 walioacha shule na mwaka 2010 ni wanafunzi 2,611. Kwa ujumla wake tangu mwaka 2009 – 2011, wastani wa wanafunzi walioacha shule ni 51.9% Wilayani Iramba.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuacha shule kwa wanafunzi wengi ni umaskini wa wazazi na walezi. Wengi wana vipato vidogo na duni, kitu ambacho kinasababisha kushindwa kumudu gharama za msingi na mahitaji ya watoto. Jambo hilo hupelekea watoto kuacha shule na kujingiza katika biashara ndogondogo na hatimaye kuishia kuishi katika mazingira hatarishi – barabarani.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wengi wa kike huacha

shule kutokana na mimba. Ukosefu wa mabweni unachangia watoto wa kike waishio mbali na shule kuingia katika ushawishi na kupata mimba. Wazazi wengine wamechangia watoto wao wa kike kuacha shule. Yapo makabila yanayowaoza watoto wao wa kike mapema kutokana na mahitaji ya fedha.

Mheshimiwa Spika, wazazi wengi bado hawana mwamko na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa elimu. Hivyo inakuwa rahisi kwao kuwaachisha watoto wao wa kike ili wakaolewe. Hata hivyo, wapo wanafunzi wengi waliofiwa na wazazi wao kutokana na janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwa kutenga bajeti ya kutosha kwani ni nyingi sana, haiwezekani kuziorodhesha zote katika karatasi hii. Aidha, watoto waliofiwa na wazazi kutokana na UKIMWI wapatiwe ufadhilli na Serikali kwa mahitaji yao muhimu kama elimu kwani ndio urithi pekee ambaao wangeweza kuupata kutoka kwa wazazi wao ambaao kwa bahati mbaya wametangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, habari ya Serikali kujiveka kwenye mtego wa kuwapatia wanafunzi elimu ya sekondari, kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne na huku bado hata utekelezaji wa awali wa shule za msingi na sekondari unashindikana kwa kutokuwa na Walimu wa kutosha, hamuoni kama mnazidi kujifunga? Ikiwa mnakusudia kufanya basi jitahidini ni mpango huo usogezwe mbele ili Serikali iweze kujipanga vizuri, usije ukaiingiza Serikali kwenye migogoro.

Mheshimiwa Spika, watoto wa miaka mitatu kupelekwa shule katika umri huo ni kukifanya kizazi kijacho kisijue hata wazazi wala ndugu na watoto hao kuona ving'amuza kama ndio ndugu zao. Umri huo wa miaka mitatu ndio wa kuanza kujua au kuona na kutambua utamu wa wazazi, ndio muda wa kukabiliwa na maradhi, ndio muda ambaao bado anaendelea na *clinic* na si hivyo tu bado

anakuwa anajinyea, wengine umri huo hawajaanza hata kutembea na wengine hata kusema bado hivi mnatupeleka wapi? Kama ni kuwapeleka kwenye vituo vya kulea watoto sawasawa kabisa, kwa hili la watoto mnazidi kujipa kazi za ziada wakati hata zingine bado zinashindikana, kwa hili siungi mkono kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, majukumu yagawanywe kati shule za msingi na sekondari, kuwe na chombo kinachojitegemea kwani shule za msingi na sekondari ndiyo mizizi ya elimu ili iweze kusimamiwa kwa ukaribu zaidi. Shule zimekuwa nyingi kupindukia na vyuo kwa vile siyo vingi kama shule za msingi au sekondari navyo viwe na mfumo wake, vijitegemee viwe na chombo chao.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanaokaa katika mazingira magumu, Serikali ihakikishe wanapewa kipaumbele cha elimu hasa Mikoa kama Sumbawanga au Mkoa wa Rukwa tuliosahaulika. Shule nyingi za Mkoa wa Rukwa ambazo ziko pembezoni hasa mwambao wa Ziwa Tanganyika hazina Walimu kabisa. Unaweza kukuta shule ina Walimu wawili au watatu, shule za msingi na sekondari Walimu wanne au watano tu, hivi hizo sekondari mtaziendeshaje kwa mtindo huo? Aidha, hazina maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, elimu imeshuka kwa kasi sana, kazi ya wanafunzi ni kujipamba na uzinzi uliokithiri mipaka. Nilidhani Walimu ndio wangeruhusiwa kujipamba kwa kiasi kwa sababu wana maisha yao lakini hawa tegemezi (wanafunzi) wamejikuta wakiwa kwenye mitego ya uchafu usiokuwa na kiasi na ulevi wa kupindukia. Hivi Serikali ina mpango gani wa kuokoa hiyo jamii juha ya wanafunzi inayokimbilia sana kwenye maporomoko ya uchafu?

Mheshimiwa Spika, katika kuwawayibisha Mawaziri wote wahusike, TAMISEMI, Utumishi wa Umma na Elimu na Mafunzo ya Ufundı, waeleze kwa nini kuna makanganyiko kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Sekondari haina gari kabisa, tunaomba mtukumbuke safari ijayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa jambo la faraja liliofanywa na Serikali kurudia kuangalia upya matokeo ya kidato cha nne. Watoto wetu walio wengi wamefarijika na wameona jinsi gani Serikali yao imeweza kuwajali na kuwatambua.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Walimu na maslahi yao, Walimu wamekuwa wakiomba sana posho ya kufundishia, posho ya kufundishia ndio msaada wa kipekee kwa Walimu. Walimu wamekuwa wakiomba 50% ya mishahara yao kama posho. Serikali langalie kilio cha Walimu kama itashindikana 50% basi wapewe hata 30%, ikishindikana 30% hata 20% angalau waone Serikali yao imewajali Walimu na kusikia kilio chao.

Mheshimiwa Spika, Walimu wamekopa mishahara yao kwa ajili ya kusomeshea watoto wao. Serikali (Bodi ya Mikopo) pamoja na kuangalia hati za mishahara ya wazazi wa mwanafunzi na kuona makato yanayowakabili wazazi wao lakini hawapewi mikopo katika vyuo (walio wengi sio wote), posho itasaidia kuishi.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Walimu sasa yaishe Serikali imalize matatizo ya Walimu na Serikali wasitengeneze madeni mapya. Walimu kutolipwa nauli za likizo ni Serikali inajiongezea madeni, posho za uhamisho na safari kutolipwa kwa wakati, Serikali inajiongezea mzigo.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa shule za awali ni mzigo kwa Walimu wakuu. Kutokuwa na fungu la uendeshaji wa shule (madarasa) ya awali ni balaa kwa Walimu wakuu. Watoto wanahitaji uji au chochote cha kuwasaidia kumudu mazingira ya shule, hakuna na uvumilivu kwa watoto ni mdogo. Naomba Serikali itenye fungu kwa shule za awali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza Wizara kupokea ombi langu la kujengwa chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Mvomero niilotoa mwaka jana. Nashukuru kuwa Mvomero imewekwa katika awamu ya kwanza katika mwaka 2013/2014, swali langu ni lini ujenzi huu utaanza na utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, pili, nashukuru kwa kusikia kilio changu kuwa Jimbo langu lina uhaba wa madarasa na uchakavu wa majengo na mwaka huu 2013/2014, Wizara imekubali kufanya ukarabati kwa sekondari za Melela, Mgeta, Dakawa, Wami, Mvomero, Doma na Mtibwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani, nauliza ujenzi utaanza lini na utakamilika lini? Aidha, napenda kujua Wami ni sekondari ipi? Maana kata ya Dakawa ina sekondari ya Wami Dakawa lakini naona Dakawa na Wami? Je, fedha kwa ajili ya *Sokoine Memorial High School* mbona haijatengwa?

Mheshimiwa Spika, tatu, niombe Serikali kuendelea kutenga fedha kujenga shule za msingi kwa lengo la kuongeza madarasa na vyoo.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba Wilaya ya Mvomero iongezewe Walimu wa shule za sekondari na shule za msingi kwa hali ilivyo Walimu bado hawatoshi.

Mheshimiwa Spika, tano, narudia ombi la kulipwa madai ya Walimu na upandishaji madaraja kwa Walimu hapa nchini na Jimbo la Mvomero. Walimu wanapata matatizo pale wanapoendelea kudai madai yao, hii inapelekeea kupungua kwa ari ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, tunachokosea Watanzania ni Serikali

kutoweka kipaumbele katika suala la elimu na ndio matokeo yake tunaendelea kuyaona na tutaendelea kuyaona kama Serikali haitachukua hatua kuhakikisha elimu inapewa kipaumbele hata cha pili basi kama sio cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya vijiji ni hata mengine yako mijini kabisa bado miundombinu ya elimu ni mbovu na sio rafiki kwa Walimu na kwa wanafunzi pia. Mfano shule nyingi zimekuwa ziko mbali sana na maeneo wanayoishi watu na matokeo yake wanafunzi na Walimu wanatumia muda mrefu sana kwenda na kurudi shule, hivyo kukosa muda wa kufundisha wanafunzi vizuri na wanafunzi wenyewe kukosa muda wa kujisomea na hasa wanaporudi nyumbani kwani wanakuwa wamechoka sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni madarasa hayatoshi maeneo mengi na pengine ni mabovu na hayafai huku yakiatarisha maisha ya wanafunzi na Walimu kwa ujumla. Vifaa vya kufundishia kama vile chaki za kuandikia, karatasi za manila vimekuwa vikinunuliwa na Walimu katika maeneo mengi ya nchi yetu, hii inazidi kumuongezea Mwalimu mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Walimu wengi hasa walioko pembezoni wamekuwa wakifuata mshahara umbali mrefu sana na pengine wanaweza kumaliza hata siku tatu (3) kwa kufuata mshahara. Mazingira haya magumu ya kazi yanachangia sana Walimu kutokwenda kufundisha maeneo haya hasa pale wanapopangiwa kwani wanakuwa kama wametupwa porini. Naiomba Serikali iangalie sasa ni jinsi gani itaweza kuwasaidia Walimu hawa kwa kuhakikisha mishahara inawafuata kila waliko, hii itaokoa muda ambao unapotea wanapokuwa wanafuata mishahara kwenye makao makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ili kuboresha mazingira mazuri kwa Walimu, posho ya kufundishia irudishwe, hii italeta morali kwa Walimu na pengine itasaidia kupunguza huu ufaulu mbovu ambao unaendelea kushika kasi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu maslahi ya Walimu yaangaliwe upya, madai wanayodai Walimu yalipwe kwa kasi ambayo itasaidia kuleta ufanisi katika kazi zao. Walimu wamekuwa wakinung'unika sana, pengine tunalalamika ufaulu mbovu kumbe ni *surbotage* kwani hata wasahihishaji ni wao wenye. Chochote wanaweza kukifanya.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa shule upo kila Mkoa na Wilaya, lakini idara hii inafanya nini? Mbona sioni tija ya idara hii? Maeneo mengi hawana magari wala pikipiki, watafikiaje shule zilizoko mbali? Kelele za ufaulu mbovu tutaendelea kuzisikia hata kama tutaziba masikio. Naomba Serikali kupitia Wizara iangalie utendaji kazi wa Idara hii kama unakwenda sambamba na kasi ya ulimwengu tulionao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tatizo linaloleta manung'uniko mionganoni mwa wanafunzi waliofaulu mwaka 2012 ambaeo matokeo yao sasa yamerekebishwa sijajua *standardization* imefanyika vipi mfano katika Manispaa ya Shinyanga shule ya sekondari Ibinzamata watahiniwa wafuatao:-

- (i) S.3351/0056 alipata Dv.II:21 na sasa ana Dv.II:21;
- (ii) S.3351/0068 alipata Dv.IV:26 na sasa ana Dv.IV:26;
- (iii) S.3351/0073 alipata Dv.III:23 sasa ana Dv.II:18;
- (iv) S.3351/0071 alipata Dv.IV:26 na sasa ana Dv.III:23.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa uwiano uko wapi? Ni vigezo gani vimetumika?

Mheshimiwa Spika, kuna kesi moja, mwingine alipata Dv. IV:27 mwenzie alipata Div.III:25 lakini matokeo ya pili yule aliyepata Div.IV:27 kapata Div.III:25na yule aliyepata Dv.III:23 kabaki palepale! Naomba ufanuzi katika hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, suala zima la kuperomoka kiwango cha elimu nchini Tanzania hakutokani kamwe na Waziri aliyeeteuliwa bali ni makosa ya watendaji walio chini ya Waziri, jambo ambalo hupelekea kutupiwa madongo Waziri husika.

Mheshimiwa Spika, sasa nNi vyema watendaji walio chini ya Waziri akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara kufuatiliwa juu ya utendaji wake ili usiathiri nia njema aliyonayo Waziri pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunahitaji Walimu bora na sio bora Walimu. Moja kati ya mambo yanayoangusha viwango vya elimu ni suala zima na ukosefu wa Walimu wenye viwango bora vya elimu lakini vilevile uchache wa Walimu ambaao hawatoshelezi kutokana na idadi kubwa ya shule na wanafunzi tulionao.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa ili kunyanya viwango vya elimu ambayo inahitajika kwa Watanzania hatuna budi kuangalia viwango vya mahitaji ya maisha ya Watanzania wa kipato cha chini. Wako vijana wa Kitanzania ambaao wana uwezo wa kuendelea na masomo lakini wanafikia hatua yakushindwa kutokana na uwezo wao mdogo wa kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya elimu ni kutowajenga Walimu kimaslahi jambo ambalo linawafanya waishi bila ya matumaini baina yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inahitaji msukumo wa mahitaji ya lazima kama vile ukaguzi wa mara kwa mara shulenii. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kutenga fungu la ukaguzi, ukaguzi ambaao utakuwa ni wa kuboresha elimu na sio kwamba watu wapatiwe fedha za kwenda kushughulikia mambo ambayo ni kinyume na elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa nia njema, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni asilimia ngapi ya Wazanzibar ambao walipatiwa mikopo ya elimu ya juu tokea mwaka 2010/2013. Ni kwa wastani gani, *ratio* ipi iliyotumika. Ni wangapi walipata mikopo na wangapi walikosa mikopo kwa Zanzibar na ni kwa sababu zipi?

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukrani kwa Mungu na kwa kwako ili niweze kutoa kero, maoni, ushauri kwa Serikali kuhusu elimu kupitia Wizara ya Elimu ya Ufundii.

Mheshimiwa Spika, japo ninayo mambo mengi ila nitajitahidi kuongea machache sana kwa kuyatilia mkazo kama vile madeni na stahili duni za Walimu. Bado upo mkanganyiko mkubwa katika ya elimu na stahili za Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ninavyoolewa, Walimu wengi stahili zao zipo TAMISEMI na siyo Wizara hii lakini Serikali yenyewe iko kimya kwenye kutoa ufanuzi wa mambo haya na kutoa elimu kwa Walimu wenyewe Wabunge na Wananchi. Ikumbukwe kuwa elimu bora ni Walimu bora nao hapa nchini wanapungua sana kutokana na hali duni inayojiteza kutokana na Serikali kulimbikiza madeni na kuchelewesha stahiki na stahili zao.

Mheshimiwa Spika, wapo Walimu ambao wanacheleweshwa sana kupandishwa madaraja na imewafanya Walimu wengi sana kuvunjika moyo na kukosa ari ya kufundisha ikiwemo ukosefu wa nyumba za kuishi na hii ndiyo inapelekea kabisa ufaulu duni ujiteze wakati wa matokeo ya mitihani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ikipanga mipango yake ya maboresho iwe sambamba na TAMISEMI ili kuainisha na kubaini mahitaji ya Walimu huku Wizara ya Fedha iwe tayari kabisa kutoa fedha zinazohitajika na zitolewe kwa wakati. Haya kama yatazingatiwa ninao uhakika kabisa matokeo yataonekana kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi kwa kuwa ipo Wizara nydingine wakati inawajibika kufanya kazi maeneo mengine, imapelekea ukaguzi kuwa duni sana. Menejimenti ya Utumishi wa Umma ingeweza kupeleka fedha moja kwa moja Wizara ya Elimu na Wizara ikasimamia idara hii moja kwa moja kama hatua ya kwanza na pia kuiongezea uwezo ikiwemo vitendea kazi kama magari na vifaa vingine vyatutimizia wajibu.

Mheshimiwa Spika, mbali na watoto wetu kusoma mashulenii, ni vizuri kuwekeza katika maktaba zetu za Mikoa. Maktaba ya Mkoo wa Mara tangu ijengwe hadi leo imekuwa mbaya kimajengo na inavuja sana, pia haina vitabu na samani zake zimechakaa sana na haifai tena kutumika. Napenda sana kuishauri Serikali kupitia Wizara hii itume Wakaguzi wake waende wakaione maktaba ya Mkoo wa Mara.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili basi ni vizuri kabisa kuangalia maktaba zetu za Mikoa, zikarabatiwe na zipewe vifaa vyatutimizia kutosha ili kuwajengea watoto wetu tabia ya kujisomea na hii itawajenga watoto vizuri kuwa na tabia za kusoma na kujisomea ili iwe rahisi sana kwa Walimu kuwafundisha watoto wenye moyo na tabia za kujisomea na hii itasaidia sana kuboresha elimu hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, ada za shule zimekosa usimamizi kwani maamuzi ya ulipaji wa ada umekuwa tena siyo huria bali holela na hiyo ni kosa na hatari kwa nchi ambayo watu wake 80% ni wakulima na wanaopenda elimu. Ni vizuri zaidi kuwa na mamlaka inayoweza kabisa kusimamia ada katika mashule binafsi. Pia mamlaka hiyo hiyo iwe na uwezo wa kupanga ubora na mahitaji kulingana na ada inayotozwa, sambamba na huduma itolewayo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaweza kuonekana gumu sana kwa mvivu na mtu aliyekata tamaa na kukosa matumaini, lakini kama litafanikiwa, basi elimu itolewayo na shule binafsi itaonekana kwa ubora wake sambamba na huduma na elimu itolewayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai yangu kwa Wabunge na wananchi, kuwa tatizo siyo watu waliopo katika Wizara bali mfumo wenyewe hata kama tutajielekeza kwenye kuwafukuza Mawaziri bado tutakuwa hatujafanikiwa sana ila kubadili mfumo ni jambo la busara zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa Walimu wapatao 236,544 kuna umuhimu wa kuwaangalia kipekee kwa kuwa na chombo cha kuwahudumia kama ilivyokuwa Tume – *TSC, TSC*. Kiwe na uwezo wa kulipa mishahara kama ilivyo nchi jirani ya Kenya na kinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tangu awali *TSC* ilikuwa ikisajili, ikichukua hatua za nidhamu, ikipandisha madaraja, ikitoa ruhusa za *secondment* na huduma zingine za kikazi. *TSC* irudishwe na ipewe madaraka ya kulipa mishahara. Kuundwa kwa Bodi hakuwezi kuchukua nafasi ya *TSC*. Bodi itasimamia taaluma tu kama ilivyo *TBS*. Bodi siyo jawabu la kuhudumia Walimu.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya nchi yetu yanatofautiana sana hasa vijijini. Kuna maeneo ambayo Mwalimu anasafiri kufuata mshahara kwa gherama zake na inabidi kulala huko ndipo arudi kazini. Hawa ndiyo wanaohitaji posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, uko utafiti unaonesha kuwa ni Wilaya zipatazo 30 tunazoweza kuanzia kuwalipa kwa kuwaacha walio makao makuu ya Wilaya. Posho hii ilikuwepo kisha ikaondolewa, tunaweza kurudisha hata kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, *skills development levy* isaidie gherama ya kutunisha Mfuko wa Elimu utakaoundwa kwa kutenga angalau 3% ya *levy*.

Mheshimiwa Spika, ili kupanua elimu ya ufundi kwa

kuunganisha VETA na *Folk Development College* na iwezeshwe kwa kupewa 3% badala ya 2% ya *skills development levy*.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nami nitoe mchango wangu wa maandishi kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ni mwaka wa tatu mfululizo kiwango cha elimu nchini kimekuwa kikishuka. Kutokana na hali hiyo Taifa hili limekuwa likipata aibu dunia nzima na kuonekana kama Taifa ambalo halina wasomi jambo ambalo sio kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa umefikia wakati ijiulize kulikoni na vilevile kulifua tilia tatizo hili ambalo limeonekana kuwa sugu na kushamiri kila mwaka. Vile vile pamoja na kuwachukulia hatua na kuwajibisha wale wote ambao watabainika na hujuma hii ambayo naamini Serikali na Watanzania wote hawaridhiki na matokeo ya mitihani ambayo yanaitia Taifa hili doa miaka mitatu (3) mfululizo. Ikiwa ni Wizara pamoja na watendaji wake wawajibishwe na ikithibitika ni Walimu pia wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimekuwa nikijuliza kulikoni, lakini baadaye huwa nasema na siamini hata kidogo kama yupo Mwalimu anayesomesha wanafunzi wake na ifikapo wakati wa kufanya mitihani wapate matokeo mabaya ya kufeli na siamini kama wapo wazazi ambao wanapenda watoto wao wapate matokeo mabaya ya kufeli.

Mheshimiwa Spika, vile vile siamini kama kuna Taifa ambalo linapenda kupata matokeo mabaya ya mitihani kwa raia wake. Matokeo mabaya ya mitihani na kushuka kwa kiwango cha elimu nchini kunatokana na Serikali hii kukataa kusikiliza kilio cha Walimu, jambo ambalo limekuwa la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali hii

kusikiliza kilio cha Walimu nchini kwani ndio wanaongoza kwa maisha magumu katika wafanyakazi wa Serikali kote nchini. Hivyo Walimu wakiwa kwenye majukumu yao ya kazi badala ya kusomesha wanafunzi darasani amefikiria familia yake itakula nini na itaishi vipi. Vipi wanafunzi wasifeli kwenye mitihani yao wakati Mwalimu hana hamu ya kusomesha wala hamasa?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa hivi ikiwa kwenye mitafaruku mbalimbali ikiwemo hata kidini, leo hii Baraza la Mitihani nchini imelifuta somo la dini ya Kiislamu shulenjambo ambalo litasababisha mtafaruku mwingine mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watoto wa Kiislamu siku nydingi na muda mwingi wako shulenisiipokuwa siku ya Jumapili na katika shule wanazosoma lipo somo la dini ya Kiislamu muda wote wazee hawa wanakuwa na imani kwamba watoto wao wataifahamu dini yao kwa sababu kwenye shulenili po somo linalofundisha kuifahamu dini yao.

Mheshimiwa Spika, rai yangu, naiomba Serikali hii ya CCM ifikirie upya kufutwa somo la dini ya Kiislamu shulenivinginevyo Serikali ijiandae na kutatua migogoro mipyambayo itaibuka kwa Waislamu na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na njama za makusudi zinazoonekana za kufelisha watoto wa Kiislamu, njama ambazo zimepangwa na Baraza la Mitihani nchini. Itakuwaje leo kwenye somo la dini ya Kiislamu linapangiwa *credit* 35 – 49 ni ‘C’ wakati kwenye somo la dini ya Kikristo 35 – 50 ni ‘B’? Je, hizo sio njama za makusudi kuwafelisha watoto wa Kiislamu? Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anipe ufanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala zima la wanafunzi kutokufanya vizuri, yapo mambo mengi yanayofanya kiwango cha elimukushuka kwa mfano:-

- (i) Kutowadhibiti mianya ya wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika kupanda madarasa;
- (ii) Kutosimamia vizuri mitihani ya darasa la nne na kidato cha pilii;
- (iii) Kitengo cha Ulaguzi kiboreshwwe kwani kitengo hiki kimetelekezwa;
- (iv) Utungaji wa mitihani uzingatia *topic* zote;
- (v) Upungufu wa Walimu, vitabu, Walimu wa Sayansi hakuna lakini wanafunzi ambao hawafundishwi masomo ya sayansi wanafanya mtihani huo, matokeo yake wanafeli;
- (vi) Masilahi ya Walimu yaboreshwe ili kurejesha uzalendo wa Walimu katika ufundishaji;
- (vii) Wasikae sehemu moja kwa muda mrefu;
- (viii) Shule ziendelee kushindanishwa kitaaluma;
- (ix) Wazazi kutokuwa karibu kufuatilia maendeleo ya watoto wao mashulenii;
- (x) Ukosefu wa posho maalum kulingana na mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya uundaji wa Bodi za Sekondari. Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho kutokana na ujenzi wa sekondari za kata, kama kuna shida sana ya kuwapata wajumbe.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwa maana ya Jimbo la Kwela t, inazo shule za sekondari za kata 15, shule ya sekondari ya misheni moja, shule za watu binafsi nne. Hivyo kutokana na shule hizo za sekondari tulionomba shule mbili zipandishwe hadhi kufikia

kidato cha tano na sita ambazo ni Vuma Sekondari na Uchile Sekondari. Naomba Waziri aniambie ni kwa nini hadi leo hizi Serikali hajazipandisha hadhi?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijenge shule ya mafunzo ya ufundi katika Wilaya ya Sumbawanga, ambayo haina hata shule moja ya mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya vifaa maalum vyatia kujifunzia na vya kufundishia wanafunzi wasioona (*perkins brailler 50 na embosser set moja*) katika shule ya walemau iliyopo Sumbawanga, eneo la Malangali. Hii ni shule maalum ya msingi ya wasioona. Shule hii ina wanafunzi 68 wasioona na ulemau wa ngozi albino ambao uonaji wao ni hafifu. Tunaoomba msaada wa haraka. Naomba Waziri wakati anatoa majibu na ufanuzi anipe majibu juu ya maombi haya.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kujitegemea ifundishwe mashulenii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia juu ya chombo kinachohudumia Wakaguzi wetu. *TSD* kisogezwe Wilayani kuliko kubaki huko Dar es Salaam (Temeke) kwani *TSD* ya huko Dar es Salaam inakuwa mbali sana na walengwa na kumbukumbu nyingi za elimu juu ya wakaguzi zinapotea. Hivyo *TSD* irudishwe Wilayani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu inashughulika na elimu ya msingi ambayo pia inashughulikiwa na TAMISEMI na kila Halmashauri zina uwezo tofauti. Hivyo Wizara haijui kama

Mwalimu shulen i kama amekwenda na anafundisha au vipi. Fedha za elimu pamoja na Wizara ya Elimu zinasimamiwa pia na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya taaluma kuwa chini ya Wizara ya elimu. Elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya ufundu visimamiwa na taaluma husika. Mathalan wanaosoma Udaktari wakati wapo chini ya Wizara ya Elimu lakini pia wapo chini ya Wizara ya Afya, Walimu wa Madaktari hao wako chini ya Wizara ya Afya maana ni wanyakazi wa taasisi.

Mheshimiwa Spika, elimu iondolewe TAMISEMI. Ni lazima tuiangalie Wizara ya Elimu kwa upana sana. Aidha ihusike na elimu ya msingi na sekondari tu na Walimu wote wawe chini ya Wizara ya Elimu na si TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu irudi iwe peke yake. Asilimia zaidi ya 75 ya bajeti ya Wizara ya elimu ni mikopo ya elimu ya juu, lakini bajeti hii inayopitishwa inayobaki kwa elimu ya msingi na sekondari ni ndogo sana. Hata mafanikio tuliyopata kwenye elimu ya msingi na sekondari itashuka kwa sababu bajeti yake imekuwa inashuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, *contractza Wahadhiri*. Kuna tatizo zito sana la Walimu (*Profesors*) katika vyuo vikuu. Ili mtu awe *Lecturer* (Mhadhiri na Mhadhiri Mwandamizi) ni lazima awe ni *Professor au Associate Profesor*.

Mheshimiwa Spika, umri wa kustaafu. Ili mtu afike kuwa *Associate Professor* akiwahi sana atakuwa na miaka 50 – 55 na kumwacha amebakiza miaka mitano mpaka kumi kustaafu wakati anastaafu ndiyo kwanza yupo kwenye *peak* ya taaluma. Wanapoomba *contract* wanachukuliwa kama fani nyingine kustaafu miaka 60.

Mheshimiwa Spika, *MUHASwatakosa Wahadhiri*. Suala hili lisiposhughulikiwa haraka, katika siku za karibuni *MUHAS* itakuwa hakuna Wahadhiri. Hali ilivyo sasa wamekataliwa kupewa *contract* ya kuendelea na kazi, Mheshimiwa Waziri suala hili linahitaji hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, mapato ya uhakika kwa *TEA*. Mamlaka ya Elimu ya Taifa (*TEA*), imekuwa ikifanya kazi nzuri sana kama ombaomba, bajeti ya Serikali haipewi kabisa au inapewa kidogo sana kwa maendeleo. Mara nyingi tumekuwa tukiona wakifanya fund *raising* halafu ndiyo wasaidie shule, vyuo na taasisi mbalimbali. Wakati umefika Serikali iamue kuitafutia Mamlaka hii vyanzo maalum vyatuhusu mapato kama ilivyo *VETA* au kama fedha za barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kwa undani suala zima la elimu na kutoa ufumbuzi wa muda mrefu.

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mungu niseme kwamba sirahisi na wala tusitegemee kupata mafanikio mazuri bila ya kuamua kuwekeza kisawasawa kwenye sekta ya elimu. Kuwekeza ni pamoja na kuwatunza Walimu kwa kuwalipa mishahara kufuatana na ngazi zao za elimu na posho ziendane na maeneo wanayofanya kazi/mazingira magumu hususan maeneo ya vijiji na upandishwaji wa mishahara kwa nyakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, makazi ya Walimu yamepuuzwa, vitendea kazi hakuna, maabara hakuna. Kwa nini Serikali isijipange kwa awamu tupate Walimu wa Hisabati, Fizikia, Chemia, Biologia ifikapo mwaka 2020 kwa lazima na hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Walimu wakaguliwe, watoto madaftari yakaguliwe na nidhamu shulenii lazima sasa irudishwe kwa vijana kukaguliwa mavazi, usafi na kadhalika na hili Mwalimu awe ni kioo cha tabia njema na mwenendo sawiya na hili ni pale Mwalimu atakapokuwa ana hakika – kuna mtu anakuja kumkagua.

Mheshimiwa Spika, vijana wenye vipaji maalum ni lazima vitunzwe na viendelezwe kwa kuwawekea shule teule za vipaji vyao ili tuweze kuwapata wanasayansi wa vipaji haswa na sio vya kulazimisha.

Mheshimiwa Spika, si kweli na wala hatuwatendei haki hata kidogo kuwaweka darasani na wenzao wasio walemavu na kwa pamoja uwapime sawa. Tuna tatizo la Walimu wa maeneo mbalimbali ya ulemavu hawatoshi kukidhi watoto walemavu tulionao. Watengewe shule zao, viziwi kwao, wasioona kwao, walemavu wa viungo kwao na wapimwe kivyao, hii ndio haki.

Mheshimiwa Spika, madaraka ya Waziri. Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye dhamana ya Wizara husika na kamwe sio mtu mwingine ye yote wala chombo chochote. Waziri awe ndiye yeye mwenye dhamana ya matumizi ya fungu la Wizara na Mheshimiwa Waziri awe ndiye yeye msemaji na msimamizi wa shughuli zote za Bodi ya Elimu na si vinginevyo. Hakuna mahali duniani ambapo Waziri wa Wizara asiwe na nguvu ya maamuzi dhidi ya Bodi ya Wizara yake hakuna isipokuwa Tanzania kwa Wizara ya Elimu na kama ipo nchini sijui.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye dhamana ya Wizara yake hivi inakuwaje Katibu Mkuu apewe uwezo mkubwa wa matumizi ya fedha za Wizara kuliko Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana? Sheria hii inayompa Katibu Mkuu wa Wizara awe ndiye mdhamini wa matumizi ya fedha ya Wizara na sio Waziri, hili life na lizikwe.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa 176, Mkoa wa Tabora, Halmashauri ya Tabora Vijijini (Uyui), kuna Majimbo mawili Tabora Kaskazini na Igalula. Ujenzi wa awamu ya kwanza shule za 235 Ikongolo na 236 Lolanguru zote ziko Jimbo la Tabora Kaskazini. Wizara kwa mara ya pili haiwatendei haki wananchi wa Jimbo la Igalula kwa kuchagua sekondari zote za Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, hii pia ni hujuma kwa Mbunge wa Jimbo la Igalula. Mara ya kwanza ujenzi wa maabara mbili Wilayani Tabora Vijijini (Uyui) zote zilipelekwa shule ya

sekondari Ndono na shule ya sekondari Idete, Tabora Kaskazini. Hivi hapo Wizarani nani anamhujumu Mbunge wa Igala? Mheshimiwa Waziri atambulike na aniombe radhi.

Mheshimiwa Spika, huo siyo uongozi bora. Wananchi wa Jimbo la Igala wapo kufuatana na Katiba ya nchi hivyo wanahaki sawa kama wenzao wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwa kuwa hii ni mara ya pili sasa ninamwandikia barua Mheshimiwa Waziri Mkuu ili tatizo hili lisirudiwe tena asilani.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 200, namba moja (1), Wilaya ya Uyui, Wilaya 27 ambako vitajengwa vyuo vya ufundi stadi awamu ya kwanza, kufuatia hali niliyoieleza hapo juu, chuo hiki cha ufundi kijengwe kata yoyote Jimbo la Igala kama Igala, Goweko au Tura ambako kuna reli, barabara na hususani Goweko au Igala ambako kuna umeme kuanzia 2013/2014 na pia kuna sekondari kata zote hizo.

Mheshimiwa Spika, Igala na Goweko maji safi na salama Mbunge amepeleka na sasa anakamilisha kata ya Tura. Tugawe na kusambaza maendeleo sawa bin sawia katika Majimbo haya mawili.

Mheshimiwa Spika, sekondari za kata Loya, Lutende, Goweko, Igala na Tura zilizojengwa kwa nguvu za wananchi zote zinahitaji mabweni kwa wanawake pia maabara.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa sayansi na vitabu vya kiada hakuna katika shule hizi. Tupate wafaulu wa kwenda vidato vya tano (5) na sita (6) *PCM, PCCB, PMMna IT*. Muhimu tusaidiwe, Jimbo zima Wahandisi ni Athuman R. Mfutakamba wa Kimwaga Mfutakamba tu. Utabibu ni Mwasiti Mfutakamba tu waongezeke.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, napenda kupata maelezo ya kutosha ya hatima ya shule ya sekondari Tandahimba kutopangiwa wanafunzi wa kidato cha tano tangu mwaka

2011 ilipopatiwa usajili namba S.677 kwa barua yenyewe kumbukumbu namba BMS.677/Vol.1/144 ya tarehe 4 Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, aidha, ikumbukwe kuwa wananchi wa Tandahimba kwa kushirikiana na Halmashauri ya Tandahimba wamefanya uwekezaji, pia Walimu wenye sifa tumewaandaa na kuwaweka pale shulenii. Tatizo ni nini wanafunzi hawapangwi?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa jambo hili ni la Ilani mwaka 2010 kwani tuliahidi kila tarafa kuwa na shule za kidato cha tano na sita. Maelezo kuwa wasichana hawapatikani si ya msingi kwani si lazima shule hiyo iwe na wasichana tu inaweza kuwa hata *co-education school*.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu *teaching allowance* kwa Walimu. Huko nyuma Serikali iliwapa *teaching allowance* Walimu, posho iliyotumika kama motisha kwa Walimu. Kwa uhakika wa kupata posho hiyo Walimu waliweza kuandaa *lesson plan*, kutafuta dhana za kufundishia na kujifunzia, kusahihisha kazi za wanafunzi, kutafuta na kusoma vitabu vya ziada ili kumwongezea maarifa katika masomo husika tofauti na sasa ambapo Walimu wanahangaikia maisha kwa kutokuwa na uhakika. Nashauri Serikali irudishe tena posho hii kwa Walimu ili kuwapa ari ya kuwafundisha vijana wetu kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwenye zoezi la ugawaji, Serikali iliwatoa Walimu wa shule za msingi na sekondari kutoka usimamizi wa Wizara ya Elimu na kuwapeleka kwenye Halmashauri. Pamoja na mambo mengine nia ilikuwa Walimu wa vyuo wakibakia Wizarani watakuwa wachache na hivyo rahisi kuwashudumia.

Mheshimiwa Spika, kinyume chake Walimu wa vyuo wana matatizo mengi yasiyoisha mfano kutopanda madaraja kwa wakati, fedha za likizo hawapati na hata maslahi ya ujumla huchukua muda mrefu. Je, Serikali inafanya nini ili kuboresha utendaji?

Mheshimiwa Spika, nne, nchi yetu inayo chuo kikuu huria ambacho kwa kiasi kikubwa kimepunguza sana *gapla* upatikanaji wa elimu kwa kutoa elimu bora na nafuu. Kwa mfano, udahili wa Shahada za uzamili (*Master*) na Uzamivu (*Ph.D*) ni 2391 kwa mwaka 2012/2013. Udhili huu ni hatua kubwa sana lakini chuo hicho hupata mafungu madogo sana ya *OC* na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema chuo hiki kikaongezewa fedha kwani ni taasisi muhimu sana ambayo udahili wake hauwezi kulinganishwa na *conversional university* yoyote nchini. Aidha, kwa upande mwingine sioni haja ya kuongeza uwekezaji wa majengo pale Kinondoni wakati kiwanja cha Makao Makuu Kibaha kikiwa hakina uendelezaji wa maana. Hivi ujenzi wa ghorofa kumi (10) wa jengo la mradi wa Sayansi, Technologia na Elimu ya juu kwa nini lisingejengwa Kibaha?

Mheshimiwa Spika, tano, Wizara naishauri kuangalia upya nafasi ya Waratibu Elimu Kata. Kada hii haina msaada wowote katika kuongeza tija ya elimu yetu. Ni vyema basi ama ikafutwa au watengenezewe utaratibu maalum wa vitendea kazi na uboreshaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri, Katibu Mkuu wa Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru Wizara kwa mpango wa kujenga vyuo vya ufundi. Kati ya vyuo 27 vya awamu ya kwanza Wilaya ya Geita pia ni mionganoni mwa Wilaya ambazo tutajengewa chuo cha ufundi. Ninaiomba Serikali iharakishe mpango huu kwani tunao vijana wengi sana wanahitaji mafunzo ya ufundi. Hivyo, napenda kujua mpango huu utaanza lini na kukamilika lini?

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa vifaa vya kufundishia ni tatizo kubwa sana hasa katika shule zote za

sekondari na msingi. Shule nyingi hazina vitabu na nyenzo muhimu za kufundishia pia kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu. Niilombe Serikali ilekeze nguvu katika kuboresha shule za vijijiini.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie uwezekano wa kuboresha mazingira ya shule kwa kuwezesha kupeleka umeme na maji. Umeme wa *MCC* unaopelekwa maeneo mengi ya vijijiini mfano, katika Jimbo la Busanda Wizara ihakikishe umeme unapelekwa katika shule za sekondari ili kuboresha mazingira na yawe na mvuto kwa Walimu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa ya madai ya Walimu. Katika Wilaya ya Geita, kuna Walimu wengi sana bado wana madai na hii husababisha kushusha *morale* kwa watumishi. Napenda kujua Wizara inao mkakati gani wa kuhakikisha madai ya Walimu yanalipwa sasa?

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara ya Elimu iboreshe Idara ya Ukaguzi kwa kuboresha vitendea kazi ili kuwawezesha kufuatilia ili tupate matokeo mazuri. Mfano, Geita Idara haina vifaa muhimu kama gari, pia mafuta ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha nami nichangie bajeti hii muhimu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri kwani imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayodhamiria kuinua vijana wake kielimu na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, elimu ndio chanzo cha mafanikio katika nchi yoyote ile duniani, lakini kwetu pamekuwa na changamoto nyingi sana kwenye sekta nzima ya elimu nchini,

ingawa Serikali inaendelea kujitahidi na kuweka juhudini kubwa lakini msukumo bado umekuwa mdogo, kwa hali hiyo hapana budi kupambana na changamoto hizo kwa kuweka mikakati thabiti ili kuondoa kero, kasoro zote katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matatizo katika sekta nzima ya elimu, mifumo yetu ya elimu imekuwa ina mkanganyiko mkubwa kiasi husababisha juhudini nydingi kutokufanikiwa, ubora wa elimu kushuka kwa wanafunzi walio wengi kufeli, kwa baadhi wanaomaliza darasa la saba kutokujua kusoma na kuandika, wanaomaliza kidato cha nne na cha sita kutokujua kuandika kwa lugha ya Kiingereza na kwa wale wanaohitimu vyuo mbalimbali kutopata ajira kwa kushindwa kufika kiwango kinachotakiwa katika (*interview*).

Mheshimiwa Spika, nawezasema elimu yetu imekuwa haiwajengi vijana wetu kufaulu vizuri bali kuwabana katika mitihani yao. Kufanya hivyo tunatofautiana sana na nchi za wenzetu kwani wao hutoa elimu kwa kuwajenga vijana kufaulu na si kushindwa. Mfumo wa elimu uliopo unahitaji maboresho mfano, ni matokeo mabovu ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu kwa Taifa kwani tunatambua Taifa lolote ili liweze kuendelea lazima liwe na wasomi wazuri. Kwa mfumo huu ambao tunao hivi sasa hakika tunahitaji kuuboresha ili tuendane na mataifa mengine ili nasi tupate wasomi wengi wenye viwango vya kimataifa kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Jimbo la Kibaha Vijiini tuna matatizo sana kwenye sekta ya elimu, mazingira duni ya shule zetu kuanzia ngazi za msingi, sekondari za kata, sekondari za Serikali na shule za watu binafsi, tuna upungufu wa Walimu, madawati, maabara kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo na hili tatizo lipo katika shule zote.

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuwa na maabara kunapunguza kasi ya kupata vijana watakaochipukia katika masomo ya sayansi ambao wangetusaidia kwenda

sambamba na karne hii ya sayansi na teknolojia. Pia vitabu vimekuwa haba kwa shule zetu kutokutosheleza kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumekuwa na upungufu wa matundu ya vyoo kwenye shule zetu ambayo hayana uwiano sawa na idadi ya wanafunzi waliopo, hivyo huwalazimu kwenda maporini ama kujisaidia katika vyoo vibovu na kuhatarisha afya zao. Napenda kuiomba Serikali kuliangalia hili na kulitafutia ufumbuzi wa haraka ili kuboresha sekta ya elimu katika Jimbo la Kibaha Vijijini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kwa Walimu wanaopangiwa kuja kufanya kazi katika Jimbo letu, kumekuwa na uhaba wa motisha, mishahara, marupurupu ya posho, malipo ya likizo, malipo ya uhamisho na halilngumu ya kimazingira. Hata hivyo, napenda kuwapongeza kwa kuwa wasikivu na wavumilivu kwa kufanya kazi katika mazingira hayo magumu. Naiomba Serikali kuwapa motisha Walimu hawa ili wawe na moyo wa kufundisha watoto wetu kwa kuwajengea nyumba za kuishi, kuwapa motisha, kuwalipa madai yao ya muda mrefu na mambo mengineyo yatakayowafanya wafanye kazi kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza na kuiomba Serikali kuititia Wizara katika Mabunge yaliyopita, kuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kuangalia kwa jicho la huruma Jimbo la Kibaha Vijijini, naomba kijengwe chuo cha ufundi kusaidia watoto wa wafugaji na wakulima kupata stadi za kuwawezesha kujajiri kwa shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Jimbo la Kibaha Vijijini ni vijana wachapa kazi na wako tayari sana katika kujifunza, kinachowapa shida ni muongozo, hata ufgugaji unahitaji stadi za kujua kufuga kisasa ili kuweza kupata mifugo na nyama bora na pia maziwa ya kutosha. Kilimo nacho kina stadi zake kujua misimu, mbegu bora, mazao yanayostawi kwa wakati, wakijengewa chuo cha mafunzo ya ufundi kwa hakika watainuka kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wanapomaliza shule za msingi na sekondari wapo baadhi yao hukosa nafasi za kuendelea kimasomo, lakini pia wana nafasi za kuendelea katika vyuo vya ufundisti ili kuweza kujajiri wenye baada ya kuhitimu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuweka mkazo katika kuendeleza vyuo vya ufundisti ili kuwasaidia vijana wetu, ila kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo hakuna budi Serikali yetu siku kuzishughulikia ili kuboresha sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko katika utoaji mikopo ya elimu ya juu, kwani kusudio la utoaji wa mikopo hiyo limekuwa likienda tofauti na vile Serikali yetu ilivyokusudia. Vijana wanaotoka kwenye familia zenyewe uwezo wamekuwa wakipatiwa mikopo hiyo na wale ambao hasa ndio kusudio wamekuwa wakikosa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia upya utaratibu wa upatikanaji wa mikopo hiyo ili kuboresha zaidi na kuweza kuwagundua wale wanaodanganya ili hali familia zao zina uwezo wa kuwasomesha (*private*) lakini hupata mikopo tena kwa asilimia kubwa huku wale wanaotoka katika familia duni hukosa kabisa huku wakiwa wamefaulu vizuri na hata wakipata mikopo hiyo ni kwa asilimia ndogo.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wanaomala elimu ya juu wamekuwa wakiongezeka kila mwaka na wengi wao wamekuwa wanakosa ajira Serikalini au sekta binafsi kwa sababu mbalimbali lakini kuna njia nydingi za kuweza kuwasaidia vijana hawa pale wanapokuwa bado vyuoni mwao kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali, elimu hiyo itawasaidia hata wakimaliza elimu zao na kukosa ajira kwani wanaweza kujajiri wenye kwa kujiunga katika vikundi vidogovidogo na kuanzisha kitu ambacho kitawasaidia.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara wangeweka utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo midogomidogo kutoka kwenye mabenki yetu ama vyanzo

mbalimbali vyatya fedha ili waanzishe miradi midogomidogo kwa njia nyingine watakuwa wamejiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaweza kuweka utaratibu wa kuchukua vyeti vyatya wahitimuhawa vyatya vyuo walivyomaliza yaani (*Original Certificate*) vikawa kama dhamana kwenye hayo mabenki ambayo watapatiwa mikopo hiyo, kufanya hivyo itawasaidia. Utaratibu huu utawasaidia sana pale tu Serikali kuitia Wizara itakapokaa na haya mabenki na kuzungumza nayo na kuangalia mahali pa kuboresha utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kuishauri Serikali kuendelea na juhudizake za kuboresha elimu nchini kwani kufanya hivyo kutasaidia vijana wetu kupata elimu bora na kuwa na wataalamu wazuri wa kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu miundombinu ya shule zetu. Shule nyingi za kata hazina maabara, madarasa, maktaba, hazina vyoo na huduma nyingine ambazo zitamfanya mwanafunzi awe *comfortable* na kuwa na uelewa mzuri. Mfano, wanafunzi hawa hasa wanaochukua masomo ya sayansi watafaulu vipi iwapo hawana Mwalimu, hawana maabara, hawana vitabu?

Mheshimiwa Spika, mfano, shule ya Ukende, Wilayani Tarime haina vyoo vyatya kutosha kitu kilichopelekea shule ile kufungwa zaidi ya mwezi sasa, hapa anayeathirika ni mwanafunzi ambaye anakosa masomo lakini atakuja kuwa *examined* kama wanafunzi wengine wenye shule zenye miundombinu yote na Walimu wa kutosha. Naomba fungu la kukarabati lilitengwa kwa ajili ya shule za Tarime ikiwemo Ukende ziende mapema ili wanafunzi warudi shule.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kuomba Serikali iangalie jinsi ya kuwa-*motivate* Walimu wanaofundisha kwenye mazingira magumu, kama vile *workload allowance*,

kwa shule zenye upungufu wa Walimu, ili waweze kuwa na moyo wa kufundisha masomo hata yale yasiyokuwa na Walimu. *Transportation allowance, housing allowance* kwa wale wanaopanga. Vilevile malipo ya ziada kwa Walimu wanaofundisha watoto wenye ulemavu. Wasilipwe sawa na Walimu wengine.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kurudisha mfumo wa ufundishaji kwa darasa la kwanza kuwa masomo matatu yaani kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya mchakato wa kujenga chuo cha *VETA* Ukerewe, nilitaka kujua mpaka sasa ni shillingi ngapi zimepelekwa Ukerewe kwa ajili ya kuanza mchakato.

Mheshimiwa Spika, tunao mchakato wa uanzishwaji wa vidato vya tano na sita katika Wilaya ya Ukerewe. Naiomba Serikali kuititia Wizara kutoa vibali mapema ili mchakato uanze mapema.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Jiografia ya Wilaya ya Ukerewe kuwa Kisiwa, Wakaguzi wa shule wanapata tabu kusimamia shughuli zao. Je, lini Serikali itawapa gari Idara ya Ugagazi katika Halmashauri ya Ukerewe?

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu na ushauri kuhusu suala hili la Elimu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba elimu Tanzania imekuwa na mwelekeo wa kudorora au kuparanganyika au kukorogeka. Jambo hili linahuzunisha sana jamii ya wazalendo wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, haihitaji hata uchunguzi mambo yako wazi kabisa. Kubwa kabisa ni suala la kutothamini watoa

elimu yaani Walimu. Walimu ni ufunguo wa matatizo ya elimu. Niwathibitishie kuwa jambo lolote linawezekana iwapo Walimu watatendewa haki, wapate posho stahiki, wapewe posho za mazingira magumu, mojawapo kubwa ni Walimu walipwe kutokana na idadi ya wanafunzi walionao darasani. Posho hii ni ya kusahihisha madaftari kwani wanatumia muda wa ziada na mafuta ya taa au umeme wanaotumia wanaposahihisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalosababisha kutosoma ni mahusiano ya Walimu na wanafunzi. Wazazi wamesababisha Walimu wawe mbali na watoto, utaona wazazi wanatumia vibaya neno la demokrasia, neno hili limewafanya watoto wafanye wanavyotaka darasani na nje ya darasa, mtoto hajishughulishi na kujifunza bali kucheza na simu tu. Ukijaribu kuwazuia wazazi wao wanakuja juu na kutaka kupiga Walimu. Katika mazingira kama haya unafikiri vipi wanafunzi hawa watafanya vizuri vipi?

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika hapa ni kubadili mitazamo ya wazazi juu ya elimu yao wao wenyewe. Wazazi wathamini zaidi elimu ya watoto wao na nidhamu yao. Mfano, China iliweza kuendeleza jamii yake kwa kuweka mkazo wa kuwaadhibu wazazi pale watoto wao waliposhindwa kufanya vizuri. Hata enzi ya Wajerumani walifanya hivyo, mwisho wakapata kizazi endelevu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuwepo mwelekeo wa kuoanisha sera na mitaala. Tunategemea kuvuna nini wakati sera inasema elimu ya ujamaa na kujitegemea, lakini maudhui yanayopasa kuleta matokeo haya yako katika vitendo vya mlengo usioleweka, ubepari si ubepari wala ujamaa si ujamaa?

Mheshimiwa Spika, kuna sababu gani zilizofanya kubadili vifaa vya kufundishia mfano, vitabu vifuatavyo viliondolewa katika mitaala (*Things fall apart the centre cannot hold*) Kitabu hiki kilikuwa kinajenga uzalendo kwa vijana wetu kilifundisha ujasiri, kujiamini, uzalendo, mshikamano, lakini kikaondolewa.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kitabu cha (*The wretched of the earth* cha *Frantz Fanoni*, Daktari huyu alifundisha jinsi ya kujitambua na kuwa mzalendo, kingine ni (*Animal farm by George Orwell*) Pia kilifundisha sana masuala ya siasa na kujiamini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lisemwalo lipo, kama halipo linakuja, kwani wahusika wamekuwa wakinunua haki ya kuandika vitabu kwa ajili ya kutumika mashulen, lakini vitabu vyenyewe havifai, lakini wale ambao hawana cha kutoa vitabu vyao havipenye. Naomba suala hili lifuatiliwe na kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu imeingiliwa na mdudu mbaya wa maadili mabovu kabisa kutokea kwa wazazi na Walimu pia, kiasi cha kuambukiza hata watoto wazuri kuwa wabaya. Hapo nyuma kulikuwepo na (*Continuous assessment*) chombo hiki bila sababu kikaondoshwa wakati kilisaidia sana katika kuonesha uhalisia wa mambo. Ombi langu ni kurudisha mtindo huu wa (*Continuous Assessment*) ili kuokoa elimu.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yanayoangusha elimu, lakini kubwa sasa ni rushwa kuanzia ngazi za chini hadi Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa Hotuba ya Bajeti pamoja na utendaji mzuri wa majukumu yao. Aidha, naomba kuchangia kwa nia njema nikiwa na lengo la kuboresha utendaji wa Wizara hii muhimu sana katika kuzalisha wataalam wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo; Bodi hii sasa inahitaji ifanyiwe maboresho makubwa sana ili iweze kukithi malengo ya kuanzishwa kwake. Watoto wengi wanaotoka katika mazingira magumu hawapati mikopo

asilimia moja. Baadhi yao wanatakiwa kulipa asilimia 40 mpaka 60. Hivi watapata wapi? Hawana wazazi wala walezi wenye uwezo, wafadhili wengi wanalipia elimu ya msingi na sekondari tu na siyo elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia vijana hawa. Aidha, mfumo wa kukusanya marejesho ya mikopo hii ni hafifu ama hamfanyi kazi yake vizuri. Tafadhalii wahusika watueleze wanayo mikakati gani ya kukusanya marejesho haya ili tuweze kuwasaidia wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya awali; napenda kuishauri Wizara kuanzisha mpango wa kuajiri Walimu wa Shule za awali ili tuweze kujenga msingi bora wa elimu kwa watoto wetu. Mfumo wa elimu ya awali uainishwe kwani kila anayeendesha shule ya awali anayeendesha kwa mtindo wake hata Walimu wengi hawana taaluma inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MEMKWA; nimepitia sana hotuba ya Waziri Iakini sijaona mahali popote anapozungumzia Elimu ya MEMKWA. MEMKWA zote za Serikali zimekuwa na zimebaki chache tu zinazoendeshwa na Taasisi za Dini na *NGOs*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali irudishe madarasa ya MEMKWA kwani mpaka sasa kuna watoto wengi ambao wana umri mkubwa na hawajaandikishwa shuleni. Kama Serikali haina mpango wa kuendesha MEMKWA basi Serikali itoe ruzuku au Walimu kwa *NGOs* au Taasisi za Dini ambazo zinabeba mzigo au kuendesha MEMKWA.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba sana Wizara iangalie kwa jicho la huruma Wilaya ya Morogoro hususani Halmashauri ya Morogoro Vijijini. Hatuna Walimu wa kutosha wa Shule za Msingi na Sekondari hususani zile za pembezoni hatuna *A-Level*, katika Halmashauri yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha Shule za Sekondari za Nelson Mandela na Ngerengere Day kuwa *High School?*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika orodha ya shule zinazokarabatiwa mwaka huu wa fedha kuna shule ambazo hazipo Morogoro Vijijini kama Mgeta Sekondari, Melela Sekondari, Lupilo, Kauzeni na Isongo. Idadi hii ni kubwa kwani zimeziba nafasi ya Shule za Halmashauri yetu kama Shule ya Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya, naomba sana shule hii iingizwe kwenye orodha ya shule zitakazokarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, idadi ndogo ya Walimu hususani Walimu wa sayansi. Naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwahamisha Walimu wenyewe shahada ambao kwa sasa wanafundisha shule za msingi. Walimu hawa wapo na ni wengi sana.

Mhesiimwa Spika, naomba hata vijana waliofaulu masomo ya sayansi wapewe leseni ili waweze kusaidia kufundisha sayansi katika shule zetu. Naomba ongezeko la Walimu liende sambamba na ujenzi wa maabara na ununuzi wa vifaa vyta maabara angalau katika sekondari moja katika Tarafa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Juu; mficha madhara kifo kitamuumbua. Baadhi ya vijana wetu hawana maadili mema hata kidogo. Baadhi yao wamejingiza kwenye tabia mbaya hata kufanya ngono zisizo salama tatizo ni nini? Tatizo hili lipo na tukilifumbia macho madhara yake ni makubwa. Tukubali kukaribisha Taasisi na NGOs ambazo zina *interest* ya kuwasaidia vijana wetu ili kutunza maadili mema na usalama wa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba vyuo vyote vihimizwe kujenga Hosteli kwa ajili ya vijana wetu ili wasiishi hovyo tu bila hata mtu wa kuwapatia mwongozo wa maisha ya ujana. Aidha, uadilifu na maadili ya baadhi ya wakufunzi wa vyuo vyta juu ni matatizo. Kuna minong'ono ya rushwa katika mitihani hata kufikia uwepo wa rushwa ya ngono kwa upande wa watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeongeza wigo wa unyanyasaji wa kijinsia. *This is a bitter pill but we have to*

swallow it in order to stop this unfortunate situation. Haya mambo yatafutiwe dawa ya kudumu ili turudishe heshima ya vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya na lishe ya watoto mashulenii; kuna watoto ambao hawafanyi vizuri darasani kwa sababu za kiafya kama kutokuona vizuri, kutokusikia vizuri, pamoja na njaa, Wizara ishirikiane na wadau wengine ili kuhakikisha kwamba watoto wanapata *medical check up especially macho* na masikio, kwani matatizo haya yanatibika, wazazi wahimizwe kuchangia angalau uji kwa watoto ili kupunguza njaa.

Mheshimiwa Spika, lishe hii itasaidia kubadili uelewa wa watoto na hii imedhihirishwa na mabadiliko ya mahudhurio na uelewa pale ambapo chakula cha mchana kinapatikana.

Mheshimiwa Spika, michango ya madawati na mitihani iangaliwe upya kwani sasa imekuwa kikwazo cha maendeleo ya elimu. Hivi Shule inachangiwa madawati kwa miaka zaidi ya kumi, kulikoni na *reamza* karatasi Shule yenye watoto zaidi ya mia tisa hazitoshii? Serikali ipige marufuku michango isiyokuwa na msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nanaomba majibu ya hoja zangu.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze Hotuba yangu kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni ili tujadili.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo ningependa kuishauri Serikali na mengine kupatiwa ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa elimu; naomba Serikali iangalie upya mfumo utakaotumika katika kuendesha elimu yetu nchini kwa sababu anguko hili la elimu tunashindwa tutoe lawama kwa Wizara gani, yapo mambo

ambayo yanasababishwa na Wizara ya Elimu, yapo matatizo yanayosababishwa na Wizara ya TAMISEMI na mengine Utumishi.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu anapata shida sana kujuu wapi awajibike ningeomba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mitaala ya kufundishia; ni vema mitaala ingeboreshwa kuanzia Shule za Msingi na Vyuo vya Elimu. Kwa mfano, katika Shule za Msingi, darasa la kwanza kuwe na masomo matatu tu yaani K.K.K (kusoma, kuandika, kuhesabu) pia katika Sekondari mwanafunzi anapoanza kidato cha kwanza Serikali isibadilishe mtaala hadi wale wanafunzi wakatakomaliza, ili wasipate athari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya Walimu na madai yao; naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aeleze, Serikali inashughulikaje matatizo yao, madai makubwa wanayoidai Serikali mpaka kila siku wanatishia kuandamana. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuboresha maslahi ya Walimu kwani Mwalimu ana uwezo mkubwa wa kuboresha elimu au kuharibu elimu. Hivyo ili Walimu wapate moyo wa kufundisha waongezewe mishahara, kupunguza kodi wapewe nyumba.

Mheshimiwa Spika, kwa Walimu wanaojiendeleza kielimu, Serikali iwapatie mikopo, Walimu wanapokwenda vyuo vikuu kwani mishahara haitoshi kulipa ada, hivyo kwa kuwa wanalipa kodi wanahaki ya kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, vitabu vya kufundishia na kujifunzia Serikali iongeze angalau kila mwanafunzi apate kitabu wakati wa kujifunza. Pia katika suala la vitabu kuwe na vitabu sawa kwa nchi nzima vinavyotambuliwa na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho katika Shule za Sekondari; niipongeze Serikali kwa kuwa na shule nyingi karibu kila Kata. Lakini kama tunaitakia mema na kukuza elimu yetu nchini tuhakikishe Serikali ijenje Hosteli ili kuwasaidia wanafunzi hasa wasichana ili waweze kupata mazingira

mazuri ya kujisomea kwani wamekuwa wakipata vikwazo vingi sana kwa kupata mimba.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine katika shule nyingi hasa Shule za Kata ni ukosefu wa maabara, hivyo tunaomba kila Shule ya Sayansi iwe na maabara ili wanafunzi wasome kwa vitendo ili waweze kuelewa vizuri na kupata wanasayansi wazuri ikiwezekana kuwepo na (*moving Laboratory*).

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Walimu wasio na ujuzi na viwango sambamba na wito katika ufanisi wao, kwa mfano, wale maarufu kama *Voda Fasta* ambao Serikali tunaiomba kuboresha vyuo vyake ili tuweze kupata Walimu waliokusudiwa kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa vitendea kazi kama chaki, madawati na vitabu kwa Serikali, hivyo basi, Serikali pia iangalie uwezekano katika kufanikisha hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vigezo vinavyotumika kugawa pesa kwa shule zenye watoto wenye uhitaji maalum (Walemavu) Shule ya Sekondari ya Lugalo iliyopo katika Iringa Manispaa, ni Shule inayofundisha watoto wenye uhitaji maalum iwapo watoto wenye ulemavu wasioona na watoto *Albino* lakini Shule hii ina matatizo ya vifaa kama *typewriter* za hawa watoto, vitabu, pia Shule hii haina uzio na wakati wapo watoto wengi walemavu wa ngozi. Naiomba Serikali iangalie shule hii kwa sababu hata katika mgawanyo katika kitabu haijatengewa pesa yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mikopo ya wanafunzi; kuna malalamiko makubwa, bado katika zoezi la mikopo katika vyuo vyetu vikuu. Ningombaa Serikali iwe na mkakati wa jinsi ya kukusanya hiyo fedha ya mkopo, kwa sababu hawa wanafunzi wengi waliopatiwa fedha hizi hazilipwi ndio maana kila wakati Serikali lazima itafute pesa nyiningine.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie nani wa kupatiwa na kunyimwa mkopo yaani kitaamu *Mini-test*

haikidhi viwango. Maafisa wanaotoa mikopo vyuoni hawana viwango. Pesa ya wanafunzi inakatwa bila ridhaa yao. Maafisa mikopo wanaweka pesa, wanafunzi wanasainishwa, fedha ya *field* wakati pesa hiyo hawapatiwi yote haya ndio matokeo ya watoto kufanya maandamano, maafisa hawa ndio wanaihujukumu Serikali yetu. Je, ni chombo gani kinachoratibu hii mikopo mbona malalamiko mengi sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kwa kueleza matatizo ya elimu kwa sekondari za Kata na nikielekeza kwa Serikali iyatatue:

Mheshimiwa Spika, kuhusu mimba; tatizo la mimba limekuwa tatizo sugu kwa wanafunzi wa kike. Mfano, Mkoa wa Katavi, kwa mwaka 2012 wanafunzi wapatao 64 walipewa ujauzito na wote ni wanaosoma shule za kutwa na tatizo kubwa ni utandawazi, maisha magumu na wengine ni vishawishi vya usafiri wa bodaboda kwa kuwa wanaishi mbali na maeneo ya shule wanazosoma.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupiga marufuku matumizi ya simu kwa mwanafunzi ye yote yule shulen. Pia naishauri Serikali ijenge Hosteli za wanafunzi wa kike ili wakae shulen kuepuka vishawishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maabara; Shule za Kata hazina maabara, sasa tunawapataje wanasayansi kwa wanafunzi wanaosoma nadharia tu? Kwa hali hii tutaendelea kuwa watawaliwa kwenye soko la ajira kwenye nchi jirani kama Kenya, Uganda kwa kukosa kujiamini na kujitambua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme na *computer* ni wazi kwamba shule nydingi hazina umeme na TEHAMA haiwezi kwenda kama umeme na *computer* hakuna. Pia kama hatujawaandaa Walimu wa hizi Shule za Kata, basi TEHAMA ni hadithi kwa watoto wetu mashulen. Naishauri Serikali kuandaa mkakati wa dharura wa miaka mitano ili kila Shule ya Kata iwe na umeme na *computer* za kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chakula mashulen; suala hili Serikali ingetilia mkazo na kuwa ni lazima kila shule iwe na chakula cha mchana, ili kuwapa wanafunzi muda mwingi wa kukaa shulen na kusoma na kutoruhusu wanafunzi kuzagaa mitaani. Mfano, Mpanda Mjini katika ya shule tisa za Kata, ni shule mbili tu ndiyo zimefanikiwa kuwa na chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutilia mkazo suala hili na ikionesha mfano wananchi watafuata. Tatizo ninaloliona hapa ni mwamko mdogo wa wazazi juu ya elimu, kwani wazazi wengi hawaipi elimu kipaumbele, zaidi wanaelekeza nguvu kwenye shughuli za kiuchumi kama, madini, biashara, na kulima mpunga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji safi na salama; tunajua maji ni uhai tena maji ni afya. Lakini Shule hizi za Kata hazina visima virefu vya kuwawezesha wanafunzi kupata maji ya kunywa wala matumizi kwenye vyoo hasa kipindi cha kiangazi ni shida sana. Naishauri Serikali kuhakikisha inachimba visima katika kila shule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya Walimu; kuna udhalilishaji unaofanywa na Serikali katika Serikali tuijulize ni kwa nini Mwalimu mwenye Digrii mshahara wake ulingane na mshahara wa mtu wa cheti cha *Nursing* tena mwenye *Division Four* au ana D mbili tu. Lakini unakuta Mwalimu amefaulu Kidato cha nne na cha sita na Chuo juu. Naishauri Serikali, Sekta zote za Umma na Wizara ya Elimu walipwe mishahara kulingana na elimu zao, yaani ngazi za Cheti, Shahada na StaShahada na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Walimu; Shule za Kata, hazina nyumba za kukaa Walimu na zilizopo hazina viwango na ramani zake zimepitwa na wakati. Mfano, Shule ya Kasimba Sekondari, Mpanda, kuna Walimu 12 nyumba zipo mbili na Walimu waliobakia wanaishi uraiani kilomita saba mpaka kumi kufika shulen. Naishauri Serikali iwajengee Walimu nyumba za kuishi au iwakopeshe usafiri kama pikipiki ili waweze kuwahi katika vituo vyao vya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taaluma mashulen; wasiojua kusoma na kuandika kuingia Sekondari. Hii ni aibu kwa Taifa, nashauri Serikali iajiri Walimu wa Shule za awali katika kila Shule za Msingi na mwanafunzi asiyejua kusoma na kuandika asiingie darasa la kwanza. Hakuna haja ya mitihani wa KK kidato cha kwanza kubaini wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika kama hayo yote yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya kufundishia; kuna *gap* katika elimu ya sekondari na shule ya msingi hasa katika lugha ya kufundishia, nashauri Serikali ianzishe Programu ya lazima kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba angalau kwa miezi sita kusoma *English Course* ili wawe na uwezo wa kumudu lugha ya kufundishia mashulen. Au kama haiwezekani Serikali ibadili mtaala kuwa masomo yote yafundishwe kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kibakie kama somo tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yafuatayo kwenye hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis:-

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Ufundis Stadi; Kwimba, Mwanza, hii hoja ni ya siku nyingi, hii ni *budget* zaidi ya tatu, hiyo inaandikwa lakini haitekelezwi, naomba mwaka huu hii miradi itekelezwe. Shule 528 kati ya 1200 zilizo katika mchakato wa tathimini ya mahitaji ya miundombinu.

- | | | |
|-----------|---|--------------|
| (i) 331 | - | Mwamashimba; |
| (ii) 333 | - | Hukubifi, |
| (iii) 334 | - | Igongwa, |

Naomba mniongeze shule zingine hizi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Orodha ya Shule za Sekondari 1,200 zitakazofanyiwa ukarabati:-

- | | | |
|---------|---|----------------------|
| (1) 747 | - | Mwanashimba, Kwimba. |
|---------|---|----------------------|

- | | | |
|---------|---|-----------------------|
| (2) 750 | - | Mwanghalanga, Kwimba. |
| (3) 753 | - | Mwamala, Kwimba. |
| (4) 755 | - | Bupama, Kwimba. |
| (5) 757 | - | Ngjido, Kwimba. |
| (6) 758 | - | Bupama, Kwimba. |
| (7) 759 | - | Kikubizi, Kwimba. |
| (8) 762 | - | Igongwa, Kwimba. |

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuweka shule zote hizi kwenye mpango wa ukarabati wa *budget* ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri tatizo la watoto kufeli na pia inachangiwa na wazazi kutotoa muda, tunaangalia watoto hao wanafanya nini shulenii, mtoto anakuwa masaa nane shulenii lakini masaa kumi na sita yuko nyumbani, waulize wazazi wangapi wamekwenda shulenii kufuatitila mwenendo wa watoto wao, kama wamefika shulenii au vipi.

Mheshimiwa Spika, lingine ningeshauri msiendelee kuajiri Walimu wapya kabla hamjafanya uchunguzi, hao Walimu mliowaajiri awali wana utaalam wa kufundisha. Nashauri tena, hao Walimu wengi walio pale kwa ajili ya mishahara na posho tu, hawana *interest* ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii inayo dhamana kubwa ya kufundisha na kutayarisha vijana wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Wizara lazima uangaliwe upya. Naishauri Serikali kupitia Wizara hii iunde Wizara ya Elimu itakayosimamia Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari. Vile vile ianzishwe Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia (*VETA*) pia chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu fedha za mishahara na matumizi mengineyo katika vyuo vikuu

vya umma hapa Tanzania, lazima Serikali itoe fedha hizo kwa wakati. Wahadhiri na wafanyakazi katika vyuo hivi wanapandishwa vyeo lakini fedha hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo katika vyuo vikuu vya umma hazi pelekwi vyuoni. Mfano, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni kitu gani kimefanyika hata Chuo Kikuu Huria kisipewe fedha zake za maendeleo kama zilivyo idhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mheshimiwa Waziri akija atuambie ili tujiridhishe.

Mheshimiwa Spika, namtaka Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini fedha ya kujenga barabara iendayo Bungo ambako ndiko kuna Makao Makuu ya *Open University* hadi leo haijajengwa ili hali Bunge hili huwa linaidhinisha fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia matokeo ya mitihani Shule za Misingi na Sekondari. Idara ya Ukaguzi ambayo iko Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, lakini utekelezaji wake uko TAMISEMI iangaliwe upya ili kuondoa mkanganyiko uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtaka Mheshimiwa Waziri afute mgawo wa ujenzi na ukarabati wa shule kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Na naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, malalamiko ya Walimu Jimboni kwangu ni kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, ni nani hasa mwajiri wa Walimu? Ni Wizara ya Elimu, TAMISEMI au *TSD* iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa wa Umma inaratibu mambo yote ya madaraja, *Promotion*, nidhamu na *dismissal*, TAMISEMI, usimamizi na uendeshaji wa shule. Ni nini nafasi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa elimu na kwa Mwalimu kwa sasa?

Mheshimiwa Spika, ni nini uhusiano wa TAMISEMI, Wizara ya Elimu na NECTA juu ya nani hasa anapaswa kutangaza matokeo ya mitihani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukuza Kiswahili, Serikali, TUKI na BAKITA waache majoribio ya kukuza Kiswahili kuititia watoto wa maskini wanaosoma katika shule za umma ambako watoto wa viongozi na matajiri hawasomi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini *TSD* au Serikali haiitambui elimu ya *Masters* kwa Walimu. Mwalimu mwenye *masters* hana tofauti na *undergraduate*. Hakuna daraja analopewa Mwalimu akimaliza *master*. Ikitokea neema anapewa *increment* mbili tu ndani ya daraja hilo hilo bila kubadilishwa, kama alikuwa *TGSE two* anapewa *TGTS Four* je, ni haki? Walimu wanaomba utaratibu wa zamani wa Mwalimu wa *masters* kupelekwa *TGTS G*, (*Principal Education Officer II*).

Mheshimiwa Spika, wanahoji ni kwa nini kuna ubaguzi ndani ya Walimu? Mwalimu mwenye *degree* anayepangwa kufundisha Sekondari anaanza na ngazi ya mshahara wa *TFTS D I* na anayepangwa kufundisha Chuo cha Ualimu anaanza na *TGSE I*?

Tafadhali naomba kupatiwa majibu juu ya hoja hizi ambazo ni za kitaaluma zaidi na ni chanzo cha malalamiko mengi juu ya maslahi ya Walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Hata hivyo, upo upungufu mkubwa ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mfumo wa utawala katika elimu kuna upungufu mkubwa ikiwemo Wizara hii kutokuwa na utaratibu unaoeleweka kwani Walimu hawa wanasihamiwa na Wizara tofauti tofauti. Mara Walimu wanasihamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa. Waziri anayesimamia Walimu ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, sasa haki za Walimu hazieleweki zinasimamiwa na nani hasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Ukaguzi nayo imekuwa katika mazingira magumu ya namna inavyofanya kazi kwani Idara hii imebakishwa kuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu wakati Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari zinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kama Idara ya Elimu Msingi na Sekondari ziko TAMISEMI basi na Idara ya Ukaguzi nayo irejeshwe huko ili waweze kupata ushirikiano katika Halmashauri zetu kinyenzo. Aidha, kuhusu ukaguzi wa Shule ya Sekondari mgawanyo haukufanywa kwa uangalifu, kwani Wilaya nzima ya Mbogwe imepangwiwa shule moja hii ya Lugunga mgawanyo huo ni aibu tupu Wizara isahihishe.

Mheshimiwa Spika, madeni ya Walimu ni muhimu yashughulikiwe haraka ili kuepusha misuguano isiyo ya lazima imalizwe. Shule zetu za Misingi na Sekondari zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa Walimu, majengo ya madarasa na nyumba za Walimu katika Wilaya ya Mbogwe. Serikali ilijitahidi kutoa fedha za kutosha ili kurekebisha hali ya mazingira wanayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kushauri ngawo wa Shule ya Sekondari zinazokarabatiwa ni shule moja tu ya Lugunga ndiyo inayokarabatiwa ni aibu jambo hili.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la madai ya Walimu, ni kipindi kirefu Walimu wetu wamekuwa wakiidai Serikali madai na maslahi yao mbalimbali, ambayo kimsingi wanastahili kulipwa. Kwa hiyo, Wizara ifanye jitihada za kuwalipa Walimu hao, pamoja na kuwasaidia kuwapatia vielelezo ili viweze kuwasaidia katika malipo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Sera ya Elimu, tunajua kwamba, Wizara imo katika jitihada za kutayarisha Sera nzuri ya Elimu yetu, hivyo kwa kasi ile ile naitaka Wizara iendelee na hatua za kukamilisha sera hiyo na kuiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mradi wa Tawi la Chuo cha Mwalimu Nyerere Zanzibar, tulipokwenda ziara ya Kamati katika Chuo hicho tuliona kasoro nyingi katika Jengo la Chuo hicho, pamoja na ukosefu wa vifaa vya kazi, ikiwemo viti, meza na *Computer* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara ilifungua Jengo bila ya kufuata maelekezo ya Kamati, hivyo naitaka Wizara ituhakikishie kuwa je, jengo la Chuo limefanyiwa marekebisho kama yalivyohitajika? Je, kuhusu suala la kupatiwa vitendea kazi katika Chuo hicho limesifikia wapi, je, kuhusu ujenzi wa *Dahalia* ya wanafunzi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari Zanzibar, katika maeneo ya Chuo hicho tayari jengo moja limeshakamilika na natarajia iwapo litaendelea kukaa bure bila ya kutumika inawezekana sana linaweza kuharibika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naiomba Wizara kupeleka vifaa/vitendea kazi kama ilivyokusudiwa, pia Chuo hicho kipatiwe miundombinu ya maji, barabara, umeme, simu na kadhalika. Wizara ikamilishe haraka ujenzi wa jengo lingine ambalo tayari jamvi au *Foundation* limeshawekwa siku nyingi.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, kuhusu Wilaya ya Uvinza inayo majengo yanayofaa kuanzia kutumika kama Chuo cha *VETA*. Nashauri Halmashauri ya Uvinza isaidiwe ingizwe kwenye mpango kwani ina raia 350,000 na inazungukwa na Sekondari 20. Chuo hapa kitusaidie sana kwani vijana wa eneo hili wapo mbali na Chuo cha *VETA* Kigoma wapo mbali na Chuo cha Ufundii, Kasulu na hivyo wanahitaji kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, elimu inakufa, moja ya sababu kubwa ni udhaifu mkubwa katika ukaguzi. Shule Walimu hawafundishi na baadhi ya wakuu wa shule hasa Wilaya ya Uvinza ni walevi na hawajibiki. Mkuu wa Shule anashirikiana na Idara ya Elimu, Wilaya kula pesa za *Capitation* ambazo zingetumika kununua vitabu. Napenda kusisitiza sana kuhusu vitabu na ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Sayansi bado ni tatizo sugu, Wilaya nzima yenye kupata mgawo wa Walimu zaidi ya 40 tunapata Walimu wa Sayansi wanne. Nashauri mkazo zaidi kuandaa Walimu wa sayansi.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, suala la madai ya Walimu lazima lifikie mahali ambapo litaturidhisha kullko ilivyo sasa. Madai yao kama yamekwishahakikiwa malipo yao vema yangewekewa utaratibu wa kuyalipa badala ya kuendelea kuyalimbikiza mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, madai ya Walimu ambayo Serikali ilisema yamelipwa bilioni 52 mpaka sasa, Walimu wengine hawajalipwa mpaka sasa kwa madai kwamba hawakukidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, hawa Walimu wenye madai yao, Serikali ikamilishe utaratibu wa uhakiki na walipwe ili kuondoa malalamiko ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, posho ya mazingira magumu ilipendekezwa na Tume ya Makwetta siku za nyuma. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba Walimu wanafanya kazi katika mazingira tofauti. Wapo wanaoishi katika vijiji vya mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya ambako hawana usafiri wa kuaminika wanatembea kwa miguu umbali mrefu na hata wakipata magari wanapata magari ya mizigo na nauli zao ni kubwa, si chini ya elfu kumi kwa mtu au zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa Mwalimu kufika kwenye Wilaya kuchukua mshahara benki lazima awe na kiasi

kisichopungua elfu thelathini. Kwa mfano, shule za Masasi katika Kata za Lipumburu, shule nane za msingi Nantuna na Sindano ziko mbali na Wilayani.

Mheshimiwa Spika, Walimu wapewe posho maalum ya mazingira magumu, Walimu ndio msingi wa wataalam wote katika nchi yoyote kama msingi wa wanasyansi, wanasheria wataalam mbalimbali wa viwandani na kadhalika. Utakuwa mbovu tangu mwanzo! ni dhahiri pia kuwa utaalam katika nchi hiyo utakuwa mbovu.

Mheshimiwa Spika, ni vema sasa mazingira ya Walimu yakaboreshwa, Walimu wapewe motisha ili kuwaongezea ari katika kazi yao. Motisha za mafunzo kazini kozi fupi, semina mbalimbali zirudishwe kwa Walimu kama ilivyokuwa zamani. Ambapo zile kozi za mafunzo za masomo husika ziliikuwa zinasaidia na kuongeza ari ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mitihani yetu ya darasa la saba haitusaidii Watanzania mitihani ya kuchagua ya A, B, C, D inampima nini mtoto? Kwa nini mitihani isipime uwezo wa kutambua ujuzi na maarifa waliyofundishwa watoto mashulen? Mitihani wanayopewa sasa watoto wetu wanaweza kuifanya hata wakiwa wamefumba macho, ni mitihani ya bahati nasibu. Mfumo huu haufai, kwa nini Serikali isirudishe mitihani ya zamani ya (a) kujieleza (b) kujaza nafasi zilizo wazi?

Mheshimiwa Spika, masomo yanayofundishwa darasa la kwanza ni mengi, yapo saba badala ya kuandika, kusoma na kuhesabu (KKK). Watoto wa miaka sita na saba wanabebeshwa mzigo mzito kuliko uwezo wao. Mambo yanayofundishwa katika stadi za kazi na haiba ni mambo ambayo watoto wangeendelea kufundishwa kama *basic skills* na Walimu wao ambapo sisi enzi zetu tulifundishwa kwa nyimbo, namna ya kutunza meno, usafi kwa ujumla, kuliko kuweka kwenye masomo yao na kuwataka watoto kuwapima katika mihula yao. Watoto wanafundishwa sayansi, hesabu, kiswahili (lugha kusoma na kuandika) stadi za kazi, haiba na michezo na TEHAMA ni mzigo mkubwa kwao.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, kama wote tujuavyo katika karne hii maendeleo ya nchi nyingi yanategemea rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, nchi iliyowekeza katika kutayarisha rasilimali watu inajikuta ikipata maendeleo makubwa. Rasilimali watu hiyo haipatikani tu bila kuwekeza, inapatikana kutokana na elimu bora.

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa elimu unahitaji marekebisho makubwa sana. Rasilimali watu haiwezi kupatikana nchini Tanzania ikiwa hatutatoa haki na fursa sawa ya elimu kwa watoto wetu, lazima sisi kama Taifa tuweke vipaumbele ili kuwapa Walimu mazingira mazuri ya kufanya kazi na ni lazima tuwalipe vizuri Walimu hawa ambao ni muhimu katika utoaji wa huduma bora ya elimu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona sekta ya elimu imetelekezwa Walimu hawana morali ya kufundisha, wengi wanakwepa kuwafundisha watoto wetu na kujingiza kwenye biashara ili waweze kumudu maisha.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa mikopo kwa Walimu ili Walimu waache kudanganywa na kujikuta wanakopa hadi hela yao ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, mitaala iliyopo ni mibovu, hakuna mtaala wa elimu wa kudumu kwa kuwa mtaala haueleweki na *syllabus* nazo henzieleweki vitabu havieleleweki na vinamtenga mwanafunzi wa kiwango hiki.

Mheshimiwa Spika, mfano, somo la *geography* mtihani mwaka 2012, kidato cha nne swali la sita ambalo ni la lazima, mtunga swali alitumia *syllabus* ya mwaka 1977 na wakati *syllabus* iliyotumika kumfundisha ni ya 2012 na katika shule nyingi ni ya 2010 ndio inatumika.

Mheshimiwa Spika, swali hilo lilikuwa *topic* inayohusu *levelling in land survey* hii ni *syllabus* ya 1997. Kwa hali hii

wanafunzi watakaoweza kujibu swali hili labda tu wale waliofundishwa na aliyetunga swali hili.

Mheshimiwa Spika, tofauti ya Mwalimu aliyetoka *UDSM* ni tofauti na aliyetoka *UDOM* sababu hakuna uhuishaji wa mitaala, matokeo yake wanafunzi wanakuwa wanaeleweshwa tofauti kwa maana hiyo kwenye mitihani ya Taifa, watakaofaulu vizuri ni wale tu waliofundishwa na Walimu waliotoka katika Chuo Kikuu alichosoma Mwalimu mtunga swali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAROUB M. SHAMIS: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) kwa neema na rehema zake nyingi kwangu na familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, elimu ndio ufunguo wa maisha ya duniani na hata maisha ya akhera (baada ya kufa) Mtume Muhammad (*Swalallah Alayh Wasalaam*) amesema: anayetaka dunia asome; anayetaka akhera (*pepo or heaven or paradise*) asome na anayetaka vyote viwili hivyo pia asome!

Mheshimiwa Spika, falsafa hiyo inatakiwa nguvu na kauli ya Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) aliyoisshusha kwenye sura ya kwanza aya ya mwanzo ya *Qur-an* amesema *Iqraa* kwa maana ya soma!

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo wa kusoma niliouonesha katika utangulizi ni lazima kuwepo na uadilifu kwa wanafunzi ili kujenga Taifa la watu wenye uwezo wa kweli wa kielimu.

Mheshimiwa Spika, tatizo liliopo katika sekta ya elimu nchini ni upendeleo wa wazi na usio na chembe ya aibu unaofanywa hasa na Baraza la Mitihani. Inakuwaje viwango vyta ufaulu (*pass marks*) zitofautiane kwa masomo ya lugha? Pia masomo ya *Islamic knowledge* na *Bible knowledge*?

Mheshimiwa Spika, kwa nini *Islamic knowledge* kuanzia 35-59 iwe "c" na kwa nini *Bible knowledge* iwe 35-49 tu ndio "c"? Mwanafunzi anayesoma *Islamic* mpaka apate kuanzia 60% ndio apate "B" wakati anayesoma *Bible* akipata 50% tu tayari ameshapata daraja "B"?

Mheshimiwa Spika, huu ni upendeleo wa dhahiri na wa makusudi na si jambo la kufumbiwa macho hata kidogo. Ni lazima waliosababisha matatizo haya wachukuliwe hatua haraka sana, kwani bila ya kuadhibiwa wahaini hawa nchi ndio itakuwa tunaichimbia kaburi; kwani watarithishana uovu. Tabia njema hurithiwa na mbaya pia hurithiwa. Ni kwa kuwajibishwa tu ndio tutajenga *discipline*, nchi itakuwa nchi ya majuha!

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine lilitotamalaki katika sekta ya elimu na hasa Baraza la Mitihani ni wizi wa mitihani! Mitihani inaibiwa kwa makusudi kabisa na kuuzwa katika shule nyingi za *seminary*, imekuwa ni biashara tu na shule hizo zinatumia fursa hiyo kujitangaza sana kuwa eti wanafunzi wote wamefaulu *Division one!* Hakuna *Division Four* kwa upeo gani walionao Walimu hao! Kama si kuwapa majibu ya mitihani.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni lazima likome sasa, na tatizo hili ndilo limepelekea hivi sasa tukawa na wasomi vihiyo, wasomi wetu hawana uwezo hata kidogo. Hii ni aibu, fedheha na janga kwa Taifa. Tatizo hili ni kubwa, tena kubwa sana na Waziri wa Elimu tutakuwa hatumtendei haki kumwachia peke yake mzigo huu mkubwa wa matatizo lukuki ya elimu. Ni lazima Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakae na wamsaidie Mheshimiwa Rais kumshauri juu ya suala hili ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nchi hii inaangamia na vyeti bandia hivi tunavyokusanya vyta nini? Tunashindwa hata katika ajira za ndani ya nchi yetu tu mpaka zinachukuliwa na wageni kwa sababu ya ukihiyo wetu. Je, tutawezaje kushindana katika ajira ya soko la *East Africa Community* na soko la dunia hii ya utandawazi kwa ujumla wake!

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Rais wangu mpendwa Dkt. Jakaya Kikwete airudishie heshima yake ya kielimu katika nchi hii. Asiwaone albu watendaji wabovu wazembe na wabadhirifu kwa makusudi hasa wa Baraza la Mitihani na Bodi yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu anajitahidi sana kutekeleza majukumu yake, lakini maji haya ni mkondo wa Nungwi, nguvu ya juu zaidi inahitajika kupiga ufagio wa chuma (*iron broom*) katika Baraza la Mitihani na Bodi yake. Pamoja na hayo, lidara ya Ukaguzi iimarishwe na motisha kwa Walimu izingatiwe hasa Walimu wa vijijini kwenye mazingira magumu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Mheshimiwa Waziri alete Muswada wa sheria ya kudhibiti wizi wa mitihani, sheria ambayo itatoa adhabu kali ya kifungo jela kwa wahusika wa kuvujisha na kuiba mitihani.

Mheshimiwa Spika, bila ya adhabu kwa wakosaji haki na uadilifu ni muhali.

Mheshimiwa Spika, inawezekana timiza wajibu wako. Nakushukuru sana.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana kama walivyosikitishwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutokana na upendeleo wa kuchagua shule za sekondari ambazo zitakarabatiwa ambapo licha ya Wilaya zingine kupewa fedha nydingi na idadi kubwa ya shule walizopewa kukarabati, Wilaya yangu ya Bahi imepewa shule mbili tu za Chibelela na Chikola. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapobatilisha, mgao huo basi pia Wilaya yangu ya Bahi ipewe umuhimu pia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya shule zilizotajwa katika kitabu cha bajeti, ukurasa wa 120 kuwa ni shule za Wilaya ya Dodoma Vijijini, Wilaya hiyo ni ipi wakati kwa mujibu wa sheria, Wilaya ya Dodoma Vijijini haipo toka mwaka 2007 na sasa

baada ya Wilaya hiyo kugawanywa tuna Wilaya ya Bahi na Chamwino.

Mheshimiwa Spika, sasa nashangaa katika idadi hiyo ya shule za Wilaya, hiyo ya Dodoma Vijjjini ambayo haipo shule ya sekondari ya Chibelela ambayo awali imeoneshwa ni ya Wilaya ya Bahi (ukurasa wa 120 na 32) na katika ukurasa huo huo wa 120, shule hiyo tena inaoneshwa ikiwa ni ya Dodoma Vijjjini ikiwa ya namba 44.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi wa jambo hilo na kama ni shule nyingine katika Wilaya yangu ya Bahi nifahamishwe. Lakini siungi mkono bajeti mpaka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amefuta mgao huo na kugawa hizo fedha kwa uwiano.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na pia kuwapa pole Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wote wawili wa Wizara hii kwa kazi ngumu ambayo inawakabili bila shaka, mlezi wa mtoto ndiye anayetupiwa lawama pindi mtoto akikosea. Hivyo, nanyi mbebe tu huo mzigo.

Mheshimiwa Spika, shule zetu zinahitaji na ni lazima ziwe na maabara za kisasa ili vijana wetu wote wapate fursa ya kujifunza masomo ya sayansi ikiwa hakuna umeme, tuweke hata umeme wa *solarambao* hauna gharama kubwa, kwani vijana hao wanafanya mitihani sawa na wenzao wala hakuna msamaha wanaopata.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Elimu itolewe TAMISEMI kwani hata gari likiwa linaendeshwa na madereva wawili kwa wakati mmoja litaanguka tu na ndio maana leo hii kuna migogoro mikubwa ya Walimu na Serikali yao kutokana na urasimu uliopo wa kuweza kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, naomba shule zote zijengewe mabweni ili kuepuka watoto wetu wa kike kubakwa ovyo

ovyo na kuuawa kutokana na masafa marefu wanayokwenda kufuata elimu.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hasa waliopo vijijiini. Unakuta Walimu hawa wanahangaika, hawana nyumba za kukaa, hawana vitendea kazi na wengine wanatoka umbali mkubwa kufuata mishahara yao na hii imekuwa kero kubwa kwa Walimu wanaofundisha vijijiini (pembezoni). Ni lini Serikali itaboresha miundombinu vijijiini na mawasiliano, huduma za benki ili Walimu wapate mishahara yao kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Walimu wamekuwa wakijishughulisha na biashara ndogondogo za kuuza vitumbua, ubuyu, karanga na kadhalika, muda mwingi wanakuwa wanajishughulisha na biashara zao tu binafsi kwa ajili ya kusomesha ili kukidhi mahitaji yao. Hii inapelekea wanafunzi ambao wanasona shule za Serikali kufeli kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itahakikisha inaboresha mishahara ya Walimu na kuwalipa Walimu madeni yao yote wanayoidai Serikali na Walimu hawa kutengenezewa mazingira mazuri ili kuipenda taaluma yao ili Walimu hawa wasiendelee kufanya biashara ndogo ndogo za kuwadhalilisha vile vile wanapodai mishahara yao wapewa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya *Nursery* (chekechea), naiomba Serikali itoe kipaumbele kwa elimu ya chekechea. Vile vile shule zote za Serikali zinazotoa elimu ya chekechea, naiomba Serikali wanafunzi wote wa chekechea wapewe uji wa lishe (lishe) kwani watoto wengi hawana lishe tofauti na enzi ya utawala wa Rais wa Awamu ya Kwanza, Mheshimiwa Mwalimu Nyerere na utawala wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa chekechea walikuwa wanapewa uji wa lishe, wanafunzi hawa wa

chekechea walikuwa wanatoka kwao na vikombe nya kuwekea uji na hata ule ufundishaji wa zamani tofauti na sasa hivi, kwani zamani wanafunzi wa chekechea walikuwa wanakwenda na vijiti, visoda, sasa hivi unakuta wanafunzi wa chekechea wanakwenda kusoma huku wamechukua *game*. Hii inajenga msingi mbovu wa elimu kwani samaki mkunje angali mbichi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufeli kwa wanafunzi kuna baadhi ya wanafunzi wanaofeli mitihani kufeli kwao mitihani haisababishwi na Walimu bali inasababishwa na Serikali na wazazi. Kwani Walimu walikuwa wanaidai Serikali malimbikizo ya madeni yao na nyongeza ya mishahara na Walimu wakatangaza mgomo hawafundishi wanafunzi mpaka wapate haki zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikawalazimisha Walimu wasomeshe kwa lazima bila hiari yao na huku wana mgomo baridi. Sasa hapo wa kulaumiwa ni nani Mwalimu au Serikali? Kuna baadhi ya wazazi hawafuatilii nyendo za watoto wao. Kuna baadhi ya wanafunzi wamejingiza kwenye starehe kwa mfano, *facebook internet*, simu za mikononi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanafunzi wanapoaga wanakwenda shule, huwa hawafiki shule. Kwa mfano, vyuo viliviyotuzunguka hapa Dodoma *UDOM, CBE* na kadhalika. Kuna baadhi ya wanafunzi wa Chuo hawashughulikii masomo kazi yao kushughulikia ngono, kupiga picha za uchi na kuzirusha kwenye *facebook* na wengine kujiuza.

Mheshimiwa Spika, je, wanafunzi hawa wakifeli wa kulalamikiwa ni nani? Nawashauri wazazi wafuatilie nyendo za watoto wao wasiwaachie Walimu peke yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ufundi stadi (*VETA*), naiomba Wizara, hii iwe chini ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia. Endapo itarudishwa katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia, tutaweza kupata vijana wenye taaluma nzuri na ambao wataweza kujiajiri wao wenyewe katika soko la ndani na soko la nje na kupunguza mzigo katika Wizara ya Elimu.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, elimu inayotolewa katika shule zetu za sekondari ukiachana na somo la Kiswahili masomo yote yanayotolewa kwa lugha ya Kiingereza wakati uzalishaji wake wa lugha ya Kiingereza inakabiliwa na changamoto zikiwemo ukosefu wa Walimu wa Kiingereza na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo wanafunzi wanaosoma kwenye sekondari zetu huwa hawaelewi ipasavyo, maneno yao kwa biolofia, fizikia, geografia na kadhalika kwa ukosefu wa kujua Kiingereza. Hivyo, hali hiyo ndio sababu mojawapo inayosababisha wanafunzi wetu kutofaulu ipasavyo. Huwa wanafunzi wamekosa msingi madhubuti kutoka shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imejipanga vipi kuondoa changamoto hizi ili elimu yetu iwe na ufanisi ukitilla maanani elimu ndio msingi wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Walimu ni wafanyakazi kama walivyo wafanyakazi wengine wanahitaji kusimamiwa katika kazi yao ya kufundisha. Kitengo cha ukaguzi hakifanyi kazi zake zinazopaswa kutendwa kwa ukosefu wa vitendea kazi. Matokeo yake Walimu kwa kukosa kukaguliwa ipasavyo wamekuwa baadhi yao utendaji wao ulio chini ya kiwango. Hivyo basi, ipo haja Serikali kukiimarisha kitengo hiki na kukiwezesha ili kiweze kufanya ukaguzi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utaratibu wa kuwa na mitihani ya Kitaifa. Ni utaratibu mzuri, lakini iko haja ya makusudi kuangalia changamoto zinazowakabili wanafunzi waliko katika maeneo ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, shule zilizo katika maeneo hayo zina upungufu mkubwa wa Walimu wa masomo mbalimbali kwa sababu Walimu wanaopangwa kwenda huko huwa hawaendi. Sasa ni dhahiri shule kama hizo kuwa na mitihani ya Kitaifa pamoja na shule ambazo za Walimu wengi tena kwa kila somo itakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Spika, ipo haja basi, Serikali kuhakikisha kuwa inaweka mazingira bora katika maeneo ya mazingira magumu ili walimu waweze kukaa katika maeneo hayo. Ahsante.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa nchi yoyote duniani kama inahitaji maendeleo ni lazima kuwekeza kwenye elimu kwa kuwa elimu ndiyo mambo yote, ninaposema elimu siyo ya darasani tu hata kutembea mahali na ukaona jambo jema na la maendeleo bila shaka utakuwa umejifunza.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliotembelea Malaysia au Indonesia utaona jinsi gani Mwalimu anavyothaminiwa kwanza mwalimu wa nchi hizo ni yule anayepata ufaulu wa juu, sio kama hivi kwetu Mwalimu ni yule wa daraja la nne. Pia mshahara wa Walimu wa nchi hizo ni mzuri na unavutia sio kama huku kwetu. Mshahara wa Mwalimu haumalizi siku hata kumi.

Mheshimiwa Spika, mshahara wa Mwalimu wa msingi ni sh. 277,000 kabla hajakatwa kodi na akikatwa kodi anabaki na sh. 220,000 hivi kweli kwa mshahara huu kwa nini Mwalimu asiuze kachori ni nini kitazuia asiuze barafu na visheti, anapata moyo toka wapi wa kufundisha kwa bidii. Hebu tuijulize haya na tuache kutafuta mchawi wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kodi wanayokatwa Walimu au wafanyakazi wa Serikali ni kubwa, ni vyema Serikali ikapunguza kodi hiyo. Pamoja na hayo, ukosefu wa vitabu na hata maabara vinachangia kufanya vibaya kwa wanafunzi mashulenii. Hebu tazama kuna baadhi ya shule za sekondari darasa moja lina wanafunzi 90, shule za msingi zingine hadi wanafunzi zaidi ya mia moja na hamsini, hilo ni darasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nyumba za Walimu ni haba au hakuna maeneo mengi, pia ubabe mwingu na kutowajibika sawasawa katika Halmashauri hapa nchini dhidi

ya Walimu. Walimu hawaendelezwi na wanapoamua kuijendeleza kwa gharama zao ili wasipitwe na wakati katika ulimwengu wa kisasa, Halmashauri zinawanyanyasa na hata kufikia kuwafungia mishahara yao ili hali sheria inawaruhusu kuijendeleza na pia inakuwa Mwalimu husika ametimiza vigezo, hivyo elimu bora inatoka wapi na Walimu hawaendelezwi. Pia kuna Walimu wanataka kuijendeleza kwa fedha zao, lakini fedha zao hazina thamani kwani hawaruhusiwi.

Mheshimiwa Spika, hebu tazama Mwalimu mwenye *Degree* anaanza kazi analipwa mshahara wa shilingi 532,000, lakini *basic salary* baada ya makato anabaki mkononi na shilingi 430,000 lakini tofauti ya fani ya Daktari na hata kada ya sheria. *Degree* wote wamesoma na hasa Mwalimu ndio mambo yote maisha wote ni sawa. Kuna sababu gani Walimu wasiwe wajasirilamali na tutazikwepa vipi sifuri kwa watoto wetu? Tazameni hili shirkianeni na utumishi mtatue hili.

Mheshimiwa Spika, kama hatutowajali Walimu kwa mishahara mizuri, madai yao kuwaongezea elimu tukukubali kuwa *zero zitaongezeka*. Kama hivyo ndivyo, ni lazima tuje tutajenga Taifa la wajinga na kuwa na matabaka ya watoto wa wakubwa ambao wanasoma shule binafsi na watoto wa walalahoi ambao wako shule za Kata ambazo ndio nydingi na hazina Walimu.

Mheshimiwa Spika, nyumba ni tatizo kwa Walimu, mazingira ni magumu, hivyo ni vema sasa Serikali iwekeze kwa nguvu zake zote. Elimu ndio itatutoa hapa kwenda sehemu nydingine kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ningependa ajue kwanza Geita sio Mkoa wa Mwanza, pili katika Jiji la Mwanza shule za ukarabati ni mbili tu na Manispaa ya Ilemela shule ni moja tu, hii sio haki, ni bora mgao huo ukaangaliwa upya ili kuleta usawa.

Mheshimiwa Spika, pia kuwe na mpango wa Walimu kuwaelimisha vijana kuhusu mitandao, faida na hasara zake

ili kuwakomboa vijana katika janga la mitandao isiyo na misaada ya maadili kwao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyosomwa na Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali inaona raha gani kila mwaka kuleta bajeti yenye upungufu na inayojirudia katika madeni ya Walimu huku ikishangaa kushuka kwa kiwango cha elimu, hebu tujaribu mwezi mmoja hasa kipindi cha Bunge kusitisha malipo yote ya Wabunge. Kuacha kuweka mafuta katika magari ya Mawaziri na Manaibu wao pamoja na watendaji wao na kusema madai maana mkuki kwa nguruwe.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali sasa tuseme madeni ya Walimu, sasa basi zitafutwe pesa na walipwe stahili zao ili tujadili mengine ni aibu kwa Serikali, kudhalilisha walimu na kuwapelekea kukopa kwa makampuni ya kitapelli kama ya *BAY PORT* yanayojipitisha huko vijijini kusikokuwa na mawasiliano ya uhakika na kufanya ulaghai mkubwa kwa Walimu na kuwatia umaskini mkubwa na kuwakata pesa zao kwa kupitiliza deni walilokopa toka sh. 1,030,000/= hadi 3,452,993.30, ongezeko la 2,742,649.35; Walimu wanataaabika, Serikali inatoa ahadi nyingi, hebu mwokoe taaluma hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwasaidie Walimu kupata haki zao mfano, Mwalimu Zeno M. Kijuu wa simu namba 0785 521708 wa Kondo Chemba, ameibiwa pesa na *BAY PORT* tangu 2008 - 2013 kwa kukatwa mshahara bila kikomo.

Mheshimiwa Spika, lishe mashulenii; nani asiyejua bila shibe uelewa ni hafifu, sisi tulisoma vizuri, leo kizazi hiki tunakitesa. Serikali iweke ulazima wa wanafunzi kuanzia awali sekondari wapatiwe chakula mashulenii. Kuhusu elimu bure si kweli, leo kuandikisha mwanafunzi wa darasa la kwanza

kuanzia sh. 15,000 hadi 30,000 michango haina ukomo tusidanganyane Serikali itoe tamko.

Mheshimiwa Spika, sekondari za Kata, wazazi hutozwa faini hadi sh. 20,000/=, iwapo watachelewa kulipa ada hutozwa hela za kusimamia mitihani, kulipia dawati, kulipia Walimu wanaojitolea wa sayansi na Mwalimu mmoja hufundisha hadi shule tatu na zaidi. Je, huo ndio ubora wa elimu? Hii ni elimu bure Serikali hayo yote ni matatizo na upungufu mnaosababisha, nataka kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa walemaru; walemaru hawatendewi haki hasa viziwi mfano, shule ya Msingi Msasani Mwalimu mmoja, wanafunzi kumi, je, ndio uwiano? Lakini wapo Walimu wanaojitolea Serikali haiwajali kwa lolote, hii ni haki? Hivi hawa walemaru walimkosea sana Mungu hadi muwatekeleze namna hii, nataka majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, je, unayo habari ya mrundikano wa Maafisa Elimu ya msingi, Wilaya ya Mvomero wapataao ishirini ambao inasemekana hawana hata kibali toka *Management* ya Utumishi wa Umma ambapo kila Mkurugenzi anateua watu wake mionganoni mwa Walimu ndani ya Wilaya hiyo na kusababisha mrundikano katika Ofisi na upungufu wa Walimu? Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hii ni taarifa toka kwa baadhi ya wakazi wa Mvomero na majina ya watumishi hao wameyataja.

Mheshimiwa Spika, nataka kauli ya Serikali kuhusu fedha za MMES na MMEM zinazostahili kupelekwa shulenii kwa kila mwanafunzi. Katika baadhi ya shule, hali ni mbaya, pesa hazipelekwi hasa vijijini, kipi kinasababisha na hata kama zikipelekwa hazizidi shilingi 300 kwa mwanafunzi tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kutoa motisha kwa Walimu wanaofundisha pembezoni na katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ni kati ya Wilaya yenye matatizo makubwa ya miundombinu hasa

kipindi cha mvua kwa kuwa ni Jimbo kubwa, Kata 23 na baadhi ya Kata hazina mawasiliano ya simu. Hivyo Walimu wanaopelekwa huko hupata maisha magumu sana. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu motisha kwa Walimu hao.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2013 niliongozana na *NMB* kupeleka madawati 76 katika shule ya msingi Mtiyangimbole na Kidete hali niliyoikuta ni mbaya, wanafunzi wa darasa la nne na tano wanasoma katika Banda la Nyasi liliilo wazi, ni miti tu, wamekaa chini hawana hata ubao, chini tope, kwa sababu ya mvua na baadhi yao hawajui kusoma wala kuandika. Je, Serikali kwa nini haipeleki hela za MMEM kama inavyosema? Ingawa Mkurugenzi anajitahidi lakini anashindwa kutekeleza yote kutokana na Hazina kutopeleka fedha kama mnavyotamka. Hii ni fedheha kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya kutatua matatizo ya Walimu na miundombinu pia upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, wakati wa maneno uondoke na iwe vitendo zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini Serikali ilinyang'anya shule za misionari halafu mmezitelekeza bila kuzikarabati, mfano shule ya sekondari Kilombero, hali ni mbaya sana na paa linavuja sana, lakini kwenye kitabu hamkuitaja.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, wataalam kwa ajili ya kazi na juhudhi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mshahara wa Walimu utazamwe upya na nyongeza iongezwe ili kuwapatia Walimu maisha bora na wao watoe elimu bora. Pia ukaguzi iwe idara huru yenyе Mkaguzi Mkuu ngazi ya Taifa na chini yake Wakaguzi wa Halmashauri awe chini yake.

Mheshimiwa Spika, Bodi za shule za sekondari na Kamati ya shule za msingi ziimarishwe na zifanye kazi ya *oversight*.

Mheshimiwa Spika, baraza la Mitihani na taasisi ya elimu zifanyiwe *overhaule* na *structure and functions* zake zione na mahitaji yetu ya elimu ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo kwa elimu ya juu iundwe upya, *composition, functions* na *procedures* ili ibaki *relevant functional efficient and transparent*.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwenye kurehemu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoa na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimestushwa sana na uamuzi wa Wizara kuondoa masomo ya dini katika orodha ya masomo yanayofanyiwa mitihani, inawezekana Serikali ina sababu nzuri ya uamuzi wake, lakini ilipaswa kuwashirikisha wadau wote. Serikali inapaswa kutafakari kwa kina mara mbili juu ya uamuzi wake huu na kufanya tathimini juu ya hasara na faida juu ya kutofanyiwa mtihani masomo ya dini.

Mheshimiwa Spika, masomo ya Dini zote yana umuhimu kwa jamii ya nchi yoyote duniani inayopenda maendeleo. Dini inajenga watu wenye heshima, watu waaminifu, watu waadilifu, watu wachapakazi, watu wasiopenda vurugu, watu wenye akili na watu wanaopenda nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kitabu kitukufu *Qur-an* inasema nanukuu: "Mtiini Mwenyezi Mungu na Mitume na wale waliopewa uongozi mionganoni mwenu." Kwa hiyo, aya hii inajenga raia wema na watiifu kwa Serikali yao. Ukienda kwenye Biblia utapata dalili kama hizo. Sioni sababu ya Serikali kuondoa masomo ya dini katika mitihani, naomba Waziri ukisimama unieleze kwa kina ni sababu gani za msingi.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono Hotuba hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani lazima lifanyiwe marekebisho. Ni wazi kuwa hatuna maelewano mazuri baina ya Wizara na Baraza, zaidi ya hayo Baraza halifahamiani na Serikali ya SMZ, kwa maana ya Wizara ya Elimu Zanzibar. Mkurugenzi huyu wa Baraza anafanya mambo anavyotaka ye ye na hakubali ushauri wa mtu yeyote. Wizara ya Elimu Zanzibar kupitia Mheshimiwa Waziri wa Elimu hailewani na Baraza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lilitotokea la wanafunzi wengi waliofelishwa somo la Dini ya Kiislamu limesababishwa moja kwa moja na Mkurugenzi. Hivyo hatua zichukuliwe haraka za kulisafisha Baraza, hatua hizo ni kulivunja Baraza na kumwondoa Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Scholarship; Scholarship* kutoka nje hazigawiwi kwa Zanzibar na kama zinapelekwa ni kidogo mno. Wakati mwingine hupelekwa zikiwa zimechelewa sana. Hii husababisha wanafunzi wa Zanzibar kukosa nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugumu wa mitihani; mitihani inayotungwa ni migumu mno. Wanafunzi hawa hawana Walimu wa kutosha pia hawana maabara na vitabu. Hivyo, wanafunzi hawa hawajatayarishwa vizuri. Hivyo, ni lazima tutoe mitihani ambayo inalingana na hali halisi ya mazingira ya shule zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo Vikuu; baadhi ya vyuo vikuu vya binafsi havina Walimu wa kutosha. Baadhi ya Walimu hao wana digrii ya kwanza tu, wakiwa bado wanasoma digrii ya pili. Vile vile *syllabus* hazimalizwi kusomeshwa. Nashauri kwa kila somo, mtihani uwe na *paper* mbili za mtihani. *Paper* moja ya mtihani itayarishwe na Mwalimu kutoka chuo kingine na *paper* ya pili itoke ndani.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mlugo, alipofanya ziara katika Jimbo langu la Kwela na alipelekwa shule ya sekondari Uchile, iliyopo mji

mdogo wa Laela, alijionea mwenyewe jitihada za wananchi na wafanyabiashara walivyojitolea kujenga ile shule. Je, ni lini ataipitisha kuwa na kidato cha tano na sita na Vuna sekondari kama alivyoahidi?

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara kwa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Walimu; Walimu hawatoshi, waliopo tuwagawe vizuri tukiangalia maeneo yenye shida zaidi, hasa pembezoni. Tuangalie haki zao na stahili zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyuo vyua ualimu; tunaomba viongezwe na kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, wazazi wajali na kuongoza wanafunzi/watoto wao, kwani wana mchango mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitabu; ubora wa vitabu uangaliwe sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya awali; elimu ya awali itiliwe mkazo ni ya msaada mkubwa. Mtoto anayepata elimu ya awali anaanza elimu ya msingi na *advantage*.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kusema kuwa siungi mkono hoja hii mpaka nipate majibu ya maswali yangu na kupata ufanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa yale yote nitakayoainisha hapa chini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu inaonekana kuyumba katika utendaji, jambo ambalo linasababisha madhara makubwa kwa baadhi ya wanafunzi. Matokeo ya kidato cha nne yanadhihirisha hayo. wanafunzi wamefelishwa na baadhi yao wamejiua kwa fedheha ya kufeli. Wizara imepitia upya matokeo hayo na wale waliofeli wamepasi. Sasa, je, Serikali haioni kuwa imesababisha vifo vyua wanafunzi kwa uzembe na kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kiini cha matatizo yote hayo ni Baraza la Mitihani ambalo mara zote limekuwa likilalamikiwa kwa mfano, mwaka jana wanafunzi Waislam walifelishwa kwa makusudi somo la Dini (*Islamic Knowledge*). Waislam walipolalamika yakafanyika marekebisho na wale waliofeli wakaonekana wamefaulu.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali haioni fedheha juu ya hili? Kwa nini Baraza la Mitihani halivunjwi? Serikali ina *agenda* gani kwa wanafunzi wa walalahoi? Mheshimiwa Waziri haoni aibu na kwa nini hajizulu ili kutoa nafasi kwa wengine? Hivi majuzi kumejitokeza minong'ono na manung'uniko kutoka kwa Waislam kuwa eti somo la Dini limeondolewa kwenye mitaala. Je, kuna ukweli kiasi gani kwenye suala hili? Kama ni kweli Waislam wakiandamana mtawafunga ghafla kwa madai ya kuvunja amani na utulivu?

Mheshimiwa Spika, Waislam walioandama kwa kushinikiza dhamana ya Muislam mwenzao Sheikh Ponda Issa Ponda walifungwa haraka haraka, lakini CHADEMA wameandamana na kusababisha watu kupoteza maisha, lakini mpaka leo wahusika wanatembea huru uraiani. Waislam wana makosa gani kwa Serikali yao?

Mheshimiwa Spika, natarajia kupata ufanuzi wa kina na majibu yanayojitosheleza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na nikiridhika, nitaunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, Elimu ya Tanzania imekuwa inashuka kila mwaka kutokana na Serikali kutosikiliza ushauri wa wadau wa elimu wakiwepo wahadhiri, wasomi waliobobeaa kwenye fani za elimu, Wabunge na hata Walimu na Tume mbalimbali zinazoundwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote isiyoweka elimu ni kipaumbele cha nchi, ni Serikali ya kuogopwa kwani waliopewa dhamana hawaelewi kuwa elimu ni kitovu cha maendeleo ya Taifa lolote na hivyo kushuka kwa elimu ni kudidimiza Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu Serikali kuchukua mifumo na taratibu zisizofanyiwa utafiti wa kina na kuweka kwenye utekelezaji. Serikali inaiga mambo kutoka nchi nyingine bila kupima na kuona itakuwa na tija ndani ya nchi au la!

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleze Bunge ni vigezo gani walivyotumia kuondoa utaratibu wa mitihani ulio kuwepo na kuweka utaratibu wa mitihani ya *multiple choice* (kuchagua ABCD)? Serikali ieleze ni vigezo gani walitumia kuondoa mitihani ya mchujo wa *form two* na *mock* ya *form four* na kuirudisha mwaka jana?

Mheshimiwa Spika, hata kama ingekuwa na shule ina vifaa vyote muhimu kama mwalimu amekata tamaa ni bure. Walimu wengi hawana moyo wa kufanya kazi yao kwa sababu ya Serikali kutosikiliza madai yao, mishahara kidogo, mazingira magumu ya kazi, kutothaminiwa na kudharauliwa.

Mheshimiwa Spika, ni miaka kumi sasa walimu wanaidai Serikali imewafanya watoto, kuwadanganya na kutumia ubabe kuzuia hisia zao. Sasa Serikali imevuna ilichopanda halafu unaunda Tume ya nini?

Mheshimiwa Spika, walimu wa Mbeya Mjini (Manispaa), waliahidiwa kupandishwa vyeo na kuongezewa mishahara sambamba na Wilaya nyingine za Mbozi, Mbeya Vijijini na kwinge hadi leo tarehe 5 Juni, 2013 hawajapandishwa vyeo wakati wale wa Mbozi na Mbeya Vijijini walishapandishwa vyeo na mishahara imepanda. Ni kwa nini hawa wa Halmashauri ya Manispaa bado?

Mheshimiwa Spika, Walimu wamekuwa hawapandishwi madaraka kwa wakati na hili linakatisha tamaa. Serikali itueleze utaratibu unaotumika kupandisha vyeo na madaraja?

Mheshimiwa Spika, shule zetu na vyuo vinazalisha watoto waliopata elimu ya nadharia tu bila mafunzo kwa vitendo. Hii ni hatari kubwa sana, wakienda makazini

wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi. Uwepo wa maabara kwa shule zote za sekondari ni jambo la lazima wale siyo hiari. Serikali itupe mchanganuo wa uhakika ni lini shule zote za sekondari zitapata maabara na vifaa vyote muhimu?

Mheshimiwa Spika, Serikali imepunguza sana na mahala pengine kuondoa kabisa safari za mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu vingi hapa nchini. Walioweka mipango hiyo walijua faida yake. Wanafunzi walimaliza vyuo wakiwa *competent exposure* na anajiamini. Leo wanatoka chuoni hawawezi ku-*compete* kwenye soko la ajira. Ni lazima Serikali ihakikishe inarudia mifumo mizuri iliyowekwa na waliotangulia kwenye Wizara na Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitamka hapa Bungeni hakuna mtoto atakayeshindwa kusoma kwa sababu ya kukosa ada au kushindwa kulipa michango mbalimbali ya Shule za Sekondari za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Walimu Wakuu wa Shule za Kata wamejiamulia michango mbalimbali ambayo wazazi wanashindwa kumudu kulipa. Pale wanaposhindwa kulipa watoto wananyimwa kufanya mitihani na wengine wanafukuzwa kabisa. Serikali itoe tamko leo hapa Bungeni na iandike barua kwa Wakuu wa Shule zote, watoto maskini wasinyimwe kufanya mitihani kwa sababu ya kukosa ada au michango mingine.

Mheshimiwa Spika, kila mtoto wa Kitanzania ana haki kupata elimu sawa na yenye ubora ule ule. Serikali imekuwa inasahau au kutoa kipaumbele kuhakikisha watoto walemavu wanapata elimu. Shule za watoto walemavu zinaendeshwa kwa sehemu kubwa na wahisani, misaada na watu wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Uhuru Mchanganyiko iliyoko Buguruni, ina mahitaji makubwa sana ya walimu, vifaa vyaa kufundishia watoto wale wenye ulemavu wa uono, usikivu na wasioweza kusema, wanahitaji vifaa maalum vyaa

kusomea na kufundishia ili waweze nao kuelewa. Serikali inatoa fungu dogo sana kwa ajili ya vifaa, miaka yote Walimu wanahaha kuomba misaada na kutafuta wahisani. Walimu wanaofundisha watoto hawa ni wenye uwezo na ujuzi maalum. Wengi wanajisomesha wenyewe, tena nje ya nchi kwa masomo ambayo hayapo Chuo cha Patandi Arusha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze imeandaa mikakati gani kuhakikisha shule hizi zinazohitaji vipaji maalum, vifaa maalum na Walimu Maalum, zinapata vifaa vyote na Walimu wa kutosha ili watoto wapate haki yao ya elimu bora.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa sana kwa miaka 51 ya Uhuru ndani ya nchi yenye rasilimali kubwa ya misitu, watoto wanakaa chini kwenye udongo, kwenye sakafu na magogo kwa shule za vijijini; ni lini aibu hii itaondoka?

Mheshimiwa Spika, Shule za *Tabora Boys* na *Tabora Girls* za Mkoa wa Tabora ni shule kongwe na zimetoa Viongozi wengi wa Taifa hili, hata Waasisi wa Taifa letu walisoma kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Spika, shule hizi zinatakiwa ziboreshwwe ziendane na hali ya sasa, mahitaji makubwa ya vifaa na miundombinu na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga kila mwaka. Miundombinu imechakaa sana, hakuna uzio, hali inayosababisha watoto kuibiwa vifaa vyao mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tunaomba shule hizi mbili ziingizwe kwenye ukarabati wa miundombinu mwaka huu pamoja na fedha za kujenga uzio.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara kubaini makosa juu ya mfumo wa kupanga alama za ufaulu (madaraja na kuamua kufanya *standardization*), tunaomba Serikali ieleze hiyo *standardization* imefanyikaje?

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu, utaratibu wa *standardization* unaongeza kila mwanafunzi aliyefanya huo mtihani awe amefaulu au amefeli. Watoto waliopata zero

kwa matokeo ya 2012/2013 wengi wamebaki kwenye zero bila mabadiliko yoyote, wengine wamepanda *point* moja tu, alipata *Division Four point* 28 amepanda na kupata *four point* 27. Mwingine alipata *Division Four* amepata mpaka *Division Three point* 23. Hakuna uwiano unaoeleweka, Serikali ilete na itoe ufanuzi wa kueleweka.

Mheshimiwa Spika, watoto walipata matumaini baada ya Serikali kutangaza kwamba, matokeo yatabadilika kwa kuondoa mfumo mpya uliotumika. Leo matokeo ya watoto wengi yamebaki yale yale ya mwanzo; Serikali imeandaa utaratibu gani wa kuwasaidia watoto wote waliofeli kwa sababu ya uzembe wa Viongozi waliotumia mfumo mpya kwenye mitihani ya mwaka 2012?

Mheshimiwa Spika, Wizara ipunguze alama za ufaulu wa kujunga na Vyuo vya Serikali na binafsi, badala ya alama 27 wachukue hata alama 28 waruhusiwe kujunga na vyuo mbalimbali na hasa kwa kuzingatia watoto wengi waliofeli ni wale wa Shule za Serikali na hasa za vijijini, ambazo zina mazingira duni na magumu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi kiondolewe kwenye Halmashauri na kuwekwa Wizarani ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi, kitengewe fedha za kutosha na viwepo vitendea kazi vya kutosha. Maafisa Ukaguzi wajengewe uwezo wa kutosha, wapewe vyombo vya usafiri wafuatilie maendeleo ya watoto mashulenii wasikae maofisini. Kazi zao siyo za ofisini ni za kutembelea shule.

Mheshimiwa Spika, wapo watu wenye uwezo mzuri sana na uelewa wa masuala ya elimu, ambao wako nje ya Serikali. Wengi wapo Sekta Binafsi na kwenye Mashirika ya Dini na Taasisi nyingine. Ili kupata mawazo mazuri na kuendelea kuboresha elimu kuendana na wakati, ni vizuri Serikali ikatumia uzoefu wa wasomi hawa kwa kuandaa makongamano, midahalo na semina mara kwa mara ya kujadili maendeleo ya elimu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke utaratibu wa kukaa

na kuongea na walimu wa maeneo mbalimbali na hasa wale wa vijiji ili kupata kwa undani changamoto wanazokutana nazo na nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, shule za *private* na *mission* zimeweka utaratibu wa kuwaita wazazi kwa mwaka mara mbili mpaka nne, kujadili matatizo ya watoto, ya shule na jinsi gani wazazi wawajibike na walimu wawajibike kuboresha elimu ya watoto wao. Serikali ihakikishe utaratibu huu unakuwepo kwenye Shule za Serikali zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inahimiza Vyuo Vikuu kuongeza udahili wa wanafunzi na kuongeza kuanzisha shahada, stashahada mpya, bila kwenda sambamba na kuongezeka kwa miundombinu, vifaa na hata wahadhiri. Miundombinu ni ile ile ila kila mwaka tunaongeza udahili. Matokeo yake, wanachuo wanakusanyika kwenye madarasa kama m Kutano wa hadhara, wamekaa chini na wengine wamesimama. Tutazalisha wasomi feki wasiojua chochote ila wana vyeti.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimoja tu cha *SUA* kimepangiwa kuongeza wanafunzi 2013/2014 kutoka wanafunzi 8115 waliopo hadi 14,498, wakati miundombinu iliyopo haikidhi mahitaji yao. Serikali ilenge kutoa elimu ya viwango kwa ngazi zote na siyo idadi kubwa ya wahitimu mbalimbali.

MHE. PROF KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitaanza na suala la Serikali kuingilia *NECTA* (Baraza la Mitihani), asasi ya kiserikali iliyanzishwa kisheria kwa kitendo chake cha kutengua matokeo ya mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2012. Kiutaratibu, Serikali haipaswi kuingilia moja kwa moja asasi za kitaaluma ilizozuunda.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kufanya, ni kuweka utaratibu wa tathmini endelevu wa kuhakikisha kwamba, taasisi na asasi zinazingatia majukumu yake kwa vigezo na viwango vilivyowekewa; na kuwa na njia nzuri na wazi za

mawasiliano na asasi hizo ili kama kuna tatizo liweze kushughulikiwa mara moja. Katika tukio hili, Serikali ilikuwa na nafasi ya kuishauri *NECTA* ifanye marekebisho kama ilibaini tatizo, kabla ya matokeo kutangazwa na kama hili lingefanyika yale yaliyotokea, wanafunzi kujua, mahangaiko mengi kwa walioshindwa na kadhalika, yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa, upevu wa Serikali yoyote ile ni kuziacha asasi zake zifanye kazi kwa kuzingatia sheria, sera na kanuni. Kitendo cha Serikali cha kutengua matokeo kilikuwa cha aibu na nadhani ni Serikali ya Tanzania pekee ambayo imediriki kufanya hivi katika historia ya mfumo rasmi wa elimu. Kama kweli Serikali iliumizwa sana na kushindwa kwa asilimia zaidi ya sitini ya wanafunzi; kwa nini haikuwaruhusu wanafunzi hao warudie mitihani bila gharama katika kipindi maalum? Kwa vyovypote vile, hiki ni kitendo ambacho hakipaswi kurudiwa.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa changamoto zinazoukabili mfumo wetu wa elimu (ukurasa wa 15 wa Hotuba ya Waziri), ambazo hazikutajwa na Waziri ni changamoto ya lugha ya kufundishia. Kuhusiana na hili, Tanzania tumekuwa tukienda mbele kisha tunarudi nyuma. Mwaka 1982, Tume ya Rais ya Elimu ilipendekeza kuwa, lugha zote ziruhusiwe, Kiswahili katika shule nyingi za umma na Kiingereza katika shule chache (hasa za binafsi), kwa bahati mbaya sana pendekezo hili halikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Rasimu ya Sera ya Elimu (2013) imelichukua pendekezo hili. Hata hivyo, pendekezo hili bado lina upinzani mkubwa kutoka kwa watu mbalimbali, pamoja na Wabunge, baadhi ya wapinzani wa pendekezo hili ni wale wanaomiliki shule binafsi zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia na wengi si wanaelimu wala wataalamu wa masuala ya lugha na jinsi inavyohusiana na elimu na maendeleo kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja wa Mbunge ambaye anapinga matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia; huyu ni Mheshimiwa Jason Rwekiza, yeye

anapendekeza Kiingereza tu ndicho kitumike kama lugha ya kufundishia. Yeye siyo mtaalam wa elimu, wala wa masuala ya lugha, yeye ni mwanasheria. Sababu anayoitwa ni ile ile inayotolewa na wapinzani wengi wa Kiswahili kuwa Kiingereza ni Lugha ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wanachosahau hawa ni kuwa Kiingereza hakujifanya kuwa Lugha ya Kimataifa; ni watu walichokifanya kiwe Lugha ya Kimataifa, kwa kuienzi, kuikuza na kuineza. Hivi sasa Kiswahili kipo katika hali nzuri kuliko Kiingereza kilivyoanza. Kiswahili ni Lugha ya Kimataifa pia kwa wigo mdogo. Kinasemwa Tanzania, Rwanda, Kenya, Uganda, Congo, Zambia, Malawi, Msumbiji, Madagaska, Comoro, Somalia, Burundi na kadhalika. Dunia nzima hivi sasa inatuangalia sisi Tanzania (kitovu cha Kiswahili), tunafanya nini. Tukianza sisi majirani zetu watafuata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili, nimeliongelea Bungeni na kwingineko mara nyngi. Yapo mambo kadhaa ambayo tunapaswa kuyafahamu kuhusiana na hili. Hakuna nchi ambayo imeendelea kwa haraka na kujiamini kwa kutumia lugha ya mkopo. Urithi wa maana ambao tunaweza kuiachia Dunia ni utamaduni wetu ambao ni pamoja na lugha kwa mujibu wa Azimio la UNESCO la mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Wanaelimu wameshathibitisha katika tafiti zao kuwa, mtoto hujifunza bila matatizo kwa lugha anayoifahamu. Nchi nyngi sana hutumia lugha zao kufunzia na kujifunzia na zinaendelea kupata maendeleo bila shida. La kufurahisha ni kwamba, nchi zote zinazotumia lugha zote zina programu madhubuti za kufunzia lugha zote kuu za kigeni na hazina matatizo yoyote ya kuwasilisha kwenye ngazi za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Rwekiza ayaelewe haya. Asije akawa anasukumwa na ukweli wa kuwa mmiliki wa shule kadhaa zinazotumiwa Kiingereza kama lugha ya kufundishia kuendelea kuupotosha Umma wa Watanzania kuhusu mada hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo Waziri amelitaja katika hotuba yake linalosababisha kiwango cha elimu kushuka ni kutotiliwa mkazo kwa ufundishaji wa ujifunzaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), ukurasa wa 17. Hili ni tatizo kubwa sana na ndilo linalopelekea wanafunzi kumaliza shule bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo hili kuendelea kuusakama mfumo wetu wa elimu, sababu kubwa ni ukosefu wa uthubutu wa Watendaji wa Wizarani. Hapa nchini tuna asasi isyo ya kiserikali inayoitwa Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania (*Children's Book Project, Tanzania*), ambao hadi sasa una shule za mradi 196 (Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma).

Mradi unatoa mafunzo kwa walimu kuhusu namna ya kufundisha, kusoma na kadhalika. Unaziwezesha Shule za Msingi kuwa na maktaba na kadhalika. Ninachofahamu ni kwamba, Wizara ina mjumbe kwenye Bodi na Kamati ya Mradi katika shule zote za mradi, hakuna mwanafunzi anayemaliza darasa la saba bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Ama hakika karibu wanafunzi wote hushinda na kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ichukue uzoefu wa Mradi huu na kuujumuisha katika mafunzo yake katika Vyuo vya Walimu na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongelee viambatisho 1(a), 1(b) na 4. Kiambatanisho 1(a), kinahusu orodha ya shule 1,200 zitakazofanyiwa ukarabati; Kiambatisho 1(b) shule 264 zilizo katika mchakato wa ujenzi awamu ya kwanza; na Kiambatisho Namba 4 shule 528 zilizo katika mchakato wa tathmini ya mahitaji ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wengine walivyokwishesema, orodha hizi zina upungufu kadhaa, lakini upungufu wa wazi ni ule wa upendeleo wa wazi. Upendeleo huu umekuwepo tangu zamani hadi kukawa na maeneo

yaliyoendelea sana na mengine ambayo yako nyuma kimaendeleo. Nimeliongelea hili huko nyuma na kupendekeza kuwa, Serikali ichukue hatua za makusudi kusahihisha kasoro hii, lakini Serikali hajasikia hadi sasa na viambatisho hivi ni mwendelezo wa upendeleo huu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia Bukombe ninakotoka, hapa kuna makosa kadhaa, (a) Bukombe imechukuliwa kuwa ni Wilaya moja kumbe siku hizi ni Wilaya mbili; Mbongwe na Bukombe. Pia Bukombe imechukuliwa kuwa ipo Shinyanga wakati Bukombe na Mbogwe zipo Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, Bukombe na Mbongwe ni eneo liliilosahaulika kimaendeleo, katika Kiambatisho 1(a) Bukombe (Wilaya mbili) imepewa shule mbili tu wakati Wilaya nyingine zimepewa shule hadi kumi na tano.

Katika Kiambatisho Namba nne, Wilaya za Bukombe na Mbogwe hazina kabisa! Wizara kama asasi ya kitaifa, inapaswa kutumia vigezo bainifu katika kugawa maendeleo, ikishindwa basi viongozi hawafai, wabadilishwe wawekwe wengine wanaofaa.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya madawati inahitaji *intervention* ya sekta nyingi, tusiwaachie Wizara ya Elimu peke yake. Watoto wetu kukaa chini kuanzia *stage* ya awali ni kuanza kuwalemaza migongo bado wakiwa wadogo. Wizara ya Elimu, TAMISEMI, wazazi, wakereketwa wa elimu, wenye uwezo wa kusaidia, sote kwa pamoja tunao wajibu wa kuona kuwa, suala la madawati katika kila eneo linapewa uzito unaofaa.

Mheshimiwa Spika, katika *stage* ya elimu ya awali, elimu ya usafi kwa watoto wetu izingatie masuala ya ukataji kucha, kuweka nywele katika usafi, zisukwe na watoto wasitiwe rasta. Wafundishwe pia umuhimu wa kupiga mswaki na kuosha mikono baada ya kutoka chooni na kabla ya kula na baada ya kula.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivi tunajenga misingi imara ya afya bora na mtoto anakuwa katika kufuata misingi hii mashulenii na majumbani. Umuhimu kwa watoto hao kutengewa muda mzuri wa michezo na mapumziko. Hawahitaji *lecture* 20 na tani saba ya madawati ya kubeba nyuma ya mipango yao.

Mheshimiwa Spika, elimu ya msingi na sekondari na changamoto zake, inasikitisha sana kusikia wanafunzi wanamaliza sekondari bila kujuua kuandika, ni aibu sana. Je, tujulize kosa ni la nani?

Mheshimiwa Spika, sisi wazee kutofutilia maendeleo ya watoto wetu, kuwapa watoto wetu vifaa vyta kuwafanya wakose muda wa kushughulikia masomo; kwa mfano, simu za mikononi badala ya kusoma na kufikia namna ya kufahamu anachosomeshwa, wao wako kwenye msg.

Mheshimiwa Spika, tunasikia simu za mikononi ndizo zinazotumika kuambizana majibu ya mitihani. Hivi walimu wako wapi? Wazazi tunayanyamazia haya? Ni kwa nini vijana wasifafulu?

Mheshimiwa Spika, upungufu wa vitabu vyta kujifunzia na kufundishia utaisha lini? Tuliwahi kuelezwaa na viongozi wetu kuwa vimepokelewa vitabu vyta kutosha juu havikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, walimu wasio na sifa nao wanachangia sana kufanya wanafunzi wasifafulu; kama walimu hawajui wanachokifundisha wanafunzi wanafafulu vipi?

Mheshimiwa Spika, tusipowajali walimu nalo ni tatizo, mishahara duni, mazingira mabaya ya kufundishia, miundombinu duni ya kumuwezesha kufika shulenii. Maisha ya walimu yako duni, nyumba wanazoishi henzieleweki, mishahara inachelewa kuwafikia huko waliko vijijini kwa wakati na kutopata vitendea kazi kikamilifu vyta kufundishia. Aidha, malimbikizo ya madeni yao mbalimbali bado ni kitendawili.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kufanya *study* ya kina na kuchambua masuala haya na kuja na mkakati thabiti wa kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ufundi; eneo hili linahitaji usimamizi thabiti. Hivi kwa nini eneo hili lisipewe watu binafsi kuliendesha? Kwa nini eneo hili lishindwe kuijidesha wenyewe? Kwa nini hakuna tija katika sehemu hii? Hakuna *marketing strategic* zozote zinazowekwa na kugeuza eneo hili na kuwa viwanda, *institution* kubwa za kujitegemea? Leo wanafunzi waende kutafuta elimu, Walimu hawana muda wa kutafuta wanafunzi? Matangazo mbalimbali na kadhalika. Sekta ya ushonaji iwe *attached* na viwanda vinavyoshona nchini. Tujitahidi kutafuta *institution* za kufanya *attachment* kwa mafunzo mbalimbali ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, Maktaba Kuu inahitaji kuwa *up to dated* kwa kuwekwa vitabu vya kisasa vya fani mbalimbali, *periodical* mbalimbali za *institution* mbalimbali nje na ndani, *updating* machapisho mbalimbali na jengo lipakwe rangi.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Viongozi wote wanaoendesha Wizara hii, kwa ujumla wanafanya kazi kubwa katika changamoto nyingi sana. Naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zinatumia lugha zao kufundishia; nchi za Ujerumani, Norway na nchi zote za Asia. Hili jambo lifanyike haraka.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbinga ina *Falk Development College*; ni lini inafanywa kuwa *VETA*? Kiasi gani imefanyiwa maandalizi ya kubadilishwa kukidhi majukumu mapya kwa majengo, vifaa vya kufundishia na kadhalika? Naomba hapa pia tuangalie vyuo hivi kwa maana ya kuwapa bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ualimu Mbinga ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni yake Mbinga Mjini. Ile sekondari ya *Mbinga Day* ilikuwa Chuo cha Ualimu na

kilibadilishwa kuwa sekondari. Mheshimiwa Rais aliahidi Wananchi kurudisha hadhi ya Chuo cha Ualimu. Naomba mchakato wake uanze ili Julai, 2014 Chuo hiki kianze. Nina hakika ahadi hii siyo ngumu kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa shule zinazofanyiwa na zitakazofanyiwa ukarabati, hauna usawa kabisa, ni vyema ukaangaliwa upya. Wilaya ya Mbinga ni shule tano tu (Kiambatanisho 1(a)). Kiambatanisho Namba 4 ni shule zile zile tena kama 1(a). Wilaya ya Mbinga ina sekondari 43. Kwa utaratibu huu shule hizi zitakarabatiwa lini? Napendekeza kwa nguvu sana mgawo huo ufanyiwe kazi upya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na TAMISEMI pawepo na mstari unaoonekana juu ya majukumu ya Wizara hizi mbili kuhusu kuhudumia elimu na jambo hili lifanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Wizara lazima imalize tatizo la madai ya fedha ya walimu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja hii katika eneo lihusulo mikopo katika elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko unaoendelea kuonekana kuwepo katika eneo hili muhimu katika maendeleo ya vijana wetu unatokana na mfumo mbovu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa, urasimu usio na ulazima na upendeleo wa waziwazi na kubwa zaidi kuliko yote ni upendeleo; wale wenye vigezo stahili wamekuwa hawapati mikopo na hata wanapopatiwa inakuwa ni kwa tabu sana, lakini wale watoto wa wenye uwezo au wenye wazee walioko madarakani kwao wao tatizo linakuwa dogo au halipo kabisa. Hivyo, naiomba Serikali iangalie mfumo mzima wa utoaji mikopo katika elimu ya juu ili haki itendeke na kupunguza malalamiko haya au kuyaondoa kabisa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi na rehema na mwingi wa ukarimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha na kwa kuwa ufunguo wa elimu anao mwalimu na walimu bado hali yao ya maisha ina changamoto nyingi. Je, hauoni kwa kuwa mwenye ufunguo wa maisha yaani mwalimu kuwa na maisha magumu hatautumia ufunguo huo kwa kuwafungulia maisha wanafunzi kwa maana tuwajali, tuwathamini na tuwaboreshee Walimu wetu kwa kuwapa mishahara mizuri, posho za mazingira magumu na kuwalipa madeni yao?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 119, orodha ya Shule za Serikali 1,200 zitakazofanyiwa ukarabati na katika ukurasa wa 133 Wilaya ya Kilwa katika Mkoa wa Lindi umepangiwa shule zitakazokarabatiwa ni tisa na katika Mkoa wa Lindi umepangiwa idadi ya shule zitakazokarabatiwa 31, wakati wilaya moja ya Moshi Vijijini 34.

Mheshimiwa Spika, hii yaonesha kuwa, Mkoa wa Lindi wote umepata na idadi ya shule zitakazokarabatiwa katika wilaya moja tu ya Moshi Vijijini, hii ndiyo sababu tunasema Mikoa ya Kusini inatengwa na kubaguliwa. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, arekebishe tofauti hii ili haki sawa kwa wote ipatikane.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna tetesi kuwa Somo la Dini limefutwa katika Mtihani wa Taifa. Kwa kuwa ni tetesi, naomba katika majumuisho Mheshimiwa Waziri aliweke wazi ni kweli mtihani wa Somo la Dini umefutwa au la na kama umefutwa ni kwa nini?

MHE. DUNSTAN D. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono Bajeti ya Wizara ya Elimu, Wizara ambayo ina jukumu kubwa la kutengeneza au kujenga rasilimali watu; rasilimali ambayo ndiyo uti wa mgongo kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa lolote.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu inakabiliwa na changamoto nyingi sana ambazo ni hatari kuachwa ziendelee kwani zinadumaza ustawi wa Taifa letu. Ni wajibu wetu tuchukue hatua za haraka kuhakikisha kuwa, matatizo ya kushuka kwa ubora wa elimu yetu yanapata suluhu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya za kipaumbele katika kujengewa Chuo cha VETA. Tunaiomba Serikali itusaidie katika kutimiza lengo hili. Tunaishukuru Serikali kwa kuweka Shule za Wilaya ya Mkinga katika mpango wa kuzikarabati. Hata hivyo, katika orodha iliyopo ukurasa wa 168 wa Hotuba ya Waziri, zipo shule ambazo zimejirudia na zipo shule ambazo zinaonekana kuwa ni za Wilaya Mama ya Muheza, lakini kiuhalsia zipo Mkinga.

Mheshimiwa Spika, naomba kupendelekeza kwa shule ambazo zinajirudia mara mbili (yaani 1171 na 1174 Mapatano, 1173 na 1190 Lanzoni), sehemu iliyojirudia fedha zake zielekezwe katika shule nyagine za Wilaya ya Mkinga, mfano, 1174 ziendelee Shule ya Bosha na 1190 zipelekwe Mwakijembe, shule ambayo ina changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa shule ambazo zimeonekana kuwa zipo Muheza ilhali zipo Mkinga, nashauri tuhakikishe shule hizo zinaonekana Mkinga na fedha zake zielekezwe Mkinga. Shule hizo ni Kigongoi (1184), Kwale (1185), Gombero (1188), Manza (1189) na Lanzoni (1190).

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la Wafanyakazi (Walimu) kupewa barua za kupanda madaraja, lakini hawajapewa nyongeza zao za mishahara stahiki. Naomba jambo hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vijana wa Kidato cha Nne wameanza kufanya Mitihani ya *Mock*. Taarifa kutoka sehemu mbalimbali zinatisha, lipo tatizo kubwa la utoro na hivyo watoto hawa kutofanya mtihani huu. Tatizo hili lipo karibu kila eneo la nchi yetu, kwa Wilaya ya Mkinga takwimu chache zinaonesha ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Manza Sekondari yenyé wanafunzi 83, wanafunzi 50 hawafanyi mtihani huu, Zingibari yenyé wanafunzi 71 wanafunzi 30 hawafanyi mtihani, Mkinga leo yenyé wanafunzi 133 wanafunzi 53 hawafanyi, nashauri tuchukue hatua kwa jambo hili.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukua fursa hii kwa njia ya maandishi, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema na ukarimu ili kuweza kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Spika, nitachangia hoja hii kwa kupitia hotuba hizi:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na ugumu wa kazi ya ualimu masilahi ya walimu bado ni madogo sana; mishahara, posho mbalimbali kama likizo, walimu hawana semina na hata hizo likizo ni ndogo, hazipatikani kwa wakati kuna urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, walimu wanahitaji kuandaliwa posho tena kwa kiwango kikubwa kwa wanafanya kazi muda wote hadi somo lifahamike.

Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Wizara una juhudii kubwa na wanastahili pongezi. Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, wana juhudii ya kufuatilia kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano; katika awamu ya kwanza ya Kamati za Kudumu za Bunge mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa muda tulishirikiana pamoja katika kusimamia shughuli za maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono Wabunge ambaao wanalaani na kutaka uongozi wa Wizara ujiuzulu. Hii ni fikra potofu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli maendeleo ya elimu

yameshuka, lakini naomba niwashauri Wabunge wenzangu, tukae chini pamoja na kuishauri Wizara ili tuandae mikakati bora itakayowezesha kiwango cha elimu kipande Taifa letu liwe la watu walioelimika na nchi yetu iwe na maendeleo ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la upungufu wa walimu naomba niishauri Wizara kama ifuatavyo:-

(a) landae walimu kwa kuwapatia mafunzo ya ualimu katika ngazi zote;

(b) longeze idadi ya walimu katika shule zetu pamoja na vyuo; na

(c) Walimu waandaliwe makazi mazuri kwa wale wanaohamishiwa maeneo ya mbali na iwaandalie posho maalum wale waliohamishiwa katika maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya wakisaidiwa na Watendaji wao.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kuboresha Hotuba ya Wizara hii katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumzia juu ya Jedwali linaloonesha orodha ya Shule za Sekondari 1,200 zitakazofanyiwa ukarabati katika ukurasa wa 119 – 165 kuwa haikuzingatia uwiano baina ya mikoa na wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya majumuisho atueleze ni vigezo gani vimetumika katika kuchagua shule hizi? Je, wanaposema shule zitafanyiwa ukarabati zitahusisha ukarabati wa maeneo gani? Naomba ufanuzi wa kina, hii itaweza kupunguza wasiwasi kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lishe kwa wanafunzi; ni lazima Serikali itambue kwamba, uwepo wa shule nyingi na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa shulenii haina maana kwamba ndiyo itaongeza kukua kwa kiwango cha elimu bila ya kuzingatia umuhimu wa wanafunzi hawa kupata lishe bora. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa utaratibu wa watoto kupata chakula shulenii unatekelezwa ili kurudisha usikivu kwa watoto madarasani na hatimaye kufanya vizuri katika masomo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto kusoma nje ya tarafa zao: Katika Wilaya ya Rufiji hadi sasa bado kuna wanafunzi wanaopangwa kwenda kusoma katika shule za kata takribani kilomita 100 kutoka katika vijiji vyao, hivyo inawalazimu kupanga nyumba, kujipikia chakula wenyewe, kwa sababu shule hizo hazina *hostel*. Je, azma ya ujenzi wa shule za kata ilikuwa ni nini? Mfano, watoto wanatolewa Kibiti kwenda kusoma Kata ya Mwaseni, ni zaidi ya kilomita 80, shule haina umeme, maji wala *hostel*. Je, tunategemea watoto hawa watafaulu kwa miujiza ya Mungu?

Mheshimiwa Spika, pia watoto wanatoka Tarafa ya Ikwiriri kwenda kusoma Tarafa ya Muhoro, Kata ya Mbweri na shule hizi hazina huduma muhimu na walimu ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali imalizie kujenga Shule ya Sekondari Umwe, ambayo ina madarasa matamno, itapunguza tatizo la watoto wa Tarafa ya Ikwiriri kwenda kusoma nje ya tarafa katika shule ambazo hazina *hostel*; hivyo, watoto wengi wa kike hupata mimba na matokeo ya Sekondari hizi ni Daraja la IV na O. kwa wanafunzi wote waliomaliza mwaka 2012 - 2013.

Mheshimiwa Spika, sasa ni zaidi ya miaka mitano shule hii bado haijakamilika, kwa sababu ya urasimu wa watu wachache ambaao unaumiza watoto wa kimaskini. Naomba majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ndiyo kioo, kama elimu ni ya mashaka ujue ndiyo mashaka yanayozaliwa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikatengeneza mkakati wa uhakika kuokoa kushuka kwa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mchango huu, naitaka Serikali, inipatie majibu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, na ubabaishaji mkubwa sana katika Bodi ya Mikopo na wale walengwa waliokusudiwa wapatiwe mikopo wamekuwa wanasumbuliwa sana na hata wakipata msaada wa mikopo, huwa wanatumia gharama kubwa katika kuwafikisha hapo. Je, Serikali imejipanga vipi kutatua ubabaishaji huo?

(ii) Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikatengeneza utaratibu wa kuangalia madeni ya walimu na itengeneze mkakati wa kuyalipa. Ni vizuri walimu walipwe haki zao ili waweze kutekeleza wajibu wao vizuri.

(iii) Mheshimiwa Spika, ni vizuri kutengeneza utaratibu mzuri wa kuhakikisha walimu wanalipwa vizuri, wanapata huduma muhimu za msingi na kuboresha miundombinu ya kitaaluma na kuwafanya walimu wafarijike na kazi watakayoitekeleza ya kuwafundisha watoto wetu.

(iv) Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaitekeleza ahadi ya Rais aliyoitoa mwaka 2010 kujenga nyumba ya mwalimu kila Shule ya Sekondari na pia kujenga maabara kwenye kila Shule ya Sekondari.

(v) Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaitekeleza suala la kupeleka Vitabu vya Hisabati, Kiingereza, Fizikia, *Chemistry* kama ilivyoahidi kwenye llani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili Serikali ipate nafasi ya kuyatekeleza haya.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi tunaomba tuongezewe shule za *A Level, High School*, kwa makusudi kabisa. Sasa hivi tuna *High School* nne Mkoa mzima wa Lindi wenyе wilaya sita; *High School* - Mbekenyeru Ruangwa; *High School* - Liwale; *High School* - Lindi; *High School* - Maliwa; bado Kilwa.

Mheshimiwa Spika, wakati mikoa mingine kuna *High School* 50 kama Mbeya na Morogoro, kuna *High School* 23, tuwezeshwe katika kusaidia upataji wa *High School* katika Mkoa wa Lindi. Tuangalieni kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, kila penye shule ya msingi pawe na shule ya awali sasa ni lazima, siyo hiari tena.

Mheshimiwa Spika, tunaomba katika Shule za Sekondari wawepo pia walimu wa kike. Nilwahi kutembelea shule 20 za Mkoa wa Lindi. Katika shule hizo niliombwa walimu wa kike wawepo katika shule za Sekondari, kama Shule ya Sekondari Mipingo Lindi Vijijini wanaomba. Nilipokuwa mashulen humo, pia walikuwa na shida ya walimu; hawatoshi kama Mkoa mzima wanahitaji walimu 1,787 walipo ni 793, pungufu ni 999. Walibahatika kupelekewa walimu wapya mwaka 2013 wapatao 333; lakini walioripoti ni 223, bado walimu 110 hawajari poti.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi tuna uhaba wa walimu sana tusaidiwe tafadhalii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba bajeti ya pesa za Chuo Kikuu, pesa za mikopo zitengwe tofauti na bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, kwani bajeti inakuwa na pesa nyingi kumbe pesa hizo siyo za maendeleo ya Elimu bali ni mikopo tu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ulaguzi wa Shule kiwe huru kisiwe chini ya Halmashauri ya Wilaya wala Katibu Mkuu. Kiwe chombo huru kwa sababu kinashindwa kujitawala katika maamuzi, pia katika kupata pesa za kazi zao, hakipewi pesa za kufanya kazi. Wakipewa magari, basi mafuta hawana na

wakipewa mafuta basi magari hawana. Mimi nilikuwa Mkaguzi wa Shule, ninajua matatizo hayo ya wakaguzi wasaidiwe.

La pili, tunaomba tusaidiwe magari katika Wilaya ya Nachingwea na Lindi Mjini, pia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kitengo cha Elimu hawana magari ya ukaguzi. Ninasema tena, tunaomba wakaguzi wapewe *OC* yao.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa Lindi karibu asilimia 40, wameenda Dar es Salaam kuitwa Wamachinga. Tunaomba *VETA* Wilaya zianzie kujengwa Lindi, mikoa ambayo ilikuwa ya mwisho kupata *VETA* Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi katika Mkoa wa Lindi zina upungufu wa Walimu 1,165. Mahitaji ni walimu 4379, wallopo ni 3,214. Tulipelekewa walimu wapya 485 mwaka 2013, mpaka sasa walimu 50 hawajarioti kwa nini? Tuongezewe Walimu wa Shule za Msingi.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nashauri mgawo wote wa ukarabati wa shule nchini uwe sawa kwa mujibu wa wilaya. Tupate idadi sawa kila wilaya kuondoa sura ya upendeleo. Zaidi, mgawo huo izingatie pia wilaya mpya kwani tayari zina Wakurugenzi na mamlaka kamili, tayari zinatambulika kisheria, ni vyema mipango ya Serikali iakisi sura hiyo badala ya kuendelea na sura ya wilaya ya zamani.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uendeshaji wa Shule za Kata urejeshwe chini ya Wizara badala ya Halmashauri. Uzoefu wangu wa ukaguzi wa Halmashauri, bado unaonesha Halmashauri zetu zina matatizo mengi na uwezo wake ni duni sana. Kuzifanya shule hizi ziwe chini ya Halmashauri ni kuambukiza tatizo kubwa la Halmashauri kwenda Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ni ndogo sana, Vyuo vya *VETA* viro kimkakati sana katika kujenga Taifa la uzalishaji. Ni muhimu nguvu iwekezwe huko kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya upungufu wa walimu: nashauri walimu wanaostaafu wakiwa na nguvu bado wapewe mikataba ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu. Walimu wengi wanaostaafu sasa ni walioandaliwa vizuri; hivyo, ni hasara kuwapoteza sasa kama bado wanawenza kutumikia Taifa.

Mheshimiwa Spika, tutakopofikia uwiano mzuri wa Walimu, ndipo turuhusu kutoendelea kutoa mikataba kwa wastaaafu. Hii ianzie shule za msingi mpaka sekondari na vyuo.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Naibu Mawaziri wa TAMISEMI na Elimu na Timu yake yote, kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Taifa na juu ya uboreshaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, nitachangia juu ya wadau wa elimu kwa mtoto (mwanafunzi).

Mheshimiwa Spika, wazazi wote wawili na hasa mama hawa ndiyo wadau wa mwanzo wa kuhakikisha elimu ya mtoto inaanza (*Informal Education*), hapa ndiyo mtoto anaanza kujengeka *brain* (ubongo). Ni wajibu wa wazazi kuwaandaa watoto wao kisaikolojia, kimaadili na kilishe ili wawe na *brains* bora za kupokea. Wazazi wakague madaftari kuona maendeleo ya watoto wao.

Mheshimiwa Spika, watoto wakishafuata au wakijengeka vizuri watahudhuria madarasani (shule), vipindi vyote watawasikiliza walimu na kuyashika au kuzingatia masomo wanayofundishwa. Utoro utapungua ama kwisha kabisa na ufaulu wao kuanzia elimu ya awali hadi Chuo Kikuu utakuwa juu (bora).

Mheshimiwa Spika, walimu waweke mbele azma ya maono yao na kwa kadiri walivyoapa kwamba watafundisha kwa kadiri ya taaluma yao inavyowataka na kwa kufuata maadili (*Ethics*) ya kialimu. Ili walimu wafundishe au wafanye kazi, lazima wafanye kazi katika mazingira rafiki na ya kukubalika, wajitoe katika kazi ya kufundisha au kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi imeundwa ili ifanye kazi ya ufuatiliaji, tathmini na usimamizi kwa walimu wanapofundisha, kujua masilahi ya walimu, kuchukua matatizo ya wanafunzi, lakini kujua upungufu na mafanikio katika shule wanazokagua ili waiwasilishie Serikali. Ni muhimu Idara hii ya Ukaguzi pia iwezeshwe kulingana na mahitaji yao yote ili wafanye kazi vizuri kwa kuinua kiwango cha ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, jamii imejisahau si kama miaka ya nyuma ilipomwona kila motto au mwanafunzi anatimiza wajibu wake wa kuhudhuria shule kwa kadiri anavyotakiwa. Pale ambapo mtoto anakwenda kinyume hata kimaadili, basi jamii ichukue nafasi ya wazazi, walimu kuwarekebisha. Jamii inaweza hata kuchukua jukumu la kukagua madaftari ya wanafunzi na kuangalia maendeleo yao kielimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni *overall*; iwawezeshe watoto au wanafunzi, miundombinu ya elimu, vifaa, vitabu vyta na ziada, masilahi ya walimu, mazingira bora ya kufundishia, kupandishwa vyeo vinavyoambatana na marekebisho ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, *last but not least*; namwomba Mheshimiwa Waziri wachunguze na wafuatie taarifa wanazoletewa na watendaji (*Progress Report*), kabla hazijachapishwa, kuwa *bindedna* kuwasilishwa kwenu, kwani *at the end of the day* wanalaumiwa wao kwa taarifa zilizo na upungufu kwani baadhi ya Watendaji siyo wa kuwaamini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asillimia mia moja.

MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuongezea mchango wangu kidogo kutokana na changamoto ambazo naendelea kuziona.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Kitabu cha Waziri, ukurasa 179, kwa mtaji huu Mkoa wa Shinyanga utabaki kushika mkia mpaka mwisho wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu, takribani masomo yote katika shule za sekondari ni mkoa huu umekuwa wa pili kitakwimu kuwa na upungufu wa walimu 4,164 ukiacha Mwanza ambayo ina upungufu zaidi ya walimu 4,235.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka kumekuwa kuna wahitimu katika vyuo mbalimbali. Je, ni sababu zippi zinafanya upungufu huu uendelee kuwepo na hasa Mkoa wangu wa Shinyanga?

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na Idara ya Ukaguzi iliyokamilika, tutaendelea kushusha viwango vya elimu katika nchi hii. Ofisi za Ukaguzi wa Shule za Sekondari kuwa kwenye kanda ni tatizo kubwa sana; kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga wakaguzi wanatoka Mkoa wa Tabora ambako ndiyo kuna ofisi na ni miaka mitano sasa hakuna shule hata moja iliyokaguliwa katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ione kuna umuhimu wa kuhakikisha Ofisi za Wakaguzi wa Shule za Sekondari zinarudi wilayani na kuzipatia vitendea kazi ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu pia wa Wizara ya Elimu kujitegemea. Kama Wizara hii habari ya mara TAMISEMI, sijui Utumishi ndiyo inaleta dosari katika ufanisi wa Wizara; Elimu itoke TAMISEMI!!

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundu pia irudi Wizara ya Sayansi na Teknolojia, kuwepo Wizara ya Elimu hakuna tija.

Mheshimiwa Spika, iundwe Tume ya Walimu itakayoweza kujikita kusimamia masilahi na shughuli zote za walimu. Tume hii itasaidia kupunguza kero za walimu.

Mheshimiwa Spika, suala la ukarabati wa Shule za Sekondari, nimesoma Shinyanga (M) kati ya Sekondari 17 za kata ni sekondari mbili tu ndiyo zimepata bahati ya kuwemo kwenye Kitabu cha Waziri. Hii ni haki? Naungana na

wachangiaji wengine kuwa, utaratibu huo hauna uwiano mzuri, kwani Mkoa wa Shinyanga uko nyuma sana kielimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kuwasilisha.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana (2012/2013) Wizara ilidhinishiwa fedha kwa ajili ya kuwalipa walimu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu hususani vijijiini. Fedha zilizotengwa ambazo zilitoka kwa wafadhili ni shilingi 500,000 kwa kila mwalimu. Mpaka sasa Serikali ipo kimya kuhusu ripoti ya fedha hizo. Je, Wizara imepeleka wapi fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, Walimu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana na hii ni sababu mojawapo ya kushuka kwa ubora wa elimu na kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika viwango vyote vya elimu. Naitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu matumizi ya fedha hizi na kama Wizara ilifanyia kitu kingine zaidi ya kulipa posho, basi itoe maelezo ya kina mbele ya Bunge jinsi ambavyo ilitumia fedha hizi ambazo zilipitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi, pamoja na majukumu yake makubwa na umuhimu wake mkubwa, imekuwa ikipuuza na Wizara kwa kutokuitengea fedha za kutosha. Idara ya Ukaguzi ndiyo pekee ambayo inaweza kuinua ubora wa elimu nchini, kwa kufanya ukaguzi mashulenii kuona jinsi ambavyo ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi unavyotekelvezwa. Kumekuwa na manung'uniko mengi toka kwa Wananchi kwamba, walimu wamekuwa hawafundishi sawasawa na pia mitaala ya elimu haifuatwi. Kitengo cha Ukaguzi tu ndicho chenye uwezo wa kutatua yote haya.

Cha kusikitisha, pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii kuishauri Serikali kutenga angalau shilingi bilioni kumi kwa mwaka huu licha ya maombi ya shilingi bilioni 13

wanazoomba, bado Wizara imeongeza shilingi 152,900,000 tu! Huu ni mzaha kwa Idara hii na pia ni aibu kwa Wizara ambayo inajinadi kwamba inategemea kuinua kiwango cha elimu kwa asilimia 80. Hili lengo litafikiwaje mwaka 2015 bila kuweka mkakati mahususi wa kukagua shule? Serikali itoe tamko ni kwa namna gani itainua kiwango cha ufaulu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali nchini wa kutumia Sekretarieti ya Ajira, una urasimu mkubwa na matokeo yake umesababisha Vyuo Vikuu kuwa na upungufu mkubwa wa wahadhiri vyuoni.

Licha ya urasimu, Sekretarieti ya Ajira wakati mwingine imekuwa ikiajiri wahadhiri wasiokidhi viwango na haya yametokea katika Vyuo vingi vya Serikali. Serikali irudishe utaratibu wa zamani wa kuviachia Vyuo Vikuu viajiri wahadhiri wake wenyewe kulingana na ufaulu wa wahitimu kwani wao ndio wanakuwa wanawafahamu vizuri wanafunzi wao.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni na mpaka sasa kumekuwa na manung'uniko kwamba, Somo la *Islamic Knowledge* limekuwa likisahihishwa vibaya na kwa uonevu na hivyo kuwasababishia watoto wa kiiislamu kufeli. Pamoja na kwamba, manung'uniko haya hayana ukweli wowote, ifike mahali sasa Serikali kupitia NECTA, ijiandae kwenye usahihishaji wa masomo ya *Bible Knowledge* na *Islamic Knowledge* na usahihishaji ufanywe na Taasisi za Dini. Hali hii ikiachwa, italeta mtafaruku mkubwa wa kidini nchini na mwisho uvunjifu wa amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumesikia juzi kwamba, Mheshimiwa Rais ameomba Walimu wa Sayansi na Hisabati kutoka Jamaica kuja kufundisha nchini. Suala hili siyo baya, lakini Wizara itambue kwamba, suala siyo ukosefu wa hawa walimu, bali ni namna ya kuwatunza na kuwafanya waipende kazi yao. Walimu wa Hisabati na Sayansi wapo wengi sana, lakini kutokana na kutokuthaminiwa na kupewa motisha ya kutosha ili kuwafanya wafundishe, wamekuwa wakionekana kama si chochote. Ndiyo maana shule za *private* wako wengi

wakati wamesomeshwa kwa kutumia mikopo ya fedha za walipa kodi wa Tanzania. Walimu watakaotoka Jamaica, watakuja na vitabu vyta hisabati na sayansi pamoja na maabara; ni mwujiza upi utawafanya wafundishe vizuri kama hilo ndilo tatizo linalowakumba walimu wetu waliopo mashulen?

Serikali ilete vitabu, maabara na vifaa, vilevile ione umuhimu wa kuwapa motisha Walimu wa Sayansi na Hisabati, vinginevyo hata tukileta walimu toka sayari ya *Mars*, tatizo litakuwa palepale.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma ya Jamii ilitembelea Miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyuo, mojawapo ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Bububi – Zanzibar. Ujenzi wa jengo hilo ulikuwa chini ya kiwango na jengo lilikuwa lina mipasuko mikubwa na hivyo kuhatarisha maisha ya wanafunzi. Kamati iliagiza Mkandarasi arudie ujenzi na kurekebisha palipo na matatizo kabla ya kufunguliwa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhara kubwa ya Wizara, walikiuka maagizo haya na kuamua kumwalika Rais wa Zanzibar na kulifungua jengo hilo lingali chini ya kiwango. Wizara ileze hiyo jeuri ya kuidharau Kamati ya Bunge imeitoa wapi? Na je, tuamini kwamba kuna ukweli wa maneno yaliyokuwa yanaseemwa kwamba Mkuu wa Chuo ana mahusiano binafsi na huyo Mkandarasi na ana *share* pale? Naitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ichukue maoni ya *TEA* kuweza kuutunisha Mfuko wa Elimu kwa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu Na. 8 wa Mwaka 2001 ili kuweza kutunisha Mfuko huu ambao utasaidia siyo tu kupata fedha za kupeleka kwenye Bodi ya Mikopo, bali utajumuisha uboreshaji wa miundombinu bora ya kufundishia na kujifunza udhibiti wa ubora wa elimu ya juu na mikopo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FAKI HAJI MAKAME: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa fursa hii ya kuchangia kwa maandishi. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Naibu wake, Mheshimiwa Mulugo, kwa Hotuba yao nzuri ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni ngumu na haina uzalishaji mkubwa, hivyo ni ya kutoa huduma zaidi, ndiyo maana lawama ni nyngi.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hawa hakuna haja ya kujiuzulu. Kuna haja ya kuendelea na jitihada zao za kuendeleza elimu nchini na kuboresha kiwango cha elimu. Hayo matatizo ya uhaba wa nyumba za walimu, upungufu wa walimu, ukosefu na upungufu wa samani (*furniture*), vyoo, maabara na kadhalika, ndiyo changamoto zenyewe za Wizara. Serikali ifanye upendeleo maalum wa kuongezea bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Taifa (*NECTA*) limejitätidi mno kurekebisha dosari zilizojitokeza, sasa mitihani haivuji. Jambo ambalo nashauri ni kuwa, vigezo vya ufaulu viwe wazi na viwe ni vilevile kwa masomo yote. Somo la Elimu ya Kiislamu kwa mfano liwe sawa na *Divinity*. Somo la Kifaransa lisitofautiane na la Kiarabu au Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Mheshimiwa Waziri za utafiti wa kupata suluhu ya matatizo yaliyojitokeza katika matokeo ya *Form IV* na *Form VI*, zithaminiwe na zisaidie kutatua matatizo. Hakuna sababu ya kumwajibisha Waziri wala Naibu wala Katibu Mtendaji wa Baraza, kuna haja ya kufanya marekebisheso ya kasoro hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo yanatosha hayo niliyosema. Ninakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika eneo moja tu. Mheshimiwa Rais, alikwisharidhia kwamba, Chuo kikongwe cha Ualimu, (*TC Mpwapwa*), kifanyiwe utaratibu mzuri wa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki (*Affiliated University*) cha Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Je, utaratibu huu au mpango huu muhimu umefikia wapi?

Utaratibu huu hauna maana ya kuvunja Chuo cha Ualimu Mpwapwa, bali ni kukiongeza hadhi tu na kutoa fursa ya Chuo Kikuu cha Dodoma kupata mahali pa kufanya mambo mengine ikiwemo *Block Teaching* za elimu.

MHE. JOHN P. J. MAGUFULI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na pongezi kwa Wizara, kwa kazi nzuri zenyehu changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri wa Elimu, ukurasa wa 125 na 126, pafanyike marekebisho shule za (166) Itale, (169) Zakia Meghji, (170) Buseresere, (172) Ilemela, (173) Nyamirembe, (175) Makurugusi, zipo Wilaya ya Chato, Mkoa wa Geita. Aidha, shule zote toka 201 – 206 katika Wilaya ya Chato zihamishiwe Mkao wa Geita na si Mkao wa Kagera. Kumbuka pia Wilaya ya Geita, ukurasa wa 192, ipo Mkao wa Geita na si Mkao wa Mwanza. Nina uhakika kuna marekebisho mengi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Butiama uharakishwe na ni vizuri Kitengo cha Maliasili na Utalii kijengwe Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafute mkopo ili kunusuru hali ya elimu nchini, kwa sababu Taifa tuna uwezo wa kukopesheka (*Credit Rating*) na pia uhimilivu wa deni (*Debt Sustainability Index*) tunao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis iyunjwe, kuwe na Wizara ya Elimu na Utamaduni (Shule

za Msingi na Sekondari) na sehemu nyingine kuwe na Wizara ya Elimu ya Juu , Sayansi na Teknolojia kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *VETA* uharakishwe na Wilaya ya Serengeti ijulishwe kwa vile eneo limetengwa ekari 70.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uimarishwe, bila ufuatiliaji na usimamizi wa karibu, upungufu katika elimu utazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ugatuaji na mgawanyo wa majukumu utekelezwe kikamilifu. Bila ya ugatuaji kukaa vizuri, migongano itaendelea na kuzorotesha elimu.

Mheshimiwa Spika, kuwe na Kamisheni ya Elimu. Kuwe na chombo kimoja kinachohudumia walimu, itarahisisha usimamizi na kuboresha utaratibu wa ajira ya walimu.

Mheshimiwa Spika, *SDL* iongezewe asilimia tano ili isaidie kuimarisha Taasisi (Mamlaka) ya Elimu (*TEA*) na Bodi ya Mikopo na pia Hazina ichukue jukumu la kutoa fedha za Bodi ya Mikopo. Hii itasaidia kutoa fursa ya fedha nyingine itumike katika maeneo mengine (*OC*).

Mheshimiwa Spika, utatuzi wa hali hii ya elimu; ni vyema uandaliwe marekebisho (maboresho) kwa kuchambua ni yapi ya muda mfupi mfano, nidhamu, madaraja na maslahi; muda wa kati; na muda mrefu mfano, sera.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wahadhiri kutopewa kibali cha mkataba mapema; hili lipo katika hali mbaya sana hasa katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (*MUHAS*). Kuna upungufu mkubwa sana wa wahadhiri hata kutishia Idara nyingine kukosa kabisa wahadhiri kama *Physiology*.

Mheshimiwa Spika, fedha ya *Capitation* haisimamiwi wala kutumika vizuri, hivyo ni vyema fedha hizi za *capitation* zikasimamiwi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kujitegemea irejeshwe mashulenii; hii itasaidia kuandaa wanafunzi kujitegemea baada ya masomo.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, bado Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambao wanajiunga na vyuo hapa nchini, ina changamoto nydingi na hii inasababishwa zaidi na upungufu wa bajeti ambayo inapewa Bodi hii kwa ajili ya kujiedesha. Pia wimbi kubwa la wale wanaopewa mikopo na bila ya kuirejesha kwa wakati baada ya ajira zao.

Mheshimiwa Spika, ombi la mikopo hii kutokuwafikia baadhi ya watu bado lipo, ambapo vijana wetu wengi hususan wale ambao wanatoka vijiji ama katika familia maskini, kuendelea kukosa haki yao hii, ilhali wale watoto ambao wapo mijini na ambao wazee wao wanajiweza kifedha, ndiyo ambao hufaidika na mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni hatua gani za makusudi alizochukua kukabiliana na tatizo hili ili watoto wa walalahoi wasiendelee kuteseka kwa kukosa haki yao?

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani au Bodi ya Kutunuku Madaraja; ni masikitiko yangu makubwa sana kuona vyombo hivi ambavyo Taifa imeviamuru na kuvipa majukumu kwa lengo la kuboresha elimu hapa nchini, vimegeuka na kuwa ni kero kwa wanafunzi na hata wazazi na walimu. Baadhi ya Watendaji wanatumia mamlaka walijonayo, kuiyumbisha nchi na kuthubutu kumpoteza Mheshimiwa Waziri, ilimradi tu Mheshimiwa Waziri aonekane ameshindwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Tume ya Maadili, iwachunguze na pale itakapobaini kuwa na uzembe ama udanganyifu wa makusudi, basi Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anatuasa kila siku

kuhusu suala la Udini, lakini imedhihirika ya kwamba, Mkurugenzi na Timu yake wanafanya matendo ya ubaguzi wa kidini dhidi ya dini nyingine. Wengi wa watendaji wa Baraza na Bodi ni Wakristo; kwa hiyo, hutumia fursa waliyonayo kuuwa Elimu ya Dini ya Kiislam.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo juu ya kadha hii ambayo tayari imeshalalamikiwa na Wadau wa Elimu hasa wa Dini ya Kiislam na atueleze hatua ambazo amechukua dhidi ya watumishi hao ama hatua ambazo anafikiria kuzichukua ili kujenga mustakabali mwema.

Mheshimiwa Spika, hali za walimu nchini ni duni na Chama cha Walimu Tanzania hakina tena nguvu za kuwatetea walimu. Naishauri Wizara na Serikali kuona haja ya kurejesha upya Kamisheni ya Walimu (*Teachers' Service Commission*) ili walimu wawe na chombo cha kuwatetea na kushughulikia matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Waziri na timu yake, watuletee Mpango Mkakati ambao Wizara imejipangia kushughulikia matatizo ya Idara ya Ukaguzi.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Kitengo cha Ukaguzi ili kuhakikisha elimu inayopatikana ni bora. Kitu gani kimetokea mpaka Kitengo cha ukaguzi kutotengewa fedha za kutosha?

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye Wakaguzi hawafanyi kazi kwa kuwa hawapewi vitendea kazi na Halmashauri zingine hakuna kabisa wakaguzi. Je, Serikali haioni kuwa shule kutokukaguliwa ndiyo maana *quality* ya elimu inaendelea kushuka? Serikali ije na majibu jinsi gani mtahakikisha ukaguzi wa shule unafanyika.

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa wanafunzi huchangiwa pia na mazingira bora ya mahali pa kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya shule hasa zile

za vijijini ni duni mno. Kama tungekuwa tunafuata *standard* za shule inavyotakiwa, nyingi zingefungwa na kama ukaguzi ungekuwa unafanyika tungeweza kubaini upungufu mkubwa. Shule zetu hazina madawati, hakuna maabara, vyoo havitoshi, maktaba hakuna, shule zingine hazina sakafu na wengine wanasomea chini ya miti.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi pia hazina Walimu, mfano Wilaya ya Kigoma Vijijini (Uvinza na Manyovu, upungufu wa walimu Shule za Msingi ni takribani walimu 600). Kwa upande wa madawati, katika Mkoa wa Kigoma peke yake, madawati shule za msingi ni 141,108, yaliyopo ni 89,206 upungufu ni 51,902. Shule za Sekondari mahitaji 90,599 yaliyopo 51,905 na upungufu ni 37,694.

Mheshimiwa Spika, vitabu pia ni tatizo, sasa hivi kitabu kimoja watoto wane, maeneo mengine hadi watoto sita, kwa shule za sekondari kitabu kimoja watoto hadi saba. Mafanikio ya elimu lazima yawe chini. Mfano mwengine mdogo; ipo shule inaitwa Mtanga, ina wanafunzi 502, Walimu sita tu na ilianza mwaka 1971, ni shule kongwe ile haipati Walimu kwa kuwa ni kijijini, ipo Kanda ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, hali ya shule hii kwa upande wa mazingira ni magumu; vyoo havitoshi, madarasa hayatoshi, yaani ni tabu tupu. Walimu wanahitaji motisha ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Nyumba za walimu ni muhimu zijengwe.

Mheshimiwa Spika, napenda Wizara itueleze lengo la kuanzisha shulenii Somo la TEHAMA liliikuwa ni la kisiasa au la kutaka kuelimisha? Vijiji vyetu vingi havina umeme, shule nazo hazina umeme huko vijijini na vilevile zipo shule mijini hazijawekewa umeme. Shule hazina maabara ya *computer*, watoto wanachorewa *computer* ubaoni; wataelewaje wakati wengine hata TV hawajawahidi kuionna? Kama Serikali ina dhamira ya dhati wekeni umeme shule zote na *computer* zinunuliwe shule zote ili mtoto aweze kuelewa kwa nadharia na vitendo.

Mheshimiwa Spika, mitaala inabadilishwa kila mara lakini walimu hawapewi semina elekezi. Kutofanya hivyo, mnawachanganya walimu na walimu, nao wanawachanganya watoto. Walimu washirikishwe kila mtaala unapobadilika.

Mheshimiwa Spika, tatzizo lingine ni la utofauti wa vitabu, sasa hivi kila shule ina vitabu vyake. Siku hizi vitabu havijulikani ni vipi vitumike? Hii inasumbua watoto na izingatiwe watoto wanachanganyikiwa na mitihani inafanana nchi nzima wakati vitabu havifanani?

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa kurejesha kusoma kuandika na kuhesabu, darasa la kwanza na la pili halafu darasa la tatu masomo yaongezeke kama zamani. Leo hii mtoto wa darasa la kwanza anabeba madaftari mengi, karibia kumi, mnawachanganya watoto kwa kuwafundisha masomo mengi. Wafundishwe kusoma, kuandika na kuhesabu. Serikali iache kutunga mitihani inayolazimisha watoto kujibu kwa kuchagua, yaani *multiple choice*. Walimu wengi pia wanapinga hili, linafanya watoto wabuni majibu ndiyo maana wanafeli.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya gherama za shule binafsi, bei zinapangwa kiholela sana. Lazima Serikali iangalie suala hili upya na iingilie katika ili Watanzania wasilumizwe na wenye shule kwa kutozwa ada kubwa pasipo sababu yoyote.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwitwa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Naibu Waziri, TAMISEMI anayehusika na shule za msingi na natumia madaraka yangu kwamba nitampa dakika ishirini. (*Makof*)

Naomba usogee hapa, dakika ishirini huwezi kukaa huko.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuititia bajeti hii ya Wizara ya Elimu,

naomba kutoa baadhi ya fafanuzi zilizojitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wakiendelea kuchangia mambo kadhaa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya michango ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakionesha sana tatizo la mfumo wa elimu nchini, ambao unaonekana kwamba labda unakwaza utendaji mzima na uendeshaji mzima wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niwajulishe nikiwa nafahamu kwamba, mabadiliko hayo wengine hawayafahamu ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kutoa huduma nzuri na bora kwa Walimu na kwa ukaribu ili kuweza kusheheneza huduma za Walimu.

Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko ya uendeshaji wa elimu nchini, kwa kugatua madaraka ya elimu ya msingi na sekondari, kuyaweka kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ili kuweza kutoa huduma hizo kwa ukaribu. Jambo hili liliifanywa likitokana na *study* ambayo tuliendelea kuiona katika uendeshaji wa elimu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi shule za msingi nchini ziliikuwa zinasimamiwa na Halmashauri kwa maana ya kuratibu utumishi wao, haki zao, stahili zao, lakini pia, ukaribu wa kufuutilia utendaji wao wa kazi na ilionekana kuwa na mafanikio zaidi wakati ule sekondari zikiwa zinaratibiwa na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na shule chache sana kufikia mwaka 2005, tukiwa na shule 581, bado Walimu wa shule ya Sekondari walikuwa wanajibika kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu. Jambo ambalo liliikuwa linakwaza sana utendaji wao kwa ukaribu kwa sababu, mwalimu wa shule ya msingi Nambilanje kule Mkoani Ruangwa Wilayani Lindi, alikuwa analazimika kuomba ruhusa ya wiki kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu jambo ambalo usafiri tu wa barua yenye kwenda na kurudi ilikuwa gumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko hayo na kufanya pia huduma za Walimu wa sekondari kurudi kwenye Halmashauri. Hili naomba nilitolee ushahidi, kwa ku-*declare interest* kwamba, mimi mwenyewe nilikuwa Katibu wa Chama cha Walimu Mkoa na mionganoni mwa mambo ambayo tulikuwa tumejadili kwa kusikiliza kero za sekondari, ni kuweza kuwarudisha na wao waingie kwenye mfumo ambao wanahudumia Walimu wa shule za msingi ili kuboresha huduma zao.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo iliyopelekea Walimu wa Sekondari, kufikia mwaka 2006, kuwa nyuma sana kwenye madaraja yao. Baada ya kuingia kwenye Halmashauri sasa Katibu *TSD* wa Halmashauri, walifanya kazi kubwa sana ya kuwapandisha Walimu wote madaraja yao na ndicho kilichosababisha kuwa madeni makubwa ya malimbikizo ya mishahara kwenye mishahara ya Walimu wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amegawa kazi hizi, Wizara ya Elimu na TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu jukumu lake sasa ni kutunga sera. Mbili ni kuandaa mitaala ya masomo mbalimbali, kufuatilia ubora wa elimu ikishirikiana na Taasisi zake ambazo ni Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Ukaguzi wa Shule. Lakini Wizara hii pia, inashughulikia mafunzo katika Vyuo vya Ualimu, VETA na Vyuo Vikuu. Wizara pia inafanya shughuli mbalimbali za utafiti juu ya masuala ya elimu, pamoja na majukumu mengine, haya ndiyo maneno ya msingi ambayo Wizara ya Elimu kwa sasa inayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inafanya kazi zifuatazo:-

Kwanza, kazi yake kubwa ni kuhakikisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za elimu za kila siku za ufundishaji mashulenzi zinafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Pia, suala la uratibu wa watumishi wake ndani ya TAMISEMI kwa maana ya Walimu na utumishi wao kwa ujumla, unashughulikiwa na TAMISEMI.

Eneo hili nataka nieleze kwamba, Walimu hawa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI sasa, wanawajibika kwa Katibu Mkuu wa TAMISEMI. Maslahi ya Walimu yasiyo ya mishahara yote yanashughulikiwa na Ofisi wa Waziri Mkuu TAMISEMI, ambayo ni uhamisho, likizo, matibabu, masomo na shughuli zote za kikazi ambazo zinahitaji kufanya malipo, hizi zinashughulikiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, pia, usimamizi wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pilii, kidato cha nne na kidato cha sita. Kazi hizo zinafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI; lakini ndiyo inayohusika na uchaguzi wa wanafunzi wana jingga na kidato cha kwanza na kidato cha tano. Hizo ni kazi ambazo zinafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa ukaribu wake wa wahudumiaji huduma kwenye maeneo ya vijiji au kwenye Halmashauri za Wilaya, ndiyo inayoshughulikia kuratibu shughuli za miundombinu. Ujenzi wa vyumba vyya madarasa, nyumba za Walimu, maabara, madawati na vyoo, hivi vinaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, pia, ndiyo inaandaa na kuhuisha takwimu za elimu ya awali, msingi na sekondari. Kwa hiyo, kwa hili tunashirikiana pia na chombo maarufu kilichopo Wizara ya Elimu ambacho kinajulikana kwa jina la *BEST*. Pia, ndicho kinachoshughulikia kuhamisha watumishi Walimu kutoka eneo moja hadi eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, pia, yako mambo mengine ambayo tunaendelea kuyafanya, ili kuweza kukamilisha huduma ya Walimu, tunashirikiana sana na Wizara ya Elimu katika kuhakikisha kwamba, shughuli zetu tunaziratibu vizuri. Kwa hiyo, katika eneo hili, tunapozungumzia maslahi, ambayo pia yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, namna ambavyo Walimu wanalamika.

Mheshimiwa Spika, matatizo tuliyonayo kwenye maslahi ya Walimu. Eneo hili ukiondoa maslahi ya malimbikizo

na mishahara ambayo sasa yale yako chini ya Utumishi, Ofisi ya Rais. Sisi tunajihuisha sana kwenye malipo katika maeneo yale ambayo nimeyataja, utaratibu tunaotumia ni kwamba, kila Halmashauri na Idara hii ya Elimu wanabaini mahitaji ya Walimu wanaotakiwa kwenda likizo na kutuletea Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, sisi tunatao fedha kwa ajili ya eneo hilo, kama ni likizo, kama ni matibabu, kama ni uhamisho wa Walimu na yale maeneo mengine kama masomo. Maeneo hayo Walimu sasa watalazimika kuandika barua kwa Mkurungezi kwenye maeneo yao, ili waweze kuhudumiwa kwa ukaribu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unaendelea na eneo hili tumejaribu kupunguza kwa kiasi kikubwa. Nataka niseme tu kwamba, kwa kuwa kada hii tuna Wallmu wengi na tunajaribu kupeleka fedha hazitoshelezi kweli kuwapa Walimu wote kwenda likizo, lakini tunajitahidi angalau wale Walimu wanaopata nafasi ya kuwekwa kwenye orodha na kwenda kwa mara ya kwanza, tunawalipa nauli kamili ya kwenda kwao wanakotakiwa kwenda. Kwa hiyo, utaratibu huu unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, walizungumzia suala la ujenzi wa shule mpya ambazo tumesema tunataka tuzikarabati shule hizi, ziwe na miundombinu inayojitosheleza, zitambulike na zionekane kuwa ni *functional school* ambazo zimeonekana kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo hili linaratibiwa na TAMISEMI na TAMISEMI tumeshaanza utaratibu wa awali na Waheshimiwa Wabunge tumewashirikisha kwa kuzibaini shule 264 ambazo kwa sasa uendelezaji wa ujenzi wake unaendelea kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka niliwaletea orodha ambayo tuliletewa na Halmashauri ya kuchagua shule mbilimbili kila Halmashauri ambazo zitaingia kwenye awamu

ya kwanza ya ukarabati na zile shule zilipoletwa hapa, niliwaletea nakala hizo Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja aone shule ambazo zimeteuliwa kutoka mahali unapotoka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, niliwaletea orodha ya fedha zilizotengwa kwenda kwenye shule hizo. Nataka niwaambie sasa kazi zile zinaendelea, ukienda kwenye Wilaya yako, ukiuliza zile shule, utaona kazi ya kukamilisha miundombinu inaendelea.

Mheshimiwa Spika, malengo yetu katika shule hizi ni kwamba, kila shule inatakiwa kuwa inaongezewa vyumba vinne nya madarasa, nyumba mbili za Walimu, vyoo matundu manane ya wanafunzi, vyoo matundu mawili ya wanafunzi. Tujenge maabara, kila shule lazima kuwe na maabara kwa hizi zinazojengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, tutaweka mtandao wa maji kama hakuna mtandao wa bomba basi watajenga matenki. Pia, umeme, kama hakuna umeme wa kuvuta, basi watalazimika kuvuta *solar*. Hayo ndiyo yanawekwa kwenye shule na ndiyo yanayoendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa shule hizi tumeziweka katika awamu, hii ni awamu ya kwanza, awamu ya pili imeingia kwenye bajeti ambayo sasa tunaendelea nayo. Tukishapitisha bajeti, sasa tutateuwa shule za awamu ya pili. Awamu hizi zilizonekana kwenye kitabu, nimezitengua jana baada ya kuonekana kwamba, Waheshimiwa Wabunge hamkuridhika na hili na zilikuwa na kasoro.

Kwa hiyo, hizi tumezisitisha, tutaandaa orodha nyiningine na tutawaletea Waheshimiwa Wabunge na tutashirikisha na Halmashauri zenu, wale wataweka vipaumbele tuanze na shule zipi ili tuweze kupata 528 ambazo zitaingia kwenye awamu ya pili na awamu ya tatu, kutakuwa na shule 408, kwa hiyo, tutakuwa tumefikia shule zile zetu 1200.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, shule hizi zinaendelea, lakini kwenye eneo hili hili zilitamkwa zile shule kongwe

ambazo sisi pia tunawajibika kuzikarabati. Shule kongwe nchini kwa kweli zina hali mbaya na zina uchakavu mkubwa, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeamua kutenga fedha kwa makusudi, ili kukarabati shule hizi kuzirudisha katika hali yake ya upya na tayari tumeshatuma fedha hizi kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 na hadi leo hii baadhi ya shule zilishapata mpaka milioni 200, kwa kuwapelekea milioni hamsini hamsini, wanakarabati miundombinu ambayo wanaiona kwamba ina matatizo ili kurudisha hali ya miundombinu hiyo kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limejitokeza pia hati kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani alipokuwa anazungumzia suala la Shule ya Sekondari ya Mzumbe kukosa Miundombinu. Mzumbe ni miongoni mwa Shule za Sekondari ambazo tumeshazipelekea fedha, mpaka sasa hivi wana fedha millioni mia moja, ziko pale, kwa hiyo, ni juu ya Bodi na shule yao na utawala wao kuchagua eneo gani walipe kipaumbele kwanza ili waweze kuliondoa.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufuatilia, wataalam walishakwenda Mzumbe, kushirikiana na kuona kwa nini kuna matatizo hayo yaliyojitokeza wiki mbili zilizopita.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaendelea na hili, kuna suala la shule ambazo Mheshimiwa Hokororo alizungumzia shule zile kongwe, zile shule ambazo tuliamua ziwe *A-Level* na tumepeleka vijana wa *A-Level*, miundombinu yake bado imebaki inaendelea haitumiki.

Mheshimiwa Spika, tumetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, tumeshawaandikia barua tayari, nadhani wanatekeleza, kwamba shule zile zote ambazo sasa ni *A-Level* na zina nafasi kubwa ya Madarasa, Mabweni na Miundombinu mingine, mwaka ujao wa uteuzi wa wanafunzi wa Kidato cha kwanza wawaingize wanafunzi wa Kidato cha kwanza ili shule hiyo pia iwe *O-Level* na *A-Level*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa namna hiyo tunaweza kutumia miundombinu hiyo ili tuweze kulitekeleza

hii na hii ni pamoja na Masasi *Girls*, Ndanda Sekondari na Shule nydingine zote nchini ambazo zina aina ya namna hii. Kwa hiyo, nendeni pia mkaone utekelezaji wa jambo hili, tutaweza kupata mrejesho kuititia kwenu pia.

Mheshimiwa Susan Lyimo, aliweza kuzungumzia suala la *capitations* zinazotumwa mashulen, naomba kumjulisha tu kwamba, *capitations* hizi tumeziratibu vizuri na tunazipeleka fedha. Mwaka wa fedha 2012/13 ambao wewe umesema kwamba hatujamudu kupeleka fedha na ukasema Shule za Msingi mpaka sasa tumepeleka sh. 6,000 pekee na Sekondari sh. 8,000, nataka nikujulishe kwamba, kwa mwaka huu wa fedha, shule za msingi tumezipelekea shilingi bilioni 60.6 na hizi fedha tumezipeleka kwa robo mwaka, kwa maana ya *quarter*.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeshapeleka *quarters* tatu, bado moja hii ambayo tunakamilisha Juni na mchakato wa kupeleka fedha hizo unakamilika na zitapelekwa fedha hizi mashulen ili kuweza kukamilisha kwenye mahitaji ya fedha hizo. Mpaka sasa Shule za Msingi kila mwanafunzi ameshalipwa sh. 7,584 kwa kiasi cha fedha ambacho tumekituma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekondari kila mwanafunzi ambaye amepaswa kupata sh. 25,000/= tumeshatuma shilingi bilioni 22.4 mpaka leo hii, fedha ambazo tumetuma zimeshafikia sh. 13,981/= na tunaendelea kutuma na zitakamilika katika mwaka huu wa fedha unaokamilika mwezi Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba *capitations* tunazozipeleka, liko tatizo, tunalipata kwa Wakurugenzi kufikisha kwa wakati kwenye mashule yetu.

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa Morogoro, tumewaambia Wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanapeleka zile fedha kwa wakati na maeneo yote ambayo yanachelewa kupeleka fedha hizi, sasa tutachukua hatua

kali dhidi yao kwa sababu fedha zile ni maalum kwa uendeshaji wa shughuli za elimu kwa shule za msingi na sekondari kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza haya, jambo hili tumelipeleka kule chini ili sasa itusaidie kushiriki kikamilifu kufuatilia kwa ukaribu na ninyi pia, tunapoyatamka haya mnawenza kutusaidia pia kufanya ufuatiliaji. Kwa sababu Takwimu tunazipata na tunawaleta ili muweze pia kusaidia kufuatilia mambo haya yanakuja na muweze kutuletea mrejesho.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia suala la upungufu wa Walimu, Mheshimiwa Hokororo pia alizungumzia suala hili la upungufu wa Walimu kwenye maeneo mbalimbali, nataka nieleze tu kwamba, suala la upungufu wa Walimu nchini, tumeendelea kulfanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mahitaji yetu kwa shule za msingi ni Walimu 297,136, hizi ni takwimu mpaka Aprili, kwa mujibu wa kitengo chetu cha takwimu pale TAMISEMI na Walimu tulionao mashulenii kwa upande wa shule za msingi sasa ni 207,144, tuna upungufu wa Walimu 89,982 kwa mujibu wa takwimu zetu.

Mheshimiwa Spika, Sekondari tunahitaji Walimu 80,486, waliopo sasa ni 49,385 na pungufu ni Walimu 31,000. Hili ni pamoja na Walimu ambao tumewaaajiri mwaka huu kuanzia mwezi wa Februari na Machi na eneo hili Serikali iliajiri Walimu 26,434 ambapo Walimu 13,527 ni wa Cheti na Shahada 8,812 na 4,095 ni wa Stashahada. Hawa wote tumewapeleka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, liko suala la changamoto za Walimu wa sayansi, ni kweli na mimi nakiri, najua Mheshimiwa Waziri atakuja kulieleza, mkakati wa Wizara kwa ujumla wake kama watunga Sera, lakini sisi tumesema, tuliowapokea kati ya hawa ni Walimu 2,019 tu ambao tumewapokea kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi kuwasambaza pale inapowezekana na kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu tayari tumeshaanza mchakato wa kupeleka *mobile laboratory* kwenye shule na tumeshapeleka, sasa Walimu hawa tunaowapeleka kwenye shule zile sasa waende moja kwa moja kwenye *practical* ili wanafunzi wenyewe shule zile wafanye mitihani ambayo ni *practical* na wala siyo *alternative*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili tunaendelea nalo, tumeshatenga fedha kwa ajili ya kuendelea kupeleka *mobile laboratory* ili wanafunzi kwenye shule zetu wasome masomo ya sayansi na wala siyo *altenative*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makalla alitaka kujua pale kwake juu ya Shule ya Sekondari ya Wami Dakawa, ni kweli shule hiyo inaitwa Wami Dakawa na siyo Wami pekee, kwa sababu Wami, pale kuna shule nydingine inaitwa Wami, shule ya msingi. Sasa shule hizi zote tumeendelea kuzihudumia na tunayo shule ambayo tumeanza kuijenga pale pale kwenye kumbukumbu ya Mheshimiwa Hayati Waziri Mkuu, Mheshimiwa Sokoine.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kujenga, kuna jengo jeupe pale, ile ni shule ya sekondari, inayolenga kumkumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alioneckana kuwa mahiri sana hata kwenye sekta ya elimu. Kwa hiyo, shule hiyo tutaaendelea kuiboresha na tayari tumeshatuma fedha za kuendelea kuijenga, pindi itakapokamilika, shule hiyo itakuwa tayari, ni shule ambayo itakuwa inajulikana kama *Sokoine Memorial High School*, ambayo itaendelea kupokea vijana wa eneo hilo na maeneo mengine nchini kama kumbukumbu ya aliyekuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo nimetakiwa sana kutolea maelezo, ni haya ambayo nimeeleza na juu ya Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliyochomwa kwa mgogoro wa Gesi kule Mtwara, ofisi hii sasa ni kweli kwamba upande wa Maafisa wetu hawana mahali pa kukaa, lakini tumeshawatafutia eneo, tumetafuta majengo ya *TANROADS*

kwa muda, lakini tayari tumeshatenga fedha za *OC* kwa ajili ya kufanya *reallocation* ili fedha hizo zitumike kwa ajili ya kununulia thamani za ofisi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumetenga fedha kuititia Mkoani na sisi TAMISEMI tutachangia na tumejiandaa kupeleka bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi hizo ili watumishi wale waweze kurudi eneo lile.

Mheshimiwa Spika, najua bado nina muda mrefu wa kuendelea kuzungumzia masuala ya Walimu, suala la mgao nimeshazungumza. Tatizo la nyumba kwa Walimu, ni kweli, eneo hili lina matatizo makubwa, nyumba tulizonazo ni chache, ingawa tunaendelea pia kutenga fedha kwenye Halmashauri zetu na ziweze kusimamiwa vizuri kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kadiri ya idadi ya Walimu ambao sasa wanazidi kuongezeka na fedha ambayo tunaitenga, tutaweza kupeleka nyumba kwenye Halmashauri zetu kadiri ambazo fedha hizi zinapatikana. Najua siyo rahisi sana kuwajengea Walimu wote 270,000 wa shule za msingi, lakini tutaendelea kujenga nyumba, lakini bado tunaendelea kuziagiza Halmashauri kuititia mipango yao ya Halmashauri kwamba waendelee kutenga fedha kuititia bajeti zao ili ziweze kusaidia Walimu hawa kukaa kwenye nyumba kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pia, nataka nieleze juu ya uhaba wa vyoo kwenye baadhi ya shule, hili ni lile ambalo nimelieleza kwamba tunayo mikakati kwenye upande wa sekondari kuititia *committee* ya fedha ya *MMES* ambayo tunaituma kwenye sekondari ili kujenga miundombinu. Ni suala la Halmashauri kuona eneo la kipaumbele, tunaanza na nini ili tuweze pia kukamilisha idadi ya vyoo na tuweze pia kuhakikisha kwamba jambo hili linakamilika.

Mheshimiwa Spika, najua tunazo changamoto kubwa pia kwenye eneo la madawati, suala la madawati nashukuru pia kwamba mchakato wa fedha ya Rada sasa unaendelea

kwenye hatua ya zabuni na wakati wowote ule madawati hayo yatasambazwa nchi nzima kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mliamua kwamba, fedha hizi zipelekwe katika Halmashauri zetu ili ziweze kupunguza tatizo la madawati. Tumechukua hilo na madawati haya tutaanza kuyapeleka baada tu ya mchakato wa zabuni kukamiliika, na wale watakaofanya kazi kwenye maeneo yale pindi watakaporuhusiwa kufanya kazi ile mara moja.

Mheshimiwa Spika, suala la Hosteli ni suala pia ambalo ni kubwa. Tuna mahitaji ya Hosteli 4,729 kwa sasa kwa shule za sekondari, pamoja na fedha ambazo tunazipeleka ili kuweza kupata Hosteli bado zilizopo sasa ni 868 pekee. Pia tunahitaji Hosteli 3,856 kwenye shule zetu za sekondari. Kutokana na upanuzi wa uwepo wa shule za sekondari, tunakabiliwa na jambo hili kwa kasi kubwa, lakini tutaendelea pia kuhakikisha kwamba, tunapata Hosteli kwenye maeneo haya ili wanafunzi wetu wapate kulala mashuleni.

Mheshimiwa Spika, hosteli ya kwanza itakayopatikana, kwanza tunaamua tutatumia busara tu ya kuwapeleka kwanza wasichana wetu kulala kwenye zile Hosteli ili baadaye tutakapoongeza miundombinu hii tuanze kuwapata wale vijana wanaotoka eneo la mbali na sasa wanafunzi wote mpaka wale wanaokaa jirani waweze kulala shuleni, wapate kutekeleza ratiba kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili sasa, nirudie tena, tunajenga hizi Hosteli kwa nia njema, naomba wananchi wote nchini, tuendelee kulinda watoto wetu wa kike, tuendelee kuwaandalia utaratibu mzuri watoto wetu wa kike, wapate nafasi ya kusoma kikamilifu ili waweze kumaliza elimu yao ya sekondari na hatimaye huko vyuo vikuu bila kuingiliwa, bila kubughudhiwa kwa ushawishi wa aina yoyote ile unaoweza kumpelekea kuondoa na kuharibu mwelekeo wa masomo yake.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo nimyeandaa na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu anayo maeneo mengi ambayo anatakiwa kuandaa kwa

mujibu wa nafasi yake ya kushughulikia suala la Sera, anaweza kuja kusheheneza sasa mfumo, anaweza pia kuja kusheheneza taratibu zote za uendeshaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, bado tunaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba, uendeshaji wa elimu nchini unapokea sana changamoto hizi kutoka kwenu, lakini pia tumetoka kufungua milango kwa wananchi kuona namna sahihi ya kuendesha elimu hii nchini.

Mheshimiwa Spika, ninayo matumaini kwamba, kwa utaratibu huu tulionao sasa wa kwamba mnapata nafasi ya kuchangia na kutoa mapendekezo yenu, mfumo huu tunaweza tukauboresha hatimaye tukapata mfumo sahihi ambao pia unaweza kutuletea mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii pia kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu na kuwasihii Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono Bajeti hii, tuweze kuipitisha jioni hii ili tuanze kazi ya kuendelea kuendesha hizi shule zetu na kuondoa upungufu wote ambao mmeubainisha.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri na timu ya Wizara ya Elimu imesikia na sisi TAMISEMI tumewasikia, katika maeneo yetu tutawajibika na tutaendelea kushikamana nao na kushirikiana na Taasisi zote ambazo zinashughulikia masuala ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa muda uliobakia, Naibu Waziri mwingine hawezi kupata nafasi sasa, ni mpaka jioni watakapoanza kujibu hoja nyingine.

Nina matangazo mawili, moja ni kwamba Vyuo vyetu Vikuu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na cha Mzumbe, wameandaa maonyesho pale kwenye Viwanja vya Maonyesho na machapisho mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge mnaweza kupitia pale na kuona.

Tangazo lingine ni kwamba, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha Dar es Salaam, Profesa Yunus Mgaya, anaomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Watumishi wa Bunge waliosoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kesho, Tarehe 6, saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa kwa lengo la kufahamiana na kuwahamasisha ili waweze kutambua na kukiunga mkono chuo hicho katika kutekeleza dira na madhumuni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kwa hiyo, wale wote waliosoma huko, kesho kuna kikao pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo, nimesema katika Ukumbi wa Msekwa, saa saba mchana.

Kwa hiyo, pamoja na tangazo hilo lakini, kuna Fomu zitakazopitishwa kwa Waheshimiwa Wabunge hao, wazijaze na kuzirudisha kwa wahusika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa. Kwa hiyo, Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ni mmoja wapo, nadhani mtapewa hizo fomu, mjaze, mkaafahamiane na wawaeleze mambo makubwa wanayoyafanya huko sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.55 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha majadiliano wakati wa asubuhi, wale wote ambao walikuwa wameomba kuchangia na walitakiwa kuchangia walishamaliza na sasa nitaanza na mtoa hoja Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika 25.

Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha

kusimama hapa leo mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii iliyotolewa jana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa busara na hekima kubwa kwa muda wote wa majadiliano ya hotuba za bajeti kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wangu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, mmeeleza baadhi ya mafanikio, lakini vile vile penye mafanikio pana changamoto nyingi, lakini tunaahidi changamoto hizo kuendelea kuzitekeleza na kuzifanyia kazi ili tuweze kuboresha elimu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yanayohusu sera atayazungumzia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, lakini mimi nitajikita zaidi kwenye kuzungumzia masuala ya *EMAC*, elimu ya msingi, sekondari, vyuo vyaa ualimu, ukaguzi wa shule, madeni ya Walimu na pia *VETA*. Lakini vilevile pia nitajibu hoja kidogo zilizojitokeza kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine tutajijibui kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge kwa sababu nina dakika 25 na Mheshimiwa Waziri ana dakika 45, najua dakika 70 haziwezi kutosha kujibu hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa toka wakati ule wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, TAMISEMI yalikuwa yanagusa elimu na siku hizi mbili yaani jana na leo.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu ikumbukwe kuwa, mnamo mwaka 2000 Tanzania iliridhia mpango wa Kimataifa yaani Elimu kwa Wote au *Education for All* Dakar, Senegal mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, katika kuridhia mikataba hiyo ilimaanisha kwamba watoto wote wenye rika lengwa waweze kwenda shule na unapotaka kuwapeleka watoto wote wenye rika lengwa maana yake miaka minne elimu ya awali, miaka mitano au sita na saba elimu ya msingi, maana yake vijiji kote na mijini watoto wote waende shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ilikuwa baada ya pale ni jukumu la Serikali sasa kuanza kujenga shule za msingi kwenye mpango wa MMEM na mpango wa MMEM huo ndio ukazaa mpango wa MMES na mpango wa MMES ukazaa mpango wa MMEJU yaani Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni katika kutekeleza majukumu hayo idadi ya shule za sekondari kwa wakati huo kulikuwa na wanafunzi 289,689 mwaka 2001. Lakini sasa mpaka hivi ninavyozungumza, tayari tuna wanafunzi 1,884,270, hizi ni takwimu za mpaka mwaka 2012. Hii ikiwa ni sawa na ongezeko la wanafunzi 1,594,571 katika kipindi kifupi tu cha miaka 11.

Mheshimiwa Spika, idadi ya shule za sekondari iliongezeka kutoka shule 1,202 mwaka 2001 hadi kufikia shule 4,528 mpaka hivi ninavyoongea. Ongezeko hili ni kubwa sana na hasa katika upande wa nchi zetu za Kiafrika, ni nchi ambazo uchumi wetu unategemea bajeti za ndani na kidogo bajeti za nje tena kwa mkopo na baadhi ya mikopo ina riba kubwa na mingine riba ndogo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali yoyote duniani katika kutoa elimu ni kuwapa fursa sawa wananchi wake, wananchi wake wote lazima wapate elimu sawa na elimu bora. Utekelezaji wa kutoa elimu kwa wananchi unaweza ukafanyika katika taratibu au *system* mbili.

Mheshimiwa Spika, njia ya kwanza, ni *Qualitative Approach*, yaani kuanza na ubora kwa kuongeza fursa taratibu. Njia nyingine ya pili tunasema ni *Quantitative Approach* yaani kuongeza fursa nyingi na kisha kuinua ubora ambayo ndio njia hii nchi yetu ya Tanzania tuliyoichukua, tunaanza na *Quantitative Approach and then tunakwenda kwenye Quality Approach*. Kwa nini nasema hivyo? Tulianza kwanza kudahili wanafunzi wakati tulikuwa hatuna majengo ya shule yaani madarasa, maabara, maktaba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, si Tanzania pekee inayoweza kufanya hivi, tuna ushahidi wa nchi mbalimbali, hata wenzetu wa Mozambique na South Korea nao walikuwa wanakwenda katika mfumo huo. Kwa hiyo, tunapowashangaa wenzetu kwamba eti ni maajabu saba ya dunia, sijui labda hiki kitu wanakitoa wapi. Lakini kwa kawaida ukianza na ongezeko kubwa la fursa kwa kuongeza idadi ya shule na wanafunzi, ni vigumu sana kufikia ubora uliokusudiwa kwa haraka. Kwa hiyo, tukasema kwamba tutakwenda kutafuta ubora kwa polepole.

Mheshimiwa Spika, mipango ya MMEM na MMES kama nilivyosema tunapoanza na mpango wa MMEM ulizaa MMES maana yake wanafunzi hawa lazima wakishafika elimu ya darasa la saba lazima waende sekondari na wakishafika sekondari ni lazima wasambae kwenye vyuo vya ufundi, VETA na vyuo vikuu na wengine kuajiriwa katika sekta mbalimbali kutokana na kiwango chao cha elimu cha kidato cha nne. Vile vile baada ya kumaliza kidato cha sita ni lazima waende vyuo vikuu ambapo ndiyo nimesema kuna mpango wa MMEJU.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wapo baadhi ya watu wanasema kwamba, Wizarani tumekaa hivi hivi, hatuna mipango ya kuendeleza elimu nchini, lakini mipango ipo. Kama nilivyosema tunakwenda kwenye mfumo wa *Quantitative Approach* na siyo *Qualitative Approach* kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, hakuna Serikali yoyote duniani

ambayo ingeweza kuchukua mfumo wa *Quantitative Approach* ikaweza kwenda kwa haraka, miaka miwili ukawa umeshakamilisha kujenga madarasa yote katika hawa wanafunzi wote milioni nane, ukawa umeshamaliza kuwa na vitabu kwa wakati mmoja, bajeti yenyewe ni kama mnavyoionna na siyo lazima fedha zote ziende kwenye Wizara ya Elimu, tunajenga barabara, tunaweka mabomba kwa ajili ya maji, tunaweka vitu kwa ajili ya kilimo na tuna Wizara nyingi kama Wizara ya Afya na yenyewe inahitaji fedha. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu, fedha tunazopipata ndiyo tunafanya hivi vitu kwa polepole kama ninavyoweza kusema.

Waheshimiwa Wabunge, mmechangia sana suala la ubora wa elimu, lakini ningeomba tu mtuelewe katika misingi hiyo kwamba, tulianza na kujenga madarasa kwanza, tukaanza kuinua watoto waende kwanza shule halafu tuje tuanze kutafuta ubora kwa polepole na siyo Tanzania pekee bali ni nchi nyingi tu ambazo zimeweza kutumia huo mfumo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunganeanza kusomesha Walimu kwanza halafu kule hakuna madarasa na hakuna wanafunzi, sijui hao Walimu tungewalipa mishahara kutoka wapi? Si ndiyo wangkuwa wanaandamana barabarani? Tulianza kwanza kujenga madarasa tuinue watoto, halafu baadaye tumeanza kutafuta Walimu.

Mheshimiwa Spika, kuna mipango kabambe ya kupata Walimu, huu ni mwaka wa sita sasa vyuo vikuu vingi hapa nchini vimeweza kufungua program za *education* na watu wanamaliza. Chuo Kikuu cha Mkwawa wanafunzi wanasoma *education* karibu 80%, Chuo Kikuu cha *DUCE*, Chang'ombe wanasoma *education*, *UDOM* ndiyo nisimene kabisa na vyuo vingine vingi tu vya ualimu tuna vyuo 30 vinavyotoa mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya Shahada, *Diploma* na *Certificate*. Kwa hiyo, nataka tu kulielezea hilo kwa harakaharaka.

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na ongezeko kubwa la shule na wanafunzi ni wazi utoaji wa elimu uliathirika na hivyo kuathiri ufaulu wa wanafunzi kwa miaka ya hivi

karibuni. Waingereza wanasema *falling down is not a defeat, but the defeat is when you fail to stand up*, ikiwa na maana kuanguka si kushindwa.

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu au minne inayokuja kama tumeanguka, tutasimama na tutaendelea mbele, lakini nia ni kwamba *education for all* kama nilivyosema kwamba tuliridhia mkataba huo kwamba, wanafunzi wote ni lazima waende shule. Ni ngumu kutofautisha labda sisi tuwe kama Walimu tunafundisha, hata kwa upande wa hotuba ya Upinzani wanasema kwamba, Serikali ama Mawaziri wa Wizara Elimu tunataka kufanya Taifa hili liwe la wajinga ili wasieleweelewe na hivyo kuweza kuangusha elimu nchini, si kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tusingeweza kuyafanya haya kama tungakuwa na nia ya kuwadidlimiza Watanzania wasipate elimu, tusingeweza kujenga madarasa, tusingeweza kuinua wanafunzi, tusingeweza kujenga hizi VETA wala tusingeweza kujenga hata Chuo Kikuu cha *UDOM* ambacho katika Afrika nadhani ni chuo cha tatu kwa ubora. Tusingeweza kufanya yote hayo kama tungakuwa na nia ya kuangusha kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kitabu chake cha *How Europe Underdeveloped Africa* Hayati Walter Rodney anasema, naomba kunukuu; "*Development is a many sided process*" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mwandishi huyu alimaanisha maendeleo ni mchakato wa muda mrefu. Hata kwenye ndoa zetu kwenye familia, ukishafunga ndoa, baba na mama mtaanza na mnaweza mkaanza maisha hata kwenye nyumba ya kupanga, lakini baadaye mtatafuta kiwanja, baadaye mtaanza kujenga msingi, baadaye mtatafuta tofali, baadaye mtatafuta mbao, mtaanza bati, mtaanza *cement*, ukuta na kisha mtajenga nyumba na baadaye mtaanza masuala mengine ya kuingiza makochi na mambo mengine yaani *decorations* za kwenye nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge mtuamini kwamba, tunafanya kazi na ipo siku mtakuja kukumbuka hii mipango ya MMEM na MMES kwamba, imefanya kazi vizuri. Lakini pia na kwa wenzetu Wapinzani, ni kweli katika siasa za dunia hii na wananchi ni vema wakatambua kwamba mtu anayeitwa Mpinzani ni lazima apinge mipango yote ambayo anaona kabisa inaelekea kwenye maendeleo. Mipango yote ambao inakwenda kwenye maendeleo, katika Serikali zozote, yule anayeitwa Mpinzani ni lazima apinge tu. Ndivyo ninavyojua na ndiyo maana mnapinga maendeleo mazuri yanayoletwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hakuna Serikali yoyote duniani inayoweza kutatua matatizo yote yanayowakibili watu wake kwa wakati, *The Government cannot solve every problem for its people at once*. Ni kweli kabisa! Hakuna maendeleo yasiyokuwa na changamoto kwani hata Roma haikujengwa kwa siku moja, kwa hiyo Serikali ya CCM isingeweza kuwa na miujiza yoyote ile ya kujenga shule, kudahili wanafunzi kwa wakati mmoja, pia kusomesha Walimu, kununua madawati, kununua vitabu na vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nianzie na hilo kwa sababu ndugu zetu hawa wanapoona tunafanya mipango mizuri daima wao wanataka waipinge ili labda tusisonge mbele.

Mheshimiwa Spika, njibu hili ambalo limekuwa ni kero leo kwa Wabunge juu ya shule 528, nadhani ambazo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri *chapters* za mwisho imeonekana kwamba, shule nyingi zimekaa kama kiupendeleo upendeleo hivi, baadhi ya Wilaya au Halmashauri zimepewa shule tano, hata kwangu Chunya nimeona wameweka shule sita tu, lakini sehemu nyingine kuna shule 20 mpaka 30.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Majaliwa kwamba tumekaa kwa

pamoja TAMISEMI na Wizara ya Elimu tumeona kwamba, *draft* iliyokuwa imewekwa kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tunaomba tui-*cancel* na tutakuja na orodha nyingine mpya itakayokwenda kwa uwiano kama tulivyofanya kwenye shule 264.

Mheshimiwa Spika, katika zile shule 264 tulifanya kwa uwiano mzuri yaani shule mbili mbili japo baadhi ya Wabunge ilionekana zile shule mbili zimeangukia kwenye Jimbo moja kama kwa Mheshimiwa Mfutakamba. Tumeliona hilo na tutakapokuwa tunagawa mgawo mwengine kwa awamu ya pili tutazingatia hilo ili Mheshimiwa Mfutakamba uweze kutendewa haki kwenye Jimbo lako la Igalula, maana shule zote zile mbili zipo kwenye Jimbo la Tabora Kaskazini. Lakini waliokuwa wamezungumza sana juu ya shule hizi naomba waridhie tu kwamba, tumeridhia ombi lao kwamba tumefuta, tutazipanga upya tena bila upendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi vile vile wamechangia juu ya suala la ukaguzi kuwa mamlaka, Wabunge hao ni Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Assumper Mshama, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa Rweikiza, Mheshimiwa Benedicto Ole-Nangoro, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe na Wabunge wengine wengi wamezungumzia juu ya Idara ya Ukaguzi kuwa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilikusudia kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa Wakala, lakini sasa hivi tunaposema rasimu ya sera mpya mamlaka hii tunataka iwe mamlaka kwelikweli itakayoweza kutoa ithibati na udhibiti wa elimu na mafunzo hasa kwa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema hivyo? Upo umuhimu wa Idara hii kuwa mamlaka maana yake itakuwa na uwezo wa kisheria wa kutoa maamuzi na kuchukua hatua pale ambapo sera, sheria, kanuni na viwango vya utoaji elimu vinapokiukwa. Kwa kufanya hivyo kutaboresha uwajibikaji

kwa watendaji katika shule na vyuo vya ualimu na hivyo kuinua ubora wa elimu, kuliko sasa inapokuwa ni idara inakuwa kama ni idara tu inayoshauri kwani haiwezi kuchukua hatua, haiwezi kumpeleka mtu Mahakamani na kadhalika kama anakosea masuala ya ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tunafanya hivi tukiwa na *reference*, *TCU* ni mamlaka inayoweza kutoa *accreditation* kwa upande wa vyuo vikuu, *NACTE* ni mamlaka inatoa ithibati na udhibiti katika vyuo vya ufundi nchini, *VETA* vyuo vya ufundi stadi na kadhalika. Kwa hiyo, tukipata mamlaka kwenye idara ya ukaguzi ikiwa mamlaka maana yake itatoa ithibati kwenye shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujafikia huko kwenye idara ya ukaguzi kuwa mamlaka hapa katikati najua tutakuwa na mchakato mrefu mwaka mmoja mpaka miwilli.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo hoja hapa Mheshimiwa Mama Margaret Sitta alikazania sana hili na wengine kwamba, tusiwe tunaziruhusu shule kusajiliwa kama hazijatimiza vigezo ama viwango. Mtakumbuka kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeleta viambatanisho ambavyo tayari kule kuna vigezo mbalimbali vya ili mtu aweze kusajili shule, kama ni shule binafsi na hata kama ni shule ya Serikali kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, niliwaagiza watendaji wangu katika Idara ya Ukaruzi kwamba, sasa hivi ni lazima tuwe makini na hasa Waheshimiwa Wabunge ni kweli mnakuja Wizarani kwa unyenyekevu mkubwa kwamba naomba shule zangu kwenye Kata zipate usajili na kadhalika. Lakini sasa hivi tutakuwa wakali kidogo kwa sababu tukija humu ndani hamtuonei huruma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri mambo mengine haya na sisi tuwe wakali kidogo kwamba, Waheshimiwa Wabunge hizi shule sasa hivi hatutazisajili kama hazina ubora. Unakuta shule ina madarasa mawili, hakuna maktaba, hakuna maabara, hakuna maji wala hakuna nyumba za

Walimu, ni vizuri Halmashauri zitekeleze kwanza hayo *and then tutazipa namba za usajili wa shule.*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba ye ye alisema kwamba, alipata usajili mwaka 2011 Julai, shule yake ikapata namba ya kuanzisha kidato cha tano, lakini hakupata wanafunzi. Ni kweli suala hili Mheshimiwa Njwayo siyo wewe peke yako bali ni Wabunge wengi hata mimi Jimboni kwangu nina shule inayoitwa Maweni Sekondari tulipata wanafunzi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu kama tulivyosema mdondoko kidogo wa ufaulu wa kidato cha nne mwaka juzi na hata mwaka jana kwamba, vijana wengi hawakuwa wametimiza vigezo vya kuingia kidato cha tano, kwa hiyo, hii ilipelekea shule nyingi za kidato cha tano hata kama tulikuwa tumeipa *accreditation* ya kusajiliwa kuwa *A-Level* wakakosa wanafunzi, lakini tuna imani Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba *Alhamdulilahi* mwaka huu tunaweza tukakupatia wanafunzi katika mgawo wa kidato cha tano ambapo tutafanya mwezi huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Njwayo uwe na matumaini na sisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *EMAC* ambalo Mheshimiwa Mbatia amekuwa akilliongelea sana. Nataka tu kumshukuru Mheshimiwa Mbatia kwani hili suala la vitabu mwaka 2012, Novemba, alituletea vitabu na nilimwomba sana, vile vitabu nikavichukua na akanionesha yale makosa madogo madogo na leo hapa ameonesha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema jana kwenye jibu langu la msingi kwamba, vile vitabu havikuwa na makosa makubwa sana kiasi kwamba Mwalimu mtaalam wa hesabu asifanikishe kufundisha wanafunzi kwenye somo husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kitabu ni kitabu, ni lazima kiwe na usahihi kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri jana kwamba, kwenye *second edition*, tutayarekebisha yale

makosa na tutayarekebisha. Si hivyo tu, Wizara iliunda kikosi kazi cha kuchunguza muundo wa *EMAC* na utendaji kazi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mbinu mbalimbali za uchunguzi ikiwa ni pamoja na mahojiano na wadau wa elimu wakiwemo vingozi wa elimu, wachapishaji, Walimu na watathmini wa Miswada ya vitabu na kupitia baadhi ya vitabu vilivyopata ithibati ya *EMAC* zilitumika. Uchunguzi ulibaini na kutoa mapendekezo kadhaa kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tulibaini na kutoa mapendekezo kwamba, muundo uliokuwepo haukuwezesha *EMAC* kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kupendekezwa kuundwa kwa chombo kingine kitakachojitosheleza kimuundo.

Mheshimiwa Spika, kwa tamko hilo nataka tu kusema kwamba, tunaivunja *EMAC* na hivyo tutatengeneza kitu kingine kitakachokuwa hata kinafanya ziara kuchunguza vitabu kwenye *libraries* huko mikoani, tuweze kuona kama kitabu ni feki, basi tuweze kuchukua hatua za kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya *EMAC* ilikuwa na uhaba wa wataalam na rasilimali na hivyo kupendekeza kuajiriwa kwa watumishi wenye ujuzi na kitengo kupewa rasilimali za kutosha. Mikutano ya *EMAC* ya kupitisha Miswada ya vitabu haikuwa ikifanyika kwa nyakati stahiki kutokana na uhaba wa wataalam na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, kutokana na upungufu huo baadhi ya vitabu vilivyopitishwa na *EMAC* vilionekana kuwa na makosa ya hapa na pale ya kichapishaji na lugha kama alivyosema Mheshimiwa James Mbatia.

Mheshimiwa Spika, katika kurekebisha hayo Wizara yangu itaboresha mfumo wa Ithibati ya vifaa vya kielimu kwa kufanya mambo yafuatayo:

Kwanza, kama nilivyosema ni kuvunja *EMAC*, kuunda kitengo ambacho kitashughulikia ipasavyo ithibati na vifaa

vy a kielimu, tuwe na chombo kama *TBS* kinachowea kukamata kitabu hata kama ni shule ya *private*, kiweze kusema kitabu hiki hakina *EMAC* na kama kina *EMAC* basi kiweze kuchunguzwa undani wake, kiweze kukamatwa na tuweze kukifuta.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeamua kufanya mapitio ya vitabu vyote vyenye ithibati ili kubaini vyenye makosa. Vile vitakavyobainika kuwa na makosa vitaondolewa ithibati.

Mheshimiwa Spika, tuliona tuyaseme hayo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walilisema hili suala la *EMAC* na Mheshimiwa James Mbatia, mwaka jana aliletu hoja hapa na alishauri tuichunguze *EMAC*. Tumeichunguza na tumeona huo upungufu mdogo kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la ufanuzi wa kuhusu fedha za rada. Mheshimiwa Kassim Majaliwa, amekuja ameliezea hapa, lakini Mheshimiwa Esther Matiko, wakati akichangia pale mchana alisema tayari vitabu vimeshaanza kusambazwa kwa fedha za rada. Nataka kusema kwamba, vitabu vy a fedha za rada havipo na bado havijaanza kusambazwa, kwa hiyo, si kweli. Bado viko kwenye mchakato wa kusambazwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui Mheshimiwa Mbunge alitoa wapi hiyo kauli, lakini nataka tu kumwelewesha kwamba, fedha za rada vitabu vyake viko kwenye mchakato wa kukamilika kule TAMISEMI, ili angalau mwisho wa mwaka huu tuweze kuvigawa kwenye Halmashauri kwa shule za msingi kama tulivyoahidi. Nataka kuelezea hilo, lakini mambo ya kuelezea ni mengi ikiwa ni pamoja na madeni ya Walimu

Mheshimiwa Spika, hata kwenye hotuba ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wamelielezea sana hili suala la madeni. Nitumie angalau dakika mbili hizi niweze kutoa ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ya kulipa

madeni ya Walimu na watumishi wengine, Wakaguzi na Wakufunzi. Aidha, waajiri wote walielekezwa kuititia Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 2009, kutolimbikiza madeni kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutokufanya uhamisho wa watumishi pale ambapo hakuna fedha. Pia kuwa na mpango wa likizo za watumishi ambao unalenga kulipa likizo kwa wale wanaostahili. Kwa hiyo, tulisema kwamba, angalau kuwe na mipango maalum juu ya masuala ya likizo na kama hakuna fedha mtumishi asihame kituoni. Mwalimu asihame kutoka mkoa huu kwenda mkoa mwingine kama Halmashauri au pale kwa *RAS* hakuna fedha za uhamisho huo.

Mheshimiwa Spika, jumla ya madai yasiyo ya malimbikizo ya mishahara ya Walimu 22,250 yenye thamani ya shillingi billioni 20.2 yamelipwa katika ya Januari 2012 hadi tarehe 30 Mei, 2013. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 90.1 ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina shillingi bilioni 22.4. Kwa hiyo, madeni ya Walimu kwa kweli jamani tumelipa, hayo mnayoona Walimu wanasema labda hatujalipa madeni, wanalamika na mnasema labda hatulipi madeni, tunayalipa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, naomba mnielewe kwamba, madeni haya hayawezi kwisha kwa sababu wale ni watumishi, wanaendelea kuomba likizo na wengine kama nilivyosema, sisi ni binadamu, Mungu anaweza kutuchukua wakati wowote, kutakuwa na madeni ya mambo ya mirathi na kadhalika, matibabu na mambo mengine. Hayo yote ni madeni ya Walimu, kwa hiyo, inawezekana hayawezi kwisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaendelea kuajiri Walimu. Tulikuwa na madeni haya mwaka 2010, lakini mwaka huo huo tukaajiri Walimu wakawa na malimbikizo ya mishahara, wakaanza kutudai mwaka 2011. Mwaka 2011 tukaajiri Walimu, wakawa na malimbikizo ya mishahara, wengine likizo na safari, wakaanza kutudai mwaka 2012. Mwaka huu vilevile wanatudai ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, hata mwaka huu kuna Walimu wameripoti, lakini kutokana na mtindo wa kikompyuta wa mishahara, wengine wamecheleweshewa mishahara kwa mwezi mmoja na wengine miwili na wanaendelea kutudai. Kwa hiyo, ni kitu fulani ambacho tumekifanya kwa ujumla kutoka mwaka 2005 mpaka 2011, tulipokusanya madeni tumeshayalipa kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, nataka vile vile hili niliweke wazi ili Waheshimiwa Wabunge waone kwamba, Serikali haijaka tu kama ambavyo inasadikika. Tunafanya kazi kubwa na mambo ya Wizara ya Elimu kama tulivyosema asubuhi na Mheshimiwa Majaliwa amejaribu kusisitizia hapa kwamba, Wizara ya Elimu ni kubwa na mambo mengine yanafanyika TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ni vizuri wakaelewa kwamba, ziko kazi zinazofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na ndiyo maana kuna Naibu Waziri Mheshimiwa Majaliwa kule. Mimi naandikiwa *messages* sana na Mheshimiwa Waziri wangu hapa tunaongea kila siku ofisini pale.

Mheshimiwa Spika, unakuta kama Mwalimu wa shule ya msingi hajapata mshahara sjui huko Magu, Chunya au Sumbawanga huko, wanatuandikia *messages* sisi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, tunaosimamia sera na kuangalia ubora wa elimu, tumebakia na mambo ya kisera zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofı*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa mtoa hoja, hitimisha hoja yako.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii

kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa ufanuzi katika hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na wajumbe wa Kamati yake. Wamefanya kazi nzuri sana na wametupa ushauri mkubwa ambao umetuwezesha kufika mpaka hapa tulipofika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe na Susan Lyimo ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Elimu kwa maoni yao, ushauri na mapendekezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo, Mheshimiwa Philipo Mulugo, Mbunge wa Songwe, kwa kazi nzuri sana ambayo ameifanya kusaidiana nami katika harakati zote hizi za kuimarisha elimu katika nchi yetu. Nawashukuru pia Kaimu Katibu Mkuu, Bwana Celestine Muhochi Gesimba, Kamishina wa Elimu, Profesa Yustella Baralusesa, Wakurugenzi katika Wizara yetu, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Wakala, Mashirika, Mabaraza na Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Wizara yangu, viongozi katika ngazi mbalimbali na wafanyakazi wote kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na maandalizi ya bajeti hii. Kazi si nyepesi, ni nzito sana. Wizara kubwa, ina mambo mengi na inatupiwa jicho na kila Mtanzania kwa sababu ndiyo uhai na mategemeo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, shukrani zangu ziwaendee viongozi wa Vyama vyta Wafanyakazi na wataalam kwa ushirikiano wao. Napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Bagamoyo. Naomba niwashukuru sana Madiwani ambao wamehudhuria hapa, wapo pamoja nami leo, pamoja na wananchi wa Bagamoyo ambao wamehudhuria

tangu jana na kuwa pamoja na mimi leo kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Bagamoyo. Nawashukuru kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu Jimboni, pia kwa kunivumilia pale ninapokuwa nimepata dharura za majukumu mengine. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri una dakika 45 tu, maneno hayo siku hizi tumeyaacha.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja zao kuhusiana na sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi. Aidha, baada ya kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu, Waheshimiwa Wabunge 48 walitoa hoja zao kwa kuongea na 63 kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, hoja za Waheshimiwa Wabunge zilihusu maeneo makuu yafuatayo:-

Elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya ualimu, ukaguzi wa shule, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya juu, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nitatoa ufanuzi kwa baadhi ya maeneo yaliyojitokeza wakati wa majadiliano, ingawa kutokana na ufinyu wa muda sitegemei kuweza kutolea ufanuzi hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, naahidi kuwa hoja za kila Mbunge zitajibowi na Wizara yangu kwa maandishi katika kabrasha moja ambalo tutalikabidhi katika Ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao waliyointoa kwa maandishi na kwa kuongea hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Michango hii mizuri

na iliyojaa busara itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii na kuboresha sekta ya elimu na mafunzo katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kutoa ufanuzi katika hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo na nitaanza na hoja zile ambazo zilitokana na michango wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuwa Serikali ifanye tathimini kuangalia uwezekano wa kubadilisha lugha ya kufundishia katika shule za msingi za Serikali ili ziweze kutumia lugha ya Kiingereza kama ilivyo kwenye shule za msingi za binafsi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufanuzi ufuatao:-

Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 ilizingatia mapendekezo ya Tume ya Mheshimiwa Marehemu Makwetta, ambapo inaeleza wazi kuwa lugha ya kufundishia elimu ya msingi ni Kiswahili na Kiingereza ni soma la lazima. Hata hivyo, baadhi ya shule za Serikali kama vile Arusha School na Kisimani ambazo ziko Arusha; Mkapa na Nuru ambazo ziko Mbeya, Diamond na Olympio ambazo ziko Dar es Salaam, Lupilisi ambayo iko Ruvuma na Mapinduzi ambayo iko Iringa, hizi ni shule za Serikali na zinafundisha kwa Kiingereza. Pia shule zisizo za Serikali hutumia lugha ya Kiingereza kufundishia ili tu kukidhi mahitaji ya wadau katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maoni ya wadau katika sera ya elimu na mafunzo ambayo inahuishwa na ambayo pia tumeshaileta Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wamepata nafasi ya kuitolea hoja mbalimbali na kuboresha. Rasimu ya sera ile inapendekeza kuwa lugha ya Kiswahili na Kingereza ziwe lugha za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo kuanzia awali mpaka chuo kikuu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja pia inasema Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na mfumo wa kupanga umri wa watoto shulenii ili kuwapima uwezo kulingana na umri wao. Mheshimiwa Betty Machangu ndiye alitoa hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wangu ni kwamba, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 inaelekeza kuwa elimu ya awali itolewe kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka mitano na sita. Waraka wa Elimu Na. 11 wa mwaka 2001 unaelekeza uandikishaji wa darasa la kwanza kuwa ni miaka saba na ndio utaratibu unaoendelea kutumika mpaka hivi sasa. Lengo ni wanafunzi wa darasa la kwanza waanze na miaka saba na wachache wenye umri unaozidi kidogo hapo nao pia wapate fursa ya kuingia darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, rasimu ya Sera mpya ya Elimu na Mafunzo inapendekeza umri wa kuanza darasa la kwanza kuwa miaka mitano hadi sita na Waheshimiwa Wabunge mmeiona na mmeiridhia, tutaipeleka kwenye *Cabinet* ikiwa katika hali hiyo.

Hoja nyingine ilihusu Serikali iondoe utaratibu wa maswali ya kuchagua, ama kizungu *multiple choice*, kwa mtihani wa hesabu wa darasa la IV na VII katika shule za msingi ili kuongeza ubunifu wa akili kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufanuzi ufuatao:-

Utaratibu wa maswali ya kuchagua, *multiple choice*, uliana mwaka 2012 kwa watahiniwa wa darasa la VII, baada ya kuanza kutumia mfumo wa usahihishaji wa kutumia kompyuta kwa mtindo wa *optical mark reader (OMR)*. Maswali ya kuchagua hayamfanyi mtahiniwa kuandika majibu kirahisi bali mfumo huu unamfanya mwanafunzi afikiri zaidi kwa vile majibu ya swali karibu yote yanakaribia ukweli. Kuna *choices* kama tano hivi, lakini zote zinakaribia ukweli, sasa kuweza kujua la kweli ni lipi, ni lazima ufanye kazi.

Mwanafunzi anapojojibu maswali haya anatakiwa kukokotoa kwanza ili kubaini jibu sahihi na ndipo aone jibu hilo liko katika herufi gani. Kwa hiyo, maswali ya kuchagua yanatungwa kitaalam na kuna utaalami wa kutunga maswali ya kuchagua, si kitu ambacho mtu ye yote yule anaweza akafanya. Ni jambo ambalo ni gumu zaidi kuliko hata kutunga maswali haya ya kawaida ambayo yanatungwa.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli itakuwa si haki kabisa kufanya maswali hayo ambayo tulikuwa tukiyafanya kwa shule za msingi mwaka 1961 wakati tunapata uhuru ambapo wanafunzi walikuwa 486,000 kwa Tanganyika yote, kabla ya Muungano. Hivi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanafunzi wa shule za msingi tunao 8,363,000. Ni ongezeko kubwa sana kutoka wanafunzi 486,000 kwenda milioni nane. Wanafunzi waliofanya mtihani mwaka jana walikuwa 986,000 kwa masomo mbalimbali. Hii ni kazi ngumu kusahihisha kwa mkono kama hutumii kompyuta kama ambavyo tunaweza kufanya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, pia tukumbuke kwamba kijana huyu amesoma kwa miaka saba, unamtahini kwa maswali machache kwa masaa machache. Yaani kazi yake yote tangu shule ya awalimpaka darasa la saba, unamtahini kwa masaa machache. Kwa sababu maswali hayo yako katika multiple choices, itabidi yawe machache, ndiyo ya-determine yeye kwenda kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa maswali hayo machache, haiwezekani kwa sababu wanasoma maeneo mengi sana hawa vijana na unataka kujua amefikia umahiri katika maeneo hayo yote au hajafikia. Unawezaje kufanya, la sivyo maswali yako yawe mengi. Utaweza kuyafanya kuwa mengi kwa kumtaka katika kila swali aandike jambo moja mpaka la mwisho badala ya uchaguzi? Haiwezekani! Kazi hii ni ya kitaalam na inafanywa kitaalam na si kila mtu anaweza akatunga maswali ya *multi choice*. Ni kitu ambacho kinaendana na utaalami.

Mheshimiwa Spika, hoja nyine ambayo ilitolewa ni

kwamba, Serikali iwawezeshe Wakaguzi wa shule kwa kuwapatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Betty Machangu, Dkt. Kebwe na Waheshimiwa wengine. Kutokana na uhaba wa muda acha niseme hoja yenye badala ya kuorodhesha majina yote.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufanuzi ufuatao:-

Idara ya Ukaguzi wa shule nchini inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinasababisha ugumu katika utendaji na ufanisi wa kazi. Changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa magari hivi sasa 56. Upungufu wa Wakaguzi, ambapo sasa hivi tuna upungufu wa Wakaguzi 289. Upungufu wa wafanyakazi wasiokuwa wakaguzi ambapo hivi sasa tuna upungufu wa wafanyakazi 1,222 na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ukaguzi yaliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, huu wa kibajeti ambao tunakwenda, Waheshimiwa Wabunge mkipitisha bajeti hii, tunachokitarajia ni kuteua Wakaguzi wapya 200, kununua magari tisa (9), kukarabati ofisi 11 na kununua samani za Ofisi tisa (9) za Kanda na Ofisi za Wilaya. Pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Serikali inaendelea na mchakato wa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa Wakala. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge mmesema sana, mmezungumza mno, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesikia, ni Serikali sikiu, inasikia na inapoahidi inatekeleza yale iliyoahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi hii tumeshaianza wala siyo katika Bunge hili, hatua iliyofikiwa mpaka hivi sasa ni kuwa, rasimu ya andiko kuhusu uanzishwaji wa Wakala tayari imeshakamilishwa, Mshauri Elekezi wa kuelekeza na kuweka utaalam wa kufanya kazi hii kwa ukamilifu ameajiriwa na kwa hiyo sasa Mshauri Elekezi atatakiwa kuititia ile rasimu ambayo kama Wizara na wataalam wa Wizara ndiyo wanasesma sisi

ndio tumefanya kwa kadri tunavyoweza. Lakini kuna wataalam hata nje ya Wizara, watu ambao wamebobeaa katika maeneo hayo ambayo ndio hao watalaam washauri watakabidhiwa hili andiko la Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya andiko hili kukamilishwa na Mshauri Elekezi, Wizara yangu itawasilisha andiko hilo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya hatua zaidi. Mategemeo yangu ni kwamba, kuwa joto hili ambalo Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza na kwa kwikwi na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi namna walivyoongea kwa jazba kuhusu hili na Ukaguzi, roho ya elimu yetu tunalifanya na tutalifanya kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kuwa Serikali iendelee kufanya mazungumzo na Chama cha Walimu ama CWT kuhusu maslahi ya Walimu ili kunusuru hali ya kuperomoka kwa elimu nchini sanjari na kuboresha mishahara na marupurupu ya Walimu ikiwemo kuongeza mishahara na marupurupu kwa watumishi wote wa Serikali, kwa vile maslahi ya watumishi kwa sasa hayalingani na hali ya maisha kutokana na mfumuko wa bajeti. Mheshimiwa Zambi alizungumza hivi kwa hali ya masikitiko makubwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengine walimuunga mkono na wakalizungumza hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi ufuatao:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ilizindua Baraza la Majadiliano ya Pamoja na Chama cha Walimu (CWT) tarehe 12 Septemba, 2012. Baada ya Baraza lilitokuwepo kumaliza muda wake Aprili, 2011. Baraza jipya limefanya jumla ya vikao vitano tangu lilipozinduliwa. Vikao viwili ni vya kisheria na vikao vitatu ni vya dharura kwa sababu hili ni jambo kubwa na ni jambo nzito, lazima twende kwenye majadiliano haraka iwezekanavyo na lazima tufanye majadiliano haya kwa nia njema, pande zote mbili Serikali pamoja na Chama cha Walimu. Kwa hiyo, vikao vitano vimeshakaa.

Mheshimiwa Spika, kikao cha mwisho kimefanyika mwezi uliopita kwa siku mbili, tarehe 24 – 25 Mei, 2013. Kwa hiyo kikao cha mwisho tumekifanya hivi karibuni ambapo Serikali iliwasilisha mapendelekezo ya maslahi ya Walimu kulingana na uwezo halisi wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, Walimu wamedai na Serikali imeangalia kwamba tutamudu kitu gani? Kwa hiyo, tumewawasilisha ili na wao waangalie hili kwa kujua kwamba nchi hii yote ni ya kwetu na uwezo ni ule uwezo wa kifedha wa nchi hii na Serikali inapata wapi fedha. Inapata kutoka kwa wananchi wake maana yake wananchi wake ni maskini, Serikali yenyewe haiwezi kuwa tajiri kama Marekani.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mishahara ya watumishi wa umma mwaka huu tunaomaliza Juni, 2012/2013, jumla yake ni sh. 3,781,000,000,000/= mishahara yote ya watumishi wa umma mwaka huu tunatekeleza. Kati ya hizo mishahara ya Walimu ni sh. 1,725,000,000,000/=, hiyo ni Walimu, wasiokuwa Walimu maana yake unachukua tofauti ile ambayo ni sh. 2,055,000,000,000/=, hiyo ni mishahara ya watumishi wale wasiokuwa Walimu, watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, sasa mapendelekezo yale ya Chama cha Walimu ya mishahara. Mishahara jumla yake ni sh. 3,452,000,000,000/=, posho ni sh. 1,795,000,000,000/=, kwa hiyo ukijumlisha madai yanakuja jumla ya sh. 5,248,000,000,000/. Maana yake kwa maneno mengine matakwa ya Walimu yale kwa mwaka huu wa fedha tunaomaliza yapo juu kushinda bajeti ya mishahara ya watumishi wote wa umma ambayo ni sh. 3,781,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kazi ndogo. Lazima Serikali ipate kigugumizi pale maana yake tunatekeleza bajeti. Mishahara yote sh. 3,700,000,000,000/= pamoja na Walimu, walimu wamekuja na madai mapya wanataka wapate sh. 5,000,000,000,000/, maana yake uchukue mishahara yote ya watumishi wote utawapatia Walimu halafu haitoshi, uongeze ndiyo ufile hizo sh. 5,000,000,000,000/= ambazo wanazitaka. Halafu sasa bado hujamaliza uondoke

hapo ukatafute hela zingine kwa sababu kuna watumishi wa umma ambao watakuwa hawajapata mishahara kabisa ni zero. Hiyo ndiyo sababu ilibidi tukae tuongee na ndiyo sababu hasa ikabidi Mahakama ikasema kakaeni muongee.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili la mishahara ni asilimia 51 ya mapato ya ndani ya fedha kwa mwaka 2013/2014 wa fedha tunaojadili, mapato yetu yote ya ndani ukiacha fedha zile ambazo tutafadhiliwa na wahisani. Ile tunayotengeneza sisi wenye we jumla yake ni sh. 10,161,000,000,000/=. Kwa hiyo, sh. 5,248,000,000,000/= za Walimu maana yake inachukua asilimia 51 ya mapato yote ya Serikali kwa mwaka huu ambao tunaujadili.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo siyo rahisi kwa Serikali kutimiza madai hayo kama yalivyotolewa isipokuwa tufanye majadiliano tuone kwamba, hizi hesabu ni za kweli, ndiyo fedha ambazo watakuwa nazo Hazina, haina siri, haina kificho, itawekwa wazi pale hata kama ikibidi Hazina ifunguliwe iangaliwe kwa sababu hata kwenye majadiliano Hazina nayo inawakilishwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wenzetu hawa wanapaswa kujua na kuona kwamba wapi tunaweza tukamudu. Majadiliano yanatarajiwa kuendelea baada ya kumaliza Bunge hili la Bajeti, lakini tunasema kwamba niwaambie Walimu nchi nzima Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi wala haina roho ya korosho na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inathamini sana elimu na huwezi ukathamini elimu kama huwathamini Walimu, kwa sababu ni kuititia walimu ndipo ambapo unaweza ukafanikisha malengo yako katika elimu bora katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tuna nia thabiti ya kuwatekelezea maslahi yenu Walimu, tuna thabiti ya kuwahakikisha kwamba tunapunguza vikwazo vyote vinavyowafanya mshindwe kufanya kazi yenu kikamilifu na tunaingia katika majadiliano kwa roho safi na moyo mmoja wa kutaka kutafuta njia ambazo zinatawaondosha katika matatizo yale ambayo yanawafanya saa zote mkae mnahangaika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa Serikali ihakikishie kuwa Vyuo Vikuu vinakuwa chini ya Wizara zinazohusika kwa mfano, *SUA* iondolewe chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo badala yake iende Wizara ya Kilimo na Chakula Mheshimiwa Jitu Soni alizungumzia hili kwa hisia kubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme hivi Vyuo Vikuu vya Umma vimekuwa vikianzishwa kwa agizo la Serikali ama *instrument* kulingana na mahitaji ya Taifa na uzoefu umeonesha kwamba tangu tupate uhuru mwaka 1961 Vyuo Vikuu vimekuwa chini ya usimamizi wa Wizara yenye dhamana ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vyuo vilivyoanzishwa chini ya Wizara mama ambavyo vilikuwa vinatoa programu za stashahada na shahada za juu. Kwa mfano, *IFM* na Vyuo vingine vya Uhasibu vipo chini ya Wizara ya Fedha. Ustawi wa Jamii ipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Chuo cha Biashara chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, wazo la kuliweka vyuo vikuu chini ya Wizara husika au Wizara mama nadhani halina uhalisia sana, kwa sababu Vyuo Vikuu vyote na Vyuo Vikuu Vishiriki vinafundisha programu mchanganyiko *multiple disciplines*, siyo *discipline* moja.

Mheshimiwa Spika, ukichukua kwa mfano, Chuo cha Sokoine cha Kilimo, *SUA* mbali na programu za kilimo pia kinafundisha ualimu, *MUCCOBS* inafundisha masuala ya ushirika, lakini pia inafundisha Wahasibu, inafundisha ujasiriamali, inafundisha *ICT* na fani zingine. *IFM* pamoja na kufundisha masuala ya Usimamizi wa Fedha mbali vile vile inatoa programu za *ICT*, Uhasibu, Sayansi ya Kompyuta na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, siyo kwamba ikiwa chini ya Kilimo maana yake itafundisha kilimo pekee yake, hapana, inatoa *disciplines* nyingi tofauti ambazo zitahudumia kilimo na zitahudumia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kimsingi wazo la kuvitawanya Vyuo Vikuu chini ya Wizara mama linaweza lisiwe na tija kwa vile kusimamia Vyuo Vikuu kunahitaji utaaliam na inaweza ikawa ni tatizo hasa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na mafunzo kama kila Chuo kitakuwa chini ya usimamizi wa Wizara mama.

Mheshimiwa Spika, Profesa Msolla alihoji mpango wa MMEJU utaanza kutekelezwa lini? Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu ambao umeanza mwaka 2010 mpaka 2015 umechelewa kuanza kikamilifu, umeanza kwa matatizo kidogo, kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ukarabati, ujenzi na upanuzi wa miundombinu unafanyika kwa fedha za bajeti ya Serikali ambazo hata hivyo hazitoshelezi mahitaji. Kwa sababu ya fedha kidogo mradi umetengewa fedha kidogo. Kazi imeanza, lakini siyo kama ambavyo tungependa ifanyike.

Mheshimiwa Spika, lakini tunashukuru kwamba pia chini ya Mpango huo, umeanzishwa Mpango ambao Benki ya Dunia imekubali kuu-*support* na huu mpango una fedha nydingi ni Mpango wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pindi Serikali itakapopata fedha za kutosha za ndani nayo itajazia katika zile fedha za Benki ya Dunia. Waheshimiwa Wabunge, nyie mnasikia wote, mradi huu umefanya makubwa sana katika Sekta hii ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mabumba alihoji bajeti ya Vyuo Vikuu vya Umma haikidhi mahitaji. Niseme ni kweli bajeti ya Vyuo Vikuu vya Umma haitoshelezi mahitaji. Suala hili linatokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali. Hata hivyo, Vyuo vinashauriwa kuwa na miradi ya ndani ya kuzalisha mapato wakati Serikali inafanya juhud ya kupata fedha za ziada za kuviezeshesha Vyuo kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii Waheshimiwa Wabunge mmesema bajeti ya mwaka jana si sawasawa na bajeti ya mwaka huu, mwaka huu fedha imeteremka na

fedha hii ikiteremka maana yake na Vyuo Vikuu vinapata haba. Hawa Waheshimiwa wanaoendesha Vyuo Vikuu ni Waheshimiwa ambao nawaheshimu sana, wanafanya kazi katika hali siyo nyepesi sana, ni wabunifu na wastahimilivu, hata Wahadhiri na Maprofesa kule ni wavumilivu sana na wao wanadai pia mabilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, lakini nawashukuru ni wastaarabu, wanazungumza Serikalini, lakini wanaisubiri Serikali iweze kuwatekelezea mahitaji yao. Wangkuwa watu wengine hapa, nadhani wangeitisha maandamano sijui kuanzia wapi mpaka wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli wenyewe lazima niseme kwa sababu siyo uongo, lingekuwa kama ni jambo la uongo nisingeweza kulisema hapa, nasema yale yaliyokuwa ya kweli.

SPIKA: Hajamtaja mtu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie kwenye hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Kamati yangu hiyo imehoji mambo kadhaa. Naomba nianze na hoja ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo iliyotolewa tangu mwaka 1994 hadi mwaka 2011. Nifafanue namna hii:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili mwaka huu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliweza kukusanya jumla ya sh. 32,970,000,000 ambayo ni asilimia 61 ya makusanyo ya mikopo ilioiva. Makusanyo ya mikopo ilioiva ndio ambayo imekusanywa, jumla yake ni sh. 53,630,000,000 kati ya hizo sh. 32,970,000,000 imekusanywa ambayo ni asilimia 61.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, hadi ilipofikia mwezi Aprili, 2013, Bodi ya Mikopo iliweza kukusanya sh. 12,820,000,000 ambazo ni asilimia 71 ya lengo la ukusanyaji katika mwaka huu wa fedha. Ni asilimia 71 ya malengo ambayo ilikuwa ni bilioni 18 na hii ni hatua

kubwa sana kwa sababu mwaka 2010 ukusanyaji kwa mwaka ulikuwa sh. 4,400,000,000/= mwaka 2010/2011, lakini mwaka 2012/2013, wamefikia sh. 12,820,000,000/= wametoka mbali sana, sh. 4,400,000,000/= wamekuja sh. 12,820,000,000/= kwamba ni jambo kubwa katika kipindi hiki cha miaka michache kama mitatu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo juhudini imeendelea katika kukusanya mikopo na niliishikilia sana Bodii hii, niliwaambia wasiwe mahiri tu katika kutoa mikopo, muwe mahiri katika kukusanya mikopo kwa sababu wanapokusanya maana yake Bodii inakuwa na uwezo zaidi wa kugawa mikopo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mikopo, Bodii iliweka mikakati ifuatavyo:-

(1) Kutumia taarifa zinazopatikana kutoka Serikali za Mitaa, kuhusu makazi ili kuwabaini wanufaika.

(2) Kuwahamasisha waajiri ili waleta majina ya waajiriwa wao ambao ni wadai.

(3) Kuhamasisha wadaiwa wenyewe ili wajitokeze kulipa mikopo.

(4) Kuwezesha urejeshaji kupitia njia ya mtandao na huduma za kibenki kupitia mtandao, kubaini wadaiwa kupitia Mawakala. Taarifa za mamlaka ya kodi Tanzania...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tupo ndani ya Bunge, naona kuna mazungumzo yanaendelea kila mahali mpaka hatuelewani. Naomba mwelewe kwamba tupo ndani ya Bunge. Naomba uendelee Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa hiyo, Bodii ya Mikopo imepanua nyenzo zile na mbinu mbalimbali za kuwezesha kukusanya mikopo hii kwa wingi zaidi na ndiyo maana sasa ukusanyaji umepanda kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wala hatuishii hapo nimezungumza mara kadhaa na Bodi na Mkurugenzi wake kwamba, wala tusiridhike na asilimia 61 au 71, tunachokitaka ni *hundred percent*, hata pale waliponiambia Mheshimiwa Waziri nenda nchi yoyote ile ambayo inatoa mikopo kwa wanafunzi hakuna ambayo imekusanya madeni *ninety percent*. Nikasema sasa sisi ndiyo tutakuwa mfano, tutakuwa wa kwanza kwa mfano, tutatolewa mfano na Bodi yetu itakuwa mfano kwa Afrika kwamba ndiyo Bodi mahiri kabisa yenye uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma ya Jamii ilihoji lifuatalo, utaratibu unaotumika kutoa mikopo haukidhi mahitaji ya watoto wanaotoka katika familia zenye vipato duni.

Mheshimiwa Spika, nitoe ufanuzi ufuatao:-

Serikali kwa sasa inapitia mfumo wa sasa wa utoaji mikopo ili waombaji wote wa mikopo wapimwe na kupewa mikopo kulingana na kigezo cha uhitaji kama Sheria iliyoanzisha Bodi inavyoelekeza. Mchakato huu siyo tu wa kupitia tena, maboresho mengi yamefanywa, lakini jambo kubwa zaidi ni kwamba, tumeanza kwenda katika mkakati ule ambaeo Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Madelu aliuletea hoja hapa kwamba Mfuko huu uwe mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Elimu uwe mkubwa, uwe na vyanzo vingi, siyo chanzo kimoja tu hiki cha Serikali bilioni 306 kutoka Serikalini, bilioni 20 ni zile zinazozungushwa na Bodi yenye we inaweka jumla 326 ndiyo inatolewa mikopo, hizi fedha zote zinatoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kikundi cha wataalam wa Tanzania mahiri wameanza kazi na wamefika mbali katika kuainisha vyanzo vingine ambavyo vitakuja kujumuishwa kuweza kutengeneza Mfuko huu na taratibu za kisheria. Kurekebisha sheria kutafanywa ili tuwe na Mfuko huu ambaeo Waheshimiwa Wabunge mnauhitaji na Watanzania wote

wanauhitaji, kwa sababu hakuna Mtanzania au mkulima au mfanyakazi ambaye angependa mtoto wake ashindwe kwenda kusoma elimu ya juu kwa sababu ya tatizo la fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya Kamati ya Huduma ya Jamii ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa fedha za kukamilisha ujenzi wa Taasisi ya Sayansi ya Bahari iliyopo Tanzania Zanzibar. Nifafanue ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi ya Bahari iliyopo chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilipata ardhi yenye ukubwa wa ekari 120 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka 2005 katika eneo la Buyu ili litumike kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi. Sababu za msingi zilizofanya ujenzi wa eneo la Buyu kusimama ni ufinyu wa bajeti za maendeleo ambazo zimeweza kutengwa na Serikali kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaelewa kuwa kwa kuchelewa kumaliza ujenzi huo gharama zake nazo zinaongezeka. Hapo awali dhamira ya Serikali ilikuwa ni kukamilisha ujenzi huu kwa gharama ya bilioni 6,391,056,108. Hata hivyo, pamoja na ufinyu wa bajeti Serikali imekuwa ikitoa fedha za maendeleo za ujenzi wa Taasisi hii kama ifuatavyo:-

Mwaka 2005/2006, ilitoa milioni 450; 2006/2007, milioni 800; 2007/2008, bilioni moja; 2008/2009, bilioni 1.12; 2009/2010, milioni 900; 2010/2011, sh. 1,212,000,000/=; mwaka 2011/2012, milioni 900 na mwaka huu wa fedha ambayo tunaumaliza ilitengwa sh. 1,100,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba hizi fedha mpaka hivi sasa ninavyosimama siyo zote ambazo zimeshatoka, lakini nina imani sana kwamba, Hazina imesikia kilio cha Kamati ya Huduma za Jamii, bila shaka kabla ya tarehe 30 Juni, Mungu akipenda fedha hizi zitakuwa zimetoka za bajeti ya mwaka huu wa fedha ambao tunaomaliza ili kuwezesha kile chuo kukamilishwa.

Ukikiona sasa hivi kwa kweli utakipenda, kimekaa vizuri, *design* nzuri, kinapendeza, nina hakika kabisa Tanzania Zanzibar inafurahi na bila shaka pengine tutapata mafanikio makubwa zaidi kwa kuweza kudahili vijana wengi zaidi katika fani hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imehoji pia utoaji posho maalum kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu na wakauliza posho ya shilingi 500,000 ilioyahidiwa itatoka lini. Naomba nitoe ufanuzi ufuatao; Serikali kwa kutambua umuhimu wa suala hili, imeunda Kamati Maalum inayofanya utafiti ili kutoa mwongozo wa vigezo vyta maeneo yenye mazingira magumu ili watumishi wa umma wanaofanya kazi katika maeneo hayo, waweze kupewa posho za mazingira magumu. Kamati hiyo inaongozwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Posho ya mazingira magumu ilitakiwa kulipwa kwa walimu wapya wanaopangwa katika shule zilizo katika mazingira magumu Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Kila mwalimu alitakiwa kulipwa shilingi 500,000 kama posho ya kujikimu anapowasili katika maeneo yale tunayoyaita ya mazingira magumu, ambapo jumla ya shilingi 1,500,000,000 zilikuwa zimetengwa. Posho ya mazingira magumu ikashindikana kutolewa, ni fedha ya mhisani imetolewa kwa ajili ya mwaka mmoja kwa ajili ya wale tu ambao wanarioti. Serikali ilipokuwa inajiaandaa kulipa, walikuwa katika maeneo yale wanaauliza wanalipwa hawa wanaokuja tu au na sisi tuliotangulia ambao tupo hapa katika mazingira magumu, tukawaambia hapana ni hao tu wanaokuja. Nina uhakika hata maofisa waliokuwa wanahuksika, kabla ya kujibu wenyewe wakaingia kigugumizi tayari. Pale yupo Daktari na pia kuna Mwuguzi na kuna Mkunga katika kijiji hicho hicho. Halafu bahati mbaya ni uhisani ambao tulikuwa tumeupata hauna uendelevu ni mwaka huo mwaka uliofuatia hakuna tengeo hilo.

Serikali ikaona hili jambo zuri kama lilivyo lakini halitoweza kukidhi mahitaji ya walimu kama ambavyo

tungependa liwe. Labda unaweza ukasema danganya toto na hatuko hapa kuwadanganya walimu, tuko hapa kuhakikisha kwamba, kama tunafanya nao kazi vizuri ili waweze kufanikisha lile ambalo tunalitaka kwa nchi yetu, elimu bora kwa ajili ya nchi yetu. Tumesita tukashindwa kufanya hiyvo.

Kutokana na makubaliano baina ya Wizara yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Benki ya Dunia ambayo ndio waliotoa fedha hii ya ruzuku, tukakubaliana kwamba sasa basi fedha hiyo bora ifanye kazi ya kununulia vifaa na vitu vingine kwa ajili ya nyumba za shule zilizopo katika mazingira hayo magumu. Nyumba ambazo hazipo katika hali nzuri zikamilishwe, zisizokuwa na umeme ziwekwe umeme, kama hakuna *electricity solar* ifungwe na kadhalika ili kupunguza mazito ambayo yanawakabili wale ambao watakwenda kule na wale ambao tayari wako katika maeneo hayo. Kwa sasa zoezi la kukusanya takwimu za walimu wapya walioripoti katika shule hizo kwa mwaka 2012/2013 linafanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niyagusie yale ambayo Kamati yangu ya Huduma za Jamii imeyataja na baadhi yake, kwa sababu nikisema niyajibu yote, bila shaka maeneo mengine sitayagusa.

Naomba sasa nihamie katika hoja ya Kambi ya Upinzani kama zilivyowasilishwa. Kambi ya Upinzani ilihoji kwamba, kuwe na utaratibu wa kuvipatia ruzuku maalum ya Serikali Vyuo Vikuu Binafsi ambavyo jumla yake ni 36 ili kuvipunguzia makali ya gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi ufuatao kwamba, Serikali inaelewa idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki Binafsi jumla yake vikiwa 36, kati ya vyuo vyote tulivyokuwa navyo na Vyuo Vikuu Vishiriki. Mpaka sasa Vyuo Vikuu hivi na Vyuo Vikuu Vishiriki vinanufaika na fedha za Serikali kwa kupata ruzuku na mikopo ya masharti nafuu kuititia Mamlaka ya Elimu Tanzania yenye riba ndogo kabisa.

Tunavi-support vyuo hivi, tunavipa fedha za ruzuku na tunavipa mikopo ya riba ndogo. Nikisema riba ndogo ni riba ambayo inatozwa kwa wale ambao wamechukua mikopo, Vyuo Vikuu Binafsi vimechukua mikopo riba yake asilimia mbili na waliokuwa juu sana ni asilimia sita, ukilinganisha na riba zile ambazo ziko kwenye Mabenki kati ya asilimia 15 mpaka 30; huu ni uwezeshaji mkubwa sana wa sekta binafsi, Mashirika ya Dini ambayo yanaendesha Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Vyuo Vikuu ambavyo vimenufaika ni pamoja na *Hubert Kariuki Memorial University, Tumaini University*- Iringa, *Saint Augustine University* - Tabora, *Saint Augustine University*- Mwanza, *Theophil Kisanji Mbeya*. Nilikwenda Mbeya pale nikazindua Maabara kubwa kabisa ambayo vyuo vingi haina hapa Tanzania.

Watu wa Chuo Kikuu cha Theophil Kisanji ni makini sana, wanasema cha muhimu ni Maktaba, Maktaba ile ina ghorofa kama nakumbuka ni tatu; ni jengo moja kubwa sana, limekaa vizuri na wameanza ku-restock vizuri sana, ni mkopo kutoka TEA wa riba nafuu. Tunawawezesha vyuo hivi binafsi na wala siyo kwamba hatuwawezeshi. *Saint John's* - Dodoma, Bugando na kadhalika. Kwa hiyo, nia tunayo lakini inaendana na uwezo pia. Hata hivyo, Vyuo Vikuu vya Umma 14 ndivyo vinavyodahili wanafunzi wengi, ikilinganishwa na Vyuo Binafsi na hawana njia nyingine. Kwa hiyo, kwa mfano, katika wanafunzi 166,000 waliopo vyuoni, wanafunzi 112,000 wanasoma katika Vyuo Vikuu vya Umma. Kwa hiyo, lazima tuweke umuhimu sana katika Vyuo Vikuu vya Umma, ndivyo vinavyosomesha wanafunzi wengi zaidi kuliko vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine; je, inawezakanaje Vyuo vya Elimu vya Juu kutoza ada kubwa kuliko kiwango kinachotolewa na Bodi ya Mikopo? Serikali inatambua kuwepo kwa vyuo vinavyotoza ada kubwa kuliko kiwango cha mkopo kinachotolewa kwa wanafunzi. Ili kuondoa changamoto hii, Serikali imefanya yafuatayo:-

Moja, imekamilisha mchakato wa zoezi la kuandaada ada elekezi na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya

Ufundi na Kamisheni ya Vyuo Vikuu. Mbili, Tume imeshakamilisha mwongozo wa utekelezaji kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Vikao vya Kamisheni na baada ya kuitishwa na Kamisheni ndiyo tutaweza kutangaza jambo hilo.

Hoja nyingine ni kuendelea kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa miaka saba mfululizo wa elimu ya sekondari. Niseme ifuatavyo: Lengo la Serikali katika utoaji wa elimu kama ilivyo kwa nchi yoyote ni kuhakikisha kuwa, Wananchi wake wote wanapata fursa ya elimu yenye ubora. Utekelezaji wa kutoa elimu kwa Wananchi unaweza kufanyika kwa kutumia mojawapo ya taratibu au *scenario* kuu mbili. Moja, kuanza na ubora kwa kuongeza fursa taratibu (*Qualitative Approach*), yaani unaongeza kidogo kidogo, *hu-load system* sana, waliopata bahati ya kuwa katika kupata elimu ndiyo hao hao waendelee. Walikuwa wachache basi waendelee hivyo hivyo, wanafunzi wale waliokuwa 524,000 mwaka 2005 ndiyo wabaki hivyo na ndiyo hao ambao waendelee tena na baada ya hapo kama tusingefanya upanuzi huu, basi ingekuwa hamna tatizo. CCM ingekuwa iko juu ingepigwa makofi kwa sababu elimu isingekuwa na kikwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, *approach* nyingine ni kuanza kuongeza fursa nyingi kama walivyofanya South Korea, India na nchi zingine chungu nzima na wakatanguliza kwanza fursa, halafu baadaye wakafuata ubora. Kwa hiyo, hii ndiyo tulichagua na tunakiri kwamba, imetuingiza kwenye kazi hii, lakini tuna hakika kwamba, kwa sababu sasa tumeacha ujenzi tupo kwenye ubora, kule tunakotaka kufika tutafika. MMES Awamu ya Pili inaangalia tu ubora, yote yale ambayo tunayafanya, fedha zote ambazo tumeweka katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili ni kwa ajili ya ubora siyo kitu kingine chochote. Kwa hiyo, Mpango huu bila shaka utatutoa ili tuweze kuirudisha hadhi ya elimu yetu.

Serikali inatambua changamoto hizi na katika hatua tunazozifanya sasa hivi ni kuandaa na kuajiri walimu kila mwaka. Kwa mfano, kumekuwa na ongezeko la walimu

kutoka 23,905 mwaka 2005 hadi walimu 65,086 mwaka jana 2012. Kazi siyo ndogo, kutoka 23,905 mpaka 65,086 katika kipindi hiki cha 2005 mpaka sasa ni kwamba, ndiyo tunaenda huko kwenye ubora. Aidha, mwaka 2012/2013 Serikali iliajiri walimu wa shule za sekondari jumla yao kwa mwaka huu peke yake ni 14,060 na kwa shule za msingi ni walimu 13,633. Kutoa ruzuku ya uendeshaji kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vitabu kwa mwanafunzi kutoka shilingi 20,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka kipindi cha MMES I mpaka kufikia shilingi 25,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka katika MMES II.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na USAID imesambaza jumla ya vitabu 1,985,530 vya sayansi na hisabati. Tunaongeza miundombinu katika shule, kununua samani na tunakarabati jumla ya shule 1,200 na tunesema ikifika mwakani katika hizi shule zetu tulizozijenga za Kata, karibia shule 3,000 tumezijenga katika miaka mitano, shule 1,200 tunataka tuzikamilishe kamili kabisa, ziwe na maabara na maktaba, ziwe na madarasa kamili na vitendeakazi na orodha tumeitaja. Waheshimiwa mmeihoji, mmeahidi kuifumua kabisa, tunaenda katika mchakato mpya ili tuhakikishe kwamba tunafanikiwa.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, tumetoa lile jedwali katika kitabu, tunalifumua halitotumika tena, tunakwenda katika mtindo ambao utakuwa na manufaa kwa wote. Tutatoa mafunzo kwa watendaji 396, lakini tutahakikisha walimu nao tutawapa mafunzo mazuri. Tumeingia kwenye mpango wa matokeo makubwa sasa wa *Big Result Now* na tumejielekeza specifically katika kuendeleza kutoa mafunzo kazini ili kuwajengea walimu uwezo wa ufundishaji na tathmini ya ufundishaji.

Kwanza, tutajikita kuimarisha mbinu za ufuatiliaji na tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kutoa mitihani ya upimaji, kufanya tathmini kubaini mada ngumu na kuweka mkakati wa kuzifundisha na kutoa mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wasiojimudu kwa muda husika kabla hawajafikia kipindi cha mitihani.

Pili, tumejipanga kuzipanga shule kwa makundi ya ubora wa ufaulu kwa kutangaza kwenye vyombo vyahabari ili kuleta ushindani kuanzia mtihani wa mwaka 2012, tutayatangaza tangu shule ya kwanza mpaka shule ya mwisho. Kule kwetu Bagamoyo wataaulizana mbona wewe umekuwa wa kumi na mbona wewe umekuwa wa mia moja na Wilaya yetu ndiyo hii hii moja, mazingira ndiyo yale yale, itakuwaje shule yako ishike mkia. Wazazi wataauliza na wadau wengine wataauliza. Tunataka uwajibikaji ili na Wananchi wote washiriki.

Tatu, katika *Big Results Now* tumejipanga kuhakikisha kwamba tunawazawadia shule zote zitakazofanya vizuri zaidi na kuongeza ufaulu ikilinganishwa na mwaka uliopita. Ukiiongeza ufaulu mwaka unaokuja, tutawazawadia shule hizo kifedha kwa mamilioni ya shilingi, shule inayopanda daraja tunalzawadia. Tumejipanga kuimarisha uongozi wa shule kwa kuandaa mwongozo wa usimamizi wa shule ama *School Tool Kit* kwa Lugha ya Kiingereza. Tumegundua kwamba, Wakuu wengine wa shule hawajui mbinu gani ambazo wanaweza wakazitumia kuiendesha shule. Tumeandaa tayari mwongozo huu, tumeufanya uhakiki na tumetumia wataalamu wazuri na tayari tunataka kusambaza miongozo hiyo na kuwafundisha Wakuu wa Shule hizi namna ya kuendesha shule zao. Viongozi wa Elimu, siyo tu Wakuu wa Shule ni na Viongozi wa Elimu tunataka.

Nne, tunajiandaa kuboresha miundombinu ya shule zilizopo katika mazingira magumu kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari. Haya tumesainiana mimi na Mheshimiwa Sana, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na nimesema nachukua *personal responsibility* ya kuhakikisha kwamba, haya yatafanikiwa. Nimesema, nachukua dhima binafsi ya jambo hili kufanikiwa na Mkuu wa nchi hii na Watanzania watanihukumu kwa ahadi hiyo na hili hakuna mbadala. Waziri Kivuli atabaki kwenye kivuli na Waziri wa Elimu ataendelea kuongoza elimu katika nchi hii. (*Kicheko/Makof*)

5 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, sidhani kama nitaweza kuzimaliza hizo hoja nyingine, kwa sababu sasa nataka kuingia katika hoja moja moja za Waheshimiwa Wabunge, nitajibu zile ambazo nitawahi kuzisema na kama sitowahi, kama nilivyoahidi zote zitakuwa katika majibu ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, alihoji Bodi inasimamia Baraza la Mitihani ivunjwe. Kamati ya Kutunuku wajiuZulu kwa sababu wameshindwa kutekeleza wajibu wao. Niseme hivi; Baraza la Mitihani linaongozwa na viongozi wasomi, makini, waadilifu, wanatekeleza majukumu yao, wanafanya kazi, maamuzi huzingatia sheria na kanuni za uendeshaji wa mitihani. Kamati ya Kutunuku hupitia taarifa mbalimbali za ufanyakaji wa mitihani pamoja na matokeo ya mitihani na kupendekeza kwa Kamati ya Mitihani ya Shule, hoja zinazohitaji kutolewa maamuzi kama vile matatizo waliyoyapata watahiniwa wakati wa mtihani. Kamati ya Mitihani ya Shule, hupokea na kujadili mapendekezo ya Kamati ya Kutunuku na kisha kuwasilisha mapendekezo yake kwenye Baraza kwa ajili ya kuidhinisha na kutangaza matokeo, ndiyo taratibu za kisheria.

Baraza mwisho, inaanza huku chini mpaka Baraza; Baraza likiidhinisha basi hayo matokeo hakuna mtu mwingine atakaye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri muda umefika.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

5 JUNI, 2013

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management* Sh. 23,520,525,000

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri hawapo, haya ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa James Mbatia.

Nitamwita Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kwanza.

MWENYEKITI: Someni kanuni ya 101 kifungu kidogo cha 4.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilitaka kufahamu namna gani Serikali itaunda chombo cha kusimamia viwango vya taaluma katika maadili, utendaji wa haki za walimu, yaani *Teachers' Professional Board* na katika majibu ya Waziri sijasikia jambo lolote katika hili. Je, Serikali inasema nini? Naomba ufanuzi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Mawaziri, naomba mnukuu vizuri mpate muda wa kujibu pamoja. Mheshimiwa Zarina Madabida!

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza *crisis* ambayo inaweza ikatokea kwa ajili ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu na hususan Vyuo Vikuu vya

Tiba, kwa sababu daktari mpaka asome kufikia Mhadhiri wa kuweza kusimamia na kufundisha inamchukua takribani si chini ya miaka 20 na zaidi ndiyo anafikia katika *level* ya Uhadhiri, ambayo anaweza kukabidhiwa wanafunzi kuweza kuwfundisha ili na wao ndiyo waje kuwa Madaktari.

Hivi sasa *by the time* yule anamaliza anakuwa karibu ana miaka 50 au 55, lakini miaka 60 anatakiwa awe amestaafu na sasa hivi Serikali imesitisha kuwapa mikataba kama ambavyo ilikuwa inafanya mwanzo kwamba, wakifika miaka 60 wanapata mikataba waendelee kufanya kazi. Matokeo yake, kuna *crisis* kubwa sana na mimi ni-*declare* kwamba ni *Chancellor* wa MUHAS, ambacho ndiyo chuo kikubwa na ni tanuli la kuzalisha wahadhiri ambao ndiyo wanatumika katika vyuo vingine pamoja na kile chuo chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri hakunijibu kwamba, hawa wahadhiri wakiondoka pale Muhimbili kama mwaka huu hawajawapa zile *contracts*, panaweza paka-*collapse* wakakosekana wahadhiri. Kama ndiyo chuo kinachotegemewa kutoa wahadhiri ambao watafundisha na vyuo hivi vya *Private* na Vyuo vya Serikali; kuna mpango gani na kwa nini wasichukuliwe hawa madkatari, hawa wahadhiri kama ni *rare profession* ili wawaongezee *contract* waweze kufundisha na tuweze kupata wakufunzi wa kufundisha vyuo vingine?

Kama mwaka huu hatutachukua hatua, Chuo cha Muhimbili kina-*collapse* na nina hakika na vyuo vingine vita-*collapse*, kwa sababu wote wanategemea wahadhiri kutoka Muhimbili. Anafundisha asubuhi Muhimbili, saa kumi na mbili jioni yuko Mwanza, saa ngapi yuko St. John's na UDOM Dodoma, wanawasubiri hao hao. Sikupata majibu, lakini hili suala nafikiri Wizara ingelichukulia kwa u-*seriousness* wake tusije tukapata hasara halafu tutakuja kukaa humu ndani tuseme madaktari wetu hawafai.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kumetokea matatizo makubwa sana ya matokeo

ya Kidato cha Nne ya mwaka 2012 na nilitegemea Mheshimiwa Waziri walau angeeleza kidogo nini tatizo hilo na nini kitafanyika, lakini hakugusia kabisa. Hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo hakuwa *serious* na hili tatizo hasa ukizingatia kwamba, kuna baadhi ya watoto walipoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kutosha nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema na naendelea kusema, kumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana na taarifa za Serikali hii hii moja zinatofautiana. Ukiangalia Ripoti ambayo tulisomewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Lukuvi, alieleza sababu za matokeo hayo kubadilishwa na akatoa sababu kwamba, baada ya Baraza la Mawaziri kukaa wallkubaliana kwamba, matokeo hayo yafutwe kwa sababu Baraza la Mitihani lilitumia mfumo mpya. Kikubwa zaidi, Baraza hilo hilo la Mitihani halikuwashirikisha wadau na wadau hao ni pamoja na wazazi, wanafunzi wenyewe na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo ukiangalia katika Kitabu cha Kamati ya Huduma za Jamii, nao wameona kwamba, haikuwa busara kutangaza matokeo hayo yanayotokana na utaratibu mpya wa alama bila ushirkishwaji, yaani *flexible*. Juzi wakati Mheshimiwa Waziri anatangaza matokeo, bado alisisitiza kwamba, matokeo ya mara ya pili, baada ya haya ambayo tunasema *politically standardized* kwamba, kile ambacho kilizungumzwa hapa Bungeni na ambacho tulikiами, kimekuwa kinyume na Waziri anasema kwamba, wameendelea kuchakata matokeo haya mapya kwa utaratibu huu mpya ambao ni *fixed* wakati tuliamiwa kwamba wanaenda kubadilisha watumie *flexible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kupata ufanuzi ni kwa nini wameendelea kutumia utaratibu mpya ambao ni kinyume na yale ambayo tuliamiwa na Mheshimiwa Lukuvi hapa Bungeni?

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Maendeleo ya taifa letu yatategemea sana namna ambavyo Serikali yetu inavyoangalia Sekta nzima ya Elimu. Sasa hivi mkazo uko katika elimu ya msingi na sekondari, lakini hawa wahitimu wa sekondari tunatarajia waingie Vyuo Vikuu. Wakati huo huo Serikali kwa muda mrefu sasa bajeti yake ya kuhakikisha kwamba, Vyuo Vikuu vinapanuliwa, vinajenga uwezo kwa wahadhiri, vinakuwa na maabara na tafiti mbalimbali ambazo zitatupatia takwimu muhimu kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya nchi yetu na uchumi wetu na jamii kwa ujumla.

Nini tamko la Serikali kuhusu sera yake ya kuhakikisha kwamba, Vyuo Vikuu vya Umma nchini vinapatiwa bajeti ya kutosha ili viweze kujipanua vizuri kuendeleza wahadhari na kusaldla tafiti mbalimbali ambazo ni muhimu kwa taifa letu? Ahsante sana.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kupata elimu bora, lazima tuwe na walimu bora, pamoja na watoto wawe bora na mazingira mahali ambapo wanosomea pia pawe bora. Nataka kujikita zaidi kwa namna tunavyowaheshimu walimu, walimu wengi sasa wamepitia Vyuo Vikuu na wanakuja katika shule zetu, lakini walimu hawa tunawaita walimu tu. Kuna haja sasa turudi kama tulivyokuwa tunafanya kazi wakati wa Tanganyika, ambapo watu walikuwa wanapata *grade*; *Education Officer I*, *Education Officer II*, kama wanavyofanya kwa madaktari na watu kama hao. Pia hao vijana wanaokuja sasa kwenye *secondary schools* zetu wapewe madaraka. Kama mtu ana uzofu amekuwa *Head Master*, akishapa *Graduate Education Officer I*, basi mumkabidhi hayo madaraka ili pasiwe tena watu wanaogombania kwamba *after all* wewe hujafika mbali lakini mimi nimeendelea juu zaidi. Naona jambo hili halijagusiwa na ni vizuri mkaliangalia.

Vilevile fedha ulizonazo Mheshimiwa Waziri kusema kweli ni kidogo, kwa hiyo, kama una fedha kidogo uangalizi wake ni muhimu zaidi. Sasa hivi tunapeleka fedha kwa

secondary school mbalimbali, hawa *Head Masters* tutawamalizaje hela? Ni afadhili turudi kwenye utaratibu wetu ule ule wa zamani ambapo *secondary schools* zinakuwa na *Bursar*. Mtu ambaye anajua mahesabu, mtu ambaye anaweza kuweka vitabu sawasawa. Tukiachia tu kwamba, tunapeleka pesa mwaka hadi mwaka na walimu hawa hawajawa na mafunzo ya kihesabu tutawafunga bure na wengi wanafungwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hili jambo la wakala nilitaka Waziri ungesisitiza kwamba, tupate wakala wa wakaguzi wa shule hizi ambao wana bajeti yao na wako huru kuweza kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu ili twende kule nyuma. Zamani wakati wa Tanganyika tulikuwa tunaona mama mmoja alikuwa anajulikana nchi nzima, alikuwa anaitwa Mrs. Hancock na alikuwa anavaa kaptura mpaka hapa. Mzungu akishafika kwenye shule hata kama ulikuwa umelala unaamka na unatengeneza mambo yako yawe sawa. Turudi huko kwenye Tanganyika ndiko tulikoanza kuwa na elimu bora. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza namna ambavyo baadhi ya shule zetu za kata zinaendeshwa bila kuwa na Bodi ya Shule. Hii ni kutockana na sifa zilizoanishwa kwa mujibu wa Sheria, watu wale hawapatikani kulingana na mazingira ya sekondari tulizonazo. Kwa hiyo, nikalomba Serikali ijaribu kufanya marekebisho ya Sheria kulingana na mazingira ya sekondari zetu za kata ziliko. Vilevile nikaitaka Serikali iwatumie Maafisa Elimu wa Sekondari wa Wilaya ndio watumike katika kutoa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Sekondari kwa sababu wao wanayafahamu mazingira.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Serikali imekubali kuvunja *EMAC*, nawapongeza kwa hilo na wamepiga hatua; na kwa kuwa tunayo Sera mpya ya Elimu iko kwenye mchakato, tukitoka kwenye Sera tutaenda kwenye Mitaala, baada ya mitaala miutasari, baadaye vitabu ambavyo vitaendana na sera husika; na kwa kuwa sasa hivi viro vitabu takribani milioni 18

na mihtasari ambazo zitatumia zaidi ya bilioni 55.2, ile chenji ya *radar* na vitabu hivyo viliidhinishwa na *EMAC* ambavyo havina ubora na havijafika kwenye shule na bidhaa yoyote ambayo haina ubora inabidi iondolewe kwenye soko:-

Serikali haioni kwamba ni busara kwanza kuunda jopo la wahariri wa vitabu kwa kuwa vitabu vingi unakuta mwandishi ni huyo huyo, mhariri ni huyo huyo, mhakiki ni huyo huyo, mchapaji ni huyo huyo na ni Mjumbe wa *EMAC*, anapitisha kitabu chake anakiingiza kwenye soko na ndiyo maana ufisadi umekuwa mkubwa sana na unaharibu elimu yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na walimu kukosa hali halisi kwenye vitabu vyatia na ziada. Je, Serikali haioni kwamba ili kuwa na ubora wa elimu; nakumbuka nikiwa mdogo mwaka 1972/1973 wakati wa Azimio la Musoma, wale wanafunzi waliokwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakafeli walivyotoka JKT, japo wakati huo chama kimoja kilikuwa kimeshika hatamu, Halmashauri Kuu ya Taifa ya TANU wakati huo ikaagiza mitihani isahihishwe upya, lakini wahadhiri walikataa wakasema wasichanganye taaluma na siasa.

Sasa kwa kuwa maamuzi hayo yalifanya elimu wakati wa Mwalimu Nyerere ikawa bora, japo chama kilichokuwa kimeshika hatamu lakini wahadhiri wakasema hapana; haya mambo ya kuchanganya siasa na taaluma ambayo yametufikisha hapo ili tuondoke huko na hatua imeshapigwa nzuri na naipongeza Serikali, basi hizi bidhaa ambazo siyo nzuri kwa utumiaji kwenye soko, hivi vitabu, waweze kuunda jopo la wataalam wavihariri kila kimoja ili vile ambavyo havifai na vinaua elimu yetu viondolewe kwenye soko tuweze kupata elimu bora ya kizazi hiki?

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu, nilizungumzia sana suala la kuangalia mfumo wa kuhudumia walimu uliopo sasa, unaosababisha walimu kukosa haki zao kwa wakati, ikiwa ni pamoja na *arreas za mishahara*,

kutokupanda madaraja kwa wakati na kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kurudisha chombo kimoja ambacho kilikuwa kinajulikana kama Tume ya Huduma kwa Walimu, ambapo chombo hicho kilikuwa kinashughulikia usajili, upandaji wa madaraja, hatua za kinidhamu, vyote vilikuwa vinashughulikiwa na chombo kimoja na kilikwenda vizuri mpaka pale ambapo Serikali ilivunja na kuunda Idara ndogo ya Utumishi kwa Umma ambayo imeshindwa kufanya kazi.

Suala hili limezungumzwa kwa hisia kali na Wabunge wengi, lakini pia ndani ya Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii tumezungumzia sana. Je, Serikali inasema nini kuhusu jambo hili? Nilitegemea lingekuwa la kwanza kwa Waziri aliposimama pale ili kuwapa walimu matumaini ya kwamba, Serikali yao cha Chama cha Mapinduzi inawajali na inawafikiria. Mheshimiwa Waziri anasema nini?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia, nilipinga vikali utungwaji wa mitihani kwa njia ya kuchagua kwa maana ya *multiple choice* hasa kwa somo la hesabu. Nilijaribu kuainisha athari moja tu kwamba, mwaka jana ilitungwa mtihani wa *mock* wa Darasa la Saba Mkoani Mara ambapo maswali kumi yalikuwa yamekosewa kwa maana hakuna jibu sahihi kuanzia (a) mpaka (d). Ukiangalia hapo ni kwamba, wale wanafunzi kwanza walipoteza muda mrefu kufanya swali ambalo halina jibu na wakashindwa kuandika ni jibu lipi sahihi.

Pia nikawa najiuliza hawa wanafunzi walipewa maksigani? Mimi ni mwalimu wa hesabu, kwa kawaida hesabu hausahihishi jibu la mwisho; unakuta kuna *formula*, unakuta kuna ukokotoaji, njia ina maksigani zake na jibu la mwisho lina maksigani zake.

Wakati Mheshimiwa Waziri, anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, alisema kwamba, wanafanya *multiple choice* kwanza ni kuweza kuweka maswali mengi ili wanafunzi wafanye maswali mengi wapimwe kwa wigo mkubwa. Nikawa najiuliza, swali la hesabu ili uweze kupata jibu lazima ukokotoe, unavyokokotoa kama ni maswali mia

yatatumia muda uleule sambamba na ambapo mwanafunzi angefanya na kuainisha maswali yote kwenye karatasi halisi. Tunaua elimu yetu, ukiangalia matokeo ya *form four* ya sasa hivi, zaidi ya asilimia 59 wamepata (f) kwenye somo la hesabu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, naona kama una-debate. Najaribu kufuatilia hoja yako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kujenga hoja yangu. Ninaamini Mheshimiwa Waziri atakuwa amenielewa. Naomba Wizara kupitia kwa Wataalam wake, pamoja na kwamba kuna mfumo wa kusahihisha *multiple choice* tu, wafanye *exceptional* kwa somo la hesabu liweze kufanywa kwa njia siyo mambo ya *multiple choice*.

Wanafunzi wapewe swalí wakokotoe kwa kuonesha njia zote na jibu mwisho. Vinginevyo, tutaua somo la hesabu na elimu nchini na kila siku tuna-*advocate* kwamba, tunataka masomo ya sayansi. Naomba Mheshimiwa Waziri akubaliane nami kwamba, sasa waondoe somo la hesabu lisiwe la *multiple choice*. Kama hawatakubaliana na hilo kwa kweli nitatoa shilingi.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, naomba sasa muanze kujibu, mtakuwa mnawataja wanaohusika.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Mheshimiwa Masoud kuhusu *Teachers' Professional Board* aliyokuwa anasema kwamba, hajasikia kwenye majumuisho ya Mheshimiwa Waziri. Ni kweli kama tulivyosema kwamba, mambo yalikuwa mengi na hivyo tutaandika kitabu kwa ajili ya kuleta majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini hili lingepatikana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, Rasimu ya Waraka wa kuanzisha Bodi imeshawasilishwa kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi ili

iletwe hapa Bungeni kwa ajili ya kuundiwa Sheria. Kwa hiyo, suala hilo tunalichukua lipo kwenye *process*.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Madabiba, alilolisema ni kweli, ni hali ambayo inaashiria kutuathiri katika Vyuo vya Umma kwa kiasi kikubwa, kwa sababu moja, kama alivyosema kwamba, inachukua muda mrefu mpaka pale mtu anapopata daraja la *Associate Professor* ama *Professor*. Kwa hiyo, *by the time* anafikia hapo na muda wake pia wa kustaaifu unakuwa umefika miaka 60. Anakuwa na miaka 55, kwa hiyo anatumikia kipindi kifupi na akiwa amefikia umahili wa juu.

Malalamiko haya tumeyapokea, kwanza, yalifanyiwa kazi kwa kutoa mikataba ya miaka miwili miwili. Hili nalo lina matatizo yake, kwa sababu huo mchakato mpaka upate mkataba, Profesa anakuwa ameshatoka au katafuta mahali pengine na tunawapoteza namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limekuwa tatizo hasa kwa sababu kuna kipindi ambacho tulisitisha ajira katika Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, kuna *gap* ya miaka kadhaa ambayo ilipita bila ya kuwa na walimu wapya katika vyuo. Kwa hiyo, sasa tuna Maprofesa na *Associate Professors* wengi halafu wanaofuatia chini ni *Assistant Lecturers* au *Lecturers*. Kwa hiyo hapa katikati *Senior Lecturers* ni wachache. Akiondoka yule Profesa maana kuna Idara zingine zinabaki hazina mtu mahili wa kuweza kuendesha Idara hiyo kwa kiwango hicho cha umahili.

Kwa hiyo, tumelipokea na tunaliangalia kwa ukamilifu wake na hata ajira yenyewe ya ualimu kuondoshwa kutoka kwenye mamlaka ya *Council* ya Chuo kwenda kwenye Tume ya Ajira nalo pia tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajitahidi kufanya mchakato huu mapema sana ili Serikali ifanye maamuzi mapema, tusije tukajikuta kwamba Vyuo hivi sasa ambavyo vinategemewa sana na Watanzania vinadidimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidi Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mchakato umeshaanza na tupo katika *advanced stage*, tutawasilisha mapendekezo kwenye *cabinetna cabinet* ikishardhia basi tutatangaza kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali lake naomba nilifafanue namna hii kuhusu matokeo ya Kidato cha Nne: Matokeo haya ya Kidato cha Nne sisi hayakuturidhisha hata kidogo na Watanzania wote hayakuwardhisha. Mimi kama Waziri na wala usingizi sikuweza kuupata kwa sababu *was a big shock!*

Mheshimiwa Suzan amehoji labda nisiende katika kuhadithia *shock* yenyewe na kadhalika, nije kwenye hoja yake kwamba kauli zilikuwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, mimi nikisema, sisemi kama mimi, nasema kwa niaba ya Serikali na kauli iliyotolewa Bungeni ingawa ametaja jina la Mheshimiwa Lukuvi, lakini siyo kauli ya Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Lukuvi ametoa kauli ya Serikali. Serikali wakati ule iliamua vile na baadaye ikaamua vingine, kufuatana na manufaa ya Watanzania na Serikali hii haifanyi kitu tofauti na manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *flexible grade range* inamaanisha kwamba, katika somo moja alama zako za D zinaweza zikawa 35 mpaka 49; kwa mfano, Kiswahili vilevile, *English* D ikawa 40 mpaka hamsini na kitu, *French* ikawa 40 mpaka 59, *Arabic* ikawa nytingine. Hayo masomo yote ya ni lugha huwezi ukayapa kila somo *grade* hiyo hiyo ya D, kila somo alama zake zipo tofauti. Kwanza, *French* ni ngumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ilifanya maamuzi ikaingia kwa kina kwani kinachotokea ni nini, ikatathmini ikaona haina tija, ikasema kuna kitu kilikosekana katika mfumo mpya ambao kama D kwenye Kiswahili ni 30 mpaka 49 au shulen i kule mnaita 21 mpaka 40, kwenye

Kiswahili na Kiingereza hivyo hivyo, French hivyo hivyo na Arabic hivyo hivyo.

Hiyo haina maneno na mtu na hakuna mtu atakayeinuka hapa aseme kwamba, mmekandamiza Waislam au mmekandamiza waliofanya French au mmekandamiza waliofanya English, maana hili suala wala siyo la dini, ni kwa sababu tu watu fulani wametoa mfano wa Islamic na Bible, lakini wanafunzi hao hao wanaweza wakainuka kwa sababu ya masomo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *system nice clean*, haina matatizo, haina hoja ili mradi uichukue na uikamilishe katika vigezo vyake vyote. Serikali ilipobaini ukweli wa mambo, ikaamua kutoa maelekezo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tutafanya kitu hivyo hivyo kwa sababu kilianza tangu mwaka 1973 basi tufanye hivyo hivyo, tutegeme matokeo tofauti na hayo tutakuwa tunapata kila siku. Lazima tubadilike, lazima tukubali *change*. Tangu mwaka 1973 Baraza lilikuwa linafanya hivyo hivyo, baada ya kugundua hivyo, basi ufanye kila siku hivyo na matokeo yatakuwa yale yale. Ili upate matokeo tofauti ni lazima ufanye kitu cha mabadiliko. Mheshimiwa Susan Lyimo pia alizungumzia.

MWENYEKITI: Taarifa ni moja tu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Mabumba, aliongelea tamko la Serikali kuhusu kuwapa Vyuo Vikuu vya Umma pesa nyngi zaidi. Nia na azma ya Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha kwamba, tunatoa pesa nyngi zaidi kwa Vyuo vyetu Vikuu, kuviwezesha kusomesha na kuviwezesha kufanya utafiti. Hivi ni Vyuo siyo *glorified secondary school*, hivi vyuo lazima vifundishe, ni lazima vifanye utafiti, ni lazima vitoe huduma ya kitaalam kwa jamii na kwa maana hiyo ni lazima wapate rasilimali fedha na vitendeakazi. Ndiyo sababu tukaandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MEJU) wa mwaka 2010 mpaka

5 JUNI, 2013

2015 na kutenga pesa ili Vyuo hivi viweze kuhakikisha kwamba, vinafanya kazi vizuri.

Tumepata mtikisiko wa kifedha, lakini tunashukuru kwamba wahisani nao wanatu-*support*. Mradi wa *STHEP* wenye dola bilioni mia, bilioni nyingi za shilingi umefanya kazi kubwa katika Vyuo vyetu vikubwa na wahadhiri wanafurahi sana, wameshukuru wanajua kwamba Serikali yao inahangaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niahidi tu kwamba, tutaendelea kwa nguvu zetu zote kuhakikisha kwamba, MEJU inafanya kazi, miaka hii mitano 2010 - 2015 tuone tofauti katika Vyuo vyetu Vikuu katika nchi yetu ya Tanzania na Vyuo hivi viingie katika *chart*.

MWENYEKITI: Maswali mengine bado.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbatia, alikuwa anazungumzia masuala ya *EMAC*. Kwa bahati mbaya wakati nahitimisha hoja yangu pale dakika 25 alikuwa alichelewa kidogo.

Nataka kumjulisha kwamba, tumeridhia kuvunja *EMAC* na tuliona kulikuwa kuna kasoro kidogo kwenye vitabu na baadhi ya vitabu ulishawahi kutuonesha na sisi tuliunda kikosi kazi cha kuchunguza vitabu vyote ambavyo vilikuwa vimepewa ithibati. Tulisema vitabu hivyo hata kama vina makosa kidogo, havimfanyi mwalimu wa hisabati ashindwe kabisa kufundisha hesabu kwenye shule za sekondari ama msingi kama kweli ni mtaalam wa hesabu. Yapo makosa mengine ya kiutaalam ambayo tumeyagundua, kwa hiyo tumeivunja *EMAC* na tutaunda kitengo kizuri sana ambacho kitashughulikia ipasavyo ithibati na vifaa vya elimu kama ilivyo *TBS*. Kitapita huko kuangalia vitabu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama nilivyosema kwamba, tutafanya mapitio ya vitabu vyote vyenye ithibati ili kubaini vyenye makosa, kwa hiyo, vitakavyokuwa

vimebainika navyo vitaondolewa kadiri itakavyokuwa inaonekana.

Mheshimiwa Esther Matiko, alikuwa anajaribu kuelezea umuhimu wa kuliangalia upya suala la *multiple choice* kwenye somo la hesabu. Tulianza mfumo huu wa *OMR* kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika kuhitimisha hoja, lakini tumeufanya majaribio kwa darasa la saba mwaka jana (2012) na umeleta mafanikio mazuri.

Mheshimiwa Matiko wewe ni Mhadhiri na ni mtaalam wa masuala ya elimu, hebu tushirikiane kwa pamoja tuliangalie kwa mapana zaidi na ningependa hata wakati wa Bunge hili tuweze kueleweshana juu ya jambo hili. Siyo kwamba tunakataa kwamba lina changamoto yake, lakini vilevile limeweza kupunguza gharama, limeweza kutoa walimu wachache sana kwenda kusimamia pale na ku-*mark*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linafanywa na nchi nyininge zote, tulibaki sisi Tanzania tu. Mama Ndlichako, alienda kupata semina hizi, walikaa pale Ghana wakaona nchi nydingi sana wapo kwenye mfumo huu na sisi tukafuata, kwa sababu tuliona una manufaa. Kama kwa nchi yetu ya Tanzania bado una *challenge* nydingi, tutaliangalia kwa pamoja upya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Majaliwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maeneo matatu, nikianza na ille suala la Mheshimiwa Cheyo la madaraka kwa Walimu baada ya kuijiendeleza. Ndiyo utaratibu ambao tunaufanya, lakini Kisera, Shule za Msingi zote wanaofundisha ni Walimu wa Daraja la III A na Shule za Sekondari wanaofundisha ni Walimu wa Diploma na Digris.

Sasa imetokea pia kuwa Walimu wa Shule za Msingi wengi wamesoma mpaka ngazi ya Diploma. Kwa hiyo, katika utoaji madaraka nayo pia tumeiangalia kwamba ni bora

tumpe mtu mwenye taaluma, anayeweza pia kuwasaidia kitaaluma walimu wenzake. Kwa hiyo, tumeanza pia Walimu wa Diploma kuwa Walimu Wakuu katika Shule za Msingi. Hali hii imeendelea pia hata kwa Watendaji wetu wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Sekondari, pamoja na Diploma na Digrii, tumeanza kuangalia pia ni Mwalimu Mkuu yupi kati yao hao wawili mwenye Diploma na Digrii, anao uwezo wa kuongoza timu ya wenzake na kuwasaidia pia kitaaluma. Kule kuna Mwalimu wa Taaluma pia wa shule, naye pia tumeweza kufanya *consideration* ya kuweza kuongoza wenzake kitaaluma.

Kwa hiyo, utoaji madaraka upo kwa utaratibu huo wa taaluma walizonazo na sasa imetokea pia walimu wengi wanajiendeleza mpaka ngazi ya *masters*. Tunaendelea pia kuwaangalia kwenye nafasi mpaka za Maafisa Elimu ili Afisa Elimu anayeweza kuwaongoza Walimu wenyne Digrii moja, Diploma mpaka Walimu wa *Grade A*, lazima sasa awe na *Masters*. Kwa hiyo, tumeendelea ku-*encourage* hiyo na kuwapa madaraka kulingana na taaluma zao. Ndiyo sababu unaona sasa kuna wimbi kubwa la Walimu wanajiendeleza na tunaendelea kuratibu hilo na Walimu sasa wanafahamu utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, lilikuwa la Mheshimiwa Malocha kuhusu uteuzi wa Bodii; ni kweli tunazo Bodii kwenye Shule za Sekondari pamoja na Kamati za Shule kwenye ngazi za Shule za Msingi. Bodii kwenye sekondari kwa sheria ya awali, aliyejewa anaweza kuidhinisha ni Waziri mwenye dhamana, lakini sasa tumerudisha madaraka haya mpaka kwa Mkuu wa Mkoa kwenye ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari husika atatoa mapendekezo ya Wajumbe wa Bodii kutoka kwenye eneo linalozunguka shule hiyo. Tumeendelea kuwasisitiza wasiteue watu wa mbali sana wakashindwa kuhudhuria vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la vikao kwenye maeneo ya Bodii, kwa hiyo, hali hii sasa katika kui-

control, tumemtaka Mkuu wa Shule apendekeze wajumbe kuzunguka eneo la shule husika. Sisi tunaamini kwamba, wale wale ndiyo waliojenga ile Shule ya Kata, wanaweza pia kujadili na kuiletea maendeleo kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, sasa Mkuu wa shule akipendekeza majina yale atampelekea Mkurugenzi wa Halmashauri, naye atafanya mapitio na kuona uhalisia wa hili. Pia mapendekezo yake yanaenda kwa Mkuu wa Mkoa, ye ye atatoa kibali kwamba sasa hii ni Bodii iliyo kamili kwa mujibu wa sheria ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni suala la Mheshimiwa Mama Sitta; jambo hili ye ye kama Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, ameendelea kulizungumza toka alipokuwa kwenye Kamati ya awali na TAMISEMI tulikuwa pale, lakini pia na Ofisi ya Rais (Utumishi), nayo pia imelichukua hilli na sasa Katibu Mkuu TAMISEMI na Katibu Mkuu Utumishi na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, wameunda timu ya kufanya mapitio ya mfumo mzuri wa kuwasaidia Walimu nchini. Kwa sababu *TSD* kama Idara ndani ya Ofisi ya Utumishi wa Umma, *ime-prove* kushindwa kufanya kazi yake vizuri kwa sababu kwanza ni Idara ndogo ndani ya Wizara ya Utumishi; lakini mbili, kwa kuwa tu Idara haijapata *consideration* ya kifedha kuendesha shughuli zao na huku chini tumeendelea *ku-experience* upungufu wa rasilimali watu kwa maana ya Watumishi na ndiyo sababu sasa tumekuwa na matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumetafuta njia nzuri ya kutatua matatizo ya walimu kupitia Idara hii, kwa kuunda Tume kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mama Sitta, kwa *study* ile au vinginevyo. Tutakuja kujumuisha pia, kwa kuwa bado ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na pia ni mionganii mwa watu ambao wametoa pendekezo hili, tutaishirikisha Kamati ile na tutashirikisha Kamati ya TAMISEMI ili kuweza kujenga mfumo sahihi utakaosaidia kuondoa matatizo ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

5 JUNI, 2013

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuridhika kabisa na majibu ya Waziri na kwa maana hiyo, naomba nitoe hoja ya kutoa shilingi ili jambo hili liweze kujadiliwa na Wabunge wenzangu.

MWENYEKITI: Sasa hapo shilingi ni hoja, *it must be specific* ili utushirikishe na sisi wenzio, ikiwa *vague* tutakataa. Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema na ninaendelea kusema kwamba, sikuridhika na majibu ya Waziri kwa sababu moja kubwa; jambo lilitotokea ni kubwa sana, la wanafunzi wetu kufeli kwa kiwango kikubwa sana, lakini kibaya zaidi ni taarifa mbili za mgongano zilizotokea.

Mheshimiwa Waziri hapa amejibu sasa hivi akasema, Serikali ni moja, kama Serikali ni moja, lakini Serikali hiyo hiyo inakuja na majibu tofauti, mimi hapo ndipo ninapopata wasiwasi sana na wenzetu wa upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe alikuwa kwenye Baraza la Mawaziri na nina taarifa hapa ya vikao ambavyo vimefanyika Wizarani na ye ye mwenyewe akiwa katika vikao hivyo tarehe 14 Novemba, yahusu utaratibu wa matumizi ya alama ya maendeleo ya mtahiniwa wa viwango vya ufaulu katika mtihani, iliyoandikwa na Kamishna wa Elimu, Profesa Baralusesa. Vilevile nina barua nytingine ya tarehe 12 Disemba iliyoandikwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Gesimba, ambapo Waziri alijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waziri huyu alikuwa kwenye Baraza la Mawaziri wakati wa majadiliano na alijua kabisa hizo *flexible grading* na *fixed grading*. Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi, baada ya kikao kile alikuja hapa Bungeni akaeleza taarifa na kwa nini wameamua kubatilisha matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, kama Waziri wa Nchi ambaye nina hakika ali-*present* Mawazo ya Baraza la Mawaziri, amekuja ndani ya Bunge lako Tukufu akaeleza kilichojiri na kwa nini Serikali imeamua kubatilisha matokeo, halafu akatoa na utaratibu kwamba sababu kubwa ilikuwa wadau hawakushirikishwa! Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, katika matokeo ya juzi anasema, mchakato huu mpya umefanyiwa utafiti wa kina na wadau wameshirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huoni kwamba hii ni *contradiction* kubwa sana? Kibaya zaidi kile tulichoambiwa kwamba, sasa matokeo ya *Form Four* yanaenda kuchakatwa kwa mtindo wa *flexible*, ule mtindo wa zamani jambo, ambalo Wabunge wote humu ndani hata Kamati ya Mheshimiwa Margaret Sitta inaamini hivyo. Leo Waziri anatoa tamko lingine na ndicho kilichofanyika kwamba, mchakato wa matokeo haya mapya yametumia *fixed grading* na siyo *flexible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kujua tatizo ni nini; inawezekanaje maamuzi ya Baraza la Mawaziri yakiukwe halafu Mheshimiwa Waziri tena bila hata wasiwasi wala aibu anasema Serikali ni moja! Serikali ni moja inaweza kutoa matamko tofauti? Kile tulichokiamini, Wananchi wote wameamini hivyo, wameenda kufanya mabadiliko mengine. Pia nataka kujua inawezekanaje *fixed grading* ikafanyiwa *standardization*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwalimu, ninavyoju *flexible* endiyo inaweza kufanyiwa *standardization*. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie na ninaomba Wabunge tuungane mkono, kwa sababu suala hilli limeleta mtafaruku mkubwa; na hata juzi matokeo ya *Form Six* baada ya watoto wengi kufeli somo la *GS*, watu wanajiuliza imekuwaje tutaenda kufanyiwa *standardization*! Kwa hiyo, sasa hivi watoto wanajua kwamba, wakifeli kuna utaratibu mpya wa kufanyiwa *standardization*.

5 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tujue ni kwa nini Waziri amelidanganya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Hoja yako ni kwamba kwa nini zipo kauli mbili?

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi, wewe umetajwa mara nyingi toka wanajadili. Kutoa shilingi ni hoja, ameshatoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, kutoa shilingi hamuungi mkono, ukisema unatoa shillingi maana yake ni hoja kwa hilo mnaanza kuchangia. Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli dada yangu yangu leo ameamka vizuri, ananitajataja sana, lakini kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, matokeo ya darasa la kumi na mbili yalitangazwa na Serikali, yalileta mshituko mkubwa na ndiyo maana Serikali ililichukulia jambo hili kwa umuhimu wake; na ni kweli Baraza la Mawaziri lilikutana, lakini kabla ya hapo Serikali iliunda Tume ya kuchunguza kilichojiri.

Nyote mnajua, Kamati ile iliongozwa na watu gani. Baraza la Mawaziri lilikutana kupokea ile Taarifa na kuitafakari. Kama mtakumbuka, siku ile nilipokuja hapa, Taarifa niliyoisoma ya Serikali ingawa sasa inaitwa Taarifa ya Lukuvi, nilisema ni Taarifa ya awali iliyotokana na matokeo ya utafiti wa awali wa ile Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukjua kwamba, awali ni awali tu, kwa hiyo, lengo kubwa la ile Taarifa ya Serikali niliyoisoma, tulichotaka ku-*achieve* siku ile ni kuwapa kazi Wizara na Taasisi zake zote warudie upya. Kubwa tulilolitaka na tulilolifanya siku ile ni kufuta yale matokeo. Katika taarifa ya awali hilo tuli-*achieve*. Serikali ilitaka kupeleka meseji, kama mapendeleko ya Kamati ile iliyoundwa kwamba matokeo haya yafutwe ili yaangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kurudia tu kwamba, hakuna tofauti wala kukinzana, Serikali ilifanya uamuzi wa awali na ninyi mnajua, Wabunge mlishinikiza sana kutaka kujua kulikoni, hata juzi Kamati ya Uongozi mmeagiza bajeti hii tipeleke mbele mpaka matokeo yatangazwe. Kwa hiyo, mlichokuwa na hamu nacho ni matokeo ya pili na ambayo Serikali imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo la Taarifa ile ya awali ilikuwa ni kufuta matokeo, kwa sababu bila kufuta matokeo haya hata hiyo kazi ambayo mnasema ni ya Kawambwa isingetokea; wangewezaje kupanga upya na matokeo yameshapangwa yameshatangazwa bila kufuta! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati ilitushauri tufute na tukafuta, lakini Kamati ile inaendelea kufanya kazi mpaka hivi sasa hajatoa matokeo ya mwisho. Kamati ile ile tena imeishauri Serikali labda tuseme kwa sababu hatukuja kutoa taarifa hii ya pili, lakini tulijua Mheshimiwa Waziri Kawambwa atatoa hiyo taarifa ya pili ya Serikali inayohusiana na utaratibu huo.

Kwa hiyo, utaratibu huo uliotumika ndiyo uliowezesha sasa kupandisha matokeo kutoka ile asilimia, nafikiri imepandishwa kwa asilimia tisa. Ufaulu sasa kutokana na matokeo ya awali na haya matokeo mapya ambayo mnayaita ya Mheshimiwa Kawambwa, yameweza kupandisha ufaulu kwa sababu tu yamezingatia taratibu zote za kisheria. Huo utaratibu umezingatia utaratibu wote wa kisheria. Nataka kuwahakikishia kwamba, utaratibu ule ule

uliotumika katika kutangaza hapa umetumika tena katika kutangaza matokeo yanayoitwa ya Mheshimiwa Kawambwa.

Kwa hiyo, nilitaka tu kumwondoa wasiwasi pamoja na dosari zote, pamoja na makaratasi yote uliyonayo Mheshimiwa Suzan, hata sisi tunayo. Hizo barua unazosoma waliandika Wataalam wa Serikali, waliandikiana tunayo na wote tumezisoma. Hatusemi haya, hayaondoi hitilafu zilizokuwepo na hiyo *shock*, hiyo *shock* tunasema hata hao marehemu wetu wanafunzi waliofariki, Mwenyezi Mungu, azilaze mahali pema Peponi roho zao. Tunasikita wote, lakini angalau tumeweza kutekeleza yale tulioahidi.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi ninaomba kuchangia kwenye hoja hii ya matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne ya mwaka jana kama ifuatavyo:-

MWENYEKITI: Hoja kauli mbili zinazokinzana.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kauli mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikaa mwaka jana mwezi Desemba, Wizara ya Elimu na Wataalam wake wamekaa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mulugo yupo, Profesa Mchome yupo, wakaelekeza kwamba, matokeo ya Kidato cha Nne kwa mwaka 2012/2013 yasahihishwe kwa utaratibu mpya. Utaratibu huo mpya ndiyo huo ulioleta hili balaa la matokeo ya mwaka huu.

Baada ya hili balaa kutokea, wanafunzi wamefeli kwa utaratibu ulioelekezwa na Waziri na watu wake. Serikali hiyo hiyo ikamteua Mjumbe wa hicho kikao, Profesa Mchome, aongoze Tume ya kuchunguza kwa nini watoto wamefaulu. Ripoti imeletwa wamefeli. Ripoti kwenye Bunge hili Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema kwamba, kosa ni Baraza

la Taifa la Mitihani lilitumia utaratibu mpya. Ripoti ya Serikali haikusema kwamba tuliwaelekeza watumie utaratibu mpya.

Kwa hiyo, Baraza la Mitihani linalaumiwa kwa kufuata maelekezo ya Waziri na Wataalam wake. Halafu tunakuja hapa tunapewa taarifa mara wanasema tulitumia utaratibu huu wa *fixed*, mara tumetumia utaratibu wa zamani! Hii habari ya kauli mbili, ndimi mbili kama nyoka, ipatiwe maelezo.

MWENYEKITI: Mtoa hoja Mheshimiwa Suzan Lyimo!

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuweza kumalizia hoja yangu. Pamoja na maelezo ya kaka yangu sana Mheshimiwa Lukuvi, amekiri kwamba, utaratibu umekiukwa na nashukuru kama ameona hilo. Siku zote tumekuwa tukisema kwamba, tunawashangaa sana wenzetu kwamba, Serikali hiyo ambayo inasemwa ni sikivu, kwani kulikuwa kuna shida gani kama Mheshimiwa Waziri wa Elimu ama Waziri ambaye alikuja kutoa taarifa mwanzoni, kuja kusema kwamba tulikosea, tulighafirika au hiyo ilikuwa ni hatua ya awali lakini sasa tumeona moja, mbili, tatu, kwa hiyo, tutaendelea na mtindo ule ule!

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala langu liko pale pale kwamba, matokeo haya wala siyo kwamba ni *shock*; kwa sababu kwa kipindi kama ambavyo taarifa yangu inaonesha na takwimu zinaonesha, matokeo ya Kidato cha Nne kwa miaka saba mfululizo yameendelea kuwa mabaya. Mwaka 2011 waliofeli kwa alama ya sifuri walikuwa zaidi ya asilimia 50. Kwa hiyo, haikuwa ni *shock*.

Vilevile niseme tu kwamba, natoa ushauri wa bure kwamba, mfumo wa elimu ni mbovu sana na hivyo, nilikuwa naomba sana kwamba ni lazima Serikali waangalie ni jinsi gani wanaweza kufanya kila linalowekena kuweza kuiokoa elimu yetu, kwa sababu ni wazi kwamba elimu yetu kwa kweli inatishia, ni tishio ipo *ICU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, hili jambo alilolifanya la *standardization* ni jambo baya sana na ninaamini Mheshimiwa Waziri unanisikia kwamba hili jambo halitatokea. Kwa sababu hawa watoto siyo tu kwamba ni watoto wa hapa Tanzania, wanaenda kushindana Kimataifa; kwa hiyo, watakapoju kwamba hawa watoto matokeo yao yalikuwa *standardized*, ni wazi watoto wetu hawana uwezo.

Kwa hiyo, uangaliwe mfumo wetu wa elimu ambaa ni mbovu ili sasa wabasilisha. Vilevile suala zima la bajeti limeongelewa, Bajeti katika Wizara hii ni ndogo. Niseme tu hiyo Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyounda ni ya kwenda kufanya *Reforms* kwenye *Education*. Inashangaza sana, Mwenyekiti wa Tume anakuwa ni *Lawyer*; hatufanyi *Law Reforms* Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kwa hiyo, naomba sana watafutwe *educationist*, tuna walimu wazuri sana. Kuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu, haimaanishi wewe ni mwalimu. Hawa wanakuwa Wahadhiri tu, wanakuwa ni wanafunzi wa kawaida, wanapopata *marks* za juu, *GPA* inapokuwa *4.5 and above*, wanabaki kama Wahadhiri. Sasa ukiniambia Profesa Mchome anaendaje kufanya *reforms* kwenye *education*, mimi sielewi. Hatuwezi kupata mabadiliko yoyote.

Kuna *educationist* wengi sana; kwa nini wasiwachukue hao? Kwa hiyo, nadhani na hii labda ndiyo sababu imemfanya mmoja wa Wajumbe ajitoe, Bwana Rakeshi. Kwa hiyo, niombe tu hii Tume ifanyiwe mabadiliko ili tuweze kuboreshe elimu ya Tanzania. Nakushukuru Mwenyekiti.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – *Finace and Accounts* Sh. 920,920,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

5 JUNI, 2013

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh. 2,656,310,000
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Sh. 386,237,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa*)

Kif. 1005 - *Procurement Management* ... Sh. 431,326,000
Kif. 1006 – *Government Communication*

Unit Sh. 199,930,000
Kif. 1007 – *Legal Unit* Sh. 100,362,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 – *Commissioner for Education* .. Sh. 9,046,881,000

MHE. VITA R. M. KAWAWA: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Kifungu 2001, Kifungu kidogo 220200. Nataka kufahamu hizi ni milioni mia nane au milioni ngapi kwenye gharama hizi za umeme na maji; ni milioni mia nane kwenye Idara hii ya Kamishna wa Elimu?

MWENYEKITI: Angalia hii hesabu, naona mkato wake umekaa mahali pasipo. Hebu ni shilingi ngapi ni bilioni au ni milioni? Umekiona?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Ni bilioni nane.

MWENYEKITI: Milioni?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Ni bilioni nane.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa*)

5 JUNI, 2013

Kif. 2002 – *Inspectorate* Sh. 17,761,374,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa*)

Kif. 3001 – *Basic Education* Sh. 1,304,189,000

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nipo kwenye Kasma hiyo hiyo, kifungu kidogo cha 221700 - *Food Supplies and Services*. Mwaka huu hakijatengewa shilingi hata moja na mwaka jana zilitengwa milioni 55.4. Kwenye bajeti ya Waziri amesisitiza kwamba, wanafunzi watapatiwa vyakula mashulenii kuanzia *Primary School*, lakini hapa tunaona kuna sifuri. Naomba ufanuzi ni kwa nini hakuna shilingi hata moja hapa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kijifungu hiki hakijatengewa bajeti kwa mwaka huu, kwa sababu kitagharimiwa na maduhuli ambayo yatakusanywa na Shule ya Msingi Arusha.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 3002 – *Adult Education and Non Formal Education* Sh. 1,555,375,000

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nami nimeshangazwa kwa sababu Wizara hii ina upungufu wa bajeti. Kifungu 221400 - *Hospitality Supplies and Services*, mwaka jana ilikuwa ni milioni 15,100,000, mwaka huu imewekewa milioni 103, mambo haya ya chakula na vinywaji tu; kwa nini fedha inakuwa nydingi kiasi hiki?

MWENYEKITI: Umekipata kifungu Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimepanda kwa sababu katika mwaka wa fedha tajwa, tunatarajia kufanya mambo ambayo hatukufanya huko nyuma na hasa ni mafunzo ya uwezeshaji wa walimu katika Mpango wa NDIYO NINAWEZA.

Huu ni Mpango mpya wa kuhakikisha tunaondosha kutokujua kusoma kwa watu wazima nchini. Tumepata ushirikiano na wenzetu wa Cuba, lakini kuna *component* ya ndani na wale wawezeshaji watachukua posho zao na mahitaji kwa ajili ya kuendesha mpango huu kutokana na kifungu hiki ambacho hatukuwa nacho kwa ajili ya kazi hiyo kabla.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4001 – *Secondary Education* Sh. 1,979,374,000
Kif. 5001 - *Teacher Education* Sh.47,494,914,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 7001 – *Higher Education* Sh. 499,681,675,000

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 7001, kifungu kidogo 270300 - *Current Grants to Non-Financial and Public Units (Academic Institutions)*. Sasa zinaonekana hela hizi zimepungua kutoka bilioni 182 kwenda bilioni 169. Naamini fungu hili ndiyo litakalolipa madeni ya Vyuo Vikuu. Nilitaja hapa kwamba, Vyuo Vikuu vinadaiwa bilioni 18, Chuo Kikuu Huria kinadai bilioni 2.5. Je, fedha hizo zitatosha na tuna uhakika vyuo hivi vitalipiwa madeni yake?

MWENYEKITI: Kwamba hizi ndiyo hela zenyewe hizo?

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, eee sawa.

5 JUNI, 2013

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa uafanuzi kwa suala la Mheshimiwa Shekifu, kama ifuatavyo:-

Kwamba, kifungu hiki kweli kimepungua pesa, upunguaji huu wa pesa unatokana na kuhamishwa kwa bajeti ya mishahara, baada ya michango kwenye Mfuko wa Pensheni, ambapo michango ile katika Mfuko wa Pensheni huko nyuma ilikuwa inawasilishwa Wizarani na inalipwa kutoka Wizarani na pia pesa za upandishaji vyeo na ajira mpya, hizi sasa kuanzia mwaka huu zimerudishwa Hazina.

Kwa hiyo, zinatengwa katika vifungu vya Hazina. Sisi tena hatutotoa yale makato ya pensheni, hatutolipa kwenye pensheni na ajira mpya hela zile hatutakuwa nazo sisi zitakuwa zimechukuliwa moja kwa moja.

MWENYEKITI: Kwamba hailipi hicho ulichokisema Mheshimiwa Shekifu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7002 – *Techn. And Vocational Training*
Division Sh. 10,043,612,000

MWENYEKITI: Wewe umesimama au umefanyaje?
Mheshimiwa Dkt. Maua! (*Kicheko*)

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kimo changu chote. *Sub-vote 7002, kifungu kidogo 230600 - Routine Maintenance and Repair of Machinery, Equipment and Plant.* Mwaka uliopita hatukutoa chochote na mwaka huu hakikuwekwa chochote. Je, hakuna vifaa vinavyohitaji hata *service* kwa ajili ya *Technical Education?* Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mmekiona? Maelezo.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa kifungu hiki kama ifuatavyo: Kwamba, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na 2013/2014, hatukutenga chochote kwa sababu kasma hii imehamishiwa kwenye kifungu 230400, ambayo ni matengenezo ya magari na kwa hiyo, kuanzia sasa pesa zake utazikuta kule kwenye kifungu 230400.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* Sh. 450,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Policy and Planning* Sh.18,337,604,700

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Najielekeza katika kijifungu kidogo 4397 - *Support VETA*, kimetengewa shilingi bilioni kumi, lakini hali halisi ni shilingi bilioni tisa milioni mia sita. Naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufanuzi kwa sababu katika kitabu chake cha Hotuba, ukurasa wa 200 hadi 206, ameordhesha Wilaya 81 akituridhisha Wabunge kwamba, *VETA* zitajengwa katika Wilaya hizo 81.

Ukienda kwenye randama, ukurasa wa 229, kifungu hiki hizi bilioni kumi zinaonesha ni kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* vinne katika Wilaya ni *VETA* vinne na vyuo vya ualimu vinne. Maana yake Mheshimiwa Waziri umetudanganya au umetuchanganya, huku unasema *VETA* vinne, huko Wilaya 81. Naomba ufanuzi ni kwa ajili ya *VETA* vinne au kwa Wilaya hizi 81 ulizoiandika kwenye kitabu chako cha hotuba?

5 JUNI, 2013

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, ukishamwambia mtu umedanganya umeshamhukumu, sasa unataka ufanuzi wa nini kadanganya basi! Haya Mheshimiwa Waziri kama hukudanganya! (*Kicheko*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa hoja hii kama ifuatavyo:-

Fedha hizi shilingi bilioni kumi ni kwa ajili ya Vyuo vya VETA vinne vya Mkao; Mkao wa Simiyu, Rukwa, Njombe, Geita na pia ukarabati na ujenzi wa Vyuo vya Ualimu Butimba, Dakawa, Marangu na Kleruu, ambavyo vinafundisha masomo ya sayansi. Nia yetu ni kujenga VETA katika Wilaya zote Tanzania. Kwa mwaka huu tumetenga pesa kwa ajili ya hivyo vilivyoainishwa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa*)

Kif. 2001 – *Commissioner for Education* ... Sh. 671,135,135

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa*)

Kif. 2002 – *Inspectorate* Sh. 1,500,000,000

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye hicho kifungu kidogo 6235 - *Strengthening Inspectorate*. Ni kweli kwamba, Wabunge karibu wote, wameeleza matatizo makubwa ya Kitengo hiki cha Ukaguzi na nashukuru kwamba, mawazo yetu kwamba kutakuwa na Wakala yanakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimetengewa shilingi bilioni 1.5, kwenye randama inaonesha kwamba, zaidi ya nusu ya fedha hizi zinaenda kwenye kununua samani. Wote tunajua matatizo makubwa sana ya Kitengo hiki ni pamoja na ukosefu mkubwa sana wa magari, jambo ambalo linafanya Wakaguzi washindwe kufanya kazi zao na hivyo

5 JUNI, 2013

kubaki maofisini. Sasa naomba kujua ni busara gani imetumika samani izidi magari, wakati magari ndiyo tatizo kubwa sana?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi *1.5 billion* zimetengwa na zimeombwa kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi wa shule. Vilevile tumetenga fedha hizo kununua magari tisa kwa ajili ya Ofisi za Ukaguzi za Wilaya na Kanda na kununua samani za Ofisi 22 kwa Wilaya na Kanda na mafunzo ya Wakaguzi wa shule mpya 100.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – Basic Education Sh. 3,302,100,000

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye kile Kifungu Kidogo cha 3280 – *School Wash Programe*, ambayo imetengewa shilingi milioni 384, lakini fedha hizo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kufahamu, kwenye eneo hili la usafi wa kuosha mikono kwa watoto ni kitu cha msingi sana na magonjwa mengi ya watoto kwenye Shule za Msingi, yanatokana na tatizo hili. Ningependa kujua programu hii itashirikisha maeneo yepi na itafanyaje kazi ili kuweza kujua tatizo hili la magonjwa ya watoto mashulenii kutokana na unawaji wa mikono linaweza kuondokaje nchini?

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa, mpaka *World Bank*, mikono? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi shilingi milioni 384, zinaombwa kwa ajili ya kugharimia shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa *School Wash*, unaotekelizwa katika Halmashauri 42. Kuna utafiti ulifanywa na Wataalamu wetu wakapata Halmashauri 42 kwanza,

5 JUNI, 2013

pamoja na kuandaa na kusambaza miongozo ya utekelezaji wa Mradi huu. Mheshimiwa Mhagama, kama utapenda tuje na *list* ya hizo Halmashauri 42, tutawalettea tu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 – Secondary Education Sh. 14,846,576,364

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 4390, naomba kujua, nakumbuka ndani ya Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, aliwahi kusema kwamba, fedha za nje hazitumiki kama posho. Katika Randama ya Wizara hii inasema hivi: *"Kutoa posho ya mazingira magumu kwa Walimu wapya ya shilingi 1.5 billion na fedha hizi zinatoka nje."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba kupata maelezo kama Waziri alilidanganya Bunge au hii ndiyo hali halisi? Na je, kama hizi fedha zinatoka nje, itawezekanaje hawa watu wapate hizo fedha hasa tukizingatia kwamba, fedha za nje hazitoki kwa wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha umelielewa swali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie tu kidogo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Mawaziri wote mkikaa hapa, Kamati ya Matumizi ni kila mtu inamhusu.

Mheshimiwa Susan, naomba urudie.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, ipo siku Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali alisema kwamba, fedha za posho haziwezi kutoka nje ni fedha za ndani. Katika Kifungu hiki inaonesha wazi kutoka kwenye Randama kwamba, shilingi 1.5 billion ni

posho ya mazingira magumu kwa walimu na fedha hii inatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ni kweli fedha za nje hazitumiki kama posho; na kama ndiyo hivyo, kwa nini sasa huku kunaonesha hivyo, ambapo ni tofauti na kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri?

MWENYEKITI: Yeyote Waziri au Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kikawaida, haziwezi zikatoka fedha, yaani Mfadhilli anakuletea anakwambia hii ni posho. Sasa hii inakuwa *embedded* katika programu nzima ambayo imo katika *project* hii, lakini haleti tu akakwambia hii ni posho lipa walimu, inakuwa *embedded* katika programu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 – Teacher Education Sh. 4,000,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)

Kif. 7001 – Higher Education Sh. 28,090,634,801

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ninajielekeza katika Kijifungu Kidogo cha 4304 - *University of Dodoma Project*. Zimetengwa shilingi bilioni moja, fedha za ndani.

Mheshimiwa Waziri, anakumbuka kwamba, Chuo hiki cha Dodoma ujenzi mwingu umeshamalizika, mabweni mengi hayana wanafunzi. Hizi hela nime-*check* kwenye Randama ni kwa ajili ya kujenga *Theatres*, Kumbi za Mihadhara, lakini inaonekana kwamba, zimeshatosheleza na wanafunzi hawapo. Mheshimiwa Waziri, kwa nini usikubaliane na mimi hizi bilioni moja tuchukue tupeleke kwenye mikopo ya

5 JUNI, 2013

wanafunzi, ambayo itawasaidia wanafunzi 500 na yale mabweni yatapata watu wa kukaa mle, badala ya kuziacha hapa wakati kule majengo mengi yamekamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, swali la hapa unauliza hizi za kazi gani, kuhamisha ni *process*, huwezi ukahamisha kwa kauli hii tu, ni *process*. (*Makof!*)

Je, hizi fedha ni za kazi gani?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi wa swali la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya wakandarasi waliojenga miundombinu hiyo, ambayo Mheshimiwa ameitaja. Hatukuweza kulipa katika Kasma ya Mwaka wa Fedha uliopita, kazi zimetekelvezwa, kwa hiyo, kwa maneno mengine ni madeni na tumeitenga kwa ajili ya kulipa madeni hayo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kifungu kidogo 6351 - *Rehabilitation and Expansion of UCLAS*. Kwanza, nataka tu nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, hakuna Chuo kinachoitwa *UCLAS* ni *ARU University*, naomba warekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni kwamba, niungane pia na Mheshimiwa Shekifu kwamba, kwa kweli Vyuo vya Elimu ya Juu, havipelekewi hela zao kwa wakati. Sasa nilieleza kwamba, kwa mfano, Chuo hiki cha Ardhi, ambapo mimi ni *Chancellor*, ni wazi kwamba, hawajapata hela kabisa za maendeleo kwa mwaka huu. Ilipitishwa shilingi milioni 100, lakini mpaka leo ninavyoongea hawajapata hata senti tano. Hivi vyuo vitaishije; wanafunzi kila siku ni migogoro? Wakuu wa Vyuo wanakuwa na matatizo kila siku wanatatua migogoro ya wanafunzi. Naomba Kauli ya Serikali; ni lini Serikali itapeleka fedha katika Vyuo vya Elimu ya Juu kwa wakati kama mpaka tunamaliza mwaka wa

5 JUNI, 2013

fedha, chuo hiki hakijapewa senti tano ya maendeleo? Ninaomba kujua wanategemea hivi vyuo vinaendaje?

MWENYEKITI: Hebu naomba ujibu, hizo hela ni za kazi gani? Hilo ndiyo jibu, hayo mengine ya kwake Mheshimiwa Susan.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi zilizotengwa, shilingi billioni mbili ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu ya mabweni na madarasa katika Chuo Kikuu cha Ardh na zile milioni 100 za mwaka huu, zote zimeshalipwa mpaka hivi sasa, siyo kweli kwamba, hajizalipwa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Aah, sikukuona Mheshimiwa Shekifu; kama hukusimama mwanzo sikuiti. Tunaendelea.

Kif. 7002 – Techn. and Vocational Training
Division Sh. 1,400,000,000

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lanqu liko katika Kifunqu Kidogo Namba 6359 - *NACTE Project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mwaka jana tu *NACTE* walitengewa shilingi milioni 400, lakini kutohana na shughuli nydingi sana zinazofanywa na *NACTE*, nilitegemea kwamba, Serikali ingewawekea fedha kidogo za maendeleo kwa ajili ya shughuli zao. Ninaona katika Mwaka huu wa Fedha, hakuna fedha za ndani wala za nie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kwa nini
NACTE hawakutengewa fedha za maendeleo?

5 JUNI, 2013

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *NACTE* palikuwa na Mradi wa Jengo ambalo lilikuwa linajengwa kwa ajili ya kusahihishia mitihani na kutunga na kadhalika. Mradi ule mwaka jana tuliusengea shilingi milioni 400 na tarehe 30, juzi tu hapa wiki iliyopita, tayari wamepewa shilingi milioni 350 na hivyo, mwaka huu hatujatenga kwa sababu ule Mradi utakuwa umeshamaliza tayari ile *Phase I*.

MHE. JENISTA J. MGAHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono swali la Mheshimiwa Bura, kwa hiyo, limeshajibowi, sina hoja tena.

MWENYEKITI: Ahsante.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge liirudia*)

TAARIFA

SPIKA: Waheshimiwa, hajatoa Taarifa yake, imekuwaje? (*Kicheko*)

Mheshimiwa mtoha hoja, Taarifa?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Mwaka 2013/2014, Kifungu kwa Kifungu pamoja na Mabadiliko na kuyapitisha kwa pamoja. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu, liyakubali na kuyapitisha makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof!*)

5 JUNI, 2013

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yako yote, pamoja na Naibu Waziri, tunawapongeza kwa kazi mliyoifanya na pia Wataalamu wote tunawapongeza kwa kazi. Mmesikia *statements* za Waheshimiwa Wabunge, nadhani wanataka mageuzi makubwa kabisa katika Wizara hii, ambayo kwa utaalamu wenu na kuwasikiliza humu ndani, bahati nzuri humu ndani mna Wataalamu wengi tu wa eneo hilo, nadhani mtachukua *seriously* kusudi mwaka ujao tuweze kupata nafuu ya kuweza kuongea. (*Makofii*)

Wabunge wenyewe, msingoje kupiga kelele hapa, elimu ikiwa inakufa unatangulia hukohuko kwanza; siyo mnasikia hapa, halafu mpaka mtu amekufa mnakuja kuzika maiti. Kwa hiyo, mshiriki, acheni siasa ndani ya elimu. Kwa sababu, mazungumzo yenu leo, mimi niliwanyamazia tu, lakini hayakuwa yanafurahisha maana mnakomoana, mara huyu anakomoa hili, Wananchi hawapendi maneno kama haya, wanataka *material* jamani; ni pande zote sisemi upande wowote hapa. (*Makofii*)

Tabia hizo hata ninyi wenyewe haziwapendezi, laiti mngejisimamisha mkajiona mnavyokazana kumsema mtu; Mbunge ye yote makini hazungumzi *people, talk about issues*, lakini ninyi mnakazana na mtu, mtu, mtu, yaani inaonekana mlivyopungukiwa kwa kweli. Mimi nasema tumepongukiwa. Tumepongukiwa kwa sababu tunatumia muda mwangi kuzungumzia watu, bahati mbaya na watu wenyewe hawamo humu ndani, mnaona hiyo. (*Makofii*)

Hawa watu hawamo humu ndani, mimi mashitaka niliyonayo kule Ofisini, mengine mpaka nashangaa hivi

5 JUNI, 2013

inakuwaje! Lakini ni kwa sababu ya kutumia midomo yetu *loosely*, ndio sababu yenyewe. *When people discuss about people*, haya ni matatizo; watu wana-discuss issues, kwa hiyo, Waheshimiwa tuna tabia mbaya hii. (*Makofi*)

Baada ya hapo, naomba niwapongeze wote kwa kazi nzuri mliyofanya. Nina tangazo moja tu; Katibu wa Bunge, ambaye ni Msimamizi wa Chaguzi zetu Ndani ya Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, zoezi la uteuzi wa wagombea katika nafasi za Uwakiishi kwenye Mabaraza ya Vyuo Vikuu na SADC PF, limekamilika leo tarehe 5 Mwezi Juni, 2013 saa 10.00 jioni.

Taarifa kuhusu kukamilika kwa zoezi hili pamoja na majina ya Wagombea walijitokeza katika nafasi husika, imebandikwa kwenye ubao wa Matangazo, Jengo la Utawala na Lango Kuu la Ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo, walioteuliwa pale, mtaenda kuwakuta huko.

Naomba niwatakie jioni njema na ninapenda kuahirisha Kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi.

Kesho, Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hakitakuwepo.

(*Saa 1.35 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 6 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)